ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13.Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
22. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
23. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
24. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
25. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
26. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
27. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
28. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
29. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe

30. Mhe. Ali Salum Haji - Jimbo la Kwahani
31. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) - Jimbo la Kijitoupele
32. Mhe. Ame Haji Ali - Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk - Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asha Abdalla Mussa - Jimbo la Kiwengwa
35. Mhe. Bahati Khamis Kombo - Jimbo la Chambani
36. Mhe. Bihindi Hamad Khamis - Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Hamad Abdalla Rashid - Jimbo la Wawi
38. Mhe. Hamida Abdalla Issa - Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Hamza Hassan Juma - Jimbo la Shaurimoyo
40. Mhe. Hassan Khamis Hafidh - Jimbo la Welezo
41. Mhe. Hidaya Ali Makame - Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) - Jimbo la Mtoni
43. Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Jimbo la Paje
44. Mhe. Khadija Omar Kibano - Jimbo la Mtambwe
45. Mhe. Machano Othman Said - Jimbo la Mfenesini
46. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti - Jimbo la Mtopepo
47. Mhe. Makame Said Juma - Jimbo la Kojani
48. Mhe. Maryam Thani Juma - Jimbo la Gando
49 Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Jimbo la Bububu
50. Mhe. Mihayo Juma N'hunga - Jimbo la Mwera
51. Mhe. Miraji Khamis Mussa - Jimbo la Chumbuni
52. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha - Jimbo la Mtambile
53. Mhe. Mohamed Said Mohamed - Jimbo la Mpendae
54. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
55. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
56. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
57. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
58. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
59. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
60. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
61. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
62. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
63. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
64. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
65. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake

66. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
67. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
69. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
70. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
71. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
72. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
74. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Jimbo la Micheweni
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
77. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
78. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
79. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
80. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
81. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
83. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
84. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Saba – Tarehe 30 Mei, 2016

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika *(Mhe. Zubeir Ali Maulid)* Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 40

Changamoto za Bodi ya Uhaulishaji Ardhi

Mhe. Ali Suleiman Ali: (Kny: Mhe. Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Bodi ya uhaulishaji Ardhi ni chombo kilichoundwa ili kufanikisha mambo ya uhaulishaji.

a) Je, tangu ilipoundwa imeweza kuingiza mapato kiasi gani katika mfuko wa Serikali na imeshakutana mara ngapi.

b) Je, ni utaratibu gani unaotumika wakati Bodi inapotaka kufanya maamuzi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: (Kny: Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira) - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 40 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuastavyo.

(a) Mhe. Spika, tangu Bodi ya Uhaulishaji Ardhi ilipoanza kazi zake rasmi, tarehe 05/03/2009 haiingizi fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hiyo ni kutokana na mfumo wa kisheria unaoongoza utaratibu mzima wa ukusanyaji na utumiaji wa mapato ya bodi, ambapo bodi inaruhusiwa kukusanya mapato kutokana na vianzo vya uuzaji wa fomu za maombi ya uhaulishaji ardhi na ada ya uhaulishaji. Mapato hayo hutumika kwa kuendeshea kazi za kila siku za bodi bila kutegemea ruzuku kutoka serikalini.

Mhe. Spika, bodi itaanza kuwasilisha mapato katika Mfuko Mkuu wa Serikali mara tu itakapoanza kuwa na ongezeko la mapato juu ya mahitaji halisi ya matumizi yaani *surplus*.

Aidha, kwa upande wa vikao, bodi hufanya vikao vyake kwa mujibu wa kanuni ambapo imeelekezwa kufanya kikao cha kawaida si chini ya kimoja kwa mwezi. Hata hivyo, bodi kwa kawaida imekuwa ikifanya kikao kimoja cha kawaida na kimoja cha dharura kwa mwezi tokea kuanzishwa kwake.

(b) Mhe. Spika, ili uhaulishaji ufanyike mambo matatu huwa ndio msingi wakutolewa maamuzi ya kuidhinishwa au kukataliwa na Bodi ya Uhaulishaji. Mambo hayo ni:

i) Mhaulishaji athibitishwe kuwa ana haki ya kisheria ya kumiliki anachotaka kukihaulisha.

ii) Ithibitike kuwa uhaulishaji husika huathiri maslahi ya wengine na ya umma kwa ujumla, na kwamba haendi kinyume na Sera, Sheria na Miongozo ya nchi yetu.

iii) Ithibitike kuwa hakuna mtu au taasisi itakayoathirika kutokana na uhaulishaji huo.

Hivyo, Bodi ya Uhaulishaji hutumia wataalamu wa Sekta ya Ardhi kama vile Maafisa wa Ardhi, Upimaji, Mpango Miji na Vijiji, Eka na Wathamini wa Ardhi pamoja na wanasheria kuhakiki masuala ya ki-jamii, umiliki, matumizi ya ardhi na upambanuzi wa mipaka ili kuhakikisha uhaulishaji salama na wenye maslahi kwa ujumla. Aidha, bodi kwa kutumia utaratibu wa kujaza fomu za uhaulishaji, hukusanya maoni ya Kamati ya Sheha na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya wa eneo linalohusika ambayo husaidia kwa kiwango kikubwa kutoa maamuzi sahihi ya bodi.

Kwa ujumla bodi hutumia utaratibu wa kuendesha kikao kila baada ya siku 14 ambapo:

- Huhakiki Fomu za Uhaulishaji zinazojazwa na pande mbili zinazohusika na uhaulishaji na kupatiwa maoni na Kamati ya Shehia na Serikali ya Wilaya.

- Hujadili na kupata ufafanuzi wa ripoti za wataalamu kuhusiana na kinachotaka kuhaulishwa kwa misingi ya miongozo iliopo na maoni ya kitaalamu.

- Kutoa maamuzi ya kuidhinisha uhaulishaji, kukataa na kutoa maelekezo ya kutekelezwa kabla ya hatua ya kuidhinisha au kukataa maombi ya uhaulishaji.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Bodi ya Uhaulishaji Ardhi ni chombo muhimu katika nchi yetu, na chombo hiki kinakusanya mambo mengi, kama uhaulishaji, sijui utoaji viwanja au uuzwaji na mambo mengineyo. Pia tumeshuhudia migogoro mingi katika nchi yetu bado inaendelea pamoja na bodi hii kufanya kazi zake vizuri.

Je, Mhe. Spika, Mhe. Waziri atalieleza nini Baraza hili ili na wananchi wajuwe, ni kiasi gani cha mafanikio kilichopatikana kwa muda wa toka mwaka 2009 hadi mwaka huu wa 2016, kwa mafanikio ya utekelezaji mzuri ili kuondoa kero kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri kwa majibu tafadhali. Mhe. Waziri mwenyewe yupo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Spika, bodi yangu imefanikiwa kwa asilimia kubwa kuondosha migogoro na kuhaulisha yale maeneo ambayo watu wameomba kuhaulisha. Nasema hili kwa sababu gani mafanikio makubwa yamepatikana, ni watu wengi wameomba kuhaulisha viwanja vyao na mali zao, lakini bodi yangu imeweza kufanya hivyo na wameweza kuhaulisha, isipokuwa tu pale ambapo pana matatizo, kwa sababu kuna sheria ambayo inafanyakazi na bodi hii. Pia ili uweze kuhaulishiwa utaratibu wake lazima Sheha athibitishe Mkuu wa Wilaya athibitishe, lakini pia na watathmini wetu na wenyewe bodi ni lazima waende wakakaguwe yale maeneo. Kwa hivyo, maeneo mengi yamekaguliwa na mtathmini ametathmini na hati ile wamepatiwa.

Mhe. Spika, lakini katika yale maeneo ambayo yanapingamizi au kuna mtu anaweka pingamizi au kuna sababu ambazo bodi inaona kwamba haina sababu ya kuhaulishwa. Kwa hivyo, hawawezi kuhaulishiwa kutokana na utaratibu na sheria iliopo. Kwa hivyo, mafanikio makubwa yamepatikana. Lakini katika

suala zima la mchango, bodi kutokana na sheria iliyopo sasa hivi wanajiendesha, na kwa sababu wanajiendesha zile pesa za mapato yanayokusanywa hayana *surplus*, kwa hiyo wanaendesha shughuli zao na fedha zile haziingii katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Ahsante *(Makofi)*

Nam. 68

Upatikanaji wa ZBC TV Usioridhisha

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) - Aliuliza:-

ZBC TV ni chombo muhimu sana kwa wananchi wa Zanzibar kwa kupata habari za ndani na kimataifa.

Je, ni sababu gani inayosababisha chombo hicho kupoteza sauti na kuganda picha mara kwa mara.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 68 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, nakubaliana kwa dhati kabisa kuwa ZBC – TV ni chombo muhimu sana kwa wananchi wa Zanzibar kwa kupata habari za ndani na za kimataifa.

Mhe. Spika, pia nikiri kuwa kumejitokeza tatizo la ZBC – TV kupotea sauti na kuganda kwa picha mara kwa mara.

Mhe. Spika, tatizo hili linatokana na kuharibika kwa chombo cha usafirishaji wa picha na sauti *Microwave*. Hivyo basi, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imechukua hatua za dharura ili kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo hili ikiwa ni kama hatua za awali.

Vile vile ili kutatua tatizo hili lisijitokeze Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo imechukua hatua ya kuiangiza ZBC – TV ifanya taratibu za haraka kutumia Mkonga wa Taifa, kwa ajili ya kusafirisha picha kutoka Karume House kwenda Rahaleo.

Mhe. Spika, ni natumaini yetu baada ya kukamilika kwa hatua hizo, tatizo hilo ama litaondoka kabisa au litapugua kwa kisi kikubwa, kwani wakati mwengine

hali ya hewa ya mvua na mawingu inaweza kuathiri ubora wa picha na sauti, hasa ikiwa umerusha mawimbi kwa kutumia *Microwave*.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya serikali yenye kigugumizi, naomba kuuliza swali moja lenye vifungu (a) na (b). Mhe. Spika, kwa kuwa tatizo hili hutokea sana wakati wa mvua na kwa sababu vile vile TV nyengine zote zilizokuwepo hapa Tanzania halitokei. Vile vile kwa sababu Mhe. Naibu Waziri amekiri kuwa kuna *Microwave* imeharibika na kuongeza katika Mkonga wa Taifa.

(a) Je, ni kwa sababu zipi au anaweza kutoa elimu gani kwa wananchi ili wajuwe TV yao imekabiliwa na tatizo gani.

(b) Mhe. Spika, kwa sababu Mhe. Naibu Waziri ameonesha chombo hiki ni muhimu sana katika jibu lake la msingi, na kwa sababu ni TV ya mwanzo ya rangi katika Afrika ya Mashariki. Je, serikali haioni haja sasa kuibinafsisha na kuendesha kibiashara TV hii.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumjibu kwamba kama lilivyojibiwa swali la awali na Mhe. Naibu Waziri. Pia nampongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yaliyokuwa sahihi na yenye ufasaha ambayo kayatoa hapa. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni wazi kwamba kweli TV ya Zanzibar kwa jina ambalo sasa hivi tunaliita ZBC televisheni, ni chombo muhimu sana kwa wananchi na kuundwa kwake chombo hiki kilikuwa kina lengo moja tu kama swali lake lilivyoulizwa, kilikuwa kina lengo la kutoa elimu kwa umma, na kazi hiyo ndio maana inaonekana tofauti baina ya TV ya Zanzibar na TV nyengine zote zile ambazo zinaonekana hapa kwetu, elimu imekuwa ni jambo ambalo limepewa msingi.

Kwa hivyo, suala zima la kutoa elimu tunaendelea nalo na TV Zanzibar itaendelea nauwezo wake na njia zake za kuelimisha umma, haitachoka kuanzia pale ilipofanyakazi hiyo tangu kuundwa kwake kwa TV ya rangi mpaka hapo tunapokwendea. Suala zima la elimu litakuwa ni suala endelevu na wananchi wetu watapewa elimu kadiri pale hali ya TV yetu inapoendelea kuboreshwa.

Vile vile nataka kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba, kweli TV yetu ilikuwa na matatizo ya kusitasita kwa sauti na picha. Lakini tatizo hilo limeondoka na hivi sasa TV yetu inarusha matangazo yake kwa kutumia njia zote mbili. Njia ya *Analogy* na njia ya *digital*. Kwa hivyo, katika kukabiliana na tatizo hili inawezekana mheshimiwa akawa na TV ambayo hairuhusu *digital*, lakini

anununwe kile king'amuzi chetu ili apate njia ya *digital* basi TV yake itakuwa ni safi na haina tatizo kabisa kwenye hilo. Kama TV inaonesha kwa njia ya *Analogy*, hapo ndio inaonekana kwamba kuna tatizo ambalo linaonekana kama picha hazionekani ziko safi. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahani Saidi (Baba Changana): Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi namuuliza Mhe. Waziri kwamba tuliondoa TVZ na kuipeleka ZBC kwa nia ya kuiboresha, lakini mpaka sasa hivi TV yetu TVZ au ZBC maeneo mengi sana hasa Pemba, inakuwa ni tabu kweli kweli kuipata na TV hii ndio TV inayosema kweli na ndio TV ambayo tunaitegemea kwa kila hali. Je, wamejipangaje kutoka kwenye TVZ kuja kwenye ZBC kwa kuboresha zaidi kupatikana bila ya king'amuzi au kwa sababu zozote, ukifungua TV basi TV iweze kupatikana kwa niaba ya wananchi wote. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri mwenyewe kwa majibu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika. Ni kweli kwamba TV yetu inaonekana pande zote visiwa Unguja na Pemba, na niwazi kwamba katika kipindi cha nyuma kidogo ilionekana kwamba matangazo na picha zinazorushwa kwa upande wa Pemba zilikuwa zinalegalega. Lakini hii yote kama tulivyojibu katika swali mama, tatizo tulipata maharibiko ya *Microwave* ambayo sasa hivi ndio tunatumia kurushia TV yetu. Suala zima la kuepuka king'amuzi, Waheshimiwa Wawakilishi huu ni ulimwengu wa *digital*, tupo katika mipango ya kutoka *Analogy* na kuingia kwenye hatua za kutumia *digital*.

Kwa hivyo, unaporusha picha kwa kutumia *digital* ni lazima kutumia king'amuzi. Lakini kwa ubora wa TV Zanzibar ilivyo ZBC TV, ni wazi kwamba hata akawa na gari, picha ya TV ya Zanzibar ataipata na kwa mwenendo tunaokwenda nao sasa hivi muda mfupi ujao, picha zetu zitaonekana zina ubora kwa sababu tutakuwa tumetoka kabisa kwenye matangazo ya *Analogy* na kutumia matangazo ya *digital*. Kwa hivyo, mheshimiwa asiwe na wasi wasi kaa mkao wa kutengeneza TV yetu itafika wakati utaona kama kwamba hakuna kiyoo pale, utatamani umguse mtu bila ya kuwa na kiyoo pale. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuweza na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Kwanza niwapongeze wafanyakazi wa ZBC TV kwa kufanyakazi katika mazingira magumu. Lakini kwa kuwa haki ya kupata habari za ndani na nje ni haki ya msingi kwa mujibu wa katiba.

(a) Je, ni kwa nini ZBC TV taarifa zake nyingi zinakuwa ni za viporo, zinakuwa zimeshapitwa na wakati?

(b) Je, wizara imejipanga vipi kulitatua tatizo hili ili taarifa tunazozitoa ZBC TV ziwe zinakwenda na wakati, ahsante.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa heshima yako napenda kumjibu Mhe. Muwakilishi swali lake la nyongeza lenye a na b.

Ni kweli baadhi ya taarifa zetu zinaonekana kama ni taarifa za kiporo, napenda kumpa elimu ndogo tu kwamba panapokuwa na taarifa za kiporo, taarifa zile ama zimepatikana *time* zidi ya jioni, au inawezekana kwamba taarifa zile ziko mbali sana na kituo cha Televisheni, inawezekana kwamba ziko Pemba.

Kwa upande wa Pemba, tulikuwa tuna tatizo zima la usafirishaji wa file la taarifa kutoka Pemba kuja Zanzibar; tatizo hilo ambalo wiki moja limewekwa sawa na sasa hivi anaweza kuwa na taarifa kutoka Pemba siku hiyo hiyo taarifa hizo zitatoka, kwa sababu taarifa hizo zinasafirishwa kwa kutumia *Internet* na wakati huo tulikuwa tuna *Megawatts* kidogo lakini hivi sasa tumeongeza *Megawatts* zetu kufikia kwenye *Kilowatts* na tunaweza kurusha *file* kutoka Pemba na likaingia Zanzibar na siku hiyo hiyo taarifa zikawa zimepatikana. *(Makofi)*

Vile vile aliuliza suala la pili, kwa nini Mheshimiwa naomba arudie kidogo swali lake la pili.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Swali la (b) nimeuliza je, Wizara ina mkakati gani ili tatizo hili kuliondoa ili taarifa zake ziwe zinatoka *up to date*.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo hivi sasa tupo katika maboresho makubwa ya kutengeneza *ZBC TV* na tunachokisema matatizo haya yote yataondoka, ikiwa tutaingia ulimwengu wa *Digital*, hatua nzuri za kufika kwenye *Digital* zimeanza kuchukuliwa. Nataka nimhakikishie tu kwamba tumeunda timu ndani ya Wizara yetu na timu hiyo inafuatilia na watu ambao wako tayari kuisaidia Televisheni, wamejitokeza tumewakubalia wapo tunafanya taratibu za kiserikali ili hatua hizo za mwisho ziweze kufikiwa. Ni muda mchache tu tatizo hilo kama nilivyosema katika majibu ya nyuma linaweza kuondoka tutakapoanza kutumia *Digital System*. *(Makofi)*

Nam. 48

Ukosefu wa Mashine ya Ukaguzi Bandarini

Mhe. Ali Suleiman Ali (Kny. Jaku Hashim Ayoub) – Aliuliza**:**

Kumekuwepo na malalamiko kwa muda mrefu kwa wananchi kupekuliwa na askari kwa kutumia mikono na kupapaswa maungoni yakiwemo maeneo ya faragha, kutokana na ukosefu wa mashine ya kukagua mizigo na abiria.

a) Mashine ya ukaguzi wa mizigo na abiria bandarini inagharimu kiasi gani mpaka Serikali ishindwe kununua mashine hiyo pamoja na umuhimu wake.
b) Serikali haioni ni uvunjaji wa haki za binaadamu kufanya ukaguzi askari kwa kupapasa sehemu za viungo vya mwili wa abiria, na kupekua bila ya kujali jinsia na mzigo wa mwanamke kupekuliwa na mwanaume.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 48 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kumfahamisha Mhe. Mwakilishi kuwa Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari imeweka utaratibu kwa wasafiri wanawake kupekuliwa na Maofisa wanawake na wanaume kupekuliwa na Maofisa wanaume pale inapobidi msafiri kupekuliwa mwilini.

Mhe. Spika, kwa upande wa upekuzi wa mizigo, hupekuliwa na Afisa yoyote aliopo wakati wa upekuzi bila kujali jinsia kwani ndio utaratibu wa kawaida katika Bandari zote.

Mhe. Spika, Wizara yangu kupitia Shirika la Bandari ilikusudia kununua Mashine za kuchungza mizigo na abiria *(X-Ray Screening Machine na Walk through Metal Detector)* katika mwaka wa fedha unamalizika (2015/2016). Shirika halikuweza kununua vifaa hivyo kutokana na upungufu wa fedha hasa baada ya kununua vifaa muhimu vya kuhudumia mizigo Bandarini.

Mhe. Spika, hata hivyo, Shirika la Bandari limeupa kipaumbele Mradi huo katika mwaka ujao wa fedha (2016/2017) na tayari limetenga kiasi cha Tshs. 450,000,000/= kwa ajili ya kununua mashine mbili za kuchunguza mizigo pamoja na milango miwili ya kuchunguza abiria katika gati ya abiria Malindi.

Mashine hizo zimekisiwa kugharimu kiasi cha Tshs. 225,000,000/= kwa kila moja ikijumuisha gharama za mashine yenyewe, mlango, ufungaji na mafunzo kwa wafanyakazi.

Mhe. Ali Suleima Ali (Shihata) Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, bandari yetu ya Zanzibar ina hadhi kubwa sana katika jengo lake na kwa wakati tuliokuwa nao dunia inategemea twenda na wakati, je, pamoja na kusema kwamba bajeti iliyopita haikuwezekana kutekelezeka kutokana na mambo tofauti na Serikali imetenga bilioni mia mbili *point* fulani, Wizara kwa kuharakisha hili haioni pana haja ya dharura kuweka mkakati mzuri wa ukaguzi, ili kunusuru jamii yetu isipitishwe vitu ambavyo havina usalama katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ni kweli tunajua kwamba usalama wa raia nchini tumeupa kipaumbele sana na sisi ndio maana tumehakikisha kwamba mashine hizi katika robo ya mwanzo tu ya mwaka huu 2016/2017 tunazinunua, ili kuondosha usumbufu kwa abiria wetu, na vile vile kulinda usalama kwa wananchi wetu na nchi yetu kwa jumla.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Naibu Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwanza Mhe. Naibu Waziri niungane na muuliza Suala kwamba mashine ya ukaguzi wa mizigo na abiria bandarini na hata viwanja vya ndege ni kitu muhimu sana, je, Mhe. Naibu Waziri ni lini Serikali itafanya juhudi za makusudi kupeleka kifaa hicho katika kiwanja cha ndege cha Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Sisi tunajua kwamba bandari na vile vile viwanja vya ndege ni muhimu sana kwa ulinizi na usalama wa raia na nchi yetu, kwa hivyo tunahakikisha kwamba vile vifaa vya ukaguzi tunaviweka sehemu hizo. Napenda kwanza kuwapongeza sana watu wa bandari kwa juhudi walizochukua mpaka kuhakikisha kifaa hiki tunakipata na vile vile watu wa viwanja vya Ndege Mamlaka wamejitahidi sana, mimi nilikuwa shuhuda juzi nilipoenda wamejiimarisha sana ulinzi nilitoka mimi. Kwa bahati kuna kitu nimesahau na nilipotoka kwa mlango huu mwengine basi nikakaguliwa tena hawakujali nafasi yangu kama mimi ni Naibu Waziri, bali walitumia wajibu wao kuhakikisha kwamba usalama wa raia unalindwa. Kwa

hivyo mimi nawapongeza sana Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Bandari kwa hatua wanazochukua kuhakikisha kwamba usalama wa raia unakuweko na wa nchi yetu.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza masuala mawili ya nyongeza yenye a na b.

a) Suala la kwanza ni suala la ukaguzi na wageni na watu wanaosafiri kukaguliwa unapotoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam. Hali kadhalika unapotoka Dar es Salaam kwa boti kuja Zanzibar. Lakini hutokezea wakati mwenginekwa upande wa watu wanaosafiri kutoka Dar es Salaam kuingia Zanzibar hupekuliwa kwa ukaguzi wa kina. Kwa sababu tayari mahala ambapo wanapotoka wameshakaguliwa vya kutosha wanapofika hapa mara nyingi hufanyiwa ukaguzi ambao unakagua kutokana na kwamba unahisi huyu anahitajika amulikwe au unamtilia wasi wasi au shaka au pengine mtu ana mizigo kupita kiasi.

Pia hufanyika ukaguzi wa kina kwa kila abiria wakati mwengine wana watoto wadogo, wakati mwengine ni wageni, wakati mwengine ni watalii ambao wametoka safari. Ni kwa nini Ukaguzi huu hufanyika kwa wale wasafirishaji wote.

b) Hili pia lilikuwa ni suala la ukaguzi wa watu wanavyopita katika masuala hili mnaita *detector* katika jibu lake alilojibu katika suala la msingi, wakati mwengine unakuta mkaguzi japokuwa mtu anamkagua abiria badala ya kuwa mkaguzi ni mwanamke anamkagua mwanamme na hutokezea wakati na nimeshuhudia mwenyewe unakuta kijana mdogo anamkagua mama mtu mzima, kwa sababu yule mwanamke anakuwa hayupo ama ameondoka kwenda kunywa chai……

Mhe. Spika: Mheshimiwa samahani hebu nenda kwenye swali.

Mhe. Simai Mohammed Said (Mpakabasi) Swali ni hatua gani za kinidhamu zinachukuliwa kwa ukaguzi wa watu wanaosafiri pale ambapo mwanamke anatakiwa amkague mwanamke mwenzake na mwanamme amkague mwanamme, hawapo. Ahante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ukaguzi anaosema ni kweli tunafanya lakini kama nilivyosema hapo mwanzo kwamba ukaguzi katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa salama ni muhimu

sana, hasa ukiangalia kwamba sasa hivi hali ya usalama duniani imeathiriwa sana na mambo ya kigaidi. Kwa hivyo sisi hata kama wenzetu kule Tanzania Bara wanafanya ukaguzi hatujui wenzetu nao huko linaweza kutokezea kosa au upungufu sehemu fulani lakini sisi lazima tujiridhishe. Mimi namuomba sana Mhe. Simai atukubalie kwa ukaguzi huu tunaofanya kwa maslahi ya nchi yetu na wananchi wetu kwa jumla.

Kwa hivyo tunamuomba sana atukubalie hili tunavyolifanya na wala mtu yeyote ambaye hana tatizo, nina hakika kwamba hatokuwa na wasi wasi pale atakapopekuliwa kwa mara nyengine tena katika bandari zetu au Viwanja vyetu vya ndege.

Suala lake la pili, kusema kweli kama nilivyojibu katika suala la msingi kwamba sisi mizigo anaweza kukagua mtu yeyote lakini iwapo kweli kuna mtu huyu amepekuliwa isivyo kihalali basi tunamuomba atuletee jina la huyo mtu aliyempekua na sisi tutachukua hatua zinazofaa Inshaala. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hapo ndio mwisho wa sehemu hii ya masuali, Waheshimiwa mtagundua kwamba leo kidogo tuna masuali pungufu sio kama kawaida na yamemalizika mapema. Tunaendelea na michango kwenye bajeti ya Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais na tegemeo letu kwamba leo leo tuhitimishe, kwa hivyo itakuwa vizuri kama tutaanza kuchangia mapema, ili waweze kupata watu wengi zaidi kuchangia. Kwa sababu walioomba mpaka sasa ni wengi. Lakini kama mtakuwa mnakumbuka kwamba tulitengua kanuni na kufanya kwamba wale watakaokuwa wanachangia watachangia kwa muda wa dakika kumi na tano tu.

Sasa kabla sijamwita Mhe. Mwenyekiti kuja kuchukua nafasi hii naomba kwanza sasa nitoe matangazo ya wageni ambao wametufikia leo hii. Wageni wetu wa mwanzo ni watoto wa Mhe. Bahati Khamis Kombo, Muwakilishi wa wananchi jimbo la Chambani, Khamis Haidar Omar na Abuu Talib Haidar, wapo kwa ajili ya kujifunza shughuli za baraza zinavyoendeshwa. Karibuni sana, naona wako hapo juu.

Mgeni wa pili ni mgeni wa Mhe. Simai Mohammed Said Muwakilishi wa Tunguu (Mhe. Mpakabasi), huyu ni Bwana Andrew Smith yule pale, huyu ni mzaliwa wa Kenya na ni Mwenyekiti muanzilishi wa Jumuiya ya Wawakezaji sekta ya Utalii Zanzibar ZATI nafasi ambayo baadae ilirithiwa na Mhe. Mpakabasi mwenyewe yaani alirithi kutoka kwake.

Pia Mr. Andrew ndio mmiliki wa Blue Bay Beach Resort na yupo hapa Zanzibar zaidi ya miaka ishirini.

Wageni wetu wanaofuata ni wanafunzi kutoka Chuo cha Diplomasia kutoka Dar es Salaam pamoja na Chuo cha Utawala wa Umma cha Zanzibar ambao wapo hapa Barazani kwa mafunzo ya vitendo yaani field, karibuni sana.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya matangazo hayo sasa naomba sasa nimuite Mhe. Mwenyekiti, ili aje achukue nafasi hii na baada ya hapo ataanza kutoa nafasi kwa waheshimiwa ili kuweza kuchangia bajeti ya hii Wizara, karibu Mhe. Mwenyekiti.

(Hapa Mhe. Mwenyekiti, alikalia kiti)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Mtumizi ya Wizara ya Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Nimuite Mhe Yussuf Hassan Iddi lakini kabla ya hapo nilikuwa naomba Ndugu Wajumbe tupunguze zile shukurani kwa sababu muda wetu ni mdogo badala ya dakika thalathini tuzitumie dakika zetu kumi na tano tulizokubaliana wiki iliyopita, kwa mazingatio zaidi.

Mhe Yussuf Hassan Idd: Ahsante Mhe, Mwenyekiti, kwa kuweza kunipa fursa na mimi mapema leo hii kuweza kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, Kwanza kabisa sina budi nimshukuru Makamu wa Pili wa Rais kwa namna alivyowasilisha hotuba hii, lakini pia niwapongeze Waziri pamoja na watendaji wa Wizara hii kwa kumsaidia Mhe. Makamu kwa kufanyakazi vizuri.

Pia nitumie fursa hii kwa kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Fuoni kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi ili niwawakilishe katika chombo hiki muhimu cha kutunga sheria kwa kupitia kikao hiki nawaahidi sitowaangusha.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza michango yangu ningeomba tu kama dakika zangu zitakwisha basi angalau uniongeze na dakika tano za ziada ili yale niliyoyakusudia kuyazungumza basi yote nipate kuyawasilisha.

Mimi nitaanza kwenye ukurasa wa 18 kwa kitabu hiki cha Makadirio kwenye ukusanyaji wa Mapato. Nataka kujua sababu zilizopelekea Idara ya Mpiga chapa mkuu wa Serikali kutofikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo katika milioni 600 walizopangiwa kukusanya wamekusanya milioni 279 sawa na asilimia 47, kwa hivyo hapa Mhe. Waziri ilikuwa naomba nipate ufafanuzi kwa nini Idara hii ya kupiga chapa haikufikia malengo.

Vile vile mkakati gani ambao wameuandaa kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017 ya kufikia malengo ya milioni 793. Halkadhalika katika ukurasa huu huu katika chanzo chengine cha Wizara hii ambacho kinakusanya mapato ni Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya kitaifa, sasa hapa mimi nilikuwa nataka kujua tu kwa nini Idara hii kiwango cha kukusanya mapato hakikubadilika kimebaki kile kile cha mwaka 2015/2016 ambapo milioni 12,360/= ndizo walizopangiwa, na mwaka huu wamepangiwa vile vile, licha ya kwamba inaonekana kwamba kwa mwaka 2015/2016 wana uwezo mkubwa wa kufikia lengo lile, ambapo mpaka kufikia Machi, 2016 wamekusanya jumla ya Shilingi milioni 10 sawa na asilimia 83. Kwa nini makusanyo yanaonekana ni mazuri lakini kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kiwango kimebaki kile kile cha mwaka uliopita.

Mhe. Mwenyekiti, niende haraka haraka katika ukurasa wa 21 kwenye utekelezaji wa fedha. Idara ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha uliopita imepunjwa sana ambapo asilimia 8.8 kati ya milioni 289,000,000 ndio wamepatiwa hawa, ni sawa na milioni 25 tu ambazo wamepatiwa mwaka mzima watu wenye ulemavu. Kwa kweli hawa wanahitaji fedha nyingi ili kuweza kutatua matatizo mbali mbali ya kiofisi.

Mhe. Mwenyekiti, matumaini yangu kwa kuwa idara hii kwa mwaka huu wa fedha ipo katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais basi mgao wa fedha utaongezwa maradufu ili kuweza kukidhi haja. Vile vile kwenye ukurasa wa 24 programu ya kukabiliana na maafa, nilipopitia kitabu hiki cha Mhe. Waziri sikuona zoezi la vitendo la kukabiliana na maafa kama ilivyofanya katika bajeti zilizopita. Kwa hiyo, nilikuwa namuuliza Mhe. Waziri yaani *simulation exercise* kwa mwaka huu wa fedha sikuona na zoezi hili ni muhimu ili kuwajenga kikosi kazi kile cha uokoaji, kuwajenga uwezo wa vitendo ili

kuweza kukabiliana na maafa. Kwa hivyo, nilikuwa nataka Mhe. Waziri atakapofanya majumuisho anipe maelezo kwa nini mwaka huu wa fedha halikuwemo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kama tunavyojua tarehe 17/04/2016 hapa tulitokezewa na maafa, hapa Zanzibar na wafadhili mbali mbali walijitolea michango yao ya fedha na vifaa mbali mbali. Sasa nilikuwa nataka kuuliza Mhe. Waziri je, ni shilingi ngapi zilizopatikana kwa wafadhili wa ndani na wa nje waliochangia waathirika wale wa maafa ya mwezi Aprili, 2016.

Pia mgawanyo wake ulikwenda vipi ni wale tu waathirika wote walipata mgao huu au ni wale waliokaa kwenye makambi ndio waliopewa fedha hizo. Kwa hivyo, nilikuwa nataka ufafanuzi katika eneo hilo. Pia nataka nijue serikali imegharamia kiasi gani makambi yale ya waathirika wa mvua zile za mwezi uliopita.

Mhe. Spika, niende kwenye programu ndogo C0122 uratibu wa sherehe na maadhimisho ya kitaifa. Ukija kwenye tabu kubwa hili fungu C01, *page* C8 kuna kifungu hiki idadi ya viongozi na wananchi wanaoshiriki katika sherehe na maadhimisho ya kitaifa yanayofanyika nje ya Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2015-2016 walioshiriki ni 300 na vile vile kwa mwaka huu 2016-2017 ni idadi ile ile. Sasa naona idadi ni kubwa na wakati katika bajeti hii 2016-2017 tuna mkakati wa kupunguza matumizi. Sasa je, ile kauli ya kupunguza matumizi mbona haiendani na data halisi zilizokuwemo katika kitabu hiki.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo katika mwaka wa fedha 2015-2016 Idara ya Sherehe na Maadhimisho ilipangiwa kutumia shilingi 987 lakini mwaka huu wa fedha, fedha hizo zimeongezwa maradufu hadi kufika bilioni 1,037,000,000. Sasa nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri tuko katika mkakati wa kupunguza matumizi, lakini mbona fungu la sherehe hizi linakuwa kubwa, na ukizingatia kwamba wenzetu wa SMT wamefanikiwa vizuri katika mambo haya ya sherehe na maadhimisho kwa kufuta sherehe nyingi. Kwa hivyo, na sisi tunatakiwa tuige mfano ili ile dhana ya kubana matumizi iwe sahihi.

Mhe. Mwenyekiti, ukija kwenye ukurasa wa 25 kwenye fungu C0123 ambayo inahusika na masuala ya Muungano. Hapa Mhe. Waziri nataka kujua mchanganuo wa nafasi za ajira kwa taasisi zetu za Muungano ukoje, tunapata asilimia ngapi katika taasisi zetu za Muungano. Na kwa mwaka wa fedha 2015-2016 tumepata nafasi ngapi za taasisi za Muungano na mwaka huu tunaokwenda nao wa 2016-2017 hizo nafasi zitakuwa ngapi.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 31 kwenye Baraza la Wawakilishi ukifungua kitabu kikubwa hiki fungu C02 *page* C27 kwenye kipengele cha changamoto. Katika kipengele cha changamoto, changamoto namba ya kwanza ni mfumo mbaya wa mawasiliano katika ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi. Tatizo hili ni la muda mrefu toka katika mikutano ya bajeti iliyopita, lakini hadi leo halijapatiwa ufumbuzi. Sasa nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri je ni lini hili tatizo la *echo* katika ukumbi wetu huu wa Baraza la Wawakilishi litamalizika kwa sababu ni la muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile kuna changamoto ya mwisho kuwepo kwa idadi kubwa ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Ni kweli Baraza hili la Tisa lina wajumbe wengi wapya nikiwemo mimi Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Masharubu). Kwa hivyo, kwa kuwa wajumbe wengi ni wapya hatuna elimu ya kisheria, kiuchumi, kiutandawazi na kadhalika je wizara imejipanga vipi kutujengea uwezo sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hasa wapya ili tukaweza kufanana kama kina Komredi Hamza na Mhe. Machano ili tuweze ku-*copy* vizuri kuweza kutetea wanachi wetu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ilikuwa nataka nipate ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile katika mijadala ya Baraza lilopita yalitoka mapendekezo kwamba ripoti za Kamati Teule ziwe na nguvu za kisheria na kutambulika kwenye vyombo vyetu ya Mahakama, sasa nataka kujua hili pendekezo limefikia wapi. Vile vile katika upande wa Baraza la Wawakilishi kuna tatizo la ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Kisiwani Pemba hali yake si nzuri na hili nataka kujua ni lini ukumbi ule utakamilika na kuweza kutumika kama kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, nije ukurasa wa 32 kuhusu Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Kwanza naipongeza Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kwa kutekeleza na kufanikisha uchaguzi wa marejeo wa tarehe 20 Machi. Lakini pongezi za pekee zimuendee Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Mhe. Jecha Salim Jecha, pamoja na Mkurugenzi wake kwa uzalendo na umakini wao wa kuweza kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Ningemuomba tu Mhe. Rais…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika mbili.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: He! Naomba uniongeze na zile tano nilizoomba mwanzo.
Kwa hivyo, namuomba Mhe. Rais watendaji hawa tuendelee kuwa nao ili ikifika uchaguzi wa 2020 tuwe nao kuweza kufanikisha shughuli zetu za uchaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa katika Tume ya Uchaguzi nilikuwa na mambo kama mawili, tunajua Zanzibar tuna majimbo 54 ya uchaguzi kwa hiyo tuna wawakilishi 54, lakini kwa upande wa wabunge tuna wabunge 50. Sasa nilikuwa nataka kujua sababu zilizopelekea kwa upande wa wawakilishi kwa nini tukawa tuna wabunge 50 badala ya 54, halafu nataka kujua je Tume ya Uchaguzi *ZEC* imeshakutana na Tume ya Taifa *NEC* kwa ajili ya kutafuta muafaka haya majimbo 4 yaliyobakia na uchaguzi wake utakuwa lini. Kwa sababu naona kuna wengine wanaanza ku-*trot* katika majimbo hayo. Kwa hivyo, tupate ufafanuzi je uchaguzi katika majimbo haya 4 utafanyika au lah.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Tume hii ACP. Kheriyangu pamoja na watendaji wake kwa kufanya kazi katika mazingira magumu. Mhe. Waziri ningekuomba tungefanya ziara katika Tume hii ili kuona ugumu wa watendaji hawa wa Tume ya Kuratibu za Dawa za Kulevya.

Pia ukiangalia bajeti yao ukurasa wa 40 ni taasisi pekee ambayo ina bajeti ndogo kuliko zote katika wizara hii ni milioni 439,000,000. Kwa hivyo, milioni 439,000,000 sitegemei kwamba inaweza ikapunguza tatizo la uingiaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, pia hapa katika dawa za kulevya nilikuwa nataka kujua tu kituo cha kurekebisha tabia kule Kidimni ni lini kituo hiki kitakamilika ili kuweza kuleta tija ile iliyokusudiwa. Vile vile nataka kujua athari kwa ujumla ya dawa za kulevya katika jamii yetu ikoje, iko juu, imepanda na asilimia ngapi.

Vile vile katika suala hili la uwazishwaji wa *Sober House* umewasaidia vipi waathirika wa dawa za kulevya na waathirika wangapi wamepata nafuu kupitia nyumba hizi za *Sober House.*

Mhe. Mwenyekiti, suala la mwisho katika ukurasa wa 20 katika kitabu hiki imeelezwa kwamba…

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii asubuhi hii na mimi nikachangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Rais.

Kwanza na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na tukaweza hudhuria katika ukumbi huu kutekeleza majukumu yetu kama tulivyopangiwa. Ila niende moja kwa moja katika kuchangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Rais na kabla sijaenda huko pengine muda wangu ukaja ukawa mdogo kwanza naiunga mkono hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza Mhe. Makamu wa Rais katika hotuba hii kwenye vipaumbele vyake alivyoviweka kwenye ukura wa 4 hasa pale kwenye kifungu cha 11 vikiwemo vya miundombinu na mawasiliano. Kwa kweli vipaumbele hivi navyo ni muhimu sana kama alivyoviona yeye mwenyewe na mimi naviona ni sawa sawa, na vina umuhimu mkubwa sana. Kwani vipaumbele hivi vilivyotajwa hapa vitapewa msukumo wa nguvu katika masuala ya mazao ya kilimo na ufugaji kwa kweli itasaidia vijana wetu ambao wako nje wanapiga kelele na ajira. Ingawa wao ukiwaambia masuala kama haya baadhi yao waliokuwa hawajaamka wanaona kwa nini hawaendi maofisini. Lakini wale ambao kuwa washaona umuhimu wa kilimo na mifugo basi wanakwambia hatutaki kazi ya ajira za serikali. Kwa hivyo, kipaumbele hiki kikipewa nguvu basi tutaweza kutekeleza ile dhana ya kupunguza ajira kwa vijana.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika masuala ya huduma za elimu. Katika vipaumbele alivyotoa Mhe. Makamu wa Rais katika hotuba yake masuala ya elimu jambo lolote la elimu ndio kwanza, kwa sababu hata Mtume wetu (S.A.W) kwanza aliambiwa soma ikijuulikana kwamba mambo yote haya tunayotumia teknolojia hizi ni kutokana na elimu. Kwa hivyo, naipongeza hotuba hii kwamba nayo imeliona ni muhimu sana, lakini tu itakapofika wakati wa utekelezaji, basi namuomba na mimi Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aiangalie katika jimbo langu kuna matatizo haya kama vile Skuli ya Shengejuu kule kuna mabanda ambayo kuwa serikali iliahidi kwamba wataweza kuezeka, lakini hawakuezeka wananchi wenyewe walijenga na baadae wakaezeka. Sasa hivi kuna skuli nyengine za maandalizi zimejengwa banda hilo linahitaji kumaliziwa, na kwa sababu tu mifuko yetu hatujajua itakuwa ni vipi naomba nguvu ya serikali ipatikane hapo.

Vile vile katika jimbo langu la Mgogoni Kisiwani Pemba kuna sehemu ya Skuli ya Mgogoni wenyewe pia liko banda limejengwa linahitaji kumaliziwa kwa kujengwa na mambo mengine. Vile vile katika skuli yangu ya Pandani ambayo mimi mwenyewe nimesoma skuli hiyo na kumalizia hapo kuna matatizo ya nyumba ya walimu. Walimu wa skuli ya hapo mara nyingi huwa wanapata walimu kutoka nje na hufikia lazima kukodi nyumba ambayo kuwa ni gharama kubwa kwa skuli, ukizingatia sasa hivi mifuko ile ya kuchangisha hamna.

Kwa hivyo, kipaumbele hicho nacho kiwepo katika ujenzi tusaidiane mimi na wao na serikali kuhakikisha zile nyumba za walimu zinatengenezwa, nyumba hizi ni za asili bado sehemu nyengine ziko madhubuti zinahitaji ukarabati lakini ukarabati mkubwa. Naomba tusaidiane kwa hili.

Pia katika vipaumbele alivyoviweka hapa Mhe. Makamu wa Rais katika hotuba yake ni suala la afya. Afya kama wanavyosema watabibu wetu kwamba afya ni tunu, kwa hivyo lazima kila mmoja awe nayo tunu hiyo. Katika jimbo langu la Mgogoni kuna kituo kizima ambapo ni kikubwa kilijengwa kituo hiki kwa ajili ya kutoa huduma mbali mbali, ikiwemo huduma ya kuweza kuzalia mama mjamzito pale. Lakini huduma hii hadi leo haipatikani mara nyingi sana nishawahi kuziona gari zinatokea sehemu kama Micheweni kukimbilia Mjini hospitali ya Wete, lakini kwa sababu uzazi haujuulikani wanasema ni kama wingu la mvua. Haijuulikani kama utafika kule hospitali ya Wete au lah hatimae hapa wazazi huzaa katika majumba ya watu binafsi nimeshayaona haya.

Kwa hivyo, kitakapoimarishwa kituo hiki kwa kupatiwa nyumba ya daktari maana ndio tatizo, tatizo sio madaktari ni nyumba ya daktari ili awepo karibu na huduma hizi ziweze kupatikana. Kuwepo kwa nyumba hiyo ya daktari kutasaidia wananchi ambao watatokea hapa Shumbaviamboni, Pandani na Mgogoni badala ya wote hawa kuelekea Micheweni au kuelekea hospitali ya Wete ambayo ni hospitali kubwa zitakuwa zina msongamano wa watu wengi. Kwa hivyo, naomba sana utakapofika wakati wa utekelezaji nafasi hii na mimi niweze kupewa uwezo katika jimbo langu.

Mhe. Mwenyekiti, pia suala la afya Mhe. Makamu wa Rais hapa katika hotuba yake inazungumzia suala la udhibiti wa malaria. Malaria ilikuwa ni sugu kwa Zanzibar lakini naipongeza serikali kwa jitihada yake mpaka sasa hatua inaendelea na tumeona kwamba malaria inapotea. Lakini pamoja na hatua ilizokuwa ikichukua kwa kupiga dawa na kutoa elimu kwa wananchi pamoja na kugawa vyandarua kuna jambo nimeliona limejitokeza, ni kwamba baadhi ya vyandarua vyetu vinavyotolewa vina matatizo.

Vyandarua vinaambiwa kwamba kabla ya kukitumia uwezo kukiweka hewani kwa masaa 6, lakini mimi binafsi nimeweza kukiweka hata kwa masaa 12, ukiweza kuingia ndani ya chandarua hicho ni muasho mkubwa naupata na huwezi kulala. Kwa hivyo, baada ya kujitibu na inakuwa unatafuta maradhi, naomba vichunguzwe vyandarua hivi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 4 kwenye suala la mafuta na gesi. Naipongeza serikali kwa kuleta jambo hili mbele yetu kuona kwamba linaanza kuwekewa vipaumbele. Suala hili lipo kwa muda mrefu katika nchi yetu ukienda katika kumbukumbu nyingi unaziona kwamba masuala ya Zanzibar kuwepo na gesi upo, lakini sasa naipongeza serikali kuona kwamba tayari imejipania kulitekeleza kwa vitendo.

Naomba suala hili lisiendelee kuwa hadithi katika masiko ya Wazanzibari, basi upatikane utekelezaji wake na wananchi waweze kufaidika na matunda haya na serikali iwache ile mambo ya tegemezi bajeti zetu tunaziona kwamba nyingi tunapata nafasi kusaidia na wafadhili kutoka nje. Lakini tutakapofanya suala hili ni imani yangu kwamba tutaweza kujikimu kwa mapato yetu ya ndani.

Mhe. Mwenyekiti, suala zima la umeme vijijini, suala hili limezungumzwa katika hotuba yetu hiyo tumeipokea, lakini pia vile vile kuna changamoto katika vijiji vilivyomo ndani ya jimbo langu. Kama vile nilivyoendelea kuzungumza kwamba kuna vijiji mpaka leo havijawahi kupata umeme na umeme ni muhimu sana. Vijiji vya Kwale Mpona, vijiji vya Bungala, vijiji vya Mvimbe Pandani watu hawa wametengwa kabisa na umeme, kijiji cha Kiungoni kule Macho si mboni na Mchambaji Pembeni vijiji hivi naomba serikali kupitia shirika hilo liweze kupeleka huduma hizo na wananchi wafaidike na nishati hii umeme.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kurudia katika sehemu ya elimu kwa maendeleo na kiuchumi. Dira ya maendeleo ya sura ya elimu imetajwa katika kitabu hotuba hii na ni nzuri sana, lakini ilivyozungumzia suala la vituo vya amali. Mhe. Mwenyekiti, vituo vya amali vimeshajengwa Unguja na Pemba lakini naomba kwanza serikali kabla haijaandaa na kujenga vituo vyengine kama vile Mtambwe na kwengineko, tufanye tathmini ya hivi vilivyojengwa vimeleta tija gani, watu wamepata mwamko gani ili tuweze kuendelea na vyengine. Kama tutaendelea kujenga vituo tu na tukasema tuna kituo hapa na hapa, lakini wananchi wenyewe hawajaanza kuvitumia ipasavyo basi itakuwa tunapoteza fedha ya serikali ambayo kuwa tungeipeleka katika kuchangia masuala mengine ya maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika masuala hayo hayo ya elimu kuhusiana na Bodi za Mikopo. Bodi za Mikopo zimekuwa zikitoa mikopo kwa wananchi wetu lakini hairidhishi. Naipongeza serikali kuandaa mfuko huo lakini bado haukidhi haja naendelea kusema hivyo. Kwa hivyo, kupitia wizara hii ofisi yako Mhe. Mkamu wa Pili wa Rais basi suala hili hiki ni kilio cha wanafunzi wetu ambao wanataka mikopo, mikopo unapewa hata robo tatu haufiki na yeye

anasoma kwa tabu hana uhakika kama atamaliza. Kwa hivyo, naomba uangaliwe vizuri zaidi kwa sababu kama tutaendelea kwa namna hiyo watoto wa kimasikini hawataweza kusoma.

Vile vile tuendelee katika mambo ya elimu tuna lugha yetu ya Kiswahili. Mhe. Mwenyekiti, tunaona kwamba tunapiga kelele hapa kwamba tukuze mila zetu, lakini leo lugha yetu ya Kiswahili tunaanza kuipoteza. Hata tunazungumza katika hotuba zetu tusichanganye lugha tutumie lugha yetu ya Kiswahili, lakini kwa nini inakuwaje leo mwanafunzi ambaye amepasi masomo ya Kiswahili anaambiwa kama hakusoma na thamani yake ni ndogo? Kwa hivyo, tutukuze kilicho chetu kwanza halafu ndio tuangalie, wenzetu sasa hivi elimu mbali mbali zinaletwa nchini Ufaransa ya Kifaransa, Kichina kinaletwa hapa, lakini sisi chetu leo tunaanza kukidharau itakuwaje, tukuza kilicho chako mpaka ustahi cha mwenzako. Hayo maneno ya hekima ya Marehemu Mzee Abeid Amani Karume tuyafanyie kazi.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kutoa mchango wangu katika Sekta ya Uwezeshaji, kupitia sekta hii naipongeza sana serikali kwani Mfumo wa Uwezeshaji kuuanzisha Mfuko huu uongezwe fedha, ili wananchi walio wengi na vijana waweze kupata na kuutumia ipasavyo tuone mafaniko yao. Naomba sana kwa serikali.

Moja kwa moja niendelee katika masuala ya mtambuka ambayo yanahusiana katika mazingira. Naipongeza serikali kwa hatua iliyofikia, kwani tunaona dunia kwamba inapiga kelele mabadiliko ya tabia nchi. Hii inatokana na kwamba miti mingi imeondoka na gesi ambayo kuwa imetanda katika hewa zetu huko dawa yake ni kupanda miti kwa wingi, lakini leo sasa hivi miti mingi inakatwa kuliko inayopandwa, ile dhana nzima ya kata mti panda miti haipo ipasavyo. Kwa hivyo, serikali itilie mkazo sana suala hili, itatilia mkazo kwanza hivyo vitalu vya miti viwepo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi nimekwenda katika sehemu za vitalu unaambiwa miche mbali mbali haipo ikitolewa tu, ikianza kufunguliwa kwamba miche tayari, basi akija mtu mmoja tu ambaye ana hamasa ya kupanda miti unakuta hamna. Kwa hiyo, suala hili nimeona ni vyema serikali kupitia vyombo vyake basi ilitilie mkazo hata wale watu binafsi au vikundi vya ushirika vinavyoanzisha masuala kama hayo wapewe kipaumbele na badala yake vitu hivi vikishakuwepo *nursery* waweze kuhamasishwa wananchi juu ya upandaji wa miti.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika suala zima la Baraza letu la Wawakilishi limezungumzwa katika ukurasa wa 15. Naipongeza serikali kwa kuendesha Baraza hili na kuweza kutoa huduma mbali mbali ikiwemo mikutano hii tunayoendelea nayo, lakini kutoa elimu kwa wajumbe hili ni jambo zuri sana na iendelee kutupa huduma kama hii. Kwa sababu kama tunavyojua Baraza letu hili lina wajumbe wengine ni wapya ili kuweza kufanya kazi zetu vizuri huduma ya elimu kwa Wajumbe wa Baraza iendelee na kupitia hata na taasisi nyengine tukiacha mfuko wa serikali.

Katika Baraza hili la Wawakilishi kupitia idara hii naomba sana Ofisi ya Baraza la Wawakilishi iliyoko Pemba iongezewe fedha katika upatikanaji wake ni mdogo sana, asilimia ni ndogo ukitizama ambayo imepatikana kwa mwaka. Ofisi hii kupatiwa pesa Pemba tutawasaidia sisi wajumbe kutoka Pemba tunapotaka kuja huku kuweza kupata nauli zetu pia na huduma nyengine ambazo zinahitajika kule Pemba. Kwani kuna ofisi, kuna majengo, magari, yote yanahitajika katika shughuli mbali mbali za serikali. Naomba sana iangaliwe ofisi yetu hii.

Pia niendelee katika suala la Tume ya Uchaguzi. Kwa kweli pongezi zangu kubwa sana kwa Tume ya Uchaguzi kwa juhudi yake iliyofanya ya kufanya uchaguzi wa mwaka 2016 mwezi wa Machi na ukafanyika kwa usalama na kwa utulivu kabisa, badala ya ule ambao ulishatayarishwa kwa kuharibika kwa watu wachache ambao wana tamaa ya fedha wakaweza kuharibu uchaguzi wetu, lakini pia hii ilikuwa ni heri na sisi tukaweza kuingia katika chombo hiki.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono katika hotuba hii kwa kupitia zaidi katika Idara ya Upigaji Chapa nayo ambayo imejitahidi kufufua idara hii muhimu. Kama tunavyoweza kumiliki vyombo vya habari kwamba viwe vya serikali na kupiga hatua katika chombo hiki cha upigaji chapa ni muhimu sana naomba kiendelee kuboreshwa. Lakini nina masikitiko kuona kwamba utakwenda baadhi ya ofisi ukaambiwa hatujapata nakala hizi kwa mfano kama vyeti vya vizazi na vifo, utaambiwa suala hili hatujapata kutoka *press* tatizo ni nini? Idara ni yetu yenyewe lakini tukaambiwa bado vyeti vya kuzaliwa havipatikani. Sasa niombe pia kwamba zile idara ambazo zinahusika zilipe yale madeni, kwa sababu hii idara kama hatutaisaidia kuipelekea pesa zake zikaweza kununua vifaa hata hivyo vyeti havitapatikana. Kwa hivyo, niiombe serikali nayo kwamba wizara husika ipewe fedha za kutosha, pia na wao wanapozipata walipe kwenye idara hii ya uchapaji iweze kufanya kazi zake kwa vizuri za serikali hata mtu binafsi iweze kuongezea pato la nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuendelea katika shughuli za maendeleo katika Mifuko ya jimbo. Naipongeza serikali kwa kuanzisha Mifuko hii ni muhimu sana, naomba isimamiwe vizuri. Kwa sababu baada ya kuangalia ripoti zilizopita wenzetu wengine walifanya ubadhirifu wakionesha miradi iliyokuwa haina uhakika, haijakaguliwa, hesabu zake hazijulikani.

Mwaka 2016/2017 naomba sana wananchi wote wakae mkao wa kula kwamba wawakilishi wa safari hii watazitumia pesa hizo kama ilivyokusudiwa na serikali. Lakini Mifuko hii iongezwe kwa sababu changamoto ni nyingi hasa Kisiwani Pemba majimbo yamekuwa mayatima. Hizo shughuli zinazooneshwa ukienda kwenye vijiji ukiuliza ziko wapi hazipo. Kwa hivyo, safari hii hayo yataondoka tukijaaliwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Umemaliza?

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika moja.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante itanitosha hiyo. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze serikali kwa kuangalia watu walemavu. Kitengo hiki ni muhimu sana kwa sote kuwa ni walemavu watarajiwa *time* yoyote. Kwa hivyo, hawa nao wasitengwe wapewe kipaumbele ndio kama idara nyengine.

Mwisho niendelee kukushukuru wewe Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii, pia naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Mgogoni. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti ahsante, namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia uzima na kuwajaalia wajumbe wote kufika salama.

Mimi nitaomba kuchangia hotuba hii na nitaanza na suala la UKIMWI. Kwa kweli UKIMWI ni hatari na ni balaa katika dunia nzima, suala la UKIMWI ndani ya Zanzibar lipo kubwa kutokana na takwimu zilizopita za mwaka 2015 UKIMWI Zanzibar inasemekana uko asilimia 0.4, hatima yake baada ya mwaka tu sasa hivi tunaambiwa upo asilimia 1. Kwa kweli kama hatujachukua juhudi za ukakamavu, za ujasiri, basi tutakuja kuumia sana na suala hili litaambukizika vibaya sana kwa mwaka ujao.

Mhe Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika hotuba yake kwa upande wa wanawake ambao wanafanya biashara za kujiuza basi takriban asilimia 19.3 wanapata maambukizi ya UKIMWI kwa njia hiyo. Kwanza tungeangalia hizi sehemu za madanguro, tunaambiwa hazipo lakini zimejaa Zanzibar, ukienda kwenye klabu zote, kwenye mabaa mfano mdogo Mbweni usiku ukipita kuanzia saa sita wanawake wanajiuza mpaka barabarani hata kwa mkopo.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar hii imeharibika hata huko kulikoanza hizi biashara za wanawake kujiuza basi hawafanyi kama wanavyofanya Zanzibar. Hivi sasa unapita sehemu unasimamishwa kama daladala ili umpate yule mwanamke ukamtumie kwa njia iliyokuwa siyo. Mimi ningeiomba sana serikali na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wakawachukulia hatua hawa watu wenye mabaa ambao wanawaleta wale wanawake kwa njia ya kufanya biashara hizi bila ya msimamo. Serikali yetu inasema haina dini lakini sisi asilimia 99.7 ni Waisilamu, kama suala hili tutaliachia basi kuna hatari hata sisi wenyewe na watoto wetu watakuja kuumia katika suala hili la UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wanoambukizika UKIMWI asilimia 11.3, vile vile kwa njia za kujidunga kwa wale wanaotumia madawa ya kulevya, wanapata UKIMWI kwa kutumiana kwa mambo ya mapenzi wavuta unga kwa wavuta unga na ndio maana wanapata hayo maradhi. Haya yote yanasababishwa kwa sababu naweza kusema wizara au ofisi iliyopita sijui imefanya kazi gani hata UKIMWI umekua kwa wingi na usimamizi wake naona sio mzuri. Kwa sababu hivi sasa Zanzibar kila kona unayoijua wewe wamejaa wanawake wanajiuza imefika hatua imeshakuwa mtihani mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala lililozungumzwa kwamba kuna wanaume wanaambukizana UKIMWI kwa kufanya mapenzi wenyewe kwa wenyewe. Kwanza mimi mwenyewe naona aibu kutaja hili suala, kwa sababu wanaume wazima tunafika hatua tunafanya mambo kama haya na tunapata maradhi kama haya.

Kwa kweli kuna siku nilizungumza suala moja hapa la kwamba sehemu za jela zetu Zanzibar zile sehemu zinatakiwa ziwekwe kamera kwenye vyumba vyao, kwenye sehemu wanazocheza na ikiwezekana hata karibu na choo. Kwa sababu kukiwa na kamera zitaweza kuwazuia kufanya yale matendo wanayofanya wanaume kwa wanaume ndani ya jela zile.

Hizi kamera tusiweke kwenye miji tu, tukaweke na sehemu muhimu kama hizi kwenye jela na sehemu nyengine muhimu ambazo zinatakiwa ziwekwe ili wale

watu waogope, wakiona kamera inarekodi wataogopa kufanya masuala yale. Kwenye jela zetu hawa wafungwa wanafanya mapenzi sana wenyewe kwa wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeomba sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ikashirikiana na taasisi za Kiisilamu na taasisi nyengine za dini ndani ya nchi yetu zikaenda kutoa elimu juu ya masuala ya UKIMWI na vile vile kufuatiliwa kwa ufanisi zaidi ili kupunguza hili suala kwa jumla. Kwa kweli masuala haya ni makubwa na ni hatarishi na tunahitaji mwongozo mkubwa sana wa kusimamisha masuala haya, tusiweke tu suala la kwamba mtu anataka kufanya mapenzi ili asipate UKIMWI akanunue mipira kwenye *pharmacy*.

Mhe. Mwenyekiti, ikiwezekana hii mipira inayoitwa *condom* serikali ipige marufuku kuingia ndani ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sisi ni Waisilamu kama mtu anajisikia mwanamme anataka mwanamke basi aongeze mke, tumepewa fursa ya wake wanne kama hawezi kuowa hana uwezo basi afunge, ndio dini yetu inavyotwambia, sio kukaa tu nje kwenda kuchukua wanawake halafu tukaongeza matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi wanawake wa siku hizi baadhi yao sio wote wapo tayari kumwambia mume bora chukua mwanamke nje lakini usiniolee mke mwengine. Hili suala lipo na linaumiza sana, naomba kwa wale wote wenye mambo haya basi wakajaribu kuyaachilia wakawaruhusu waume zao ili yakapungua haya maradhi na wale wanaume wenye matatizo ambayo wanahisi hawawezi bila kufanya mapenzi na wanawake basi waowe sio wakanunue wanawake na kuharibu wanawake wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda kwenye Tume ya Kudhibiti na Kuratibu Dawa za Kulevya. Mheshimiwa Dawa za kulevya Zanzibar zinaongoza na inawezekana hata hii idadi tunayoletewa kutoka huko kwenye hizo wizara au idara ikawa ni za uongo, wavuta unga ni wengi sana Zanzibar. Suala hili linatokana na kwamba wizara husika naamini haijashirikiana vizuri kukamata hawa wanaoleta unga ndani ya nchi.

Wauza unga Zanzibar watu wengi wanawajua lakini hakuna hata mmoja aliyekamatwa, kila siku serikali inakamata wavuta unga lakini sio waletaji. Naomba sana wizara hii kwa mara ya kwanza kuwa imeingiziwa hizi idara ifanye kazi kihaki lil-lahi ili kupunguza hili suala la madawa ya kulevya.

Mimi nasimama hapa kutetea wananchi, kutetea serikali yangu na kuhakikisha wanaofanya mambo haya wote wanakamatwa kwa njia yoyote ile. Zanzibar

tunajua na polisi wengine wanajua sehemu fulani kunauzwa unga, Miembeni mjini kunauzwa unga lakini mpaka leo hakuna sehemu iliyofungwa na wanaendelea kuuza na wavuta unga wadogo wadogo wanadhalilishwa wanakamatwa, lakini wale waletaji hawakamatwi.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana polisi wakapewa nguvu zaidi za kuwakamata hawa watu, najua hili suala ni zito na gumu, sio Zanzibar tu dunia nzima la kukamata hawa wenye kuleta madawa ya kulevya. Naomba sana serikali na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iimarishe zaidi ulinzi hata upande wa bandari. Kwa sababu uletaji wa unga unaletwa kwa njia tofauti sio uwanja wa ndege tu, kwenye bandari ndogo, bandari kubwa na sehemu nyengine za ujanja ujanja zinatumika. Mifano midogo tu nchi za nje mpaka majeshi wanashiriki kuleta unga kutia kwenye manuari zao.

Mara ya mwisho mwaka 2014 Uingereza ilikamata manuari ya kijeshi ina unga karibu tani 20,000 kwamba wale wenyewe majeshi wanashiriki kwenye masuala haya. Sasa ningeomba sana serikali hata hawa waliowapa majukumu haya kusimamisha masuala ya unga, basi na wao wenyewe wakawachunguza kwanza utendaji wao wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ingenieleza au ikanipa takwimu ni wangapi wanaoleta unga nchini Zanzibar wamekamatwa kwa mwaka 2010 hadi 2015 na wangapi walioleta kutoka nje ya nchi ambao sio Wazanzibari wamekamatwa hapa nchini. Ningeomba nije nipate takwimu hiyo ili niweze kujua.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema vile vile bajeti hizi zinazowekwa katika suala la UKIMWI, suala la Madawa ya Kulevya, Idara ya Mambo ya Ulemavu, kwa kweli ni ndogo sana. Kama walivyoeleza wajumbe wenzangu idara ya mambo ya sherehe shilingi 1,037,000,000 lakini ukiangalia hizi idara zote tatu haijafikia kiwango hicho. Hii ni kweli tunaomba tuliangalie sana.

Kwa hivyo, masuala ya kudhibiti madawa ya kulevya ningependelea sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais serikali yake ikajenga kila mkoa eneo kubwa lenye vyumba kama hizi *sober house* wanazojenga watu binafsi ikajenga serikali, ikawakamata hata wavuta unga wadogo kwa nguvu wakapelekwa kwenda kuachishwa unga sio itegemee tu. Kwa sababu wazee wengine wanatozwa shilingi karibu laki tatu au nne mtu mmoja kumuachisha unga, wazee ni masikini hawana uwezo wa shilingi laki nne mtoto wao kuachishwa unga. Naomba sana hata kama kuna bajeti inayotaka kupitishwa kununua magari yetu

wawakilishi au mawaziri naomba sana yasinunuliwe magari hayo na pesa hizo zikajengewe nyumba kwenye madawa ya kulevya ili kuachishwa watu kula unga.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi sisi viongozi tunajiangalia sisi tu nikiwemo mimi mwenyewe. Mimi naomba sana kama kuna jambo la muhimu basi waangaliwe watu hawa sio pesa ziwe ndogo mambo mengine yawe makubwa. Naomba sasa hivi idara ziangaliwe wajengewe kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu serikali itakuwa na uwezo nao ijenge majumba mazuri iwachukuwe hawa hata kwa nguvu na kuwakamata na kuwaachisha ungua. Binaadamu hawa wengine uwezo wao mdogo hawatoweza kulipa laki nne kuwenda kuachishwa mambo ya unga wanapata tabu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeendelea na suala la ulemavu au Idara ya Ulemavu. Kwa kweli Idara ya Ulemavu inastahiki haki kubwa kwa sababu hata ukiangalia serikalini si wafanyakazi wengi walioajariwa ulemavu tunaajiriwa sana wazima wazima lakini walemavu kazi hawapewi.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana bajeti yao ingeangaliwa hawa kwa sababu mimi mwenyewe nimeangalia hotuba hii ni nzuri lakini waliosidiwa kupewa vifaa hawafiki hata 80. Ni kitu ambacho kidogo sana walemavu ningeomba sana wangelitafutiwa utaratibu wakaekewa bajeti kubwa kuna walemavu hawana miguu wanataka miguu ya bandia wanunuwe uwezo hawana, mguu unafika laki sita unaambiwa Mnazi mmoja mguu mmoja, kuna walemavu hawana mkono wanataka mkono pesa hawana wanatembea bila ya mkono ambao serikali ingewapa ule mkono wangeweza kukamatia kitu lakini hawana kwa sababu hawana pesa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna walemavu wa macho , kuna walemavu wa masikio wanataka mashine za kusikia lakini serikali utoajiwa wake wa vifaa bado ni mdogo. Kwa kweli sisi ni binaadamu na hapa tupo tu tmekuja kwa sababu tumepata nafasi za ukubwa lakini tunajisahau. Kwa sababu mimi mwenyewe binafsi kama nitaambiwa serikali haina pesa ya kununua hivi vifaa vidogo vidogo basi mimi niko tayari kwenye pesa zangu zote za masuala ya semina zote nifipewe mpaka nimalize miaka mitano, lakini pesa zikatiwe kwenye masuala hayo.

Mhe. Mwenyekiti, tusikae tu tukafikiria sisi tutafaidisha vipi kujenga majumba mazuri ya serikali tutanunua magari mazuri, tutafanya hivi, na hawa lazima wawekewe bajeti yao watumie tusijifikirie sisi tu. Mhe. Mwenyekiti,

ikiwezekana hata mimi pesa zangu za semina zote zinazohusu semina za nje nikatwe kwa miaka mitano lakini zikaingiziwe huko Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine la mambo ya Muungano, Muungamo tuko nao tunaupenda na uko mzuri lakini ningependa kumuuliza Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Makamu wa Pili kwamba sisi Wawakilishi tukifika Dar- es Salaam tuna *status* gani kwa sababu tunachukuliwa tu kama madiwani. Mhe. Mwenyekiti, ...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-wardy: Mhe. Mwenyekiti, naomba dakika tano za nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, Wawakilishi tunapofika Dar- es Salaam tunachukuliwa nafasi zetu .....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia, dakika tano sio makubaliano yetu. Umepewa dakika 15 umebakisha dakika .

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-wardy: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, juu ya yote niliyozungumza naunga mkono hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nampongeza sana Mhe. Makamu wa pili wa Rais kwa hotuba yake nzuri aliyoisilisha hapa. Na mimi naomba kuchangia hotuba hiyo naanzia sekta ya afya.

Mhe. Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuboresha huduma za afya kujenga vituo vingi sehemu za vijijini na kujenga nyumba hizi za madaktri katika kila kituo cha afya kilichopo vijijini.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo kubwa katika vituo vya afya ambavyo vimejengwa. Huduma za afya bila ya kuweka daktari kwa kweli inakuwa bado haijawa huduma sahihi na vituo vyetu hivi vya afya vina upungufu mkubwa wa madaktari na hata hawa wahudumu wa afya za mama na watoto.

Kwa kweli tunaiomba serikali ichukuwe juhudi za makusudi kuweza kuleta wafanyakazi katika hivi vituo vya afya ukizingatia nyumba zipo. Kwa hivyo, madaktari hawa wanaweza kukaa pale na kuweza kutoa huduma kwa

wananchi. Kwa sababu vituo vingi vya shamba aidha ndani ya jimbo langu huduma zinatolewa mpaka saa 9:30. Ikifika usiku mngonjwa yoyote inabidi asafirishwe aletwe Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, hili tatizo limekuwa ni kubwa tunaiomba serikali ijitahidi kuajiri wafanyakazi waweze kukaa pale pale karibu na kituo cha afya kuwapatia wananchi huduma.

Aidha Mhe. Mwenyekiti, hawa madaktari wengine ambao wapo ndani ya vituo vya afya wanakaa mbali na wanashindwa kukaa pale anafika mtu saa nne hajafika kwenye kituo cha afya. Akifika pale unamkuta mama kafika toka saa moja na nusu asubuhi au saa moja kamili anasubiri huduma za afya. Lakini daktari yule akifika saa nne pale anaweza kuwaambia kina mama nitawahudumia nusu waliobakia waende zao na siku ya pili, wanaweza kuja daktari yule hayupo. Naiomba serikali hawa watu wetu wa afya ambao wameajiriwa basi wakumbushwe wajibu wao na wajue kwamba pale wamekwenda kwa shughuli gani.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la elimu pia naipongeza serikali kwa kujenga skuli nyingi katika vijiji vyetu. Lakini skuli hizi nazo ukizingapia nazo pia zina upungufu wa walimu. Hili linatokana na wakati wa uajiri wa walimu zinapotangazwa ajira hususani zikiambia ajira hizi zinakwenda mashamba wale wanaokwenda kuomba ajira kila mmoja atakwambia mimi naishi Mahonda, mimi naishi Bumbwini, mimi Mangapwani sababu anafata apate ajira.

Wale wazaliwa waliopo katika maeneo yale wakati na wao wana uwezo wa kufanya kazi ile wanaachwa hawaajiriwi wanachukuliwa wengine ambao wako mbali, hatimae haufiki hata mwezi wale wote wanaomba uhamisho unalipelekea lile suala la walimu kubakia tatizo liko pale pale, kila siku skuli hizi zinakosa walimu. Kwa hiyo, naiomba serikali wakati wa kuajiri basi izingatie sana wale ambao wanatoka ndani ya maeneo husika.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala hili la walimu ambao walikuwa wanasoma Elimu Masafa. Walimu hawa wanaosoma Elimu Masafa walikosa sifa ya kuingia kwenye Vyuo vyetu vya Ualimu wanasoma pale kwa kupata cheti cha ualimu. Kuna walimu takrbani wamemaliza karibu miaka mitatu iliyopita baadhi yao wameweza kupatiwa nyongeza zao za mishahara. Lakini baadhi yao mpaka hivi sasa nyongeza zao bado hawajapata na wameshamaliza masomo yale. Naiomba serikali hawa ambao bado hawajapatiwa stahiki zao na wao washuhulikiwe ili waweze kupata stahiki yao hii wanayohusika.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye suala la Mtaala wa Elimu. Kwa kweli Mtaala wa Elimu uliobadilishwa sasa umekuwa una masomo mengi sana kwa

wanafunzi wetu wa msingi, ukiangalia mwanafunzi wa darasa la kwanza hadi darasa la nne anasomeshwa masomo manane na ukimuangalia mtoto yule ni mdogo na uwezo wake pia ni mdogo. Kwa hivyo, hapa tunaweza kupata matatizo watoto hawa wanapunguza ufahamu wao. Lakini pia watoto hawa wanakuwa wanapunguza hata ile hamu ya kujifunza.

Kwa hivyo, tukiangalia lile lengo hasa la kupata wanafunzi bora na wanafunzi wenye ubunifu linapungua kwa sababu haya masomo mengi sana. Kwa hivyo, naiomba serikali ikae chini pamoja na Wizara ya Elimu iangalie kwa kina masomo haya wanayopelekewa hawa wanafunzi wetu ambao ni wadogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la umeme. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika hotuba yake lilizungumziwa suala la umeme vijijini kwamba maeneo yote ya vijijini limeenea suala hili la umeme. Lakini ndani ya Jimbo langu kuna kijiji kinaitwa Panga tupu, kijiji hiki kiko mbali sana na eneo la Bumbwini ingawake kimo ndani ya jimbo langu la Bumbwini. Hiki kijiji kwa kweli mahitaji mengi muhimu kimekosa ukiangalia umeme hakuna, hakuna huduma afya wala hakuna maji. Kwa kweli naomba serikali itizame kwa jicho la huruma kijiji hichi na ikiwezekana tushirikiane waweze kupatiwa umeme kijiji hiki ili na wao waweze kunufaika na huduma hizi zinazopatikana.

Mhe. Mwenyekiti, tukija kwenye suala la maji, ukizingatia sasa hivi tunakaribia na mwezi mtukufu wa Ramadhani katika eneo langu lina upungufu mkubwa wa maji, naiomba Wizara ya Maji kuna visima ambavyo vimechimbwa na Ras-el-kheima ambavyo bado havijaanza kutumika nawaomba tushirikiane tukiimarishe japo kisima kimoja kiweze kufanya kazi ili wananchi hawa waondokane na usumbufu wa maji kwa mwezi mtukufu huu wa Ramadhani.

Ukizingatia kina mama hawa ndio waathirika wakubwa wa suala hili wanasumbuka sana kutafuta maji na yale maeneo ambayo yana visima yanatoka, lakini maji yenyewe ya mgao inabidi mama huyu atoke usiku ende akatafute maji, kutwa ahangaike na shughuli nyengine jioni ashuhulike na masuala la maji. Kwa hivyo, naiomba serikali, naiomba wizara tushirikiane ili tuweze kukifunga kisima hichi kimoja katika visima viwili ambavyo vimechimbwa na Rasilhema kiweze kusambaza maji ndani ya jimbo langu la Bumbwini kuwaondoshea wananchi hawa usumbufu mkubwa wa maji.

Mwisho nawashukuru sana wananchi wangu wote wa jimbo la Bumbwini kwa kuweza kunipatia nafasi hii nikaweza kuwa Mwakilishi na nikaweza kuwasilisha yale mambo ambayo wanaweza kunituma. Nami naungana na wenzangu kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii asubuhi hii ya leo. Naomba moja kwa moja niende kwenye mada na mada yenyewe ni kujadili Afisi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Naomba kwa dhati kabisa tumpongeze yeye mwenyewe kwa hotuba nzuri yenye takwimu nyingi, utendaji mwingi na inaonesha kielelezo tosha ya utendaji wake kwa serikali yetu hii. Nampa pongezi sana yeye mwenyewe pamoja na timu yake nzima.

Mhe. Mwenyekiti, Afisi imefanya mengi katika kipindi kilichopita hasa katika suala zima la kuratibu shughuli za serikali na kama alivyosema Mhe. Makamu wa Pili kwenye hotuba yake kwamba ukurasa wa 23. Azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa awamu ya saba ni kutoa huduma bora za serikali kwa jamii.

Hili ni suala la msingi sana na ndio lengo letu na Afisi hii ndio inayoratibu na ili maana ya ratibu iwe kweli maana ya kuratibu shuhuli zote za Serikali hili ni suala la msingi sana na nimeona masuala yanayoratibiwa siyo kama yote inayopaswa iwe serikali hasa. Kwenye hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Programu C012 kumetajatwa mambo kama matano ambayo wanaratibu, maafa, sherehe za maadhimisho ya kitaifa, shughuli za SMZ na SMT, shuhuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dae-es Salaam na usimamizi wa masuala ya watu wenye ulemavu. Hiyo ndiyo inayoitwa kuratibu kwa shughuli za serikali.

Kwa muono wangu Mhe. Mwenyekiti, nafikiri iko haja tuende zaidi ya hapo kama ni Afisi ya Mhe. Makamu wa Pili ndio mtendaji wetu Mkuu tunatarajia yeye kweli asimamie wizara zote ipasavyo, kwa nini nikasema hiyo Mhe. Mwenyekiti. Mimi ningeshauri wenzetu Bara kule wanayo Afisi ya Waziri Mkuu na Waziri Mkuu ndiye mtendaji mkuu wa serikali. Kwa hiyo, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Afisi yake ingekuwa na vitengo kama vya kuanzia kama alivyosema kwenye ukurasa wa 3,4 kusimamia masuala ya afya, maji, masuala ya Kilimo, masuala ya Elimu. Haya ni masuala ya msingi sana yanahitaji uratibu wa karibu zaidi.

Mhe. Makamu wa Pili namshukuru anafanya ziara nyingi anatembelea. Lakini iwe *order of the day* Afisini kwake tuwe na maofisi ambao wana *senior officer* wanao-*coordinate* wanaoratibiana na hizi wizara zenyewe kusimamia wizara, kwa kuanzia tumesema hizi nne.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nikasema hivyo, mimi ni mdau na mdau wenyewe sasa nimekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu na Afya kwa muda mfupi tu tumeona kweli kuna mambo Mhe. Mwenyekiti, yanataka majibu lakini hayajibiki, unaiuliza wizara yenyewe wanashindwa kujibu kwanini mmelipeleka serikalini hili aah tumelipeleka lakini hatujajibiwa mmekwenda Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Sasa ndio pale *point* yangu nasisitiza kwamba kweli lazima tusimwachie Mhe. Rais, Mhe. Rais ana mpango wa Bango la Tita lakini ni mkubwa sana wizara zote, lakini uafatiliaji upo chini hiku ndio muhimu sana. Nitatoa mfano Wizara ya Elimu wameomba kuajiri wanafanyakazi 900 mwaka jana waalimu 900 wameruhusiwa walimu 90 tu mwaka jana *gape* hiyo iko wapi na wapi. Sasa kweli tunataka kweli ki-*improve* elimu *gape* hilo la elimu tuta-*improve* kweli elimu hiyo Mhe. Mwenyekiti.

Sasa hili tumeuliza toka mwaka jana wamesema wamelileta serikalini ndio wakapata 90 mwaka huu halimo kabisa. Sasa walimu hawa wengine wamesha-g*raduate* na digirii zao watabaki hapa kweli tuta-*improve* elimu kweli.

Sababu ndio pale niliposema tumuombe Mheshimiwa aratibu kweli haya masuala yote yaratibiwe ipasavyo ndani ya afisi yake Mhe. Mwenyekiti hayo machache lakini ukienda kwa afya nazungumzie hizo wizara mbili nilizoziona tu na nimetoa mfano humu kuna walimu wa Sayansi mimi baadae nitampa Mhe. Waziri *list* nzima walonipa Wizara ya Elimu.

Kuna walimu wa Sanyansi humu wanataka walimu wa Sayansi 300 hawakupewa wana wataalamu wa *IT* wameshasoma na Digirii zao watabaki kweli hawa Bara huko wameshafungua milango wanasema keshokutwa Julai wanaajiri waalimu thalathini na tano elfu watakwenda zao wote hawa na tumewasomesha kwa pesa zetu.

Sasa mimi naomba sana Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais yupo mimi nitakupa hii *list* tuitizame kwa jicho la huruma. Hatukati tuna *review* sasa hivi suala zima la ajira, lakini suala la walimu tulitizameni kwa jicho la huruma, Kwa kweli tunataka ku-*invest* kwenye elimu wanafunzi wetu wafundishwe ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda haraka harakwa kwa sababu umetupa muda mdogo sana. Kwenye matapo naomba nizungumzie kidogo, maana nisije nikasahau Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hotuba hii asilimia mia juu ya mia. Haya tunayoyazungumza tunajaribu ku-*improve* kuendeleza hotuba hii na utendaji wetu uonekane mzuri na makosa madogo madogo, tuliyoyabaini kwenye mabuku yarekebishwe isiwe sote tumeyaona tunayaacha hivyo hivyo.

Ukienda kwenye ukurasa wa hili buku kubwa C18 muhutasari wa mapato kikasma ukiangalia C18 ile jumla ilioko pale ukilinganisha na kitabu alichosoma Mhe. Makamu wa Pili kwenye ukurasa wa 39 nafikiri kuna tafauti ya jumla naomba tuirekebishe kwenye buku jumla ya mapato yaliowekwa ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni milioni mia saba tisini na tatu mia saba sitini na sita elfu. Lakini ukiangalia kitabu ni milioni mia nane na sita mia moja ishirini na sita elfu hiyo ndio *total*. Sasa nafikiri kuna matatizo katika kujumla pale hilo naomba kidogo tuliweke sawa.

Jengine hapo hapo Mhe. Mwenyekiti katika mapato Afisi hii ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali mwaka 2014/2016 walikisia kuchangia laki sita, mwaka 2015/2016 walichangia tena laki sita mwaka ule wa 2014/2015 laki sita walikusanya laki mbili mia mbili tisini na tano milioni sawa sawa na asilimia 49%. Mwaka 2015/2016 katika hizo milioni mia sita walizoweka lengo walikusanya mia mbili sabini na tano milioni, sawa sawa na arobaini na saba. Mwaka huu 2016/2017, *target* ni milioni mia saba thamanini na moja, mia nne na sita. Ni kidogo mno. Hii *increase* Mhe. Spika, ni kidogo mno. Kwa sababu gani nikasema ni kidogo mno. Mwaka huu tayari Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ana mitambo mipya, ana jengo jipya, kila kitu kizuri na alhmdulillahi vitabu vyetu vya bajeti vyote vinachapa huko. Kwa hivyo ninafikiri hili pengo, hii *target* muliyoweka safari hii ni ndogo mno. Matokeo yake atakuja kutwambia hapa kwamba kapindukia lengo. Hebu tuone kidogo tumuongeze, tutafute *independent* mtu *surveyor* au kuweka yale malengo mazuri tuone *performance* yake inavyopaswa.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia hili buku kwa jumla. Ile ninafikiri siyo Ofisi halipo kwenye ofisi hii tu lakini ni ofisi nyingi. Ukiangalia hili buku kwa ujumla katika utendaji wote kasma za bajeti zile kwa mwaka 2015/2016, utakuta muna maziro tu yote. Mfano *page C23* hali halisi kwa 2014/2015 wacha mbali sana huko, lakini makisio kwa mwaka 2015/2016 muna maziro moja kwa moja.

Sasa mimi ninajiuliza Mhe. Mwenyekiti, kama maziro, yaani pesa hazikutiwa au hazikukisiwa. Lakini kitabu cha bajeti ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais

ninamshukuru sana, kwenye kitabu chake cha bajeti ukiangalia jadweli liliopo kwenye ukurasa wa 41. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kiambatanisho Nam. 1 kaelezea matumizi ya kazi za kawaida kwa kipindi cha Julai hadi Machi mwaka 2015/2016. Katoa *breakdown* yote na *percentage* ya asilimia ya pesa alizopewa na alizotumia. Ninamshukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais lakini kwenye buku kwa nini halioneshi kama hivi.

Hapa ina maana kama ni ziro tu mote. Ina maana pesa hazikutiwa. *Zero is a figure statistical.* Sasa ukiweka ziro ina maana hapakutiwa kitu hapa. Hili kosa lirekebisheni. Huku kitabu kinaonesha mapesa yaliyotiwa na yaliyotumiwa. Lakini kwenye buku muna maziro tu. Hiyo Mhe. Mwenyekiti, inamaanisha pia hata sisi tutakapokuwa tuna-*compare* na *contrast* matumizi na pesa iliyotiwa na yale majukumu yaliyowekwa. Hapa hatuioni.

Sasa hili tatizo, ndiyo pale ninaposema suala la uratibu, hili liliratibiwa vizuri kati ya Ofisi yako ya Baraza, Wizara ya Fedha na watu wa bajeti. Ninafikiri tuna tatizo. Utatueleza ilikuwaje. Haya maziro yote lakini pesa imetiwa na imetumiwa na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kiasi kikubwa haikuwa na *changes* kubwa, wameongezewa tu baadhi ya vitengo. Mhe. Mwenyekiti, ninakwenda haraka haraka kwa sababu muda uliotupa ni mdogo.

Jengine ambalo naona nimalizie...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa umebakiwa na dakika moja.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Mwadini Makame: Ninakushukuru sana. Mengine nitaweka kimaandishi.

Naomba niende kwenye Tume ya Ukimwi. Kuna kada moja pale, kuna Katibu wa Sheha kwenye AC nambari ngapi, nitatoa kwenye maandishi. Lakini Katibu wa Sheha kwenye Tume ya Ukimwi kada hiyo inahusu nini.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema nina mengi lakini tunaomba sana, hii ni roho ya serikali. Makamu wa Pili wa Rais ni roho ya serikali siku moja kuijadili Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii haitoshi. Hivyo naomba kiti chako ulifikirie tena uamuzi huo. Kilillahi tuwe tunaichangia hii Ofisi tulete msisimko na tulete hasa utendaji.(*Makofi*)

Kuna suala la *ICC*, tunashitakiwa huko. Jee, serikali kweli *CUF* watushitaki kwenye *ICC*. Sisi tunayo mengi ya kuwashitaki wao kuliko sisi. Serikali itolee maamuzi suala hili. Itoe kauli tuisikie. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwinyihaji Mwadini Makame. Anayefuata Mhe. Bahati Khamis Kombo na mwengine ni Mhe. Miraji Khamis Mussa akifuatiwa na Mhe. Zaina Abdalla Salum.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi fursa hii asubuhi ya leo nikaweza kuchangia Hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Kwanza kabisa nichukue fursa hii Mhe. Mwenyekiti, ya kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kwako na leo hii ikawa upo mbele yetu kuliongoza Baraza letu Tukufu. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Makamu wa Pili wa Rais alioupata kwa Mhe. Rais wa Zanzibar kuona kwamba Mhe. Balozi Seif Ali Iddi ni mchapa kazi mzuri na anayeweza kuiongoza Zanzibar wakishirikiana kwa pamoja. (*Makofi*)

Pia niwapongeze sana Mawaziri wote, Wawakilishi wote waliochaguliwa na wale ambao walioteuliwa. Nimpongeze sana mume wangu pamoja na watoto wangu kwa kuniamini na kunikubali vizuri kwamba mimi nitaweza kusimamia kutekeleza wajibu wangu wa Jimbo langu la Chambani. Ninawashukuru wanachama wote wa Jimbo la Chambani kwa kuniamini kwamba nitaweza kuzitatua changamoto ambazo tunazo kwenye jimbo letu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika mada. Mimi nitakwenda sana katika huduma za jamii kwenye ukurasa wa tano nambari kumi na tano. Mhe.Mwenyekiti, nitakwenda kwanza kwenye suala la elimu. Elimu ndiyo manufaa yetu ya Watanzania. Lakini Mhe. Mwenyekiti, inaonekana kwamba tunajenga skuli nyingi lakini walimu ni kidogo. Ninaiomba Wizara ishirikiane na wazee pamoja na Masheha wetu kuwaona wale walimu ambao hawajaajiriwa wapeleke taarifa zao ili na wao kusaidiwa ajira kwa kutatua yale matatizo yaliomo kwenye zile skuli zetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia niseme kwamba watoto wetu sasa hivi hususan Pemba wanakosa kufaulu kwa kiwango kikubwa kutokana na kutokuwa na mashirikiano baina ya walimu, wanafunzi pamoja na wazee. Wanafunzi wengi wanakosa nidhamu skulini. Wakielekezwa na walimu wao tayari wanakwenda nyumbani kusema maneno yasiyostahiki na wazee wanakwenda kwa walimu kutoa maneno kwa walimu. Hili ni moja wapo ambalo kuwa linawarudisha nyuma walimu kutokuwa na mashirikiano mazuri baina yao na wazee.

Ninaiomba serikali ikae pamoja na wazee, walimu na wanafunzi ili wapate maelekezo mazuri kwa kuweza watoto wetu kufaulu kwa kiwango kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende suala la maji. Mhe. Mwenyekiti, tayari miji yetu imetanuka kwa kiwango kikubwa. Lakini baadhi ya Shehia bado maji hayajafikiwa. Kipindi hichi tunachokwenda na mwezi Mtukufu wa Ramadhani, wananchi wanahitaji kusaidiwa sana kuondosha tatizo la maji. Kwa hivyo ninaiomba sana serikali ijipange vizuri kuondosha tatizo hili hususan kwa mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani.

Pia niiombe Wizara inapopelekewa huduma hizi za maji tunafanya kazi kwa mazoea. Wafanyakazi wengi sasa hivi wamekuwa ni wivu hawataki kufanyakazi inavyopaswa. Pengine mimi nina tatizo katika Shehia yangu, atapelekwa mtu wa maji kuja pale kuliangalia tatizo lile. Basi ataliangalia kwa anavyotaka yeye, litachukua muda miezi mitatu au miezi sita tatizo lile bado halijatatuliwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana sisi wanawake ndiyo tunaopata taabu kwa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la umeme. Watu wa umeme ninawaomba sana wanapotupitia majumbani kutaka kujua huduma hizi za umeme, wengine tayari tunakuwa hatupo nyumbani na watoto hawajui kama mama kalipia umeme au mama hakulipia umeme. Tunajua kwamba zile namba zilizokuwepo pale ndizo zinazofuatwa lakini baadhi yao wanakiuka taratibu. Na wanakuja usiku majumbani mwetu kuangalia kama kweli huu umeme upo vipi. Mhe. Mwenyekiti, ninaiomba Wizara husika iwaangalie vizuri wafanyakazi hawa ambao wanakiuka taratibu majumbani.

Pia Mhe. Mwenyekiti, niende katika suala la afya. Tuna vituo vya afya lakini wafanyakazi wa afya ni kidogo. Tukiangalia kwenye Hospitali yetu iliopo Mkoani ya Abdalla Mzee, ile hospitali ila huduma wengi sana. Lakini tatizo liliopo pale ni kutokuwepo wafanyakazi wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, daktari mmoja anaweza kuhudumia wagonjwa ishirini waliojipanga foleni, waliopo nyuma huku foleni kama yule daktari ana majukumu mazito. Wanaanza kutoa lugha chafu ndani ya serikali. Ninaomba Mhe. Mwenyekiti, madaktari waongeze na kuona kwamba lile tatizo liliopo pale la Hospitali ya Abdalla Mzee linaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hospitali yangu iliopo katika Shehia ya Ukutini. Ile hospitali ni kubwa lakini wafanyakazi ni kidogo. Kwenye nyumba za afya, pale Ukutini nyumba za afya tunazo lakini kwenye Shehia iliopo Chambani

pale hospitali na ile hospitali inawahudumia akina mama wakati wote. Hapana daktari ambaye anabakia pale kwa sababu hapana jengo la hospitali. Kwa hivyo, ninaomba tujengewe lile jengo pale, ili daktari aweze kuhudumia mama waja wazito pamoja na matatizo mbali mbali yaliopo kwenye sehemu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na ninaiunga mkono hii asilimia mia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Bahati na sasa Mhe. Miraji Khamis Mussa kama yupo. Mhe. Miraji naona hayupo tuendelee Mhe. Zaina Abdalla akifuatiwa na Mhe. Suleiman Makame Ali na ajitayarishe Mhe. Rashid Makame.

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kufika hapa tukiwa na wazima na salama.

Pili Mhe. Mwenyekiti, ninapenda nichukue fursa hii adhimu kwa hii leo kunipatia fursa hii ambayo ndiyo mara yangu ya mwanzo ili niweze kuchangia Hotuba hii ya Makamu wa Pili wa Rais. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, naomba samahani nipe dakika tatu na mimi niweze kutoa pongezi kwa viongozi wetu ili na mimi niungane na wenzangu.

Kwanza kabisa ninapenda kutoa pongezi kwa Mhe. Rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ushindi wake mkubwa ambao alioupata katika uchaguzi wa tarehe 20 Machi, 2015.

Pili ninapenda kumpongeza Mhe. Balozi wetu Makamu wa Pili wa Rais kwa kupata uteuzi wake huo pamoja na Mawaziri wake ambao waliokwisha kuteuliwa pamoja na Manaibu. Vile vile ninapenda kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa ushindi wake mkubwa alioupata. (*Makofi*)

Vile vile pongezi hizi ninapenda ziwafikie Wawakilishi wenzangu wote wa majimbo pamoja na viti maalum ambao waliokwisha kuteuliwa. Pongezi hizi pia zimfikie Spika wa Baraza letu la Wawakilishi kwa uteuzi wake ambao alioupata ushindi mkubwa pamoja na Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Pia ninapenda tena pongezi hizi ziwafikie wale wote ambao walioniwezesha mimi kufika hapa nikiwa ni miongoni mwa wanawake wenzangu wa Mkoa wa

Mjini/Magharibi, pamoja na Baraza Kuu kunichagua mimi kufika hapa. Pongezi hizi za mwisho ziwafikie wanafamilia yangu wakiwemo watoto wangu na mume wangu na mama yangu ambao walikuwa wakinisaidia kwa kila hali. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninataka nielekee katika mchango wa kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais. Mimi nina machache nitakayochangia kutokana na muda hautoshi na Wajumbe wanatakiwa ni kumi na tano.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu nilikuwa ninaanza kwa kukatisha tu katika Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi tumeona Tume hii, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ofisi yake ilisomesha wafanyakazi wawili ambao wafanyakazi hao walitumia fedha nyingi za kuwasomesha ili waweze kuwezesha vizuri kazi na wale ambao waliopatiwa mafunzo. Lakini hatimaye yake imekuwa katika uchaguzi kuwa serikali imeingia gharama kubwa au hasara kubwa kwa kusababishwa na wao wenyewe miongoni mwao. Kwani miongoni mwao wafanyakazi hawa walikuwa wame-*base* sana katika vyama.

Kwa hivyo wananchi wengi wana imani nao, wanataka wasikie kwamba kumetolewa uamuzi ambao wa kutoa fidia katika serikali yao. Hivyo wanaona serikali ipo kimya mpaka sasa hivi haujatoka uamuzi wowote kuhusiana na watu hao. (*Makofi*)

Pia ninapenda nichangie katika sehemu ya rushwa. Suala la rushwa Mhe. Makamu kasema kwamba yeye ataiundia mamlaka. Lakini mamlaka haya kabla haijaundwa, hebu tungepata kigezo cha Rais wa Jamhuri ya Muungano. Kwani Rais wa Jamhuri ya Muungano baada ya kuapishwa tu, ninahisi kama sikosei ni siku kumi tu akawa kishasafisha Wizara zote na Ofisi zote.

Kwa hivyo unaweza kuiundia mamlaka wakati kitu ambacho kuna uchafu ndani yake. Sasa kile unachokiunda je, utakiamini vipi. Ilikuwa kwanza wajibu wa serikali iingie kwanza isafishe ndani ya Ofisi ya Kiserikali ili kuhakikisha kuwa inakuwa safi, halafu ndipo inapoundwa mamlaka. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, vile vile mchango wangu unahusiana sana na watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu hivi sasa bado wapo chini. Tukiangalia tatizo sijui nini. Lakini mimi Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Makamu kasema kwamba kwa jamii kuipa elimu. Lakini naona jamii mpaka sasa hivi ishakuwa kidogo kuna baadhi imeshapata uelewa.

Pia serikali hapa imesema kuwa itapitia tena Sheria Nam. 9 ya 2006 ya kupata haki na fursa. Kwa maana hiyo hapa inaonesha kuwa serikali bado haijaweza kutambua vizuri suala la watu wenye ulemavu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nikisema jamii kuwa inauelewa kwa watu wenye ulemavu. Kwa maana hiyo inakuwa baba kazaa mtoto wake na mama, lakini baba yule anachukua juhudi ya kumsomesha mtoto wao yule, anapofikia miaka saba anampeleka skuli anamsomesha mpaka kidato cha tano au cha sita na kutoa fedha nyengine kugharamia kwamba kufika mtoto yule anapata masomo ya juu. Hatimae serikali inapokwenda kuomba ajira inakuwa ajira ile haipati. (*Makofi*)

Kwa hivyo hapa tatizo ni jamii au tatizo ni serikali. Hivyo tunaiomba serikali iwapatie ajira vijana. Kwa kweli Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ikiwa kama utakubaliana na mimi tufanye ziara katika Chama cha Watu Ulemavu. Chama hiki kina jumuiya nyingi. Kina Jumuiya za Viziwi, kuna hawa albino, kuna watu wasioona lakini kuna vijana wengi sana wana elimu za juu. Lakini hawana ajira.

Wamepata mafunzo ya ujasiria mali. Hawana miradi, hawana fedha za kuanzishia miradi, hawana maeneo ya kufanyia miradi, hawana masoko kwa wale wanaojishughulisha na miradi hawana. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba sana suala hili lizingatiwe. Na ikiwemo kuzingatiwa kuzingatiwa suala la ajira, watu hawa wapunguziwe masharti makali katika *interview*. Kwa sababu *interview* inakuwa inawafanya wale watu wanakosa ajira kutokana na ukali wa *interview*.

Mhe. Mwenyekiti, utakuta zinatoka nafasi za kusema kuwa wanataka kuajiriwa na walemavu wawili au watatu. Basi walemavu wale wanatoka na viongozi wao, wakishafika pale, kunatokea kiongozi fulani au anawapita, hata akishauliza vipi. Anawaambia nyinyi walemavu hamuwezi kuajiriwa nendeni zenuni musipoteze muda wenu. Sasa hii hali kidogo inavunja moyo kwa watu walemavu na serikali yao.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo naomba sana Mhe.Makamu wa Pili wa Rais uipitie hii na upunguze masharti, ili tuone kwamba walemavu wanaweza kupata ajira na fursa sawa kama wengine. Kwa maana hiyo wale wote ambao wanaoshughulikia na masuala ya ajira, wanapotoa tangazo la kuwa watu wanataka kuajiriwa basi ahakikishe kwamba anapata maelezo ya kujua kwamba kuna vijana wangapi waliokuja wenye ulemavu na wana ulemavu wa kiasi gani, kwa sababu unaweza kumuona mtu anatembea lakini kumbe

usikivu wake ni mdogo au pengine uonevu wake wa macho ni mdogo, kwa maana hiyo ni lazima ujuwe kwamba huyu ni mlemavu wa kiasi gani, ikiwezekana kama ni mlemavu asiyesikia madhali ana uwezo na ana Stashahada ile ambayo inatakiwa na ana fani ile inayotakiwa, basi apewe fomu yake na vizuri usaili wake ufanywe kwa fomu apewe ajaza ile *interview* yake.

Yule ambaye hawezi kutembea na pengine hana kisaidizi basi asaidiwe asishughulishwe kwenda huku na kule hatima yake ili mumchoshe na avunjike moyo, basi asaidiwe, achukuliwe na kama ni interview asogezwe pale au isogee pale, ili na yeye aweze kufanya, kwa sababu uwezo wa kufanyakazi anao, nia anayo na moyo anao wa kufanyakazi katika serikali yake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia tu, mimi naomba kama ni ushauri kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tuone sisi walemavu tuundiwe sera au sheria ya shirikisho ili tuweze kushirikishwa vizuri katika vyombo vyote vya serikali.

Kwa mfano, kama vile hata kuwa Mkuu wa Wilaya ni mlemavu, basi Afisa Tawala awe ni mzima wa kuweza kumsaidia, maana atakuwa na uwezo wa kufanya kazi ile na elimu ile anayo. Kwa hivyo, mimi kwa mchango wangu huu, naungana na wenzangu wote kwamba naiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, napenda kumpongeza tena Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa hotuba yake nzuri ambayo imepangika vizuri sana, imejadili mambo mengi na imezungumzia mambo mengi kwa ufanisi mzuri. Kwa hivyo, namuombea dua Mwenyezi Mungu amjaalie aweze kufanikisha haya yote ambayo amekwishayapanga. Nakushukuru sana ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Rashidi Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ya kuichangia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Kabla ya kutoa michango yangu nichukuwe fursa hii kumpongeza mwenyewe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa hotuba nzuri iliyopangika na iliyosheheni mambo mengi.

Vile vile niipongeze ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati yenye kuhusiana na hilo, kwa mambo mengi ambayo umeyaweka kwa uwazi. Niwashukuru na niwapongeze wachangiaji waliotangulia. Pia nitowe pole kwa wananchi wote ambao katika mvua zilizopita walipatwa na maafa ya mafuriko. Mwenyezi Mungu awape kila la heri katika maisha yao mapya na Mwenyezi Mungu vile

vile aendelee kuipa uwezo serikali yetu, ili kuweza kupunguza matatizo haya ya majanga ya kila muda.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye michango yangu katika kuifanya hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili iwe bora zaidi. Suala la kwanza ambalo ningependa kulichangia mbalo lipo katika programu ya pili, ukurasa wa 23 uratibu wa shughuli za serikali. Mhe. Mwenyekiti, katika programu hii ina vifungu vitano, lakini mimi kwa uoni wangu imekosa kifungu kimoja muhimu sana kinachohusu uratibu wa utekelezaji wa mfuko wa maendeleo ya jimbo. Mfuko wa Maendeleo wa jimbo Mhe. Mwenyekiti ni moja kati ya kazi ambazo zinapaswa kuwa endelevu mwaka hadi mwaka, lakini la kushangaza kifungu hiki hakimo.

Suala la Mfuko wa Jimbo limeripotiwa katika kitabu hiki cha Mkaguzi na Mdhibiti lina matatizo mengi, likiwemo Mwenyekiti kutokufahamiana na wajumbe, lakini kukosekana vile vile kwa vitabu vya hesabu na mambo mbali mbali. Sasa tunapoiona hotuba hii haina kifungu hiki ni jambo la kushangaza kidogo. Lakini vile vile sisi wajumbe tunalazimika kupata semina juu ya mfuko huu na vile vile kamati zetu ambazo tumeziunda, ili kuona kwamba pesa za wananchi zinatumika ipasavyo. Kwa hivyo, ningeishauri sana Ofisi ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kuweza kukiona kifungu hiki katika programu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika suala la uratibu wa shughuli za Makamu wa Pili wa Rais, programu ya kwanza ukurasa wa 23, kifungu (e) kinahusiana na kuratibu na kutekeleza ahadi zinazolenga kuleta maendeleo katika jamii. Imeelezwa kuwa katika ukurasa huo huo kwamba kuna ahadi 10 ambazo zimetekelezwa katika kipindi kilichopita, ningependa kufahamu ahadi hizi 10 ziliahidiwa mwaka gani, ili tuweze kuona kwamba kitengo kinachohusika na uratibu kwamba kinatenda haki katika utekelezaji wa ahadi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, ahadi ni deni, ingawa kule kwetu Makunduchi kulikuwa kuna gari moja ilikuwa imeandikwa kuagana sio jambo, kwa Kimakunduchi inasema 'kulagana si jambo'. Sasa ahadi ni deni, na mimi namuelewa sana Mhe. Makamu wa Pili kwa utekelezaji wa ahadi mbali mbali, kwa sababu ahadi hizi ambazo anazitekeleza anaamini kwamba zinasukuma maendeleo katika jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kidogo nina utata katika hili. Katika mwaka 2012 Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aliahidi taasisi moja katika jimbo langu, na taasisi hii ina mchango mkubwa sana katika kuleta maendeleo ya nchi hii, hususan katika suala la ajira. Lakini la kushangaza mpaka mwaka huu watendaji wangu wamekwenda na kurudi katika kufuatilia ahadi hiyo, lakini mpaka mwaka huu

ahadi hiyo haijatekelezwa, ukizingatia kwamba taasisi hii ina mchango mkubwa kwa serikali na hata katika jimbo lake taasisi hii ilipeleka msukumo katika masuala hayo. Ningependa sana kuona kitengo kinachohusiana na ahadi, basi kinaratibu vizuri na kusimamia ahadi zake, ili wasije wakamfanya mheshimiwa wetu kuonekana msanii katika masuala ya ahadi.

Mhe. Mwenyekiti, nije sasa katika programu inayohusiana na madawa au udhibiti wa madawa ya kulevya. Katika hotuba yetu hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kifungu cha 3 pamoja na wadau wengine, imeandaa miongozo ya kuzawadia watoa taarifa kuhusu uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya. Mhe. Mwenyekiti, suala hili ni zuri sana na mimi nalipongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba suala la madawa ya kulevya ni suala pana na lina mitandao madhubuti sana. Mitandao hii ni karibu ya serikali, niiombe tu katika uratibu wa masuala haya ya kutoa zawadi, basi kuweza kuona kwamba wale ambao watajitokeza katika kutoa yale yanayohusiana na wale wahusika wakuu katika usambazaji na uletaji, basi wanatunziwa siri zao. Lakini vyenginevyo, inawezekana vichwa vyao vikawa halali ya hawa matajiri wakubwa au vigogo wa madawa ya kulevya.

Mhe. Mwenyekiti, suala la madawa ya kulevya nchini ni kubwa na linaendelea siku hadi siku, majimbo yetu mengi hivi sasa unamopita basi vijana wengi sana utawakuta wameathirika na madawa ya kulevya. Tunaamini kwamba suala la madawa ya kulevya waingizaji ni matajiri wakubwa pamoja na vigogo wengine ndani ya serikali. *(Makofi)*

Kwa hivyo, sisi wananchi tuko tayari kuweza kutoa au kuwafichua watu hawa, lakini utaratibu huu wa kutoa zawadi wahakikishe kwamba unawalinda wale wote ambao watakuwa wanawafichua watu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika suala la miradi ya *TASAF*. Hivi sasa tuko katika awamu ya tatu ya mradi wa *TASAF* ambao unahusikana na suala zima la kunusuru Kaya masikini. Niseme tu kwamba mradi huu unaendelea vizuri, lakini una mapungufu vile vile. Baadhi ya wakati utakuta kwamba Kaya amabazo zinapata misaada, ukipima katika kiwango cha umaskini, basi utaona kwamba watu hao wasingehusika katika kuweza kupata misaada hiyo inayohusiana na kunusuru Kaya masikini.

Ningeomba sana kitengo ambacho kinahusiana na mradi huu kuwa makini kwa kushirikiana na viongozi wa Serikali za Mitaa, ili kuona wale wanaohusika ndio ambao wanapata fursa hizi za kuweza kupata misaada ya aina hiyo.

Vile vile nije katika suala hilo hilo la *TASAF* kuna awamu mbili zimepita, lakini Mhe. Mwenyekiti, ni la kushangaza sana, kuna miradi mbali mbali ambayo hivi sasa kama itafanywa tathmini na ufuatiliaji, basi utaikuta miradi hiyo imekufa. Miradi iliyobakia sana ya awamu ya pili ni ile ambayo ni ya ujenzi wa mabanda ya skuli na vituo vya afya. Lakini ukienda katika miradi ambayo inahusiana na vikundi vya uzalishaji, iwe vya uzalishaji wa kilimo, mboga mboga, vya ufugaji au hata vikundi vya ufundi basi utakuta kwamba vikundi hivyo hivi sasa vimekufa.

Kwa hivyo, ningekiomba sana kitengo kinachohusiana na TASAF, kuweza kufanya suala zima la ufuatiliaji la tathmini kwa miradi ya awamu iliyopita awamu ya pili na awamu ya kwanza, kuona kwamba zile pesa ambazo zimetoka basi zimeweza kuwanufaisha wananchi, na kama miradi hiyo imekufa basi iweze kuhoji kwa nini imekufa, kwa sababu pesa nyingi zilikuwa zinatumika katika kuona kwamba tunawapunguzia wananchi wetu hususan wanyonge hali ngumu za uchumi walizonazo. Hayo ndio yalikuwa malengo ya *TASAF* zote tatu ambazo zimepita.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie sasa katika suala zima la majanga. Katika programu ya uratibu wa shughuli za serikali, CO12 2015/2016 ukurasa 11 - 13 kifungu cha 6, ofisi imeratibu na kutoa huduma katika majenga na maafa katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Niishukuru na niipongeze sana serikali yetu kwa kuweza kutekeleza mambo hayo, na ndani ya mambo hayo kwa kweli yameleta manufaa sana kwa wale wote ambao wameweza kupata majanga, naishukuru sana idara inayohusika na majanga kwa kuweza kuratibu shughuli hizi na *Alhamdulillah* hivi sasa nchi iko katika hali salama, hususan ukiangalia kwamba mvua ambazo zilipita za mwezi Aprili, hivi sasa watu wamerudi katika makazi yao ya kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mvua za vuli zinakuja, hapa nitowe indhari tu kwamba idara hii ya majanga imejiandaa vipi, kwa sababu katika mvua zilizopita mimi nilikuwa shahidi, Jimbo langu la Magomeni lina mabonde manne, lakini sikuona mtu yeyote anayehusiana na idara hii kutembelea na kuweza kufanya tathmini katika suala hili.

Vile vile kama haitoshi tarehe 17 kwenye saa 12 nilitembelea kwenye kambi ambayo ilikuwa katika Skuli ya Nyerere Sekondari, kambi ambayo nilipata taarifa kwamba imeandaliwa na Kamati ya Maafa ya Wilaya. Ningependa kupata ufafanuzi kwamba Kamati ya Maafa ya Wilaya inauhusiano gani na Idara ya Maafa katika Ofisi ya Makamu wa Pili, kwa sababu saa 12:00 nilipopita wananchi ambao wako pale basi hawajapata kula.

Hilo ni jambo la kusikitisha sana tunaposema kwamba tuna idara ambayo inashughulika na maafa. Mimi mwenyewe nilijitolea kama chakula cha mwanzo kilicholiwa katika kambi ile, basi Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni alichangia. Niwapongeze sana wawakilishi na viongozi katika majimbo mengine waliopeleka misaada pale.

Vile vile kama haitoshi, siku ya pili nilitembelea tena kambi ile kwenye saa 10:00 watu hawajala vile vile watu, naambiwa chakula kinasubiriwa kutoka jamatini au *passing show,* ni jambo la kusikitisha. Maafa Mhe. Mwenyekiti, ni kitu ambacho kinatokea bila ya kutarajia, kwa hivyo...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, malizia.

Mhe. Rashidi Makame Shamsi: Ahsante sana. Tumetegemea kwamba Kamati za Maafa za Wilaya na ile Idara ya Maafa inajiandaa vizuri ili kukabiliana na maafa hayo. Baada ya kusema hayo machache Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Vile vile niseme tu kwamba naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia, na niwapongeze sana viongozi wote waliohusika katika kuiandaa hotuba hii, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Rashidi Makame. Anayefuata Mhe. Ali Salum Kirova kama yupo. Mhe. Suleiman Sarahan Said akifuatiwa na Mhe. Masoud Abrahman Masoud. Mhe. Hamza Hassan Juma jitayarishe.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii na mimi naungana na wenzangu haraka haraka kumshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na Mtume wetu Muhammad (SAW), pia namshukuru Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein na Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi, pia mama yangu mzazi pamoja na mke wangu na wawakilishi wote, ahsanteni sana pamoja na wewe Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nianze tu kwa haraka haraka kwa sababu muda hautoshi, mimi nizungumze tu habari ya kitabu hiki nimesoma na nimeona hali halisi yote iliyoombwa humu, mimi sina wasi wasi nayo na bado tu nasemea labda mfuko hautoshi, lakini bado nasema hizi pesa ni kidogo ilikuwa ziongezwe lakini inaonekana hali halisi ndio hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niendelee na suala la majanga ya maji. Mimi niulize tu kwamba sijui serikali mpaka sasa hivi imefanya tathmini gani, maana yake Kama nasikia sijui kuna nyumba zimejengwa kwenye maeneo, kwa nini

hazivunjwi haraka haraka zikaondoka ili maafa yaliyotokea yasitokee tena. Mhe. Mwenyekiti, hili tunalisema hivyo kwa muhutasari najua kwamba hali halisi najulikana hivyo.

Pili, nasema Mhe. Mwenyekiti, kwa ofisi zetu za Pemba zote ambazo ziko Chake Chake kwa Afisa Wadhamini pamoja na ofisi zao, mheshimiwa hali zao haziridhishi. Mimi ningeshauri na wao wapewe pesa za kujikimu wanapoteuliwa, kwa sababu mheshimiwa Afisa Mdhamini anakwenda pale na kanda mbili au sijui amevaa nguo gani.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeomba sana hao Maafisa Wadhamini wanapoteuliwa wapewe pesa za kujikimu kidogo, angalau watu wakienda ofisini kwao wajuwe kama kama huyu ni Afisa Mdhamini, ana cheo karibu na Katibu Mkuu nafikiri kama sikosei. Pia ofisi ambazo wanakaa hazikidhi haja, ofisi haina kiyoyozi, feni lenyewe silo. Mimi ningeshauri sana hizo ofisi zingefanyiwa ukarabati wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni la uajiri. Mhe. Mwenyekiti, uajiri mpaka sasa hivi tunapeleka vyeti, tunawaambia tu kwamba tunataka vyeti kila mtu, lakini mheshimiwa mtu aliyesoma darasa la saba, la kumi, au la kumi na mbili mpaka kidato cha sita wanatiwa katika kundi moja, watu wote hao ni wapiga kura wetu, na kila mmoja aliyekuwa anaiweza kazi hii. Nashauri tu kwamba sasa hivi mheshimiwa wakati wa kuajiri, tunasema tunataka watu wa darasa la saba hatutaki vyeti vya *Form Four* na wale wapate ajira, hiyo hiyo ya daraza la saba hata kukata bustani wanaweza, unampeleka na cheti cha Form Four utamchukua nani, si utamchukua *Form Four*, matokeo yake anachukuliwa wa *Form Four*, *Form Six* na Chuo Kikuu anachukua mkasi kukata majani au kusafisha vyoo, baada ya wiki mbili ana-*apply* anasema yeye anataka Uafisa Mdhamini au cheo chengine, kuosha choo haoshi tena, kukata majani hakati tena, rank yake ni kubwa ya elimu.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunataka watu wa kukata majani, basi darasa la saba wapo na kama tunataka watu wa darasa la kumi wapo. Kwa hivyo, nashauri kwamba ikitolewa ajira iambiwe hii ni ya darasa la saba, tena utachagua vigezo vyengine, elimu ni moja usichanganye elimu mheshimiwa, hizi kidogo zinawauwa wale watu wa chini. Nashauri hilo likiwezekana mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia nilikuwa nasema kwamba suala la wazazi wale wanaozaa watoto wawili kwenda mbele, wale wasaidiwe na serikali, wale majukumu yao yanakua mazito, japo shilingi 50,000/- wapewe kila mwezi

wenye watoto wawili au watatu na wataongeza *speed* ya kuzaa zaidi Mhe. Mwenyekiti. Hii nafikiri itakuwa changamoto.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kuhusu *sober house*. Najua serikali iko mbioni sana kutafuta uwezekana wa kulimaliza suala hili la madawa ya kulevya, lakini imekuwa kwamba mzazi anapotaka kwenda kumpeleka mwanawe *sober house* ni lazima atowe pesa na kuna vigezo vyengine. Kwa hivyo, mimi ningeshauri tu, hizi sober house zitengenezwe ziwe kama ni za serikali na uwezo wao wa chakula, umeme kwenye majumba na kukodi, hili suala litoke serikalini ili kuwasaidia wazazi kuondokana na matatizo kama haya.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niseme kwamba Mhe. Rais amejitahidi vya kutosha kuhusu wazee. Wazee anaowakimu kwa kila mwezi wale waliokwisha kufikia umri wa miaka 70. Ningemshauri Mhe. Rais kuhusu walemavu waingizwe kwenye kundi hili, kwa sababu na wao wanakuwa na shida kweli kweli, wapate pesa za kujikimu kila mwezi ziingizwe katika mfuko huu, hili ningeshauri kama litawezekana na bajeti inayohusika.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niseme kwenye uandishi wa habari, TV yetu hii ya Zanzibar ya *ZBC* viwango vyake bado ni vidogo, tuseme ukweli lazima, ukweli bado waandishi wake bado hawajasomeshwa vya kutosha, hawajaweza hata kutembea na kompyuta juu wakaranda kwenye ile room yao, inakuwa ni ile ile *analogy* inayozunguruka. Kwa hivyo Mheshimiwa Mwenyekiti, haya maneno ya kila siku *ZBC* yaondoke tena tulete chombo cha uhakika ambacho waandishi wakasomeshwe, wapelekwe nje wapate vigezo na ofisi yao iwe na vigezo vya uhakika. Kwa hivyo hilo nashauri ikiwezekana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nashauri kwamba ofisi ya Wanawake na Watoto, hii sasa hivi ulimwengu umekua, ningeshauri sana baada ya hii ofisi ya wanawake pia ifunguliwe na ofisi ya wanaume. Wanaume nao wanadhalilishwa sasa hivi, wanapigwa na wake zao kama watoto wa shule kuliko ofisi ya wanaume ifunguliwe kwa sababu sasa hivi wanapigwa majumbani wanadhalilishwa pa kwenda hawana, wakenda polisi wanarudishwa, ndani ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais iwemo ya wanaume wanaodhalilishwa. Wanaume wamepanda chati na wao sasa hivi. Kwa hivyo ifunguliwe ofisi ya wanaume maana yake hali imekuwa mbaya, wanawake wamekuwa ma-*jutary* kweli kweli.

Pia kwenye suala la viongozi hatusemani vibaya lakini wanawake humu wanapata uongozi wanakaa na mume wake kwa sababu hana kitu akipata anatafuta sharubaro, kwa hivyo lazima amlipe Mheshimiwa lazima mali

igawiwe sio tu tukagawe kwa wanaume na wanawake vile vile wanaojifanya wababe nao mali zao zigawiwe, apewe yule mzee aliyemstahamilia miaka hiyo, hili nashauri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa pia nashauri kuhusu habari ya Magereza, Rais wetu wa mwanzo Marehemu Abeid Amani Karume wa mwanzo alisema sio magereza ni chuo cha mafunzo, mtu anakwenda kule kujifunza sasa hivi tumeingia mkondoni moja kwa moja tunajiita magereza. Kule magereza sio kama kila anayekwenda anakosa wengine bahati mbaya tu wanakwenda kule. Kwa hivyo hapa tunapiga vita unyanyasaji, tunapiga vita madawa ya kulevya, tunapiga vita UKIMWI, tunapiga kila hali huko jela nako ndiko kunakotawanywa mambo haya. Ningeshauri ikiwezekana nao wajengewe hosteli kule magereza, kwa sababu mtu anapofungwa familia yake inatawanyika kila mwezi apate akakae na mama watoto na watoto wake, akae astarehe siku nzima ile, aachiwe akae na mama watoto ili Mheshimiwa angalau yule baba akifungwa ata miaka mitano bado mumewe anamuona na bado mambo yanakwenda sawa.

Kwa hivyo ningeshauri badala ya Magereza kuwekwa kumi kumi, sawa lakini siku moja awekewe siku maalum akakae na mama watoto wake na watoto wake chumba *private* na choo chake na kila kitu na mambo yote siku hiyo yawe ya kifamilia. Ningeshauri sana Mheshimiwa suala hili likiwezekana likachukuliwa hatua kwa sababu nalo linavunja ndoa , baba akifungwa miaka mitano au kumi ndoa imekwisha familia imetawanyika, lakini kama kila mwezi atakuwa yule baba anapata mama anakuja, bado ndoa inaendelea na mambo mazuri na inshaallah atatoka salama, mambo yataendelea. Kwa hivyo ningeshauri sana Mheshimiwa likiwezekana liwe hilo. *(Makofi)*

Jengine Mheshimiwa nasema kwa Mji wangu wa Chake Chake, Mheshimiwa nataka muliangalie kwa undani sana, mji wa chake chake ni mji wa pili ni mji unaofikia viongozi wote, ni mji ambao kwa kweli ulikuwa na haiba yake. Mji huu hata sio Makamu wa Pili lakini hata Waziri katika Ofisi ya Makamu wa pili ambaye tatizo lake ni kwao tuungalie mji huu Mhe. Spika. Kuna njia ya msingi, njia hii tokea asili mpaka leo ni njia yenye watu wengi iko mjini watu walikuwa wanatembea jioni sasa hivi hawatembei tena, imekuwa tatizo la karo na kila kitu.

Mhe. Pia kuna mazingira upande wa Qatar hali tunafuata mazingira ya watu kwamba sijui kuna mikoko, kuna kitu gani mji ambao umeteremka saa hivi ni Qatar, kwa hivyo ningeomba Qatar Mheshimiwa ije ikaguliwe, kuna uwezekano wa kuongeza ardhi sehemu ile, ili kupata eneo kubwa la *parcking* ya magari na kila kitu na kutengeneza kila kitu.

Mhe. Spika, sasa nazungumzia kidogo hali halisi ya chakula, ukilisha chakula vizuri nyumbani watu wakila vizuri hawaendi hospitali bado vyakula ni ghali, ramadhani inakuja kwa hivyo ningeshauri Mhe.Waziri tatizo la nyama nasema tena ng'ombe ghali na watu wanataka kula nyama penye uweze.

Mheshimiwa sasa Hospitali ya Chake Chake, ni kubwa yenye watu wengi hali halisi mpaka sasa hivi imetupwa haipo katika viwango, hata kwenye upereshini yake hali ni mbaya sana, ningeshauri sana Serikali yangu tukafanya kila jitihada tukaikagua, tukaweka katika viwango ikasaidie wananchi. Sina mengi ya kusema. Muda nahisi umekaribia lakini ninachokisema tu nawatakieni heri, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia na awapatie watendaji wote kheri. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza nataka nikushukuru kunipa nafasi hii, nikaweza kuchangia hotuba hii ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli kutokana na muda ambao naambiwa mlikubaliana ukweli dakika kumi na tano, hazitoshi. Kanuni inasema dakika ishirini na dakika kumi za Spika, kwa hivyo katika hizo dakika kumi na tano mlizokubaliana bado nitaomba zile dakika zako Mhe. Mwenyekiti, tano ikibidi basi uje unigaiye ili niweze kuweka mambo sawa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kwanza nimpongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na kwamba nilikuwa sipo lakini hotuba yake niliisikiliza kwa utulivu kabisa na pia imeeleza mambo mengi mazuri sana na hasa malengo ya Serikali kwamba kipaumbele kwa kipindi tunachokwenda nacho ni kuweka mbele masuala mazima ya huduma za jamii, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais lakini vile vile nataka nimpongeze na Waziri pamoja na watendaji wao wote kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nianze moja kwa moja kwa kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar kwa ile ahadi yake aliyoitoa wakati wa kampeni kwamba atawaongezea wafanyakazi wa kima cha chini cha mshahara kwa asilimia mia moja. Hili tayari Mhe. Waziri wa Fedha alipokuja hapa alilitamka na kwa kweli tunaomba kheri lakini vile vile na wafanyakazi wetu wajitahidi kuweza kusimamia vizuri mapato ya Serikali, ili hili lengo la Serikali liweze kufanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa pia nataka kutoa ushauri kwa Serikali, baada ya kutangaza itaongeza mshahara wananchi wengi wameanza kuwa na wasi wasi ya kwamba bei za vyakula zitaongezeka, sasa mimi mpaka sasa hivi sijaona

sababu ya bei za vyakula kuja kuongezeka kwa sababu katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha tumekubaliana kwamba mwaka huu hakuna kodi yoyote ambayo itaongezwa kwa ajili ya kuongeza kodi. Aidha kwa wafanyabiashara au kwa mambo mengine mbali mbali. Kwa hivyo kwa kuwa Serikali ilikwishakutoa tamko hatutegemei kwamba kutakuwa kuna kitu ambacho kitakachosababisha kuongezeka kwa bei za vyakula. Kwa hivyo hili nitaomba sana Mhe. Mwenyekiti, kupitia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais lakini vile vile na Waziri wa Biashara kuweza kusimamia, ili kuweza kuratibu na kuona kwamba bei za vyakula na bei za mambo mengine zinaendelea kubakia kama zilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, pia naendelea kuipongeza sana Serikali kwa kuweza kutoa msamaha maalum kwa vyakula vinavyoingia nchini, hasa mchele, unga na sukari. Suala hili kwa kweli Serikali yetu inahitaji kupongezwa sana, kwa sababu suala la bei za vyakula hivi Serikali inapotoa msamaha maalum inakuwa inawasaidia sana wananchi hasa wale wanyonge, kwa sababu kuna mambo mengine ya *luxury* mtu anaweza akastahamili, lakini suala la chakula hawezi akastahamili hata siku moja bila ya kula.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, suala hili viongozi wetu wanapata thawabu kubwa inaonesha pengine watu hawajui lakini viongozi wetu kutokana na maamuzi sahihi ya kusamehe baadhi ya kodi kwa kuweka asilimia maalum kwa kodi ya vyakula, kwa kweli hili linawezesha sana Serikali na sisi tutakuwa pamoja na Serikali yetu kuhakikisha kwamba bei za bidhaa zinaendelea kubakia kama zilivyo. Kwa hivyo nadhani Mhe. Waziri atakapokuja kutoa maelekezo yake au atakapokuja kutoa ufafanuzi nafikiri hili atalisisitiza, kwamba Serikali haikusudii kuongeza kodi ya aina yoyote na hakuna mfanyabiashara yeyote atakayeachiwa akaongeza bei ya bidhaa ya aina yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, hili niliamua kulisema kwa sababu hapa kati kati saruji iliadimika mfuko wa saruji ulifika ukawa unauzwa mpaka shilingi Elfu ishirini na tano, lakini Serikali ilikuwa kimya sasa suala hili hatulitaki tunataka Serikali wafanyabiashara wanapoongeza bei wakati kodi ipo pale pale lazima Serikali ichukue nguvu yake.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nimejaribu kuangalia kwa haraka haraka Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika hotuba yake alieleza suala zima katika ukurasa wa nne, kifungu kumi na mbili ziro alisema, kuhusu suala la mafuta na gesi Serikali imeshakamilisha utayarishaji wa rasimu ya sera inayoashiria mafuta na gesi asilia ambazo zinatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2016/17 na kuletwa hapa Barazani. Mhe. Mwenyekiti hapa mimi nilikuwa naiomba sana

Serikali katika eneo hili tusifanye haraka sana tunataka sote tuvune rasilimali ya mafuta na gesi iliyokuwepo ardhini, lakini katika jambo ambalo lina mtihani mkubwa ni suala la matumizi na usimamizi wa rasilimali ya mafuta na gesi.

Kwa hivyo naomba sana hiyo rasimu ya sera ambayo Serikali tayari imeshaanda sera hiyo iwe *public*, wananchi watoe maoni na sisi vile vile Wawakilishi tupate nafasi tutoe maoni *otherwise* Mhe. Mwenyekiti, tunaweza tukaja tukaingia katika mkondo wa nchi ambazo zina mafuta na gesi lakini wananchi wao wanaishi katika hali ya umasikini mkubwa. Leo ukiangalia Nigeria dhofulhali, wana mafuta ya kutupwa, Angola dhofulhali, wana mafuta ya kutupa. Juzi niliangalia kwenye Aljazira tumeona wenzetu *Venezuela* katika nchi ambayo inazalisha mafuta kwa wingi sana duniani, lakini juzi bei ya mafuta imeshuka wananchi wanapiga foleni wanaomba omba.

Kwa hivyo suala la mafuta na gesi naomba sana Serikali isifanye haraka sana, sera hii ishuke kwa wananchi, wananchi watoe maoni ili waelekeze fedha hizi zitakazopatikana asilimia fulani iende wapi na wapi ili tunapokuja kuptisha sheria tusije tukajuta baadae.

Mfano mdogo Mhe. Mwenyekiti, wenzetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania sera ile ya gesi na mafuta ilileta mgogoro mkubwa sana mpaka Serikali ikaahirisha zoezi lile, sera ile ikashuka kwa wananchi wakatoa maoni halafu ndio ikaenda Bungeni. Sasa na hili naomba sana na mimi kwa kuwa kamati yangu inasimamia suala zima la nishati nitajitahidi kumuomba Mhe.Makamu wa Pili wa Rais airuhusu kamati yangu itembelee nchi mbali mbali ambazo tayari zimezalisha gesi na mafuta, ili twende tukajifunze na kurudi hapa tuje kuishauri Serikali namna bora ya kuweza kushughulikia suala la gesi na mafuta.

Mhe. Mwenyekiti, waheshimiwa wananipigia makofi wanaona ni masihara ni kitu *serious* lazima twende katika nchi ambazo zilizofanya vizuri katika gesi na mafuta na twende katika nchi zilizofanya vibaya halafu sasa ndio tuje tuishauri Serikali. Sitokubali kuja kupitisha sheria, kuja kupitisha sera ambayo hatujaifanyia utafiti wa kutosha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hii yote katika lengo la kuhakikisha kwamba hizi rasilimali zikipatikana basi shida na kero za wananchi zinaondoka, tunaweza kuneemeka na sisi kama sisi viongozi wetu wanakwenda Arabuni kwenda kuomba misaada sasa watu watoke huko waje waombe misaada Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti hili nilisema niliseme kwa nguvu kubwa, nilitilie mkazo ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inaweza kuneemeka na rasilimali hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa haraka haraka Mhe. Makamu wa pili alivyokuwa akieleza katika sekta mbali mbali za huduma za jamii alieleza katika ukurasa wa nne, katika usambazaji wa umeme, mimi naishukuru sana Serikali katika nchi za Afrika sio Afrika ya Mashariki, Zanzibar sisi tuko mbele sana katika huduma za jamii. Hivi karibuni tulitembelea Pemba kamati yangu niliomba kabla ya kupitisha bajeti kwanza niende nikaangalie shughuli zinazofanywa na taasisi zangu.

Mhe. Mwenyekiti, huwezi kuamini Pemba sasa hivi umeme mpaka kuna nyumba moja tu na mikarafuu ishirini umeme umeshafika, barabara wewe utatamani ulale pale barabarani yaani barabara zilizokuwepo Pemba unazikuta *Itali* sio katika nchi za Afrika. Kwa kweli tunawapongeza sana Serikali kwa kazi nzuri na huduma hizi za jamii tunaomba waendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tatu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokuomba dakika tatu na zile zako tano basi nitaomba niweze kumalizia.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa una dakika tatu, tano hazijakubalika kutokana na makubaliano ya wajumbe wote, waliridhia hoja ile.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Nimekubali Mhe. Mwenyekiti, nyengine nitaweka hapo baadae lakini nataka nije katika suala zima la miradi ambayo Serikali inakusudia kuitekeleza. Kuna tatizo kubwa sana na hili naomba sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais waweze kulisimamia vizuri, leo sisi tunapitisha bajeti inayozingatia program, lakini ukiangalia kuna miradi Mhe. Mwenyekiti, imeshakaa zaidi ya miaka mitano, sita haijamalizika. Je, hii PBB kweli tunaitekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kuna miradi ambayo tayari imeshakamilika mpaka leo kuna madeni makubwa kwa wakandarasi hawajalipwa. Miradi hii Mhe. Mwenyekiti, kila tunapokwenda mbele inaongezeka *interest* kwa hivyo ina maana tunapitisha bajeti sio *realistic*, kwa hivyo tunaomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais iko miradi na iko katika Wizara yangu ya miundombinu ninayoismamia fedha zake zimeshakaa muda mrefu, wakandarasi hawajalipwa na fedha zile zinaendelea kuzaa riba. Kwa hivyo ina maana ile PBB tunayoisema itakuwa sio sahihi. Kwa hivyo naomba Mhe. Mwenyekiti na hili kwa kweli tumeshakubaliana vizuri na Mhe. Waziri anasema atalifanyia kazi, lakini naomba na Serikali vile vile iliingilie kati.

Mhe. Mwenyekiti, suala la viwanda, suala la viwanda tunashukuru Serikali yetu imeanza kuzungumza hapa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na ametaja kiwanda cha Mahonda, lakini bado katika kiwanda cha Mahonda Serikali iweke macho yake kwa uzuri sana, kiwanda kile sasa hivi kimerudi kinafanyakazi wananchi wetu wanaanza kupata ajira, lakini bado kuna migogoro baina ya muwekezaji na wananchi suala hili tunaomba lichukuliwe vizuri, ili wawekezaji wengine wasije ogopa kuja kuwekeza Zanzibar kwa sababu wawekezaji watakuwa hawana raha.

Nataka kumalizia Mhe. Mwenyekiti Mradi wa *ZUSP*, nina wasi wasi mradi huu Mhe. Mwenyekiti, usije ukafikia pahala ukaja ukaengezeka bei kama inavyoongezeka miradi mingine mfano miradi ambayo iliyorithiwa katika wizara ya Miundombinu, bajeti yake mradi unaanza na bilioni sabiini, mradi unamalizia na bilioni mia moja na arubaini maradufu. Sasa na huu mradi wa *ZUSP* mpaka sasa hivi kuna miradi imejengwa Jang'ombe na sehemu nyengine, lakini ule mtaro mkubwa unaopita ndani ya Jimbo la Shaurimoyo, mradi ule mpaka leo haujaguswa tunaambiwa hakuna fedha za *compensation* na hivi fedha.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Naam!

Mhe. Mwenyekiti: Umalizie.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kwa hivyo fedha hizi zikicherewa ina maana mradi huu vile vile kama ilivyokuwa na miradi mingine badala ya kwamba imetengewa labda bilioni utakuja kutumika zaidi ya bilioni mbili kwa mradi ule ule kutokana na ucherewaji wa fedha. Kwa hivyo nilikuwa naomba sana Mhe. Mwenyekiti.

Pia naomba kwa kumalizia Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli dakika mlizotupa ni chache na wakati wa bajeti ndio wakati wa kuzungumza matatizo ya wananchi, wakati mwengine wowote hautoweza kutusaidia. Nashukuru sana Mheshimiwa naunga mkono hoja.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa. Nichukue nafasi hii kwanza kwa kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais kwa kusoma taarifa yake vizuri, lakini pia niwapongeze watendaji wake jinsi walivyokaa kwa pamoja wakatuandalia taarifa hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na huduma ya afya ndani ya visiwa vyetu vya Zanzibar yaani Unguja na Pemba. Tayari Serikali kwa kupitia wahisani wamejenga vituo vingi vya afya, lakini kwa bahati mbaya baadhi ya vituo mpaka leo bado havijafunguliwa, sina uhakika kama ni upungufu wa madaktari au Serikali bado haijajipanga. Kwa hivyo nimuombe tu Mhe. Makamu wa Rais atapokuja atupe taarifa hivi vituo viko vingapi na kwa nini mpaka leo havijafunguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye nafasi hii hii niwapongeze madaktari wetu wa vituo mbali mbali pamoja na wauguzi. Lakini nichukue nafasi hii kuwapongeza madaktari wa Kituo cha Afya KMKM, bahati nzuri mimi ni jirani na jimbo langu kutoka Bububu kwenda Jimbo la Mtoni. Kituo hiki hata ukienda saa saba za usiku, ukienda saa nane za usiku pale pale unapewa huduma. Lakini baadhi ya vituo wenzangu juzi walisema kwamba inawezekana ukienda saa saba za usiku ukafika mpaka saa kumi na mbili au saa moja na nusu utamsubiri daktari. Kwa hiyo, naomba sana nichukue nafasi hii kuwapongeza madaktari wetu na wauguzi wa Kituo cha Afya KMKM, naomba na vituo vyengine viige mfano wake.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la elimu bahati nzuri ni Mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii juzi walitufata wanafunzi wa Vyuo Vikuu ambao wanasoma Tanzania Bara na wengine wanasoma Vyuo Vikuu hapa Zanzibar. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti ni suala la kusikitisha sina uhakika kama Mwenyekiti wangu alilizungumza au vipi. Ni kwamba wale vijana wanasema wana *semester* ya tatu hawajapewa pesa za kujikimu, walisikitika sana na walihudhunika sana mpaka wakaonesha dalili ya kutaka kulia maana yake wamekuja kwa wazee wao.

Kwa hiyo, naiomba sana serikali kupitia hii mifuko ambayo wanakopeshwa vijana wetu wa elimu ya juu wapewe kwa wakati. Wale waliokuja walikuwa ni vijana wa kiume lakini walikuwa wanawasikitikia sana vijana wetu wa kike, wako Tanzani Bara hana baba, hana mama hajui atoe chakula cha asubuhi wakati upi na chakula cha mchana atakipata wapi. Kwa hiyo, naomba sana suala la kupata mikopo ya elimu ya juu serikali iangalie kwa jicho la huruma kwani vijana wetu wanapata tabu na vijana wetu wazee wao ni wanyonge, nawaomba sana serikali isiahidi kwa maneno iahidi kwa vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, niende suala la huduma za kijamii. Mheshimiwa bahati nzuri Jimbo langu la Bububu limekuwa ni miongoni mwa majimbo ya Mjini, liko Mkoa wa Mjini Magharibi lakini ni jimbo la Mjini. Lakusikitisha sana kule tayari kuna majumba mengi na majumba ambayo yamepangika ki-*plan* lakini

barabara zake ni mbovu sana. Inapotolewa huduma ya kuangaliwa angalau barabara za kifusi, aghlabu wanaangalia eneo la Mbweni ambalo viongozi wetu wakubwa wanakalia huko. Kwa hiyo, naomba sana kwa mwaka wa fedha 2016-2017 serikali iangalie uwezekano wa kuhakikisha angalau baadhi ya barabara katika jimbo langu la Bububu nazo ziweze kuangaliwa kwa jicho la huruma.

Mhe. Mwenyekiti, suala la athari la mvua za Masika, hatimae tukubali tu kuwa serikali hatutimizi wajibu wetu, kwa sababu wananchi wetu walio wengi akijiona hana kiwanja anaamua kwenda kujenga kwenye mabonde ya mpunga. Sasa hivi imeshakuwa Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na Waheshimiwa Wabunge inapofika wakati wa mvua za Masika wote roho zao zinakuwa juu, kwa sababu wana hakikisha mvua ikiwa kubwa basi lile tatizo kutoka kwa mwananchi aliyekuwa kajenga linakuwa kwake dogo. Lakini Mhe. Mbunge na Mhe. Mwakilishi na Madiwani sasa hivi ndio inakuwa tatizo kubwa linawafika wao halafu ndio linaenda kwenye serikali kuu.

Mhe. Mwakilishi wa Magomeni amesema hapa aliwakuta wananchi wake wamefika saa kumi na moja hawajapata chakula. Serikali kuu pale haipo lakini ikabidi yeye awajibike kuhakikisha wale wanapata chakula siku ya kwanza na siku ya pili. Kwa hiyo, niombe sana kupitia taasisi zetu mbali mbali ikiwemo mipango miji pamoja na halmashauri zote tuhakikishe wananchi hawajengi kwenye mabonde ya mpunga ili kupunguza tatizo la hii kadhia ambayo inawafika Waheshimiwa Wabunge na Wawakilishi inapofika wakati wa Masika.

Mhe. Mwenyekiti, jambo hili linaungana pia na suala la kipindupindu, mimi bahati nzuri nina eneo pale Bububu linaitwa eneo la Kisima Majongoo, nilikuwa sijawahi kufika lakini wakati wa mvua hizi za Masika mara hii nilifika. Lile eneo liko kama hapa tulipo liko chini kabisa, kwa hiyo yale maji maeneo yote yanayotoka yanaishia pale, kwa hiyo kisima kilichochimbwa pale, shimo la karo lilochimbwa pale nyumba zote zimejaaliwa mpaka kwenye mapaa, pale tayari tunakaribisha kipindupindu. Kwa hiyo, naiomba sana serikali bado niendelee kusema yale maeneo ambayo ni hatarishi tuhakikishe tunayasimamia mapema ili yasiweze kujengwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la *TASAF III*. Niipongeze serikali kwa kuamua tu kwa makusudi kuwasaidia wale wazee ambao wamefika miaka 70. Serikali ina nia nzuri lakini kwa bahati mbaya kuna baadhi ya watendaji wameingizwa watu ambao bado hawajafikia miaka 70. Niombe tu kama

serikali ina uwezo basi tuhakikishe tunafanya uhakiki ili wale wazee waliobakia wenye miaka 70 nao wapate kusaidiwa.

Vile vile nimuunge mkono Mhe. Suleiman Sarahani na hapa tuende na watu wenye ulemavu. Kuna watu walemavu hawana uwezo, kuna watu wazee wana miaka 70 lakini walikuwa ni watumishi wa serikali wana hali nzuri za kimaisha na wanaendelea kupata. Lakini kuna watu wamezaliwa na ulemavu, familia zao ni za kimasikini kwa hiyo iko haja na wao kuangaliwa ili wakapata hizo fedha za shilingi 20,000 kila mwaka ili na wao wakapata kukidhi mahitaji yao.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo niseme kwenye *TASAF II* baadhi ya maeneo yenye kilimo cha umwagiliaji walisaidiwa kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji. Lakini tokea wakati huo mpaka leo bado maeneo yale hayajapelekwa umeme ni vizuri ile miradi ambayo tunaianzisha basi tuweze kuimalizia ili wananchi wafaidike. Tusitengeneze miradi nusu nusu ikaendelea kubakia serikali haifaidiki wala wananchi hawafaidiki. Kwa hiyo, iko haja nimuombe Mhe. Waziri hapa aje atwambie maeneo haya ambayo tayari yalikwisha tayarishwa kwa ajili ya umwagiliaji lini yatapelekwa huo umeme ili wananchi wetu wapate kufaidika.

Mhe. Mwenyekiti, suala la madawa ya kulevya. Niseme tu kuwa madawa ya kulevya zaidi yanakuwepo maeneo ya miji, lakini sasa hivi na maeneo ya vijijini tayari yameshaanza kufika. Niiombe tu serikali kwa kupitia wachangiaji wenzangu waliozungumza hapa wauzaji wanajuulikana na waletaji wanajuulikana, lakini wanaokamatwa ni wale vijana ambao wanatumia. Serikali bado iandae utaratibu mzuri wa kuhakikisha haya madawa ya kulevya ikiwa *airport*, ikiwa bandarini au kwenye bandari ndogo ndogo kunawekwa ulinzi mkali ili yasipitishwe. Lakini ikiwa sheria bado ni za ile miaka ya 50 au 60 huko nyuma haina meno, basi wakae wana sheria wabadilishe ili atakapokamatwa mtu na unga huko nchi za wenzetu nasikia unanyongwa.

Kwa hiyo, kama kuna adhabu kama hizo licha ya kunyonga adhabu nyengine mbadala lakini ziwe kubwa kidogo angalau mtu awe na hofu nikikamatwa na unga basi adhabu fulani itanifika. Lakini kwa bahati mbaya niseme siku zote wanaokamatwa na unga ni wale wateja wadogo wadogo, Mhe. Nadir amesema hapa ni wale wadogo wadogo wale wakubwa hawakamatwi. Kwa hiyo, tunaomba sana kwa kupitia kikao hiki Mhe. Mwenyekiti wale wenye kazi zao, yaani watu wa Usalama wa Taifa wafanye kazi ili wakamatwe, wasilindwe wao halafu wakaja wakakamatwa hawa wadogo wadogo ambao wao wanakuja kupewa kwa hatua ya mwisho.

Mhe. Mwenyekiti, niende na suala la kilimo kuhusu uwagizishiaji wa mchele. Serikali inatumia pesa nyingi sana kuagizia mchele Ulaya sisemi Tanzania Bara, Tanzania Bara mchele wao ghali zaidi kuliko wa Ulaya. Nataka niseme jana nilibahatika kwenda Kiwengwa na nikapita Kilombero, yale mabonde ambayo pengine serikali ilikuwa inafanyia hesabu ya huo mchele ambao unafanyiwa makisio kuwa utapatikana tani fulani za mchele, sasa hivi mabonde yale yote yanalimwa miwa na kupelekwa Kiwanda cha Sukari. Bado niseme kauli yangu ya mwanzo kwamba Zanzibar chakula kikubwa zaidi tunategemea mchele. Kwa hiyo, niiombe serikali iangalie huu mpango wa kulima miwa kwenye mabonde ya kulimwa mpunga inaweza ikatupunguzia ile hesabu ambayo tulikuwa tunaitegemea kuipata. Kwa hiyo, niombe sana serikali ifanye utafiti wa kina ili tuhakikishe chakula kile ambacho nilitegemea kizalishwe Zanzibar kiweze kuzalishwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye suala la umeme, niipongeze tu serikali kwa mpango wake wa kusaidia vile vijiji ambavyo havijafika umeme. Mimi nishukuru eneo langu la Mbuzini Shirika la Umeme imenipelekea umeme mpaka eneo hilo niiupongeze uongozi wa shirika, lakini pia niipongeze serikali. Lakini bado tu niseme baadhi ya maeneo umeme bado haujafika, kwa kupitia kikao hiki nimuombe waziri anayehusika pamoja na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais watusaidie yale maeneo ambayo hayajafika umeme yaweze kufika kwa sababu sasa hivi mshakuwa na majumba ya wananchi. Kama huna umeme huwezi kupata maji, tunaweza tukaisaidia serikali kuchimba visima vidogo vidogo wenzetu wakafaidika, lakini bado niseme kama umeme haupo hayo maji hayawezi kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho niupongeze tu uongozi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais akiwemo Waziri katika Ofisi ya Rais na watendaji wake kwa hotuba nzuri na naipongeza hotuba hii na naiunga mkono asilimia mia kwa mia mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Bububu. Nakushukuruni. (*Makofi*)

Mhe. Mussa Foum Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nikupongeze wewe kwa kunipa fursa hii wakati huu wa asubuhi na mimi kupata nafasi ya kuchangia. Pili nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo hapa wakati huu tukiwa wazima, na tatu nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa ukakamavu wake mzuri wakati ambapo anaiwasilisha hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, na nne pia niwapongeze wapiga kura wangu wa Jimbo la Kiwani kwa kunichagua mimi kuingia katika Baraza la Wawakilishi ili kuwaletea yale yote ambayo wanayahitaji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo na mimi nianze kwa kuchangia hotuba hii, kwanza nianze na huduma za jamii, mimi nitaanza na suala la umeme. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali kwa jitihada zake kubwa za kuwasambazia wananchi wake umeme. Mimi katika jimbo langu naipongeza sana serikali kwa sababu tulikuwa tuna baadhi ya shehia ambazo umeme bado ulikuwa haujafika. Mfano, Shehia ya Jombwe ilikuwa bado haijafikishwa umeme, lakini sherehe za Mapinduzi zilizopita mara hii katika shehia hiyo umeme umekwenda kuzinduliwa na Mhe. Mohammed Aboud alikuwa ni mgeni wa heshima.

Pia ilikuwa imebaki shehia ya Shamiaji Mwambe lakini kwa taarifa niliyonayo kwamba umeme umeshafika na wananchi wako katika harakati za kuungiwa umeme. Kwa hivyo, niipongeze serikali kwa jitihada zake hizo na kuna baadhi ya sehemu ya vijiji tu ambavyo bado haujafikishwa lakini kwa jitihada za serikali pamoja na kusaidiana na mimi mwakilishi basi tunategemea kwamba sehemu hizo nazo zitapata umeme.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuondoka hapo sasa mimi niende katika mfuko wa jimbo. Mhe. Mwenyekiti, mfuko wa jimbo hasa maelezo yake katika ukurasa wa 12 (ii) hapa umeelezwa vizuri. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali kwa jitihada zake za kuweka fedha ili zitumike katika majimbo yetu ya Unguja na Pemba, hili ni jambo zuri kwa sababu ni pesa ambazo zinasaidia wananchi. Lakini mimi kidogo nimekuwa na masikitiko baada ya kukipata kitabu hiki ambacho kinatueleza ripoti ya ukaguzi wa hesabu za serikali kwa mfuko wa maendeleo ya jimbo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi masikitiko yangu ni kwamba fedha zilikuwa zinatolewa, lakini ufuatiliaji wa fedha hizo za serikali juu ya yale mambo ambayo kuwa yalikuwa yanasaidiwa wananchi ili kupata maendeleo zaidi hapa ndio palipokuwa na matatizo. Wafuatiliaji wakuangalia fedha ambazo vipi zimetumika ilikuwa kila unapoangalia basi utakuta kwamba ukaguzi haukuthibitishwa. Sasa sijui kwa nini kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze ni kwa sababu gani fedha zilikuwa hazifuatiliwi matumizi yake na vyombo vya kufuatilia vipo je kulikuwa kuna nini? Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, nimeona katika kitabu hiki kwa mfano katika jimbo langu mimi katika mwaka 2011-2012 kulikuwa na usambazaji wa maji safi na salama Ulingo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa yako hii sehemu inayoitwa Ulingo hii ni sehemu ya Makaani tena hili ni pango ambalo kuwa mwenyezi Mungu aliliweka tokea alipoanza kuweka dunia hii, ni pango ambalo kuwa linatumika kwa wachunga

kuwapa wanyama wao maji. Sasa hapa panazungumzwa ni maji safi na salama, hii tukiizungumza hivi hivi utaiona kwamba ni maji ambayo kuwa yanasambaziwa wananchi ili wapate huduma.

Hili pango linatumika na huko kwenye hilo pango ni kwamba hakuna nyumba hata moja, hili ni pango linalotumika kwa ajili ya kuwapa wanyama maji. Na hapa pamezungumzwa kwamba zimetumika milioni tatu kilichofanyika hapa ilijengwa ngani ya kuteremkia kule chini ili wale wachunga wapate kutoa maji kwenye pango na kuwapa wanyama wao. Sasa hii ni moja kwa moja ingaliwakuwa hii miradi inafuatiliwa basi haya nadhani ingelionesha vichekesho vikubwa.

Kwa hiyo, naiomba serikali kupitia Ofisi hii ya Makamu kwamba masuala kama haya yafuatiliwe ili mambo kama haya yasitendeke. Kwa sababu kuna mambo yakifuatiliwa zikiwepo zile kamati na hasa hasa Kisiwani Pemba kwenye miradi hii mambo yalikuwa sio mazuri. Kwa hivyo, mheshimiwa nadhani kuna mengi yakueleza juu ya mambo haya lakini ni vyema kuonesha hizo alama na kwa mara hii tunaomba haya mambo yafuatiliwe vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo sasa niende kwenye Baraza la Wawakilishi. Mhe. Mwenyekiti, katika Baraza la Wawakilishi ukurasa wa 32 hapa imeelezea imeanza ukurasa wa 31-32 lakini mimi nataka nizungumzie hii (g) inayoelezea kwamba kuendelea kuweka mazingira mazuri ya majengo na kumbi za mikutano.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali juu ya maelezo haya na ni mazuri na vile vile nipongeze kwamba ofisi yetu iliyopo Unguja hali yake ni nzuri, ukumbi wetu ni kama huu tulionao ni mzuri lakini mimi nitoe masikitiko yangu makubwa sana kwa ofisi iliyoko Pemba kwa ukumbi wake.

Mhe. Mwenyekiti, ukumbi ulioko Pemba hauko vizuri, hauwezi kufanyika mikutano. Tunavyokumbuka kwamba huko nyuma Baraza la Wawakilishi lilikuwa na kawaida kila mwaka lilikuwa linafanya mkutano mmoja Pemba na ulikuwa ukifanyika wakati wa Mwezi wa Nne (Aprili). Hivi sasa kwa muda mrefu sana mikutano ile haifanyiki Pemba na ukilinganisha na hali ilivyo utaona huko nyuma mambo yalikuwa sio mazuri ukilinganisha na sasa. Sasa sijui ni kwa sababu gani kwamba hali ya uchumi wetu nyuma ilikuwa sio nzuri lakini ukumbi wa Pemba ulikuwa mzuri na unafanyika mikutano, lakini hivi sasa *Alhamdulil-lahi* kidogo mambo mazuri, lakini ukumbi ule kwa muda mkubwa sana mikutano haifanyiki.

Sasa tunamuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atapokuja kutoa majumuisho atueleze na kiufupi atupe matumaini ya mategemeo pengine tukifika mwaka fulani au muda fulani ukumbi wetu ulioko Pemba nao tutaanza kuutumia. Kwa sababu ukumbi ule tukiutumia basi wananchi wetu watajenga matumaini mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile muda unakuwa mdogo sana sasa mimi nigusie kidogo Tume ya Uchaguzi. Kwanza niipongeze kwa kazi nzuri sana iliyofanya na mpaka wakati huu tukiwa katika hali ya amani ya nchi yetu, amani nzuri tu lakini nataka niseme kwamba uchaguzi umemalizika aliyeshinda kashinda, aliyekuwa hakushinda basi apumzike asubiri mwaka 2020.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani tume ilipotangaza kwamba uchaguzi wa mwanzo ule umefutwa na ikasema uchaguzi utarejewa, kuna baadhi ya vyama vilishiriki, kuna baadhi ya vyama havikushiriki, hayo ni matakwa yao wenyewe. Kwa vile vyama ambavyo havikushiriki basi tulitegemea vitatulia, vipumzike na visubiri kipindi kijacho, lakini kwa masikitiko wenzetu wamekuwa sivyo tulivyotegemea, wamekuwa mfano wa yule mtu aliyeacha mke bado anamtaka. Bahati mbaya basi, wameacha kuingia kwenye uchaguzi lakini bado uongozi wanautaka. Sasa hawa watu wamemuacha mke wanamtaka na mke huyo wamemuacha talaka tatu, harejeleki mpaka watoe muhalili na muhalili wake mpaka mwaka 2020. Sasa tunawaambia kwa kupitia Baraza lako hili tukufu tunaomba kwamba watu watulie.

Hivi sasa mke keshaolewa na waliyomuowa hawawezi wakamuacha. Sasa wasubiri mwaka 2020 ikiwa huyo aliyeowa atakuja kumruhusu amuache, hiyo ni hiari yao wakati huo. Lakini kiufupi tunawaomba watulie hii nchi ni yetu sote na tunataka kuishi kwa amani, wasubiri ndio hali ya mambo ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani baada ya maelezo hayo mimi niseme kwamba naunga mkono hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa niaba ya wanajimbo la Kiwani kwa asilimia mia moja ahsante sana.(*Makofi*)

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Pili, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana kwenye kikao chetu hiki cha kujadili na kupitisha bajeti za wizara mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa kuwapongeza viongozi wote wa wizara hii kwa kutuletea bajeti yenye mwelekeo mzuri na yenye kuonesha mafanikio ya

serikali yetu. Nimpongeze kwa dhati Mzee wangu Makamu wa Pili wa Rais kwa usimamizi mzuri kwa serikali yetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye eneo la ukusanyaji wa mapato katika Idara ya Uchapaji. Nimeangalia hapa katika kitabu kilichosomwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, idara hii katika malengo yake iliyojiwekea haikufika hata nusu ya matarajio au malengo waliyojiwekea. Ni wazi kwamba yapo mawizara, mashirika na taasisi za serikali bado hawajatoa mashirikiano ya dhati ya kwenda kwenye kiwanda chetu hiki kilichoanzishwa kwa lengo hasa la kupunguza matumizi ya serikali.

Naomba sana kwenye eneo hili viongozi wote wanaoongoza mawizara haya watoe msisitizo maalum kwa watendaji wetu ili kuona machapisho yote ikiwezekana kutoa toleo maalum ambalo litaelekeza machapisho ya risiti na vitabu vyengine vyote ambavyo vimo ndani ya matumizi ya serikali basi yanakwenda katika idara hii ya uchapaji.

Kwa sababu kama tunakubaliana sote machapisho yanakwenda kule kwa sababu mashine zetu ni mpya tumezifunga karibuni tu na zina uwezo mkubwa; kwa nini sasa watendaji wa serikali watoke nje wakati nafasi ipo ya kwenda kuchapisha katika kiwanda chetu cha uchapaji ambacho kina mashine nzuri zaidi. Mimi naomba sasa serikali itoe msisitizo na toleo maalum kwa watendaji wote wa serikali mwanzo waende kule kupeleka kazi zao na kama kutakuwa kuna tatizo la mitambo basi wagonge muhuri nyuma na waandikiwe tu kwamba sasa hivi kuna dharura, ili tukitoa toleo hata ma-*internal* na *external auditors* watakuwa wanajua serikali imeelekeza hivi na kama hakuna uwezo kwa sasa au kwa wakati ule basi una uwezo wa kutoka nje na kufuata yale machapisho ambayo yanatumika katika idara zetu na mashirika ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kama tukiendelea kuacha mwanya huu watu wetu wataendelea ku-*declare interests* zao, watatoka katika viwanda hivi vya watu binafsi tutawajengea uwezo na uchumi wote tutaupeleka kwao wakati serikali hii inataka ijiongezee uwezo na kukusanya mapato katika idara na taasisi zenyewe za serikali.

Eneo la pili, ni eneo la uwajibikaji, utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze sana serikali kwa kuanzisha kitengo hiki. Lakini ni wazi kwamba mashirikiano tunayowapa katika kufanikisha kazi tuliyowatuma ni madogo kweli, sio kwa taasisi za serikali haziendi katika lengo tulilolikusudia la utawala bora na utumishi tunaoukusudia.

Mhe. Mwenyekiti, yako malalamiko mimi binafsi nimeyasikia yanatoka katika taasisi kubwa tu katika serikali yetu ni *ZRB.* Suala la rushwa na uwajibikaji hapa niseme sijui wanaongoza au wana nafasi kubwa ya utekelezaji wa kutowajibika vizuri, lakini niseme tu katika miongoni mwa vitengo pale ni cha *auditing and investigation.* Wao hawa kabla ya kwenda katika zile taasisi zilizokusudiwa, kwenda kwa wale wafanya biashara ambao ndio walengwa katika kukusanya mapato ya nchi, ile *bargaining* inafanyika kabisa na wanamwambia hasa wakati mwengine mfanyabiashara kuwa tunakuja huko, ukitaka kufanyiwa *auditing* yako vizuri basi toa hiki. Mamlaka ya rushwa ipo na jamii hii tunayoishi nayo ndio inayopokea vitu kama hivi. Kwa hiyo, mamlaka hii iongeze kasi ya uwajibikaji ili serikali inusurike na mambo mengi ikiwemo haya ambayo tunayoyazungumza.

Mhe. Mwenyekiti, tunawapongeza katika maeneo mengine, idara au taasisi ile lakini kitengo hiki kinaongoza sana, kina rushwa kubwa sana. Sasa katika uwajibikaji wa idara inayodhibiti na kuzuwia rushwa, hebu hapo fanya urafiki wa karibu na wafanyabiashara mbali mbali tutakamata wengi sana na tutaisaidia sana serikali. Pia, niiombe kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ichukue jitihada binafsi ya kuongeza kasi na kuonesha kuwepo kwa mabadiliko katika eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika eneo la Kipindupindu. Kwanza niipongeze serikali kwa jitihada waliyoichukua kudhibiti mripuko wa maradhi haya. Mimi ni miongoni mwa sehemu ambayo naathirika sana na maradhi haya ya Kipindupindu, lakini sana niwashukuru wananchi wa Jimbo la Chumbuni kwa taaluma na elimu mbali mbali walizozipata mara hii angalau hesabu imeshuka ya watu wetu ambao waliumwa na maradhi haya. Mpaka sasa na kwa miezi saba nyuma tumepata watu 11 tu na wanane walitibiwa wakarudi nyumbani na watatu walilazwa.

Pia, niiombe serikali pamoja na jitihada inazozichukua basi pia itoe jicho la huruma kwa wananchi wa Jimbo la Chumbuni. Najua wana huruma kubwa, lakini niwaombe kwa udhati wa nafsi yangu kuwa basi katika kujipanga na kudhibiri maradhi haya mpaka lile eneo linalofanyiwa tiba tutafute namna ya kutafuta *centre* nyengine ambayo pia haitatoa manung'uniko kwa baadhi ya watu na wananchi walioko katika maeneo hasa ya Chumbuni, Mto Pepo, Karakana na Maruhubi, kwa kuzingatia tunapowapeleka wagonjwa pale katika hospitali ya Karakana huduma zote ambazo walitakiwa wapate wananchi wa maeneo yale ambao pia katika dhana nzuri tu walianzisha hiki kituo kwa nguvu zao na serikali ikasaidia mpaka hatua hii tunayokwendanayo.

Kwa hivyo, tukiweka *centre* ile kama ni sehemu ya matumizi ya kudumu ya maradhi ya Kipindupindu basi mpango wa serikali pia uelekeze kwa dhana ile ile ya kusogeza huduma kwa wananchi wa Jimbo la Chumbuni; huduma ya matibabu, huduma ya kupima wajawazito na watoto, lakini kupata tiba pale ambapo wanaumwa na maradhi madogo madogo, basi serikali ielekeze tunaelekea wapi. Kwa sababu wao mpaka wanaanzisha hospitali hii na serikali inasaidia walikuwa wakifuata huduma eneo la mbali; wako ambao waliokua wanafuata Saateni, Mnazi Mmoja na Sebleni. Kwa hivyo, niiombe sana serikali pamoja na dhana nzuri basi dhana ya kushughulikia kutengeneza *centre* ambayo haitaathiri huduma za wananchi wa Jimbo la Chumbuni lizingatiwe.

Mhe. Mwenyekiti, Tume ya Uchaguzi. Katika eneo hili kwanza niipongeze serikali na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kukamilisha vizuri zoezi la uchaguzi. Wenzangu wamesema na mimi narejea kusema ni kweli uchaguzi umekwisha na kama kuna mtu ambaye anakariri uchaguzi haujesha basi kichwa chake sio kizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini wapo watu bado wanaendelea na chokochoko zao za kuwapotosha wananchi wa nchi hii, wanakwenda katika mikoa mbali mbali. Mimi natokea Kaskazini, wapo waliokwenda Kaskazini wakajifanya wao kuwa ndio wenye nchi hii, wakapigiwa vidufu ambavyo havina mwelekeo. Mimi niiombe serikali pamoja na mimi kwanza kulani vitendo vinavyoendelea kuwapotosha wananchi, nalaani leo na nitalani kesho na hatuwezi kuwavumilia watu hawa. Sasa niiombe serikali vitu kama vile ambavyo vinaashiria uchochezi wa wananchi wetu, yaani kuwapotosha wananchi vidhibitiwe, nikiamini hakuna mtu aliyekuweko juu ya sheria, akivunja sheria mtu yeyote adhibitiwe, hakuna wakati wa kumuogopa mtu, vimefanyika vingi tumestahamili basi stahamili zifikie mwisho, tuwashughulikie.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, naomba umalizie.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante naomba nimalizie dakika zangu mbili, nimalizie katika eneo la mapambano dhini ya UKIMWI...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, una dakika moja naomba umalizie.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na Mhe. Hamza Hassan Juma, dakika hazitoshi, kwa hiyo, nitachangia maeneo mengine kwa maandishi, lakini niseme tu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chumbuni naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa imani yako ya kunipa na mimi angalau dakika 15 nikaweza basi kuchangia hotuba hii inayoendelea. Kwanza niwashukuru sana wananchi walio wengi wa Jimbo la Mpendae kwa kuendelea kunipa imani ya kunichagua na kuweza kuendelea katika jimbo hilo.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwanza nimshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa uwasilishaji wake katika hotuba hii, lakini timu nzima kutoka Mhe. Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ambayo imeandaa bajeti hii ikiwa katika hali nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiri kuwa bajeti ni ndogo mno kwa shughuli za serikali, kwa sababu tukisema Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ndio muhimili mkubwa sana, ndio shughuli zote za serikali yetu zinafanywa pale na zinaratibiwa pale.

Lakini vile vile tunalaumu sana mjadala huu kuendelea wa dakika 15. Asubuhi nilitaka kutoa utaratibu ili tuone shughuli hizi za serikali ndio shughuli muhimu tutasemea wapi, hapa ndio pa kusemea na wizara hii ndio wizara mama katika wizara zetu, mkiwa hamtupi nafasi kuzungumza hapa hatuwezi kuwatendea haki wananchi wetu. Lakini tutaendelea kadri ya muda utakavyokwenda, nadhani na nyinyi mtaelewa ili tuone kuwa tunachangia kwa uzuri zaidi. (*Makofi*)

Kwanza niipongeze bajeti hii imenda vizuri sana. Mimi nitaanza kuchangia katika bajeti Namb. C01011 Shughuli za Utaratibu wa Serikali. Mhe. Mwenyekiti, bajeti iliyoletwa hapa ni bajeti ndogo sana, lakini kwa umahiri mkubwa nadhani wizara hii itaweza kuelekeza katika shughuli zake nyingi na kutelekeza vile tulivyojipangia. Kodi za ndani ndio msingi wa matumizi yetu imara sana. Sasa nataka kuipongeza kwa dhati sana kwa sababu nikiwa hapa hakuna msaada wa mtu yeyote ulioletwa na hizi kodi zetu za ndani ndio zitatunufaisha na ndio bajeti halisia ambayo safari hii tunatarajia tutaitumia vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna shughuli za uratibu wa Serikali za SMZ Dar-es-Salaam. Ofisi ile ni muhimu sana kwetu. Lakini cha kusikitisha sana jengo la ofisi ile ukienda tu linavyovuja na thamani yake si la kuingia mle ndani. Sasa niiombe serikali ofisi hii na dhana yake ni kubwa ya kuweza kuratibu shughuli zetu Dar-es-Saalam au katika Muungano wetu na Muungano ndio muhimili mkubwa sana.

Niiombe serikali kwa dhati sana na niishauri kuweza kuiendeleza ofisi ile lakini shughuli zake ziwe nzuri na wawatilie fedha za kutosha. Kwa sababu hata hicho kidogo wanachopangiwa hakiendi, yaani hakipatikani kwa muda. Tunaomba sana serikali ifikirie kuiendeleza ofisi ili tupate manufaa mengi na michango mingi kutoka kwa mabalozi mbali mbali ifanywe kama ilivyokusudiwa shughuli zake pale katika wizara ile.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende tu kwenye Programu ya Uchapaji. Mhe. Mwenyekiti, kwanza tuipongeze sana serikali kwa kusema inataka kuanzisha Kamisheni. Lakini pana changamoto zake, tumeanzisha Kamisheni nyingi sana na mamlaka nyingi sana lakini haziendi, kule kwetu Donge wanasema "Kila tukikoka moshi, tunaanza kuumia macho tu lakini haviwivi, kuni bado mbichi".

Tumuombe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, mimi naamini uongozi wake ni mzuri pamoja na Mhe. Waziri, kwa sababu ndio 'majembe' yetu na hakuna siri ya kusema. Mhe. Mwenyekiti, Makamu wa Pili wa Rais tumpongeze sana ndio 'jembe' haki yake apewe "Mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni".(*Makofi*)

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ametukwanwa sana kwenye mitandao ya kijamii, kila pahala. Lakini tumuombe basi asife moyo aendelee na uzi wake huo huo. Mhe. Mwenyekiti, "mti wenye matunda haukosi kupopolewa". Mhe. Makamu wa Pili, wewe ni 'jembe' endelea na kazi yako. (*Makofi*)

Lakini tukuombe sana katika uratibu huu wa uchapati taasisi nyingi sana ni taasisi za serikali na tuna mazoea makubwa sana kuona taasisi za serikali hazilipi huo ndio ukweli wenyewe. Sasa tutaiendesha vipi shirika hili. Tujitahidi sana hapa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ili kuona basi tunaendelea vizuri. Lakini Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na tumeona katika uchapaji tumetengewa milioni mbili na laki tano, fedha hizi zimetengewa kwa kununuliwa vespa, honda na siao tuseme wazi hapa Mhe. Waziri, umetupiga changa la macho, haiwezekani vespa peke yake ndio milioni mbili na laki tano, sasa mimi sikubaliani na hii. Niseme ukweli kwa hili sikubaliani nalo.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi tuipongeze sana kwa ujasiri mkubwa iliyofanya. Lakini niseme tu na nipige *salute* Bwana Jecha "Shikamoo". Huu ndio ujasiri uliofanyika na hapa ndipo tunapopataka. Mhe. Mwenyekiti, tuna vijana pale wanatumikia Tume ya Uchaguzi wengi sana kwa muda kwa mikataba. Tungemuomba sana Mhe. Waziri, vijana wale wamekuwa wazoefu tuwafikie kwanza vijana wale kuwaajiri. Kuliko kuwaita, tukawaondoa, tuite, tumekuwa kama samaki

tunawakaanga upande huu na tunawarudisha upande huu, tuombe sana tuweze kuwaajiri vijana wale ili wafanye kazi nzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, jana kwa jicho langu nimeanza kuona nilipokuwa hospitali ya Mnazi Mmoja pale msafara wa aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na njia imefungwa akipita katikati wakati njia imefungwa ile ya Ikulu. Mhe. Mwenyekiti, hii si haki, sheria msumeno inarudi. Tunaomba sana serikali kulichukulia suala hili kama imefungwa barabara asipite mtu yeyote mwenye uwezo wa kupita ni Mhe. Rais peke yake. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Haji Omar Kheri, yupo na ninamuamini sana katika kutekeleza majukumu yake na ana vikosi ambavyo viko imara sana. Ningemuomba sana suala hili aweze kulishuhulikia ili watu wasivunje amani ya nchi hii. Wenzangu wamesema uchaguzi umekwisha na hapa kazi tu.

Mhe. Mwenyekiti, kama kanuni ingekuwa inaniruhusu ningekwambia sasa nipige "*push-up"* niweze kuonesha kama kazi inafanyika. Nchi hii ni nchi ya Mapinduzi, tusianze kuzungumza tu midomoni Mhe. Mwenyekiti, tukasema nchi ya Mapinduzi lakini haina vitendo vya Mapinduzi, hii nchi isichezewe na mtu mmoja tunahatarisha hali ya amani nchi kwetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi mikutano imepigwa marufuku lakini kuna watu bado wanafanya na wanavaa sare za vyama, hawaitendei vyema nchi hii. Nchi yetu tunataka ende vizuri "kama umesusa basi sisi wengine tunakula" na mhalili hapa haupatikani. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye Tume ya Dawa za Kulevya. Mhe. Mwenyekiti, nikiri sana kuwa katika jimbo langu limeathirika na dawa za kulevya muda mwingi sana na kama utaniuliza tume hii iwepo mimi nitakuwa haina haja tume hiyo kuwepo. Mhe. Mwenyekiti, tunatumia pesa nyingi sana za wavuja jasho kuweka tume ile. Lakini sasa serikali imekuwa na taratibu nyingi; Tunaanzisha Mahakama ya Rushwa, tunaanzisha Mahakama ya Wahujumu Uchumi, kwa nini tisianzishe na Mahakama ya kuweza kuwahudumia hawa wafanyabiashara wa dawa za kulevya.

Serikali ilete mswada hapa tuukubali. Lakini tunakuwa tunaimba nyimbo ikawa hatutaipa memo, mkurugenzi hatumpi meno yoyote, anasema yeye anaratibu tu, unaratibu nini, nani anaetaka kuratibiwa hapo, tuweze kuipa meno tume hii iweze kufanya kazi zake vizuri. Iko haja ya kuunda Mahakama ya dawa za kulevya ili tuweze kuwapa meno kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nirudi kwenye Tume ya Ukimwi, kwanza tume hii niwapongeze sana, wamefanya kazi nzuri sana na maambukizo mengi kutokana na takwimu zao yamepungua hivi sasa. Lakini nianze kuwashauri waanze kuzipitia AZAKI zilizokuwa za kiraia ambazo zinatoa Elimu ya Afya kuweza kuziratibu, je, hizi AZAKI zina ukweli wowote au AZAKI hizi zinafanya kazi mifukoni na mikobani hazina ofisi ili waweze kuona ni jambo gani linaloendelea na kuweza, kuratibu vitu hivi vizuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye jimbo langu huu wa *ZUSP* Mhe. Hamza Hassan Juma, amesema kwa jimboni kwake lakini mimi jimboni kwangu mimi ndio ulipoanza. Lakini mradi huu umekuwa kama kifukufuku, kifukufuku anarudi nyuma. Kwa hiyo, na mradi huu unarudi nyuma, umenza Mpendae, ukwenda Magomeni umerudi Kwamtipura, sasa hivi uko Kijangwani. Bado hatujamaliza, tunaomba serikali sana na tuishauri serikali itoe pesa ili tuone wapi itapatikana pesa Makamu wa Pili wa Rais anajua jinsi gani za kufanya tukapata pesa hizi ili tukawaokoa wananchi wetu. Safari hii tumepata mafuriko makubwa sana.

Lakini niseme pamoja na hayo, shughuli hizi ambazo zinaratibiwa na hii Idara ya Maafa bado haijafanya kazi inavyopaswa, kuna wananchi wangu pia wamepata maafa mengi na watu wameratibiwa mbali mbali kwa kupitia kwa Sheha na kwengine. Lakini mpaka leo hatujaona lolote ambalo limeweza kufanyika. Tunaomba serikali kama ilikuwa na dhana ya kweli basi izidishe mwamko huu tuone jinsi gani tutaweza kuwaokoa wananchi wale wachache waliopata na mafuriko yale lakini waliopata matatizo makubwa na vitu vyao kuharibika.

Mhe. Mwenyekiti, tukija kwenye dawa za kulevya lakini vile vile kuna kitu kinaitwa 'Elimu Feki'. Wenzetu sasa wameanza kupiga na Vihio, wale ambao wanatayarisha wanakuja na vyeti bandia, wanakuja na elimu bandia ambazo tunaweza kuwaajiri tukoana tuna wataalamu wazuri. Lakini wataalamu wa vyeti. Nimuombe Waziri wa Elimu aweze kufuatilia suala hili kidogo kidogo na tuone basi tumekaa vipi katika jambo hili la Elimu na vile vile, tuone wataalamu wetu wana kigezo gani, kwa sababu tunawategemea wao na tufanye yale mambo ya kitaaluma ili serikali yetu tuandike miradi mingi ili tufanikiwe. Kwa sababu sasa hivi kama unavyoona hata hao wenye misaada hawatusaidii. Kwa hivyo, tutegemee wataalamu wetu wa ndani lakini tutapokuwa na elimu zilizokuwa bandia hatuwezi kufanya kitu.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema na mimi nichangie hapo, lakini naunga mkono hoja asilimia 99% na 1% nataka niibakishe ili nitape ufafanuzi kwa yale mambo niliyoyatoa. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Shaib Said Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kabisa kwanza nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi kuichangia hotuba hii ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe shukurani zangu za dhati kwa Makamu wa Pili wa Rais kwa bajeti yake hii ilivyopangika, ingelikuwa si kuichangia kidogo kuipiga fagio tungeliipitisha moja kwa moja, lakini na sisi tunataka tutoe maelekezo yetu ili aweze kuchukuliwa kwa kuifanikisha hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niichange hotuba hii kwanza kabisa niseme kwamba muda usije kunimalizikia kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Chonga basi hotuba hii naipitisha kwa asilimia mia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze na suala zima la kisiasa Pemba, ukifungua ukurasa wa pili kifungu 7.0 kinazungumzia kwamba hali ya Kisiasa. Tume ya Uchaguzi Zanzibar iliendesha Uchaguzi Mkuu, marudio tarehe 20 Machi 2016, jumla ya vyama 14 vilishiriki. Nafupisha maneno haya kwa sababu muda wangu ni mdogo, lakini kulitokea vitendo vya wananchi kule Pemba visivyokuwa na maana kabisa.

Lakini nasema kwamba vitendo hivi bado Pemba vinaendelea kuwepo. Wananchi bado wa Kisiwa cha Pemba tunabaguana katika mazishi, magari, masuala yote ya kijamii na hata sisi Wawakilishi wa Pemba hivi sasa muelekeo wa kutoa huduma za Pemba basi kama serikali haitochukuwa mipango thabiti kabisa huenda tukashindwa kabisa.

Kwa sababu wenzetu wamejipanga, sisi tunapotaka kutekeleza wao wabomoe. Mhe. Mwenyekiti, kuna mifano kadhaa ambayo inatendeka hivi sasa kwa Wawakilishi wote tulio humu wa majimbo ya Pemba tumefanyiwa, mimi jimbo langu la Chonga, Pujini kuna banda la Kilimo limeunguzwa moto kabisa kwa masuala haya ya kisiasa. Kwa hivyo, naiomba serikali isijipange itoe uamuzi kwamba hili suala la kisiasa Pemba likomeshwe kabisa. Kwa sababu bila ya masuala haya tutashindwa sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Pemba kuleta maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ardhi, alitamka baba wa Taifa katika Azimio la Arusha ili tuendelee tunahitaji mambo manne; siasa safi, uongozi bora, watu na

ardhi. Lakini Mhe. Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba jamii inaongezeka lakini ardhi haiongezeki na mipango ya ardhi hivi sasa inavyoelekea ni kwamba badala yake wananchi tutakosa pakujenga, tutakosa pakulima, tutakosa hata pakufugia kutokana na uchafuzi unaondelea wa ardhi.

Kwa hiyo, naiomba serikali kwa dhati kabisa masuala ya ardhi yaangaliwe ili iwe na muelekeo mzuri kabisa katika kufanikisha suala zima la ardhi hapa iliyobakia basi iweze kupanga mipango mizuri wananchi wasiichukuwe bure, kuna watu sasa hivi ardhi wanaidhibiti na hawaifanyii kazi hawaishughulikii, lakini anaetaka kuishughulikia hapati fursa hiyo.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, nije katika masuala ya mazingira. Mhe. Mwenyekiti, katika eneo langu la upande wa Mashariki katika jimbo langu la Chonga katika ukanda mzima wa Mashariki Pemba, hili limechafua mazingira kabisa kabisa. Kwa hivyo, naiomba serikali kabisa suala la mazingira kwa sababu sasa hivi mazingira Pemba ni magumu sana, watu wanakata miti ovyo, watu wanachimba mchanga ovyo, watu wanachimba mawe ovyo, kwa hivyo, inakuwa ni mtafaruku mkubwa sana ulioko Pemba sasa hivi. Kwa hivyo, naiomba serikali ipange mipango madhubuti ya hali ya mazingira kabla ya hali ya hewa haijachafuka zaidi ili wananchi na kule Pemba tuweze na sisi kufaidika na matunda yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niinge kwenye madawa ya kilevya. Mhe. Mwenyekiti, haya madawa ya kulevya sasa hivi katika jamii yanakuwa ni mazito sana. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi vijana wetu wengi sasa hivi wamepotoshwa kabisa na madawa ya kulevya na mimi nataka niulize haya madawa ya kulevya yanapita wapi na nani anayeleta haya madawa ya kulevya, kwa sababu yanapika katika visiwa vyetu vyote na bandari zetu pamoja na viwanja vya ndege na unakaguliwa hadi wewe unavua kuanzia viatu, mkanda, miwani, kila kitu unavua, haya madawa yanapitia sehemu gani mpaka hawa watu ikawa hawakamatwi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwenyekiti, kama wanavyochunguzwa watu pale basi na haya madawa ya kulevya yachunguzwe. Katika hii mipango tuandae utaratibu, tupange, tuelekeze. Mhe. Mwenyekiti, tuamue kwa kunusuru vijana wetu na madawa ya kulevya.

Mhe.Mwenyekiti, sasa nije katika masuala ya mvua, sasa hivi tumeshakuwa na woga kwamba mvua zinaponyesha baada ya kuwa mvua ni faida hivi sasa tunasema kuwa ni athari. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nasikia kuna nchi ambayo sasa hivi wao maji ya mvua wanayahifadhi, wao wanaomba mvua inyeshe ili

maji ya mvua wayahifadhi. Kwa nini sisi hatufanyi mpango huo wa kuhifadhi maji ya mvua baada ya kuwa mvua ni neema kwetu huwa ni athari.

Kwa hiyo, Mhe.Mwenyekiti, nakuomba haya maji ya mvua hasa ukija katika ukanda wangu mimi wa Mashariki mvua ya masika namna inavyonyesha tunapata kwa muda wa miezi miwili, lakini kule upande wa Mashariki ya Pemba hupati mvua ya Vuli, hupati ya Mchoo, isipokuwa ni mvua ya masika tu ndio unayopata kule sasa hivi kutokana na hali ya uchafuzi wa mazigira sasa hivi. Naomba haya maji ya mvua ya masika inayonyesha basi yahifadhiwe pahali ili wananchi wafaidike nayo katika masuala ya kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nije katika masuala ya kiuchumi, kuna suala zima la mapoto hili. Mapato katika jimbo langu kuna kijiji changu kimoja cha Mgelema ni kijiji ambacho Mheshimiwa kinazalisha karafuu kwa wingi. Kuna wakulima wengi lakini kuna njia ambayo haipitiki kuleta mazao yao katika sehemu ya kuuzia. Na sasa hivi walanguzi wanatumia Kijiji cha Mgelema katika kununua mazao ya wakulima kwa sababu hawana njia ya kupitisha mazao yao. Ninaiomba serikali Mhe. Mwenyekiti, wakione kijiji hichi na waitengeneze njia ya Mgelema ili zile karafuu ziliopo kule basi ziuzwe katika hali ya usalama zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie katika masuala ya *TASAF III* na msaada wa wazee. Mhe. Mwenyekiti, masuala haya kwenye majimbo yetu wakati utafiti unafanywa sisi tulikuwa hatushiriki kabisa, tulikuwa bado hatujapata fursa hii. Lakini Mhe. Mwenyekiti, safari hii suala hili limekuwa ni sugu kwa sisi Wawakilishi kutoka majimbo yote. Kwa sababu anakujia mtu, yaani mzee anakujia anakuonesha na anakupa mfano ulio hasa kabisa. Niangalie mimi nimepata msaada na huyu aliyepata msaada wa *TASAF*. Anakuonesha hasa kwamba yule mzee unavyomuona unahisi kwamba na yule mtu aliyepata msaada ule kuwa hawalingani kabisa. Unamuona mzee wa miaka tisini hakupata msaada lakini kuna watu wa miaka arobaini, hamsini wamepata msaada huu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, ninasema kwamba suala hili la *TASAF III* na wazee waliopata msaada lichunguzwe tena ili sisi Wawakilishi tusipate aibu ya kule vijiji kwetu.

Baada ya hayo kutokana na muda niseme tu kwamba naipongeza kabisa hotuba hii ya Makamu wa Pili wa Rais. Ni hotuba ambayo ina mwelekeo na dira nzuri. Kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Chonga, ninaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwenye mia.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwakilishi kwa mchango wako. Bado tuna dakika kama kumi. Naomba nimwite mchangiaji mwengine kama dakika zitatosha achangie ni Mhe. Abdalla Maulid Diwani, kama yupo.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii.

Ninafikiri nilikupa taarifa kuwa mimi nitachangie jioni kutokana kwamba hivi sasa sijisikii vizuri. Hivyo, hata hizo dakika kumi hazitonitosha. Naomba kwamba nafasi yangu nitakuja kuanzia jioni ukiniruhusu.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Abdalla Maulid Diwani, lakini kutokana na taratibu jioni kutakuwa na wachangiaji wawili wa nafasi za Uwakilishi, baadae tutawapitisha Mawaziri nao pia wachangie. Na mwisho kabisa Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kabisa nilikuwa nichangie lakini madhali umeniomba basi nitachangia japo kidogo dakika mbili, tatu nizungumze.

Haraka haraka mimi nitachangie juu ya suala zima la mabadiliko ya hali ya nchi. Kama unavyofahamu kwamba Jimbo langu la Jang'ombe ni sehemu moja yenye matatizo ya kutokea mashimbo kila mara baada ya kutokea mvua kubwa. Kipindi kilichopita tuliwahi kutembelewa na Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayeshughulikia mazingira kuhusu namna gani tutafanya kuondoa matatizo yale kwenye Jimbo letu la Jang'ombe sehemu ile ya Jang'ombe Mshelishelini ambayo imetokea mpaka kuzama zaidi ya nyumba mbili na kutokea mashimo kila muda.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba katika majumuisho ya Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais, ile sehemu yangu ya Jang'ombe sijui imechukuliwa hatua gani mpaka sasa hivi. Kwa sababu imekuwa ni nyimbo ya muda mrefu sana lakini utekelezaji wake bado mpaka dakika hii. Hivyo, naomba utakapokuja kufanya majumuisho na mimi unielezee *at least* wananchi wangu walionituma Jimbo la Jang'ombe waone kweli nimelizungumzia juu ya suala lao zima la sehemu ile.

Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kuchangia juu ya suala zima la madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya ni janga la taifa letu ni kwetu kabisa kama yalivyo majanga mengine. Na wenzangu waliopita walizungumza sana tu kwamba waletaji madawa wanajulikana, wauzaji madawa wanajulikana lakini

hatua za kuchukuliwa hao wauzaji madawa au waletaji madawa imekuwa donda ndugu katika nchi yetu hii hususan serikalini, kama tunaogopana.

Sasa ikiwa siku zote ukichelewa mwana kulea mwisho utalia wewe. Na kweli kabisa tunapoteza nguvu kazi nyingi sana ya vijana ambao tuliwategemea kuja kuwa viongozi wazuri tu katika nchi hii. Sasa Mhe.Mwenyekiti, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ninafikiri na hili vile vile ulichukulie maanani sana katika suala zima la uingizaji wa madawa Zanzibar na utumiaji.

Ninashukuru kuna *sober houses* nyingi ambazo zipo za watu binafsi zimefunguliwa. Na vile vile nitoe *my interest* katika Baraza hili na mimi ni mlezi wa vijana walioacha madawa ya kulevya katika Hospitali ya *Mental* ambao pale wanakuja kupata dawa kila siku ya Mungu. Hivi sasa nina vijana karibuni mia moja na thamanini ambao kwa hiyari yao waliamua kuacha madawa ya kulevya bila ya kupitia *sober house* kwa kuja kunywa dawa ambayo inawasaidia sana kutokana na utumiaji wa madawa yale. (*Makofi*)

Lakini siyo sababu ya kutafuta dawa ya kuacha kutumia. Kwa nini watumie madawa ya kulevya? Ninafikiri jibu la wengi linakuja kwamba kutokana pengine elimu imekuwa ndogo, ajira hamna. Kwa hivyo, wanakaa katika magenge yaliyokuwa siyo salama na vishawishi vimekuwa wingi na wale watu wanaingia katika majukumu kama yale.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kama utatafuta njia mbadala kwa vijana wetu kuwatafutia ajira zisizo rasmi. Kwa upande wetu Jimbo la Jang'ombe tunajitahidi katika hicho, kwa sababu tuna mpango wa kutengeneza *entrepreneur house* kwa ajili ya kuwakusanya wale vijana wote ambao walioacha madawa ya kulevya. Lakini tutaomba na serikali itie mkono wake mkubwa ili kuona lile azimio letu tunalotaka katika jimbo letu lifanikiwe na kupunguza kasi kubwa sana ya utumiaji wa madawa kwenye maeneo mbali mbali, siyo Jimbo la Jang'ombe tu bali ni kwa Zanzibar nzima. (*Makofi*)

Baada ya hapo Mhe.Mwenyekiti, nitakuja kwenye suala zima la ardhi. Kama ilivyozungumzwa kuwa tatizo la ardhi ni tatizo kubwa sana kuhusiana na upatikanaji wa ardhi kwa watu wetu kwa shughuli za maendeleo. Ninazungumzia suala la ujenzi wa nyumba. Katika kisiwa chetu ardhi haitanuki bali ardhi inaliwa na bahari. Sasa tusipokuwa makini, tukatoa ardhi kwa uangalifu *at least* watu wakaleta maendeleo kwenye ardhi, baada ya muda si mkubwa tutakuja kukosa hata sehemu za kuzikiana. Sasa hivi tukiangalia mfano kwenye upande wa Kilimani kule, bahari inakula, yaani bahari inakula sivyo kama miaka ya nyuma ilivyokuwa. Miaka ya nyuma ilivyokuwa

kulikuwa na mita nyingi mpaka kufika kwenye maji. Lakini sasa hivi maji yanapofika kwenye ukanda ule inaonesha wazi kwamba bahari inakula sana ardhi yetu. Lazima tutafute njia mbadala.

Sasa hivi tu, juzi nilifanya mazoezi kule pwani nimeona sehemu ile ya Ikulu (nyumba ya Rais). Kuna eneo kubwa sana limeporomoka udongo na kuhatarisha hata ule ukuta wa Ikulu kuja kuanguka. Sasa ninafikiri Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hili jambo liangaliwe *at least* tusije kujenga mpaka limeshaanguka. Hivi sasa linahatarisha usalama kabisa kwa sababu ni eneo kubwa sana na ukuta ule umeshafika ukingoni kuanguka. Sasa suala la mazingira hilo, tujue suala la ardhi tuliangalie kudhibiti ardhi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, na vile vile, ningependa kuzungumzia juu ya suala zima la afya. Imekuwa sasa hivi baada ya kumalizika uchaguzi huduma zetu za afya zimekuwa na matatizo Mhe. Mwenyekiti. Tunatibiwa kwa chuki katika nchi hii. Wanaangaliwa watu wanaitikadi gani na hiyo imeshakuwa ni nyimbo siku nyingi tumeshasema. Imekuwa hata baadhi ya wafanyakazi kupangiwa sehemu za kazi kwa kukomoana. Kwa sababu akijuulikana tu huyu mtu ana msimamo wa upande fulani, basi anakuwa stahiki zake au mambo yake yanayomlazimu yanapindishwa pindishwa siyo kama atakavyofanyiwa mtu wa upande mwengine. Kwa hivyo, hiyo ni donda ambalo tayari mimi nimeshawasiliana na Waziri husika kwenye suala hilo. Lakini ninazungumza kama ni mtendaji mkuu wa shughuli za serikali hilo suala ulijue, na haraka iwezekanavyo tulipatie ufumbuzi ili tusiendelee na vidonda hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, ninataka kuzungumzia suala la Tume ya Uchaguzi. Tume ya Uchaguzi imefanya kazi nzuri sana, ninashukuru sana katika hilo. Lakini baada ya uchaguzi wa tarehe 25 Oktoba, 2016 tuliambiwa kwamba uchaguzi ule uliharibika na watu walioharibu uchaguzi ule wanajuulikana. Sijui mpaka dakika hii kama wizara yako imechukua hatua gani kwa wale watu ambao waliosadikiwa kuharibu uchaguzi ule.

Tumethubutu kupoteza mapesa mengi sana ya serikali hii na tukarudia uchaguzi wa tarehe 20, lakini uchaguzi wa tarehe 25 umeharibika. Na mumethibitisha kwamba wapo watu ambao munajua wameharibu uchaguzi kwa namna moja au nyengine. Sijui kama serikali imechukua hatua gani mpaka dakika hii. Bado tunaambiwa uchunguzi haujakamilika, lakini hatujaona kilichotokezea mpaka dakika hii. Ninajua serikali sikivu na ina mkono mrefu na yote wanayafahamu na tunaendelea kusubiri.

Lakini tusisubiri mpaka ikawa zile subra zetu zikafika mpaka. Tunataka tuaambiwe au tujue hasa aliyeharibu uchaguzi wa Zanzibar wa tarehe 25, hawa na hawa na tumechukua hatua hizi, hizi kwa ajili ya kuwafahamisha kuwa serikali ina nguvu. Siyo kila mtu ufanye unavyotaka na halafu hakuna chochote kinachoendelea.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, ningependa kuzungumzia juu ya suala zima la upatikanaji wa maji. Kama ilivyozungumzwa juu ya upatikanaji wa maji kwenye mji wetu upo asilimia 87 kwa mjini. Kwenye karatasi ni kweli upo asilimia 87 lakini kwa uhalisia katika miji yetu bado haijafikia hata asilimia 50, ni tatizo. Katika maandishi yanaandikwa vizuri lakini kiutendaji bado ni ziro. Mpaka dakika hii Mhe.Mwenyekiti, mimi kama ni Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe kuna sehemu miaka mitano *pipes* zimefungwa kwa sababu mfanyakazi hajapewa pesa tu ya kuweza kufungua ile *cork*. Na anasema kama mimi hamjanilipa basi ninafunga hii *cork* na ni kweli. Kwa taarifa yako Mhe. Mwenyekiti, juzi Jumamosi iliyopita nimefanya hilo zoezi na tayari nimeshaifungua ile sehemu na tayari nimeshapeleka mipira zaidi ya mitatu kuunga maji kuwapatia wananchi wetu wa Jimbo la Jang'ombe. (*Makofi*)

Na ninathubutu kusema kwamba sehemu zile zipo nyingi sana tu ambazo mtu kwa utashi wake tu mtu anajiona yupo juu zaidi kwa sababu ni fundi wa sehemu ile kufanya uharibifu wa makusudi ili kuwakosesha huduma ya maji watu na kuweza kuipaka matope serikali yetu ambayo inayo nguvu na sababu ya kusimamia huduma ile inapatikana kwa wakati muafaka. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ukitaka hata leo nitaweza kukueleza namna gani jinsi ilivyofanyika suala hilo, lakini madhali tupo Barazani mengine haturuhusu kuzungumza moja kwa moja. Lakini nitazungumza hapo mpaka dakika hii.(*Makofi*)

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwambia kwamba sipo vizuri sitoweza kuchangia sana kwa muda huu. Ninafikiri baada ya haya machache tu, ninathubutu kusema kwamba ninaunga mkono hotuba ya Makamu wa Pili wa Rais, mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Jang'ombe na ninaikubali kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Abdalla Maulid Diwani, lakini pia nikupe pole umechangia vizuri ijapokuwa ni mgonjwa. Ahsante Waheshimiwa wote muliochangia lakini kutokana na muda kabla ya majumuisho ya Mhe.Makamu wa Pili wa Rais, kutakuwa na wachangiaji wawili. Mhe. Ussi Yahya Haji pamoja na Mhe. Hassan Khamis Hafidh na baadae watafuata Mawaziri na Manaibu Mawaziri.

Waheshimiwa Wajumbe, naahirisha Baraza mpaka saa 11: 00 jioni.

(Saa 6:50 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa Mhe. Ussi Yahya Haji, baada ya hapo atafuata Mhe. Hassan Khamis Hafidh.

Mhe. Ussi Yahya Haji: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia uzima jioni hii ya leo na kuwa hapa katika Baraza lako tukufu na kuchangia hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Naibu Spika, kwanza ni wajibu wangu kukishukuru Chama changu cha Mapinduzi ambacho ndicho kilichoniwezesha kusimama hapa leo na kuzungumza machache kuhusu hotuba hii. Pili, niwashukuru kwa dhati kabia wana-CCM wa Jimbo la Mkwajuni kwa kunipa kura nyingi sana na kuniwezesha kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, katika Baraza hili la Tisa la mwaka 2016.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwanza niwashukuru wana-CCM kwa kumchagua kwa kura nyingi sana Dkt. Ali Mohammed Shein na baada ya kwisha kumchagua Dkt. Ali Mohammed Shein, tukapata baraka zake hapa kwa kulifungua Baraza lake la Tisa, tukapata muongozo, hamasa, ukweli na uaminifu aliotuhutubia hapa, ambapo na sisi tunapaswa kuuendeleza. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Dkt. Ali Mohammed Shein baada ya kuteuliwa kwa kura nyingi, akatuchagulia jembe na hilo jembe, hee! mimi naweza kusema Fagasan la trekta ndugu yetu Mhe. Balozi Seif Ali Iddi. Pia, nikishukuru Chama cha Mapinduzi kwa upande wa Tanzania Bara kwa kumchagua kwa kura nyingi sana Dkt. John Pombe Magufuli, pamoja na Makamu wake wa Rais Ndugu Samia Suluhu Hassan.*(Makofi)*

Lakini shukrani zote kwa dhati kabisa baada ya kuwashukuru hao, tunawajibu wa kuwashukuru waasisi wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Abeid Amani Karume na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Hao

ndio waliotufanya leo kuwepo hapa na tukawa na Baraza la Wawakilishi na tuna na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu sisi tunaunganishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali mbili hizi kila serikali ina Katiba yake; kuna Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuna Katiba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi tupo hapa kwa mujibu wa Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais naomba kuchangia ukurasa wa 2, kifungu namba 6 kinachozungumzia Tume ya Uchaguzi. Mhe. Naibu Spika, kwanza nipongeze kwa dhati kabisa Tume ya Uchaguzi, kuweza kupitisha uchaguzi tarehe 20 Machi, 2016 kwa salama na amani mpaka tukapitishwa tukawa wawakilishi katika Baraza lako tukufu. Baada ya kuwa wawakilishi katika Baraza lako tukufu, naomba nizungumzie machache sana.

Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki kinazungumzia kwamba uchaguzi kulijitokeza hali ya uvunjifu wa amani kwa baadhi ya wananchi kuchoma moto mali za serikali na za wananchi wenziwao, vikiwemo vituo vya afya, mashamba, mikarafuu, nyumba na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, tunavyojua sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeundwa na ipo madarakani, chini ya Rais Dkt. Ali Mohammed Shein. Tunavyojua sisi Mhe. Naibu Spika, uchaguzi umekwisha katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Lakini kinachostaajabisha tunaona vurugu za hapa na pale.

Kwa mfano, juzi kulitokea matatizo makubwa yanayosababishwa na mtu wa kawaida tu ili kuwahamasisha vijana kutaka kufanya fujo ambayo haifahamiki. Yeye anasema; 'mimi ni Rais'. Rais ni mmoja tu Dkt. Ali Mohammed Shein Zanzibar. Dkt. Ali Mohammed Shein hakujiweka yeye kama Shein, Dkt. Ali Mohammed Shein amekaa kwa mujibu wa Katiba, katiba zetu zote mbili zimemuweka Dkt. Ali Mohammed Shein. Ukifungua Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuna kifungu cha 102, 103, 104, 106,107, vyote hivyo vinahalalisha Urais wa Dkt. Ali Mohammed Shein. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ukija katika Katiba ya Zanzibar utakuta kuna vifungu 26, 27 na 28. Sasa huu ujabari wa mtu wa kawaida tu kusema yeye ni Rais na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikamuachia anakwenda huku na huku, ameipata wapi? Namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais akatueleza kwamba huyo aliyeyafanya hayo anayafanya kwa mamlaka gani na kama hana mamlaka kwa nini afanye? La ajabu zaidi sisi hapa kabla ya hotuba hii kulikuwa kuna hotuba

ya Waziri wa Fedha tulizungumzia zaidi kuhusu kodi za serikali na mtu huyo huyo nasikia anawaambia watu wasilipe kodi, na serikali inamuacha tu. Ikiwa sisi tunawahimiza watu wetu walipe kodi halafu anatokea mtu anasema msilipe kodi, serikali inachukua hatua gani. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, atueleze, kwa nini huyu anaachiwa kuranda na kuyafanya hayo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, la ajabu zaidi ati anawaambia wenzake hadhiri nadhiri kwamba wananchi wa Unguja tunawaombeni muwaunge mkono wananchi wa Pemba.Wakauliza tuwaunge mkono nini. Akasema muwaunge mkono kukata mipunga ya watu, kugomea maduka, wana-CCM musiwazike, wana-CCM musiwachukuwe kwenye magari. Nawaambia ndugu zangu wa Unguja, hilo si suala jema. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko katika madaraka na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kazi yake moja kubwa ni kulinda usalama wa wananchi.

Sasa ikiwa kuna mtu anawaambia muunge mkono yale yanayofanywa kule, haya yalifanywa zamani, na baada ya kufanywa haya ndipo Chama cha *Afro*-Shirazi *Part* kikaweza kufanya Mapinduzi kwa kufanywa haya haya. Ndio maana tukapata shamba letu linaitwa Kilombero. Kilombero lilikuja kwamba wanyonge wa nchi hii waling'olewa mazao yao, wakakatiwa migomba, wakafukuzwa katika ardhi na hayo ndio yaliyotufanya tufanye Mapinduzi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nawaomba ndugu zangu wa Zanzibar wasiyapokee hayo. Tena nasema kwamba haya yanayofanywa na wenzetu hao hawaitakii mema Zanzibar, hawawatakii mema wananchi wa Zanzibar. Ninawaomba wenzangu wa Zanzibar wasiyaunge mkono hayo. Wanasema ati Dkt. Ali Mohammed Shein ataondoka madarakani bila ya kujua. Ataondoka bila kujua vipi? Asome katiba kifungu nilichokitaja cha 26, 27 na 28, kinasema;

"Dkt. Ali Mohammed Shein atakaa madarakani kwa muda wa miaka mitano".

Kabla ya miaka mitano hawezi kuondoka madarakani. Sasa yeye anasema ataondoka kiaina, atueleze ataondoka vipi, kama yeye anajua ataondoka kabla ya miaka mitano basi atueleze na sisi tujitayarishe. Kama yeye atamuondoa na sisi tunasema huyu haondoki hapa.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na hayo naomba sana tena sana serikali itueleze kwa nini huyu mtu anaachiwa avunje amani katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Hatuwezi hata siku moja kuvumilia hayo, sisi nchi hii imepatikana kwa

Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari na tumepindua kwa sababu ya madhila, sasa kama kuna watu wanataka kuturejesha huko, hapana. Ati wanasema sisi Zanzibar tuwe na mamlaka kamili, mamlaka kamili yepi ya 1963, mamlaka ya 1963 hapa hayarudi ng'oo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mamlaka wanayoyataka kifungu cha 5 cha Katiba ya 1963 kinasema hivi; 'Mfalme wa nchi hii tuliyempindua sisi tarehe 12 Januari, ati awe ndiye Rais wa nchi hii na akiondoka yeye mwanawe, mjukuu wake na kitukuu chake', hilo haliwezekani tena. Kwa hivyo, mamlaka ya visiwa hivi yamepatikana tarehe 12 Januari 1964.

Mhe. Naibu Spika, naendelea na kifungu cha 1200, kuhusu suala la mafuta na gesi serikali imekamilisha utayarishaji. Naiomba serikali lazima sasa hivi serikali ichukuwe juhudi na maarifa ya kuwasomesha vijana wetu mambo ya mafuta na gesi, bila ya kuwa na wataalamu ambao watashughulika na mafuta na gesi, tutakuja kupata matatizo kama yanavyopatikana nchi nyengine. Kwa hivyo, tuwasomeshe vijana wetu kuhusu mambo ya mafuta na gesi.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuhusu kifungu cha 24, athari za mvua za masika. Mhe. Naibu Spika, hali ya hewa duniani haitabiriki. Masika tuliyopata kipindi kilichopita hatufikirii kipindi kijacho masika yatakuwa kama yale au sio kama yale. Matatizo makubwa tuliyoyapata katika mafuriko yale ni kwamba miundombinu yote iliyopangwa na serikali iliharibiwa. Kwa hivyo, tunaiomba serikali wale wote ambao wamejenga katika sehemu ambazo hazitakiwi nyumba zile zivunjwe mara moja. Kama si hivyo, 'mchelea mwana kulia atalia yeye'. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache sana, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa jioni hii na mimi kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho. Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia na kumshukuru Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi 'jembe', kwa kutusomea kitabu hiki cha bajeti kwa mbwembwe na kwa kujiamini sana, Mhe. Balozi, hongera sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kitabu hiki kilichosomwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais majuzi kina ukurasa karibu 40, lakini kurasa zote 40 kimejaa maneno ya utendaji na utekelezaji. Kwa upande wangu nitaanza na ukurasa wa tano wa kitabu hiki kuna neno 'huduma za jamii'. Katika maelezo yangu ya juzi ya

kuchangia hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango, niliongelea kuhusu Magharibi, na leo nitaongelea kwa uchache kidogo kwamba, kwa heshima kubwa Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atembelee huku Magharibi.

Kwanza kuna sifa moja, kuna watu wengi wanaishi Magharibi kuliko kokote Zanzibar. Lakini sifa ya pili kuna maeneo mazuri yenye majina mazuri. Kwa mfano, Hawaii, Uholanzi, Miembesaba, Nyarugusu, huko kute Mhe. Makamu wa Pili wa Rais majina hayo mazuri lakini yeye hakujui na yeye ndiye mtendaji mkuu wa serikali. *(Mkofi)*

Mhe. Naibu Spika, kero kubwa zilizokuwepo Magharibi ambapo kunaishi watu wengi ni kwamba huduma za jamii hakuna kabisa na huko ndio kunakoishi watu wengi. La kusikitisha huduma za jamii bado zimeelekezwa mjini kunakoishi watu wachache na watu ambao huduma zipo karibu kwao wao. Sasa naomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakapokuja Mhe. Naibu Spika, anijibu au anijuze serikali ina mkakati gani wa kuiangalia hii Magharibi inayoishi watu wengi na ambapo hakuna huduma za jamii. Je, wana mkakati gani wa kuwapelekea watu hawa huduma za jamii? Eneo hilo hakuna barabara, maji, hospitali, hakuna chochote, kila siku dada zetu na mama zetu wanazaa njiani. *(Makofi)*

Mchango wangu mwengine Mhe. Naibu Spika, kuna watu maarufu katika dunia yote au nchi yoyote wanaitwa 'wafanyabiashara'. Wafanyabiashara Mhe. Naibu Spika, wana sifa mbili kuu; sifa yao ya kwanza hawana dini, dini yao ni faida. Sifa yao ya pili hawana kitabu wanachokifuata cha aina yoyote, kitabu chao hilba na udanganyifu. Hiyo ndio sifa mama ya wafanyabiashara.

Nitakupa mfano Mhe. Naibu Spika. Juzi Darajani pale palipokuwa pakipita daladala wauza mbatata waliambizana, tuuze mbatata kilo shilingi 2,500/- kwa umoja wao wakakubaliana. Halafu wakaanza siku ya kwanza na ya pili. Mmoja akaona mbona mbatata zangu siuzi, akawa anauza shilingi 2,000/-, lakini mteja anapokwenda anamuambia mimi nauza shilingi 2,000/- lakini usiwaambie watu. Wakamuona mbona huyu anauza sana, wakamchunguza wakamkuta yeye kapunguza bei wakamdunda ngumi. Kama uliwahi kusikia kulikuwa kuna ugomvi Darajani kwa wauza mbatata ilikuwa ni wenyewe kwa wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, jana mimi nilitembelea sokoni nikauliza bei za mbaazi na kunde, nilikuwa nafanya huo utafiti. Lakini mbaazi zilikuwa zinauzwa shilingi 2,100/-, lakini kuanzia jana mbaazi zilikuwa zinauzwa shilingi 2,400/-, nikamuuliza jamaa mmoja ana sijida, nikamwambia aah! Mbona

mmeshapandisha bei na Ramadhani inakuja, akaniambia aah! Hujui kama Ramadhani kwetu sisi ndio jangusho.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nasema hii ina-*verify* kwamba wafanyabiashara hawana dini na kitabu chao ni hilba na udanganyifu. Naiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mara nyengine tena, irudishe Tume ya Bei. Dunia nzima Tume ya Bei ipo, jukumu lake kubwa ni ku-*monitor* zile bei, ingawaje serikali ile inafuata mfumo wa kibepari, lakini haina maana bwanyenye au mfanyabiashara ndio kaachiwa tena awakomoe na awakomeshe wananchi, haina maana.

Linalofanyika sasa hivi Zanzibar Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara wanatukomoa sisi wananchi kwa sababu hakuna chombo kinacho-*regulate* kuweka bei zao, wanaweka wanavyotaka wenyewe na wanafanya wanavyotaka wenyewe.

Namuomba Mhe. Makamu wa Rais, anapokuja hapa atujibu Serikali ina mkakati gani wa kuweka utaratibu wa uratibu hizi bei zinazowekwa na mabwanyenye hawa wanaoitwa 'wafanyabiashara' wasio na dini.
Hoja yangu ya tatu Mhe. Naibu Spika, juzi nilipokuwa jimboni kwangu nilimkuta mtu kapigwa panga, eeeh! Nikamuuliza umepigwa panga umefanya nini? Akanambia bwana eeeh! Kuna mbwa mwitu, mbwa mwitu? Mbwa mwitu. Mwengine akanambia sijui mbwa koko, mwengine akanambia ubaya ubaya, nikataka kujua zaidi nikaambiwa bwana siku hizi huku Welezo na maeneo mengi ya Magharibi hakutokeki usiku na mchana; kuna vijana wana mapanga yao wakikuona na simu wanataka.

Sasa wananchi wangu wakaniagiza wakanambia Mheshimiwa tunakuomba, tushachoka sisi kupigwa mapanga kwa sababu pesa za kutibiwa hatuna, na watu wenyewe kila siku tunaripoti polisi hakuna linalokuwa na wanajulikana, sijui ukenge, sijui nani, wanajulikana kwa majina. Sasa mimi nikajiuliza hii polisi kazi yake nini, si kulinda raia na mali zao, na mimi nilizaliwa katika polisi, kuna kitengo cha *CID* kazi yao kufanya upelelezi wa kujua wale ambao wanafanya uharabu waweze kuwafikisha katika kitengo cha sheria.

Lakini Mhe. Nabu Spika, cha kusikitisha katika nchi hasa majimbo ya Magharibi kuna watu kwa mfano kule kunakoitwa Fuoni kwa Balozi hakupitiki ikifika saa moja, hakupitiki unapigwa panga utoe simu, sasa wananchi wangu wameniagiza kama Serikali imeshindwa kuwalinda raia na mali zao, wananchi wangu wako tayari kujilinda wenyewe, lakini wasije wakalaumiwa kwa sababu wanasema kama madam wanamjua watamfuata mtu kwao watu kufika sitini

wakampige kwa mapanga watamuua. Mimi nikawaambiwa wananchi chonde chonde msifanye hivyo nitakwenda kulisema.

Sasa nakuomba sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makamu wa pili wa Rais anapokuja hapa aniambie Serikali imejipangaje hasa hichi kitengo cha polisi cha *CID* wapo wanajulikana, mishahara wanayolipwa polisi mikubwa, tunawatibu katika mahospitali makubwa lakini wanashindwaje kutulinda sisi raia, tunapigwa mapanga na watu tunaowajua, hawa *CID* kazi yao nini? Upelelezi washashindwa, kama wameshindwa wanijibu mimi nikawajibu wananchi, aa! Serikali imeshindwa, wananchi endeleeni, hiyo ya pili.

Mhe. Naibu Spika, la tatu, kumevuka vuguvugu la kisiasa Zanzibar, juzi mwananchi alinijia akanambia Mhe. Hassan, nataka kuhama Zanzibar nirudi Bara, kwa nini? Kaskazini kumeanza shida, nasikia kumekwenda kushapigwa na kushafanywa nini, sijui, nataka kurudi Bara, hapa naogopa, ishakuwa vita vinakuja, Pemba vimeshaanza na Kaskazini vimeshaanza, jana nimeona rova za *FFU,* mswalie Mtume. Sasa naomba kusema kitu kimoja, waswahili wanasema; 'usipoziba ufa utajenga ukuta'. Zanzibar hii hii tuliwaachia watu wanaitwa jina baba sitaki kulitaja, tukawaona aaa, tukawadharau, na leo hii Mhe. Naibu Spika, tayari kumeanza vugu vugu, moto unaanza kufuka wa kutaka kuharibu amani ya Zanzibar iliyokuwepo.

Mhe. Naibu Spika, natoa wito kwa Wazanzibari wenzangu na Watanzania wote kwa jumla amani na salama hii tuliyonayo baadhi ya nchi kama Somali, Ruwanda, Burundi wanaitamani kwa sababu ukiingia chooni unataka kufanya haja unasikia bunduki unatoka mbio, Zanzibar mpaka mtu kufikia miaka 40 hajawahi kuona bastola hajawahi kuona bunduki kwa sababu tuna amani na uvulivu, natoa ombi tuendelee kuilinda, kuidumisha amani yetu na wale wote wanaotaka kuharibu Amani ya Zanzibar kuwa tusicheze tarabu hapa, tukastarehe nchi yetu Mungu awalani, Amani hii ikitutoka hatuwezi kuipata tena.

Lakini chengine naiomba Serikali, Makamu wa Pili wa Rais, aje hapa anijibu, hii Polisi na watu wengine wamejiandaa je katika kulinda, kuwalinda wananchi wa Zanzibar na mali zao na mambo kama haya yasitokezee. Maana yake unajiuliza Balozi yuko wapi, amri yake iko wapi na yeye ndio Makamo wa Pili wa Rais, amri yake risasi? Mhe. Naibu Spika, nataka anijibu kwa sababu wananchi washakuwa wanapata wasi wasi haiwezekani kuishi katika nchi yetu mwahali ulipozaliwa ukawa na wasi wasi, mimi siwezi kuishi nchi yangu lakini nikiwa na wasi wasi, nchi ya mwenzangu naweza kuishi, lakini si nchini kwangu kuwa na wasi wasi. Mhe. Naibu Spika, nataka sana Mhe. Makamu wa

Pili wa Rais, aje anijibu kajipangaje, ana mkakati gani ili nikapate kwenda kuwaambia wananchi wangu walale kwa salama na amani.

Mhe. Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa 'maafa' na kuna kamati za Wilaya za Maafa, majukumu makubwa ya Kamati za Wilaya ninayo sheria hii hapa nilikuwa naisoma, sasa nasema hii Sheria ya Maafa kumbe kazi yake imekuwa kama mchimba makaburi, mchimba makaburi kila siku anaombezea watu wape ili apate kazi ya kuchimba kaburi, na hii Sheria ya Maafa kila nikiisoma imekaa kama mchimba makaburi kwa sababu inaombezea maafa yatokezee ili ipate kukabiliana nayo. Lakini haina kipengele kinachosema; itaweza kulinda na ku-*manage* maafa haya, itayalinda wapi, kwa hivyo, nilikuwa naomba na haya maafa yako ya aina mbili; kuna maafa yanaitwa *Natural disaster* na kuna *Man-made disaster,* yaani ya maumbile na yanayosababishwa na mwanadamu na utafiti ulio wazi kabisa Mhe. Naibu Spika, unaonyesha Zanzibar maafa mengi yanasababishwa na wanadamu sii wenyewe.

Mfano, Kipindupindu kilichotokea juzi kimetumia karibu dola milioni moja lakini ukiangalia kwa asilimia kubwa Kipindupindu hichi kina sababishwa na sisi wenyewe, kwa mfano kuchimba vyoo ovyo, kuchimba visima ovyo, kujenga katika maeneo ya maji, watu kuiba visima, watu kufanya wanavyotaka na Serikali ipo imenyamaza kimya. ukiyatizama yote haya ni maafa ya *Man-made* yamesababishwa na wanadamu. Sasa hii Tume ya Maafa imekaa macho wazi na inatizama, inasubiri Kipindupindu kitokezee ndio iingie kati ili tutumie pesa nyingi ambazo ilikuwa tuweze kuzitumia kwa mambo mengine.

Sasa nilikuwa naomba sana Mhe. Naibu Spikka, Mhe. Makamo wa Rais anapokuja hapa atujibu, mimi naomba hii maafa ipewe jukumu pia la kulinda maafa, sio kushauri tu, kulinda haya maafa yasitokezee, kama ilivyopewa jukumu Wizara ya Afya ina kazi ya kutulinda, kututibu na kutulinda tusipate maradhi. Kwa hivyo, hii ina jukumu moja tu kama mchimba makaburi kusubiri maafa yatokezeem inakuwa mimi nahisi haipendezi.

Mwisho kabisa, Mhe. Naibu Spika, nataka kuongelea kitu kinachoitwa 'rushwa' Zanzibar ni nchi ndogo na sote tunajuana, lakini kwa sababu ya umasikini wetu unaweza ukahisi hapa Zanzibar rushwa si kubwa kama nchi za wenzetu, lakini kutokana na umasikini wetu Mhe. Naibu Spika, hapa rushwa ipo na kubwa na inaendelea tena ya kila aina. Juzi kuna mtu mmoja kagonwa na gari, basi alipogongwa na gari kila mtu kaona hasa kwa watu wa pale kwamba, kosa la mgongaji, lakini polisi wamekuja na mchoro umemtia hatiyani mgongwaji, wale watu wakanambia kapewa rushwa? Kwa hivyo, najua ipo ZAHEKA, naijua, lakini hebu Mhe. Naibu Spika, tuache kidogo tuzitake hizi taasisi Mhe.

Makamu zifanye kazi zao kama wenzetu kule Bara wanafanya kazi, hakini hapa hii kujuana undugu-*nization* na muhali wakati *sometimes* unatukwaza.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, akija pia hebu atujuze kidogo kwamba hii rushwa ina majukumu gani na mpaka leo inafanya vipi na inafanya nini katika kutekeleza majukumu yake na imefanikiwa kwa kiasi gani, ina mkakati gani na malengo gani katika kumaliza rushwa Zanzibar?

Mhe. Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa Kipindupindu, sitaki nikizungumze sana Kipindupindu kimeanza kwisha, lakini nasema hivi Mhe. Naibu Spika, Zanzibar Kipindupindu hakishie mpaka tutakapoweza kurekebisha matumizi mabaya ya ardhi, kuna taasisi moja Mhe. Naibu Spika, inaitwa *Globo Land Monetary Agency* imefanya utafiti na imegundua kwamba Zanzibar ni visiwa, lakini matumizi ya ardhi yapo mabaya na kila siku yanaongezeka na yanawaengezea umasikini Wazanzibari.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nataka kumuuliza Makamu wa Pili wa Rais, lini Zanzibar itaingilia kati na kuondosha kabisa haya matumizi mabaya ya ardhi kwamba kila mtu anayetaka kujenga mpaka anamaliza hajenda kwa Sheha, hajenda Wilayani wala hajenda popote na anajenga akahamia, utafikiri kama kwamba nchi hii hakuna Serikali na ipo, na majenzi hayo wanajenga kihorela.

Mhe. Naibu Spika, huko mitaani Kwarara, Nyarugusu hakupitiki hata baskeli haipiti kutokana na majenzi yaliyojengwa, juzi nilikuwa natoa mfano nikawaambia Dunia nzima Mji mpya unakuwa mzuri kuliko Mji wa zamani, lakini Zanzibar kinyume yake, Kwahani ni nzuri kuliko Kwarara kwa sababu Kwahani imepangika ukikaa jaani Mwembenjugu unaona mpaka ukuta wa Kariakoo, lakini leo Kwarara hakupitiki na ni Mji mpya usiokuwa na umri wa zaidi ya miaka ishirini.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache mwisho naomba kusema kwamba umefika wakati sasa Gander alisema; *'Actions speak louder than wards'* umefika wakati wa kuchukua hatua sio tena wakati wa kusema, kama tutaendelea kuendesha Serikali kwa kuoneana muhali bila ya kuchukua hatua hatutofika. Sijataka kusema kuhusu Hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini sijapata kuona pahali pana watendaji wajeuri, wasiokuwa na maadili ya utendaji kazi kama hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mimi binafsi naandika *document* ya kusema kwamba Mnazi Mmoja watendaji Manasi na Madaktari umefika wakati tuwape leseni, ili akifika mtu akifanya

mambo yasiyotakiwa yanayokwenda kinyume na kazi yake tumnyang'anye leseni ili asiweze kufanya kazi pengine, nitatoa mfano, juzi mtu mmoja alimnyanyasa mtu akamwambia sikiliza bwana, mimi nina elimu yangu na taaluma yangu nikifukuzwa Mnazi Mmoja nitakwenda kufanya kazi kwengine, mtendaji wa Mnazi Mmoja anamtolea jeuri mgonjwa.

Kwa hivyo, umefika wakati tufanye kama nchi za wenzetu wanavyofanya, wafanye kwa leseni ili tukimfutia leseni akae asifanye kazi tena mpaka atakapofunguliwa leseni yake. Kwa utaratibu huu tunaweza tukapata watendaji wa Mnazi Mmoja wakawa angalau wana heshima na adabu kwa kifupi.

Mhe. Spika, mimi binafsi nipo ninafanya *research* kuleta *document* ya sheria hapa ya pendekezo la kwamba tuwape leseni watu wale ili waweze kutuhudumia vizuri kama sheria yao inavyowataka. Baada ya hayo machache na mimi napenda kuchukua fursa hii kuipongeza sana hotuba hii ya Makamu wa Pili wa Rais na kuiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia na kumtakia kheri Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, aendelee kutuhudumia, lakini pia namualika rasmi katika Mkoa wa Magharibi Jimbo la Welezo aje kutembelea mwenyewe aone kwa macho jinsi gani wananchi wanavyopata shida, miundombinu mibovu na ndiko kwahali ambako kunaishi watu wengi.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana nakuombea dua na wewe Mwenyezi Mungu akupe uhai mrefu wenye manufaa na wewe ili uweze kutuelimisha kutoa hutuba kama hizi katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba kuwasilisha kwako. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Hassan, nakushukuru sana, sasa waheshimiwa Wajumbe, tunaanza na Manaibu Waziri, kwa hivyo, Naibu Waziri wa mwanzo atakuwa ni Naibu Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji Mhe. Mohammed Ahmada na baada ya hapo atafuata Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Mhe. Lulu Msham, baada ya hapo atakuja Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Mmanga Mjawiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi jioni hii ya leo kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa mwaka huu wa Fedha 2016/2017.

Nami nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, na vile vile kuchukua nafasi hii kumpongeza msaidizi wake wa karibu Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, pamoja na watendaji wake wote kwa kuweza kutuwasilishia hotuba hii ya Makisio ya Bajeti ambayo kusema la kweli imesheheni mambo mengi tu yenye kuonyesha mwelekeo na mustakbali mzuri wa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kutekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya CCM kama tulivyoahidi kwa wananchi wakati wa kampeni, katika sehemu tofauti.

Mhe. Naibu Spika, nina imani kubwa sana Wawakilishi wenzangu watakubali na kuiunga mkono hotuba hii bila ya pingamizi yoyote, kwani kama tunavyojua Serikali yetu ina nia ya dhati kabisa katika kuwaletea wananchi wake maendeleo bila ya kujali itikadi zao za kisiasa, bila ya kubagua kijinsia, bila ya kubagua rangi, bila ya kukagua dini. Sote ni mashuhuda kwa jinsi gani Serikali yetu hii ilivyoeneza huduma muhimu za jamii katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu, mimi napenda kuwaeleza Waheshimiwa Wawakilishi kwamba, lazima tukiri kwamba licha ya changamoto tofauti zinazokubaliana nazo sasa katika uendeshaji wa Serikali yetu.

Lakini tumepiga hatua kubwa sana kimaendeleo na nchi nyingi sana duniani zinatolea mfano nchi yetu ya Zanzibar katika maendeleo ya aina tofauti; tumefanikiwa kujenga vituo vya afya sehemu tofauti na vile vile kufikia malengo ya *millennium* kwamba vituo vya afya viwepo katika maeneo yasiyozidi kilomita tano, nasi hilo tumepiga hatua kubwa sana na wawakilishi leo ni mashuhuda.

Nina imani kubwa sana si katika vituo vya afya tu, lakini vile vile maskuli tunaona jinsi skuli zetu zilivyokuwa nzuri zenye kila aina ya vitendea kazi na ambavyo vimepigiwa mfano, ndio maana *World Bank* na wafadhili wengine wameendelea kutuchangia na hivi sasa washatuchangia katika hatua kuwa sana kujenga shule zenye ghorofa na za kisasa kabisa ambazo huzikuti sehemu nyingi za Nchi ya Afrika ya Mashariki. Ni hatua kubwa sana, inabidi sisi kama Wawakilishi tukubali kwamba Serikali yetu imefanya mambo mengi na hatuna budi kuiunga mkono, sio katika mambo ya mashule tu, lakini vile vile ukija katika mambo ya barabara miundombinu ya kiuchumi nakusudia Serikali yetu imepiga hatua kubwa sana na ya kupigiwa mfano na nina imani kubwa sana.

Hata hizo changamoto zilizokuwepo hivi sasa kama alivyozungumza Mhe. Hassan Hamis Hafidh ya kusema kwamba Halmashauri yake hakuna miundombinu ya jamii wala ya kiuchumi, naamini kwamba kama ingekuwa hakuna miundombinu ya kiuchumi na kijamii basi ile Halmashauri yake

isingepandishwa kiwango na kuwa Manispaa, huwezi kupandishwa Manispaa bila ya kuwa na vigezo maalum na viwango maalum katika huduma za kijamii na huduma za kiuchumi.

Namuomba sana Mhe. Hassan Hamis Hafidh, akubali hilo na ajue kwamba Serikali yake au Serikali yetu iko makini katika kuhakikisha kwamba huduma za kijamii na za kiuchumi zinafikiwa katika maeneo yote kwa muda ambao fedha zitatuwezesha kufanya kazi hiyo basi tutafikisha huduma hizo bila ya kujali kwamba huu ni Mkoa gani au sehemu gani, Serikali haibagui wala haichagui katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, nije sasa katika masuala ya barabara kama walivyochangia wajumbe, napenda kuwaarifu kwamba tuna nia ya dhati kabisa kuhakikisha kwamba barabara zote hizi zitakuwa zenye kupitika ima kwa lami au kifusi pale uwezo ambapo nchi yetu itakuwa nao basi hatutosita kufanya hivyo, ilani yetu imeelezea barabara gani tunataka kuzijenga na nina imani kabisa kwamba katika kipindi hichi cha miaka mitano tutazimaliza barabara hizo na kutakuwepo na barabara nyengine pia tutazifanyia kazi ili wananchi wetu wapate huduma nzuri za kijamii na kiuchumi na waweze kurahisisha kupata maendeleo yao ambayo ndio dira yetu ya maendeleo ya 2020 ambayo tunataka twende huko kuhakikisha wananchi wote wanaondokana na umasikini na wanaenda katika uchumi wa kipato cha kati.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii vile vile kuwatoa shaka wawakilishi kwamba nia ya serikali si kwamba inataka kubagua watu wake, mimi mwenyewe nilikuwa Pemba hivi karibuni niliona kuna baadhi ya madereva walichochewa kufanya migomo, lakini baada ya kukaa nao vizuri wakatueleza kwamba migomo ile haiwasaidii wao wala kwa nchi yetu na wengine wamekiri makosa yao na wameomba radhi kabisa kwamba kweli kosa tulilolifanya ni kosa la kisheria na hatutorejea tena.

Sisi tumewaambia kwamba sheria itachukua mkondo wake kwa wale wote watakaovunja sheria hasa za usalama barabarani ikiwa kwa njia ya migomo au kwa njia yoyote. Kwa hiyo, nachukua nafasi hii kuwaomba sana madereva na wale wote ambao wanaohusika na sekta yoyote ile wasikubali kuingizwa katika vishawishi vya migomo, kwani hivyo havitawasaidia wao wala familia zao, wala nchi kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, ningependa kuzungumzia kwa ufupi tu suala alilolizungumzia Mhe. Mohammed Said Mohammed. Mimi nichukue nafasi hii nimwambie kwamba nchi nyingi za wahisani wanaendelea kutusaidia katika

sekta mbali mbali za kiuchumi. Dalili hii inaonesha kwamba Zanzibar inakubalika kimataifa na wahisani tofauti wanatuchangia katika miradi mbali mbali ya kimaendeleo.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais tumeona kwamba wahisani watatoa kwa njia ya ruzuku na kwa njia ya mikopo pesa zisizopungua bilioni 8.6 ili kuonesha wazi kwamba Zanzibar inapokea misaada tofauti kutoka kwa wahisani wake na vile vile imeaminika kibajeti hadi kupewa mikopo tofauti.Mimi napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza sana wale wahisani wetu wote wanaotuchangia katika miradi yetu ya maendeleo na wale ambao hawakubahatika kutuchangia safari hii nina imani kubwa kwamba mwakani watatuchangia kwani wataziona juhudi zetu za kutaka kuwaletea maendeleo wananchi wetu bila ya kujali itikadi zao za kisiasa.

Mhe. Naibu Spika, sitokuwa mwizi wa fadhila bila ya kumtaja Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wetu. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza kwa uvumilivu wake na busara zake na hekima kubwa katika kuongoza nchi yetu bila ya yeye nina hakika kabisa nchi yetu hii ingeyumba. Kwani tunaona viashiria vingi vimetaka kutokea vya watu kutaka kuhatarisha amani na utulivu wa nchi yetu, lakini kwa uongozi wake wa busara na makini hali hiyo imeweza kutulia na hivi sasa nchi yetu ni salama na watu wanaendelea kufanya kazi zao za kila siku bila ya kubughudhiwa. Kama kuna vitendo au viashiria vyote vya kuhatarisha amani nina imani kwamba vitendo hivyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar havitoviachia bali itahakikisha kwamba vinachukuliwa hatua za kisheria kwa wale wote watakaotaka kuleta tatizo au kukiuka misingi yetu ya Katiba na sheria za nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nchi yoyote ya demokrasia inaamini kwa utawala bora, utawala bora ni kuhakikisha kwamba hata wale wachache wanasikilizwa, sisi hata wale wachache tutawasikiliza na wengi tutawaunga mkono na tutafanya nao kazi kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, kuna jambo hapa liliuliziwa na Mhe. Mohammed Said Mohammed, kuhusu Mhe. Makamu wa Kwanza Mstaafu kutumia barabara ile ya Ikulu. Nijuavyo mimi barabara hufungwa kwa mujibu wa vyombo vya usalama vya nchi yetu vinavyoamua. Barabara ya Ikulu imefungwa kutokana na sababu maalum na vile vile barabara hiyo huruhusiwa kupita watu kwa sababu maalum.

Kwa hiyo, iwapo Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu ametumia njia hiyo kama tunavyojua sisi viongozi wetu wastaafu wanakuwa wanalindwa kisheria

na vile vile wanakuwa wanawekewa viguzo sehemu ambazo wanapita. Nina imani kabisa Jeshi la Polisi lilikuwepo na linajua kama amepita njia hiyo basi kafuata taratibu. Na iwapo hakufata utaratibu basi ninamuhakikishia Mhe. Mwakilishi, tutaangalia hatua gani za kisheria zichukuliwe. Lakini nina imani kabisa Jeshi la Polisi linafuata Sheria za usalama barabarani katika kuhakikisha taratibu zote zilizowekwa zinafuatwa.

Mhe. Naibu Spika, sasa nichukue nafasi hii na mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Malindi kuchukua fursa hii kuwapongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na wasaidizi wake kwa hotuba hii ya bajeti waliotuletea leo. Kusema la kweli naomba sana waheshimiwa wenzangu waiangalie vizuri baada ya hapo waitafakari, waipitishe kwani hii ndio hotuba ya muhimili wa nchi yetu na kama yeye akiwa kiongozi na msimamizi mkuu wa shughuli za serikali basi tumuamini na sote tumuunge mkono ili hizi bajeti nyengine zitazokuja za mawizara nazo zipite bila ya wasi wasi wowote.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Malindi kuiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa asilimia mia kwa mia, na ninawaomba wenzangu vile vile waiunge mkono ili tuendelee kuwa na amani na utulivu na vile vile maendeleo ya nchi yetu. Baada ya kusema hayo, ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Manaibu Waziri na Mawaziri naomba sana tu-*focus* moja kwa moja kwenye kujibu masuala na kuikubali hoja, kwa sababu muda hautatosha. Kwa hiyo, wakati tunajieleza nyinyi kazi yenu sasa hivi ni kujibu zile hoja za wajumbe ambazo wamezitoa. Kwa hiyo, naomba sana tu-*focus* huko zaidi. Nashukuru.

Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipatia nafasi hii kuweza kujibu hoja za wajumbe waliochangia.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja kwenye hoja aliyochangia Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) kuhusiana na vijana kupatiwa nyenzo za kuvulia. Mhe. Naibu Spika, kwenye hili wizara yangu imejipanga kuimarisha sekta ya uvuvi, ikiwemo uvuvi wa bahari kuu pamoja na kutoa mafunzo maalum kwa wavuvi na kutengeneza ajira kwa vijana hususan wale ambao wanaishi kwenye maeneo ya bahari.

Mhe. Naibu Spika, pia, Mhe. Shihata, alizungumzia suala la maboti, aliuliza maboti yale yako wapi? Mhe. Naibu Spika, maboti haya ni kweli serikali ilitoa

maboti hayo na baada ya kumalizika kwa Mradi wa *MACEMP* wale wananchi walishindwa kuyahudumia maboti yale na kidogo kidogo wakaanza kuyauza. Mhe. Naibu Spika, namuomba mheshimiwa anipe muda ili niweze kujua maboti mangapi yameuzwa na maboti mangapi bado tunayo.

Mhe. Naibu Spika, pia, naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar, alitoa ushauri kwamba kilimo kipewe kipaumbele. Mhe. Naibu Spika, kilimo tumekipa kipaumbele, wizara yangu kupitia Idara ya Kilimo imejipanga kununua matrekta 100 kutoka katika Kampuni ya *Mahindra and Mahindra* ya India. Vile vile, hayo matrekta ambayo tunayo sasa hivi yameshashughulikiwa na kufanyiwa matengenezo na kuwa tayari kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo na tutaanza na kilimo cha alizeti, kunde na kuendelea na kilimo cha mpunga.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, serikali hainunui mchele Ulaya, kwani biashara hii ni biashara huria ambayo ina wafanyabiashara tofauti. Na kuhusiana na mabonde ya mpunga kulimwa miwa, mabonde haya ni kweli yanalimwa miwa lakini sio mabonde yote ni baadhi tu ya vieneo na hilii ni wakulima wenyewe wameingiana mkataba na Kiwanda cha Miwa.

Mhe. Naibu Spika, nategemea nimejibu hoja zetu Waheshimiwa Wawakilishi, kama yule ambaye yupo hajaridhika basi naomba asubiri siku yetu ya bajeti ili tuweze kumtolea ufafanuzi zaidi. Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono asilimia kwa mia hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.(*Makofi*)

Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii kujibu kwa uchache sana baadhi ya masuala na hoja ambazo zimetolewa na wawakilishi wenzangu, na baadhi ya hoja atakuja kujibu waziri wangu hapo baadae.

Mhe. Naibu Spika, ningependa kujibu hoja inayohusiana na tathmini katika vituo vya amali. Ni kweli kwamba tathmini ni jambo muhimu sana na ndio mwelekeo wa Wizara ya Elimu kwamba kila jambo katika Wizara ya Elimu linafanyiwa tathmini za aina tatu; Tathmini ya awali, tathmini ya kati na tathmini ya mwisho. Halafu pia tunafanya tathmini ya ujumla ya mradi wenyewe. Kwa hivyo, tathmini ambazo zimefanyika mpaka sasa zinaonesha kwamba bado jamii ya Zanzibar inahitaji kuwepo kwa vyuo vya amali, na kwa maana hiyo wizara itaendelea kujenga vituo vya amali kadiri uwezo utakapopatikana na wafadhili watakapopatikana.

Jambo hili linatokana na ukweli kwamba hapo awali idadi ya wanafunzi tulipoanzisha vituo hivi ilikuwa ni kubwa zaidi kuliko hivi sasa na ile

uliyosema utafiti uliofanya tukaona kwamba kuna kupungua kwa wanafunzi ambao kwa kiasi fulani kunasababishwa na wazazi kutoelewa umuhimu wa elimu ya amali. Kwa hivyo, wizara itaendelea kuwaelimisha wananchi umuhimu wa elimu hii ya amali na wakishaelewa tunaamini kwamba kutakuwa na idadi kubwa ya wanafunzi watakaojiunga na vyuo hivi.

Aidha, wizara inaamini kwamba wakati wa utekelezaji wa Sera mpya ya elimu itapofikia vijana wetu kufikia darasa la kumi au darasa la kumi na mbili pale sasa tutakuwa na mikondo miwili; watakaokwenda katika fani ya *academic* na watakaokwenda katika fani hii ambayo tunaita vyuo vya amali. Pale tutawatangaza wote, wizara itawachagua na itatangaza hawa watakwenda katika mrengo fulani na hawa watakwenda mrengo fulani, pale ndipo itapoonekana umuhimu wa vyuo hivi vya amali katika kujenga ajira na katika kujenga mwamko wa vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine hili ambalo linazungumzia kuhusu Bodi ya Mikopo, hili limezungumzwa na Mhe. Mattar Mwakilishi wa Jimbo la Mgogoni. Ni kweli kwamba vijana wetu wanapata usumbufu kidogo katika suala hili la kupata malipo yanayohusiana na mikopo. Lakini pia ningependa mheshimiwa yeye na wajumbe wengine waelewe kwamba Bodi ya Mikopo inatoa zaidi msukumo wake na mkazo wake katika ada (*tuition fees*) hii ndio msisitizo zaidi na baadhi ya mazingira hutoa pia posho ya kujikimu. Kwa hivyo, mpaka sasa tunadaiwa na wanafunzi kutoka vyuo vya Bara *semester* moja tu, wala sio tatu kama ambavyo mwakilishi alisema na *semester* ya pili. Tumelipwa *semester* ya kwanza mwaka huu, basi bado *semester* ya pili. Kwa hivyo, Bodi ya Mikopo itaendelea kulipa hatua kwa hatua kadri uwezo utakavyopatikana.

Mhe. Naibu Spika, mantiki yakuwalipia posho na *tuition fees* inatokana na ukweli kwamba kama wote tutawalipia *hundred percent* watakaosoma ni wachache mno kwa kweli, na lengo letu ni kusomesha watu wengi kadri inavyowezekana.

Mhe. Naibu Spika, kuna hoja hii iliyotolewa pia na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Bumbwini na Mhe. Bahati wa Chambani, kuhusu suala la ajira. Ni vyema Mhe. Naibu Spika, wawakilishi wakaelewa kwamba mfumo wa uajiri sasa hivi katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar unasimamiwa na Tume ya Utumishi Serikalini, Wizara ya Elimu tunapeleka tu mahitaji yetu. Tume ya Utumishi ya Uajiri Serikalini inafuata misingi yake ya ajira na wanatizama zaidi sifa na uwezo na mahitaji.

Kwa hivyo, mpaka sasa hatujawa na sera katika ajira yetu ya upendeleo katika maeneo fulani, kwa hivyo, nafasi itakapopatikana zinatangazwa na wenye sifa wanaomba. Lakini pale inapotokea haja ya kufanya hivyo katika maeneo mahsusi taarifa hupelekwa kwa masheha na masheha wakatoa maoni juu ya watu kama wanawaelewa kweli au la wanatoka katika shehia zao au laa. Kwa hivyo, ikiwa sheha atatoa taarifa ambazo si sahihi basi tunaomba wananchi watueleze ili kuweza kuchukua hatua zinazofaa.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala hili ambalo liliulizwa juu ya walimu wetu ambao tulikuwa tunawaendeleza mpaka kufikia cheti, kupitia njia ambayo tunaita elimu masafa (*distance learning*). Ni kweli wahitimu hao tunao na sasa hivi tunaendelea kuwaingiza katika mchakato wa kuwarekebishia mishahara yao pale hali ya fedha itakaporidhisha. Lakini wizara inajitahidi kufanya kila linalowezekana ili kurekebishwa mishahara yao. Kwa hivyo, tunaomba wawe na subiri kidogo mchakato huu unaendelea.

Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya Mhe. Mattar, suala la kusheheni kwa masomo katika mitaala yetu. Sisi kitaalamu hatusemi kusheheni, kwa sababu masomo hayo au wingi wa masomo hayo umetokana na utafiti uliofanywa wa kuwahoji wadau wote wa elimu Zanzibar na wao waliweza kuthibitisha kwamba masomo hayo ni kiasi kuweza kusomwa na wanafunzi wetu. Lakini pia suala hili ni suala la kisera hatuwezi kulibadilisha mara moja, na kwa kuwa suala la sera na sera ina muda wake wa kufanyiwa tathmini basi wakati utapofika wa kufanya tathmini suala lako litazingatiwa.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine ambalo alilizungumza vile vile mheshimiwa huyo nalo ni suala la kutilia mkazo lugha ya Kiswahili. Vile vile, ni suala la kisera, Sera ya elimu inaeleza wazi kwamba katika skuli za maandalizi na msingi mpaka darasa la nne, Kiswahili kitatumika kufundisha masomo yote, na katika ngazi nyengine Kiswahili kitabakia kama somo, pia ni suala la kisera hatuwezi kulichukua maamuzi haraka mpaka muda wa kufanya tathmini utapofika tutatathmini na tuone wadau watasemaje juu ya masuala haya ya kisera.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala jengine ambalo liliulizwa nalo ni suala la Mhe. Mattar, juu ya umalizaji wa vituo au umalizaji wa skuli ambazo au madarasa ambayo yamejengwa kwa nguvu ya wananchi. Suala hili lina mpangilio wake mzuri katika Wizara ya Elimu kwamba wananchi baada ya kufanya kazi ya kujenga madarasa ikifikia ngazi fulani wanaikabidhisha kwa maandishi Wizara ya Elimu ili kumalizia sehemu iliyobakia.

Lakini pia Wizara ya Elimu ina utaratibu kwamba umalizaji wa madarasa kama haya hutegemea pesa za miradi zinavyoingizwa katika wizara, lakini pia unategemea wafadhili. Hivi karibuni tumekubaliana au tunatarajia kukabiliana na shirika moja ambalo limekubali kufanya ukarabati umalizaji wa baadhi ya skuli, kwa hivyo, huenda pengine skuli yako ikazingatiwa muda utapofika.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la nyumba za walimu, nalo pia tutalizingatia labda linaweza kuingizwa katika utaratibu ule ule wa ukaratabati wa mali na nyumba za wizara. Na kwa kumalizia suala la Mhe. Ussi Yahya Haji kuhusu utayari wa serikali katika kusomesha vijana katika fani ya mafuta na gesi. Kwa hakika jambo hili linaeleweka na katika vipaumbele vya serikali vilivyotolewa na Tume ya Mipango, fani ya mafuta na gesi imepewa kipaumbele cha juu kabisa. Kwa hivyo, serikali itaendelea kuwafadhili vijana wetu ambao wanasoma katika fani hii na fani nyengine ambazo zimepewa kipaumbele. Kwa hivyo basi, namtoa wasi wasi Mhe. Ussi Yahya, juu ya suala hili.

Mhe. Naibu Spika, katika azma yetu ya kutoa elimu bora Mhe. Waziri amekuja na kauli mbiu yake ambayo tunaitumia sana kule wizarani, nayo ni "elimu bora kwanza". Kwa hivyo, tunawasihi na tunawaomba wadau wote wa elimu watilie mkazo suala la elimu bora ambayo ndio itatusaidia katika kujenga jamii bora iliyoelimika na kuerevuka na tutapofikia hatua hiyo, twabaan natarajia kipindi kifupi tunaweza kufikia hatua hiyo, basi jamii yetu itakuwa inaishi kwa amani na utulivu zaidi kuliko hivi sasa ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kuunga mkono hotuba hii na endapo tunataka na sisi wawakilishi sote majina yetu yakumbukwe kwa michango yetu, basi tuiunge mkono hotuba hii. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kuniona na kunipa nafasi hii ya kuweza kufafanua kidogo zile changamoto ambazo waheshimiwa wamezichangia wakati walipokuwa wakichangia hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza naomba nianze na mchango aliochangia Mhe. Shehe Hamad Mattar, kwamba kituo cha afya cha Finya kukosa huduma ya uzazi kutokana na kukosekana kwa nyumba za *staff*.

Mhe. Naibu Spika, serikali kupitia Wizara ya Afya ililiona tatizo hili na kwa nguvu zote iliamua kulifanyia suluhisho kwa kutekeleza Sera ya Afya ya mwaka 2011 inayosisitiza kutoendelea kujenga vituo vipya vya afya na badala yake kuviimarisha vilivyopo kwa kuvifanyia matengenezo stahiki na kuongeza vifaa na kujenga nyumba za wafanyakazi. Katika kipindi hiki cha 2016/2017,

serikali kupitia Wizara ya Afya itajikita zaidi katika kutekeleza hilo. Nawaomba waheshimiwa wale wote ambao wamechangia kuhusu changamoto hii katika vituo vyao ya kukosa nyumba za wafanyakazi, hili litapata suluhu katika kipindi hiki, naomba wawe watulivu lakini pia wizara tunaomba mashirikiano yao.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la vyandarua ambalo pia alichangia Mhe. Shehe Hamad Mattar, kwamba vyandarua vinavyoletwa kwa misaada vina tatizo la muwasho. Mimi nataka nimueleze tu kwamba vyandarua hivi vinakuwa viko *treated* ili kuweza kumuangamiza mbu wa malaria asimuathiri binadamu. Dawa hii inachukua kipindi kisichopungua miaka mitano hadi sita haiishi ndani ya chandarua, kwa hiyo, ni dhahiri kwamba dawa inakuwa ni nyingi.

Serikali kwa kuwajali wananchi wake nawahakikishia kwamba haipokei tu vyandarua na kuvisambaza kwa wananchi, bali huvifanyia utafiti yakinifu na kuona kwamba dawa ile iliyowekwa katika vyandarua hivyo haiwaathiri binadamu kiasi kikubwa au haiwaathiri kabisa, bali inawasaidia kumuangamiza mbu wa malaria. Ninawashauri wananchi wafuate maelekezo yanayotolewa, wawe na tahadhari zaidi kwa watoto wachanga, lakini wasiendelee kuviogopa na kutokuvitumia vyandarua hivyo. Lengo na madhumuni ya vyandarua hivyo ni kutokomeza malaria na hali hii imeshafikia katika hali nzuri na ndio maana mara nyingi vyandarua hivi inakuwa wengine vinawawasha lakini wengine haviwawashi kwa sababu dawa ile haina athari kubwa kwa binadamu.

Tatizo la upungufu wa madaktari, hili lilichangiwa na Mhe. Mtumwa Peya Yussuf. Mimi naomba nimueleze kwa niaba ya wananchi kwamba, Wizara ya Afya, *strategic plan* ya wizara kwa mwaka 2016/2017 ni kulifanyia kazi kwa nguvu zote tatizo hili la uajiri wa madaktari, Inajipanga kuajiri madaktari wenye sifa katika vituo vyote na kawaida kila mwaka huwa inaajiri madaktari. Tuna madaktari wengi ambao wako katika vyuo tunawasubiri wamalize lakini wengine wameshamaliza wote hawa tutajitahidi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ili waajiriwe katika vituo vyetu waweze kufanya kazi kwa bidii.

Suala la kuchelewa na kuondoka mapema kazini pia alilichangia Mhe. Mtumwa Peya, kwa baadhi ya wafanyakazi. Mimi nasema huu ni ukosefu wa nidhamu kazini na kwa bahati nzuri wafanyakazi wetu serikalini wanaongozwa na kanuni na sheria za utumishi. Tunaomba mashirikiano ya wananchi kupitia wawakilishi wao waliomo katika Baraza hili ili kututhibitishia ni wafanyakazi gani wenye tabia hizo. Hatua za kisheria zitachukuliwa zidi yao, kwa sababu lengo la serikali ni kuhakikisha huduma za serikali zinatolewa vizuri kwa wananchi na sio kubabaisha babaisha.

Kuhusu kuhamisha kambi ya Kipindupindu katika sehemu za maeneo ya wananchi. Suala hili huwa linachangiwa mara kwa mara hasa na Mhe. Miraji Khamis Mussa pamoja na Mhe. Machano Othman Said. Mimi naomba nilitolee ufafanuzi kidogo kwamba kambi za Kipindupindu mara nyingi kama mmepeleleza zinawekwa katika sehemu ambazo zinaathirika na Kipindupindu, haiwezekani na haipendezi hata kidogo tuhamishe kambi za Kipindupindu ilioko Chumbuni mfano ipelekwe Mombasa au sehemu nyengine yoyote ya mbali, wakati wagonjwa wa Kipindupindu wengi wanatokea katika maeneo yale. Wao wenyewe wananchi wakae wafikiri kwamba mgonjwa wa Kipindupindu yuko *serious* anatolewa Chumbuni, Daraja Bovu au katika maeneo yale na kumkimbiza katika sehemu ambayo ni mbali, kweli tutafika naye yuko hai mgonjwa huyo? Mimi nahisi mgonjwa huyo tukifika naye katika kituo cha Mwanakwerekwe au kwengine atakuwa ameshapoteza maisha na lengo ni kumsaidia, ni kum-*save* ili aendelee na maisha.

Kwa hiyo, mimi nawaomba kwa kupitia suala hili na kwa sababu limeshasemwa mara nyingi, wizara italiangalia kwa kina na ifanye utafiti kwamba athari za kuondosha kituo pale kikawekwa mbali na wagonjwa kukimbizwa mbali, au athari za kukibakisha na wagonjwa wa kawaida ambao sio wa mripuko wa Kipindupindu kufuata huduma katika sehemu nyengine bora ni ipi. Naomba hili Mhe. Mwakilishi, aliangalie vizuri lakini na wizara itakaa iliangalie baadae tutapata *solution* ya pamoja.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala moja linalohusu kubaguliwa katika huduma za afya na kubaguana kwa wafanyakazi kwa ajili ya siasa. Mimi nawaomba niwahakikishie wananchi kupitia Baraza hili kwamba, serikali haina dhamira ya kuwabagua wananchi wake katika huduma yoyote sio ya afya tu. Kwa hivyo, kama kuna wafanyakazi ambao wanafanya kitendo hiki, wanafanya makosa makubwa kisheria na wizara itakapowabaini na tunaomba mashirikiano yenu ya kutosha ili tuwabaini ambao wanabagua au wanatoa huduma kwa ubaguzi huyu ndiye, huyu siye, wananchi wote wanastahili kupata huduma za afya na huduma nyengine zozote ndani ya nchi yao, tunawaomba mtujuilishe kwa njia yoyote na tutawafanyia kazi na sheria zitafuata mkondo wake, hili halitovumiliwa katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mwisho, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wete na kwa niaba yangu binafsi, naomba nichukue nafas hii kuunga mkono hotuba hii asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Said Soud Said (Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum, Uteuzi wa Rais): Mhe. Naibu Spika ahsante, awali ya yote napenda nitoe shukurani kwa

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuboresha Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na kufanya serikali hii kuwa ni ya vyama vinne badala ya viwili kama ile iliyoondoka.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia, natoa shukurani zangu kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kutuongoza vyema na *inshaallah* ataendelea kutuongoza vyema kwa miaka mitano ijayo.

Baada ya hapo ningetaka niseme kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni ofisi kubwa inayozingatia mambo yote ya Zanzibar zikiwemo sheria na taratibu za kuishi watu katika visiwa hivi vya Unguja na Pemba. Kama tunavyoelewa Zanzibar ni nchi inayofuata mfumo wa vyama vingi vya siasa na hakuna njia mbadala ya kupata serikali zaidi isipokuwa uingie katika uchaguzi. Kwa maana hiyo ni kwamba, sasa vyama vingi vilivyopo Zanzibar au Tanzania, Zanzibar imekuwa ni sehemu moja ya kuashiria fujo katika utendaji wa vyama hivi.

Mhe. Naibu Spika, nashangazwa sana na utaratibu uliozuka wa baadhi ya Chama cha Siasa kuanzisha migomo. Taathira ya migomo ni kubwa sana, kwa sababu sasa hivi imefikia watu kutokuuziana biashara, watu kutokupanda magari, watu kutokuvushana, yaani kupanda dau kutoka sehemu moja kwenda nyengine, watu kutokuzikana na hatimaye hata kususiana kwenye misikiti. Ni jambo la kusikitisha sana kuona kwamba hata maiti anasusiwa wakati hatapiga kura tena wala hatarudi katika ulimwengu huu.

Mhe. Naibu Spika, ni jambo la ajabu kuona kuna Chama cha Siasa kinachofanya wivu wa aina yake kuona kwamba sasa serikali imeundwa na inaendelea kuwepo, lakini pia namna ya kuweza kuifanya isifanye kazi yake ni kuanzisha chokochoko ambazo hazina maana katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Hili mimi nasema ni choyo cha kisiasa na kwa sababu gani ni choyo cha kisiasa? Kwa sababu wenzetu hawa walikuwemo kwa muda wa miaka mitano ndani ya Baraza hili, lakini hakuna siku sisi tuliashiria kwenda Mahakamani, wala *ICC*, wala kupinga Katiba, wala kufanya lolote, zaidi walikaa kwa muda wa miaka 20 mpaka wamemaliza juzi na hatuna lolote tulilokuwa tumewafanyia wao, kwamba labda wamekwenda kinyume au wanaendeshwa kinyume. Sasa inatushangaza sana kuona kwamba wanatokwa na denda baada ya kuona Serikali ya Umoja wa Kitaifa sasa inaendelea kuwepo.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ningetaka niseme kwamba kwa sababu vyama vingi vinaendeshwa kwa mujibu wa sheria, Sheria Nam. 5 ya mwaka 1992 ambayo

msajili wa vyama vya siasa ana mamlaka ya kukubali chama na kukifuta chama, sisi kama serikali tunamuomba msajili wa vyama vya siasa aende Pemba akafanye utafiti wa kina kabisa juu ya hoja ya Chama cha *CUF* jinsi wanavyoendesha siasa yao ya ubaguzi.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni Mwenyekiti wa Chama cha Siasa Tanzania. Kwa hivyo, utaratibu wa kuunda chama na taratibu za chama cha siasa nazielewa. Sasa chama hiki kimeshatoka nje ya reli na kwa sababu kimetoka nje ya reli pia kinahitaji kufutwa hakina haja ya kuwepo Tanzania hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ningetaka niseme kwamba, haiwezekani kwamba chama hiki cha siasa kiwepo katika nchi halafu kiweze kuanzisha mambo kama walivyoanzisha Burundi na Rwanda. Kwa sababu unapoleta masuala ya migomo taathira yake ni watu kuleta *Gorilla War*. *Gorilla War* ni vita vya wenyewe kwa wenyewe, hatimaye nchi hii itaingia katika fujo na sio lengo la Tanzania. Tanzania ni nchi ya amani na Zanzibar ni kisiwa cha amani, kwa hivyo, tunahitaji msajili achukue hatua za haraka juu ya suala hilo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, watu wengi katika visiwa hivi wamekuwa wakikejeli maendeleo yaliyofanywa na serikali hii kwa muda mrefu.Lakini namuomba Mhe. Wazirim ili aje awaeleze Wazanzibari nini amefanya Dkt. Ali Mohammed Shein kwa miaka mitano iliyopita. Kwa sababu sisi kama serikali tumeshagundua mambo mengi aliyoyafanya na sasa hivi nchi hii inaishi katika mazingira ya amani na utulivu.

Piam ningetaka nichukue nafasi hii kuwaeleza hawa ambao wana nia ya kwenda *ICC,* eti wanakwenda kushtaki amani na utulivu maana hakuna jengine lililotokea hapa zaidi ya amani na utulivu.Napenda kulithibitishia Baraza hili pamoja na mimi kama serikali kwamba tutakwenda pamoja *ICC* kwenda kutoa ushahidi wa matendo yao waliyoyafanya kabla na baada ya uchaguzi. Kwa sababu vitendo vyao havikuwa vya siri kila mtu aliviona na mimi mwenyewe nikiwa kama Mgombea wa urais katika visiwa hivi niligundua hayo. Hivyo, wanapokwenda *ICC* wasifikirie wanakwenda peke yao na wataulizwa peke yao, itabidi twende na tukaeleze yale waliyoyafanya.

Mhe. Naibu Spika, nashangaa sana kuona kiongozi kama huyu ambaye ameongoza nchi hii kwa muda wa siku nyingi, lakini leo amekuwa anababaika mpaka anafika hatua ya kwenda kushitaki Waziri wa Mambo ya Ndani, eti kwa sababu kaleta jeshi jingi la polisi na jeshi la wananchi. Sasa mimi namuuliza kama serikali, je, yeye alitaka watu wapigane na wauwane? Sasa hicho ni kitu ambacho kwa nchi yetu kimeipatia sifa maana hakuna hata paka aliyeuliwa

katika uchaguzi uliopita.Kwa maana hiyo, napenda kumthibitishia sisi kama serikali kwamba tuko pamoja na mapambano yake na yote anayoyafanya sisi tunayajua na tunayasikia na kwa vyovyote vile tutapambana naye. Napenda kuwaambia Wazanzibari kwa sauti kubwa kwamba hakuna namna yoyote ya kuiondoa serikali hii mpaka mwaka 2020. *(Makofi)*

Vile vile, nachukua nafasi hii kuwaambia kwamba, kwa wakati huu na wakati huo tunaoendelea nayo, kwa mivutano hii tunayokwenda nayo isiyokuwa na mwelekeo wala dira, CCM itashinda tena mwaka 2020. *(Makofi/Kicheko)*

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru sana Mhe. Said Soud Said kwa mchango wako mzuri na tumeona kwamba umetufurahisha sote na yale ambayo umeyaomba Mwenyezi Mungu ayatakabalie. Sasa tunaendelea na mchangiaji wetu Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira na baada ya hapo atakuja Mhe. Waziri wa Elimu na baada ya Waziri wa Elimu atafata Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na baadae tutampa nafasi Mhe. Waziri wa Habari Utamaduni, Utalii na Michezo. Mhe. Salama Karibu.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba mkuchangia na kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya hoja ambazo Waheshiwa Wawakilishi wamezitoa katika bajeti ya Wizara ya Nchi Afisi ya Makamu wa Pili ya Rais.

Naomba kuchukuwa nafasi kwanza kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa juhudi kubwa anayoifanya katika kusimamia taasisi zake. Lakini vile vile kumpongeza Mhe. Waziri wa Afisi hii pamoja na watendaji kwa kazi nzuri ambazo wameifanya katika kutuwasilishia bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, na mimi naanza kujibu hoja ambazo zimetolewa na baadhi ya Wajumbe wa Baraza lako hili. Naanza na ile hoja ya Mhe. Mtumwa Peya, ambayo ni lini kutakamilika ile miundombinu ya vile visima vyetu viwili vya Rasilhema ili maji yapatikane. Nataka kumuhakikishia kwamba eneo la Bumbwni kwa hivi sasa linapata maji safi na salama kutoka katika visima vyetu viwili ambapo kimoja kipo Kidazini na Makoba na ni kweli visima hivi havitoshelezi kutokana na ongezeko la mahitaji. Hivyo, serikali kwa kushirikiana Rasilhema imechimba visima viwili katika maeneo ya Misufuni na Makoba. Visima hivyo vitasaidia upatikanaji wa maji katika eneo hilo.

Baada ya kukamilika miundombinu yake basi maji safi na salama yatapatikana ya kutosheleza katika eneo hilo na naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Mwakilishi kwa juhudi zake ambazo anazifanya kuhakikisha kwamba visima hivyo vinakamilika kabla ya muda ambao katika Mpango kazi wetu tumeupanga kuvikamilisha na yeye amesema atashirikiana nasi ZAWA kuhakikisha visima hivi vinafanyakazi.

Lakini vile vile naomba pia nimjibu Mhe. Bahati Khamis Kombo wa Jimbo la Chambani suala lake la mgao wa maji katika eneo la Chambani. Naomba kumuhakikishia Mhe. Bahati Khamis Kombo kwamba baada ya kukamilika kwa kisima chetu kile cha Rasilhema ambacho kiko eneo la Chambani, wananchi wa eneo la Chambani watapata huduma ya maji safi na salama bila ya kuwepo kwa mgao. Sasa hivi maji yapo lakini kwa sababu maji yale hayatoshelezi na tunataka wananchi wote wafaidike na maji yake basi mgao ndio upo lakini tukeshakamilisha miundombinu ya kisima hiki kikubwa basi maji yatakuwa hayana tena mgao.

Lakini pia nimuhakikishie Mhe. Bahati Khamis Kombo kwamba, tuna mpango mkakati kwa mwezi mtukufu wa Ramadhani ambayo Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji kuendeleza nia yake na mpango wake kuhakikisha kwamba wanagawa maji katika mwezi wa Ramadhani katika yale maeneo ambayo yana uhaba mkubwa wa maji katika kipindi chote cha mwezi mtukufu wa Ramadhani. Napenda kukuhakikishia kwamba hakutotokea malalamiko kwa wananchi kwa tatizo la maji katika kipindi chote hiki kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, pia, naomba nijibu lile suali la Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), kuhusu Kwarara Madina. Katika eneo la Kwarara Madina tayari tumeshachimba kisima kwa kushirikiana na Rasilhema ambacho kitaendelea katika mwaka wa fedha ujao na pia naomba nichukuwe nafasi hii tena kumshukuru Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), kwa juhudi kubwa anazozichukuwa kwa kushirikiana na ZAWA kuhakikisha kwamba kisima hichi kinaanza kazi kabla ya mpango ambao tumeupanga. Tunamshukuru sana na *inshaallah* Mwenyezi Mungu atamjalia Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata). (*Makofi*)

Lakini pia naomba kupitia Baraza lako hili niwashukuru sana Waheshimiwa wa kwanza Mhe. Hassan Khamis Hafidh, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), Mhe. Mtumwa Peya Yussuf na Mhe. Omar Seif Abeid wa Konde Pemba kwa juhudi kubwa wanazozichukuwa kuhakikisha kwamba visima hivi vinakamilika kabla

ya wakati ule ambao sisi tumepaga kwa kushirikiana na sisi na kujitoa kwa hali na mali, nawashukuru sana.

Lakini naomba kwa suali la maji nimalizie kwamba serikali tuna mpango madhubuti katika kuhakikisha kwamba upatikanaji wa maji katika maeneo yote ya mjini na vijijini maji safi na salama kwa wananchi wetu yatapatikana ukimaliza ule mpango wetu na tuna mkakati mzuri ambao tunao.

Lakini naomba vile vile sasa hivi nijibu swali la Mhe. Mwakilishi ambaye aliuliza tatizo lilipo baina ya mgogoro uliokuwepo kati ya Kiwanda cha Sukari na wananchi. Kusema kweli mgogoro upo na serikali inajua, lakini hata hivyo wizara yangu imeanza kuchukua hatua za kulitatua tatizo hili kwa kulifanyia utafiti kwa maeneo yote yenye mgogoro, baada ya hapo eneo hilo litapimwa na yale maeneo yenye mgogoro ambayo wananchi wanadai tutaona kwamba kuna umuhimu wa kuwapa basi tutawapa. Lakini tunaangalia fursa ya ziada kwa wawekezaji ili waweze kukidhi mahitaji yao, kwa sababu kiwanda kile bila ya kuwa na mashamba au bila ya kupatikana kwa miwa basi hatuwezi kuendesha. Pia, serikali inaendelea na juhudi za kuelimisha wananchi juu ya sheria na taratibu za umiliki wa ardhi.

Vile vile, naomba nijibu swali la Mhe. Shaib Said Ali. Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba idadi ya watu inaongezeka kwa kasi wakati ardhi yetu haiongezeki. Ili kukabuliabna na changamoto hii hatuna budi ardhi tuliyonayo tuitumie kwa uangalifu mkubwa, kwa kulitambua hilo serikali tayari imeshaanda mpango mkakati wa matumizi ya ardhi. Katika mpango huo vipaumbele vimewekwa shughuli mbali mbali za wananchi uwekezaji, utunzaji mazingira na kadhalika. Kutoka na mpango huo serikali kwa kushirikiana na wananchi itahakikisha ardhi chache iliyopo itatumika kwa ufanisi kwa vizazi vya sasa na vizazi vijavyo.

Vile vile, suala la upatikanaji wa ardhi ambayo Mhe. Shaid Said Ali, aliuliza kwa kuzingatia uhaba wa ardhi na ongezeko la mahitaji wa ardhi kwa maakazi miundombinu na uwekezaji na kadhalika,Wizara imejiandaa kwa kutayarisha mpango madhubuti ya matumizi ya ardhi kwa ngazi mbali mbali ikiwemo ngazi ya Taifa, ngazi ya Mkoa na ngazi ya maeneo ya *local plan*. Sera ya maakazi inalenga kuwa na miji ambayo ujenzi wake ni wa kushikirikiana ambayo itawezesha wakaazi wake kuishi wafanyakazi kupumzika na kufanya shughuli nyengine katika masafa mafupi, hivyo, kuwezesha matumizi ya ardhi kidogo kwa makaazi na matumizi makubwa kwa shughuli za kilimo, Uwekezaji na maendeleo mengine ya nchi.

Vile vile, kulikuwa na masuala ya umeme ambayo yamejitokeza, naomba niyajibu kidogo kidogo ambayo Mhe. Mtumwa Peya Yussuf, aliuliza swala la kufikisha umeme katika eneo la Pangatupu. Mhe. Naibu Spika, azama ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kupeleka huduma za umeme katika vijiji vyote vya Unguja na Pemba na utekelezaji wake unafanywa hatua kwa hatua kwa mujibu wa hali ya kifedha inavyoruhusu.

Hivyo, katika mpango wa kupeka umeme vijiji vilivyosalia kijiji cha Pangatupu kimebahatika kusambaza umeme katika mpango wa mwaka ujao wa fedha 2016/17 na hili utekelezaji wake Mhe. Mwakilishi, tayari umeanza umeme wa Pangatupu hauwezi bila ya kupita Zingwezingwe. Zingwezingwe sasa hivi wameshapata umeme kufika bajeti ya mwaka uliopita na mwaka huu tutaendelea kuwapelekea Pangatupu.

Vile vile, kuna swali lilijitokeza kwa Mhe. Bahati Khamis Kombo na hii imetokana na wale watu ambao wanavunja nidhamu, lakini kwa kawaida kwam Shirika la Umeme kufanya ukaguzi wa wateja ambao wafanyakazi wanaofanya ukaguzi huo huonesha vitambulisho vya kazi kwa wateja wao wakaguzi. Hata hivyo, kumejitokeza tabia ya baadhi ya watu kujifanya wafanyakazi wa *ZECO* na kuwashangaza wananchi. Hivyo, tunatoa wito kwa wananchi kutokubali kufanyiwa ukaguzi na watu ambao hawajaonesha kitambulishi halali cha umeme, na hili baada ya kujitokeza lile suala alilolizungumza Mhe. Bahati Khamis Kombo, tumeona kwamba inawezekana watu hao si wafanyakazi wa Shirika la Umeme, lakini wale watu ambao si waadilifu, kwa hivyo, wanaweza kutumia mbinu na hila katika ku-*harass* watu, lakini linafanyiwa kazi.

Lakini vile vile kama kuna wafanyakazi wa Shirika wa Umeme wanafanya kazi hiyo kinyume na utaratibu basi hatua kali za kisheria zitachuliwa kwani suali la uwajibikaji na uadilifu ndio mipaumbele chetu na wasiweza tumesema watupishe.(*Makofi*)

Vile vile, kulikuwa na swali la Mhe. Mtumwa Peya Yussuf, katika maeneo ya Umwagiliaji maji. Lakini nataka kumuhakikishia Mheshimiwa kwamba katika maeneo ya kilimo ya umwagiliaji maji umeme upo wa uhakika na wizara yangu kupitia Shirika la Umeme haina taarifa kwa kuwepo kwa hitilafu za kiumeme katika maeneo ya umwagiliaji. Aidha, kama kuna maeneo mengine ya umwagiliaji maji ambayo huduma ya umeme haijafika, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme itawasiliana na wahusika kwa ajili ya kupatia ufumbuzi tatizo hili.

Naomba nitoe wito kwa Mhe. Mwakilishi na watu wenye maeneo hayo kama kuna tatizo na kama kuna sehemu haina umeme ambayo wizara yangu kwa sasa haijui katika kumbukumbu zake basi tunaomba mtufahamishe.Vile vile, Mheshimiwa Mwakilishi wa Kiwani alizungumzia maeneo ambayo bado hayajafika huduma za umeme.

Naomba kuhakikishia Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, kwamba ni Shehia chache sana ambazo sasa hivi hazijafika umeme, lakini Shehia karibu nyingi zimeshafika umeme kwa asilimia 86% kwa Pemba tumebakisha tu Minazini na kisiwa cha Fundo ambacho hakijafika umeme na kwa Zanzibar kuna maeneo ambayo yameibuka ni maeneo mapya ambayo Mheshimiwa mmoja alisema ni maeneo yanayoishi watu wengi zaidi ya Magharibi. Lakini wizara yangu kwa kushirikiana na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi basi itahakikisha kwamba katika maeneo hayo pia umeme unafika kwa muda mfupi sana. (*Makofi*)

Lakini vile vile kulijitokeza swali la Kwarara Madina la Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata), lakini tunamshukuru sana Mheshimiwa tena kwa juhudi yake kubwa ambayo ameifanya kuhakikisha kwamba na hapa alisema atachangia nguzo ishirini. Lakini baada ya kusema atachangia nguzo ishirini basi kila siku anafatilia. Kwa hiyo, ule muda ambao tumeupanga ulikuwa ni Febuari mwaka 2017 katika Mpango kazi tuliona kijiji cha Kwarara Madina kupata umeme. Lakini kwa juhudi ya Mheshimiwa Mwakilishi huyo basi umeme ule utafika kabla ya Febuari 2017. Naomba nimshukuru sana na nimpe hongera sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kumejitokeza msawali kuhusu mazingira, suali la ukataji miti ovyo na uchimbaji wa michanga Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Chonga alilizungumzia hilo. Lakini Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu na kumfahamisha kwamba serikali kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka imeweka utaratibu wa ukataji wa miti hapa Zanzibar, utaratibu huo hauruhusu miti kukatwa bila ya kuwa na kibali. Hivyo, kwa mujibu na utaratibu huo ni makosa kukata mti bila ya kuwa na kibali cha kutoka Idara ya Misitu.

Utaratibu wa kupata kibali ni lazima muhusika ajaze fomu ambayo huanzia kwa Sheha. Hivyo, naomba nitoe wito kwa wananchi wote kuacha tabia ya kukata miti ovyo wakitaka kukata miti basi lazima wafate utaratibu uliopo na kuomba kibali kutoka sehemu husika na hili tulikuwa tunaomba tushirikiane kwa pamoja ili tuhakikishe kwamba tunalinda mazingira yetu na miti haikatwi tupeane taarifa. Vile vile, Mheshimiwa Mwakilishi, aliendelea kwa

kuzungumzia suala la michango lakini Mhe. Naibu Spika, naomba pia nimueleze kwamba kuhusu uchimbaji wa michanga ovyo ni kwa serikali imefuta Sheria ya Mazingira mwaka 1996 na kuunda Sheria mpya ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2015 ambayo pamoja na mambo mengine imeweka taratibu wa uchukuaji wa michanga na kudhibiti uchukuaji kiholela wa michanga hiyo.

Serikali kupitia mamlaka ya usimamizi wa mazingira kwa wameshirikiana na Idara ya Misitu, Jeshi la Polisi na taasisi nyengine zitaendelea kufanya upereshen wa kuwakata wahusika wanaochimba mchanga kiholela ili taratibu za kisheria zichukuliwe zidi yao.

Vile vile, nilikuwa naomba kujibu suali la Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la mnongonyoko wa fukwe, ni kweli kuwa mnongonyoko huo unaongezeka siku hadi siku katika maeneo mbali mbali ya fukwe zetu Unguja na Pemba. Kasi ya mnongonyoko huo inaongezeka kutokana na tatizo liliopo la dunia na mabadiliko ya tabia nchi. Kwa ajili ya kukabiliana na suala hili naomba nitoe wito kwa wananchi na wawekezaji wote kuacha tabia ya kukata miti ovyo iliyopo kwenye fukwe kuchukuwa mchanga wa pwani kuharibu matumbawe na kujenga karibu na fukwe. Naomba tushirikiane kwa pamoja kulinda mazingira yetu.

Pia, kulijitokeza suala kuhusu kuleta mapema ile Sheria ya mafuta na gesi ambayo Mhe. Hamza Hassan Juma, napenda kuungana na hoja yake kuhusiana na umuhimu wa uwelewa wa maswali ya Sheria mafuta na gesi kwa madhumuni makubwa ya kuchangia kikamilifu katika maswali ya sheria yetu ya mafuta na gesi. Wizara yangu baada ya kuliona swali hili na umuhimu wake imejipanga kuandaa mipango maalum ya kukuza uwelewa kwa masuala ya mafuta na gesi kwa wananchi katika mwaka wa fedha 2016/17.

Madhumuni ya mpango huu ni kuwawezesha wananchi wetu kuwa na uwelewa wa kutosha na kushiriki katika harakati mbali mbali zinazohusiana na sekta hii ya Nishati. Mpango kama huu uliandaliwa katika miaka iliyopita na kuelimisha viongozi na watendaji wakuu wa serikali katika kupata uwelewa wa masuala ya mafuta na gesi kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, mpango huu kwa upande mwengine utahusisha Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili kupitia semina maalum zitakazowesha kupata uwelewa wa kutosha na hasa kuhusiana na sheria hii kwa kutumia wataalamu wa ndani na nje ya Zanzibar. Semina hizi zinategemea kufanyika

katika robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17. Napenda kuchukuwa nafasi hii kuwajulisha Waheshimiwa Wajumbe kuwa katika matayarisho ya msaada wa sheria hiyo wataalumu wetu walichukuwa uzoefu wa sheria za nchi mbali mbali za mafuta na gesi na hasa za nchi jirani kama vile Tanzania, Uganda, Kenya, Sudani ya Kusini na kadhalika. Hivyo, nawaomba na kuwashauri Waheshimiwa Wajumbe, kutumia fursa kama hiyo katika kujifunza uzoefu wa sheria za wenzetu na kutumia uzoefu huu katika kuimarisha Mswada wa sheria yetu.

Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe kuhusu suala la ziara za kimafunzo nje ya nchi ni suala la kulitafakari kwa kuzingatia muda tulionao na hali ya kifedha inayotukabili. Hata hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, suali hili tunalichukuwa kwa madhumuni ya kulifanyia kazi zaidi.

Pia, mwisho lilijitokeza swali la Mhe. Ussi Yahya Haji Mwakilishi wa Jimbo la Mkwajuni, kuhusu kuwa na wataalamu wa ndani na serikali kujipanga kusomesha vijana wetu. Naomba nimuhakikishe kwamba Mhe. Ussi Yahya Haji kwamba, serikali na wizara imejipanga vizuri kuhakikisha kwamba tunafanikisha sekta hii kuwa na wataalamu wetu sisi wenyewe. Sasa hivi jumla ya vijana kumi wamesharudi ambao tayari wataalamu hao tunao lakini wengine tayari wako nje ya nchi na vyuo mbali mbali jumla ya wanafunzi 38 wameenda kusomea *Petroleum Industry* ambao wako nje sasa hivi na baadhi ya wanafunzi ambao sasa hivi mwaka huu watakwenda karibu 50 kwenye Chuo cha Dodoma na Dar-es-Salaam na nje ya nchi kuchukuwa fani hii.

Kwa hiyo, naomba niwatoe wasi wasi Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, kwamba serikali imejipanga vizuri na hata sekta hiyo ikifika muda wa kuanza basi tayari tuna wataalamu wa kutosha ili tuweze kujiendesha sisi wenyewe.

Mwisho kabisa naomba kuunga mkono hoja asilimia mia juu ya mia na naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu basi waikubali na kuipitisha Bajeti hii ya Wizara ya Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nichukuwe fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia neema hii ya uhai ambao tumeweza kusimama hapa jioni hii ya leo.

Lakini pili kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuweza na mimi kuchangia machache kuhusiana na hotuba ya bajeti ya Makadirio ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzabar.

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii kwanza kuwashukuru Wajumbe wote ambao wamechangia hoja hii au bajeti hii lakini zaidi niwashukuru wale ambao wamechangia zaidi katika masuala ya elimu. Naomba nitoe ufafanuzi kwa yale masuala machache ambayo yamebakia bado hayajapata ufumbuzi hasa katika sekta ya elimu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Bahati Khamis Kombo, alielezea suala zima la mashirikiano, anadhani kwamba kukosekana kwa mashirikiano ya pamoja kati ya wizara, wazazi pamoja na walimu kunapelekea ufaulu mdogo wa wanafunzi. Napenda nimuhakikishie Mheshimiwa Mwakilishi pamoja na Wawakilishi wengine kwamba sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunafanya kazi hii ya kushirikiana na wazazi kwa kupitia kwa walimu wetu kwa asilimia mia moja.

Lakini tuseme kwamba sisi wizara na zaidi hapa nazungumzia walimu pale ambapo walimu wanakuwa wanaita wazazi kwa ajili ya kufata maendeleo ya wanafunzo wao baadhi ya wazazi wanakosa kushiriki katika suala hili. Sasa hapa tuseme kwamba ni kweli yale baadhi ya mashirikiano yanakuwa yanakosekana. Lakini kupitia kamati za skuli wizara inafanyakazi kubwa sana kuwashajihisha wazazi wawe wanafatilia sana maendeleo haya.

Lakini pia nichukuwe fursa hii kuwaomba sana wazazi wenzangu tuwe tuna tabia ya kufatilia maendeleo ya watoto wetu. Wazazi tunakaa tunasubiri mpaka mwanafunzi ameshafeli ndiyo tunakuja kusema kwamba mtoto wangu amefeli, mtoto wangu amefeli. Kumbe tulikuwa hatufuatilii kuona maendeleo yake yanakwenda vipi. Lakini kama tutakuwa tuna utamaduni wa kuweza kuona maendeleo ya watoto wetu tokea mapema, basi tutaweza kujua watoto wanakwenda kwa hatua gani. Kwa hivyo, kwamba tukishirikiana kwa pamoja juu ya hili wazazi wangu basi tuseme kuwa maendeleo ya wanafunzi wetu yatakuwa mazuri, lakini vile vile maendeleo ya elimu yatakuwa zaidi ya vile ambavyo tunataka yawe. Na ile kauli mbiu yetu ya 'elimu bora kwanza' itaweza kufikiwa.

Lakini jengine ni Mhe. Bahati Khamis Kombo, pia alisema kwamba walimu ni kidogo na skuli ni nyingi. Hili tuliseme kwamba ni kweli tunakiri kwamba kuna upungufu wa walimu, lakini sisi Wizara tayari tumeshapeleka ombi hili kunakohusika na baada ya muda mfupi *inshaallah* walimu wataajiriwa. Na watakapoajiriwa hawa walimu wengi ni kwamba hili tatizo la uhaba wa walimu likakosekana na kila skuli itapata walimu wa kutosha ili kuweza kuwapa elimu wanafunzi wetu.

Lakini suala la mwisho ambalo halipata ufumbuzi ni suala ambalo Mhe. Mohamed Said Mohamed, amelitoa kama ni ushauri na zaidi alizungumzia suala la vyeti feki. Tuseme kwamba sisi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tutahakikisha kwamba kama kuna wafanyakazi wetu ambao wana vyeti feki, basi hao hatutowaachia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tutapitisha utaratibu wa kuvifuatilia na kila taasisi kupitia muhusika yeyote ambaye anahusika tuone kwamba ni nani ambaye ame-*forge* na kuweza kupata ile ajira. Kwa sababu kama ametumia vyeti feki, ina maana kila anachokifanyia kitakuwa ni feki feki. Kwa hivyo, kwa hilo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haitovumilia kabisa. Hivyo, nimuhakikishie kwamba tutalifanyia kazi na *inshaallah* litakapobainika wale wote ambao watastahiki watapata ile zawadi stahiki. (*Makofi*)

Mwisho, niseme kwamba nami binafsi yangu na kwa niaba ya wanawake wasomi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja naunga mkono hoja ya Makadirio ya Mapato ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa asilimia mia moja.
Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Sasa ni zamu ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Balozi Amina Salum Ali.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na uwezo wa kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Mhe.Makamu wa Pili wa Rais.

Na mimi nitafanya kama walivyofanya wenzangu kwa kujibu zile hoja ambazo Wajumbe wengi wamechangia zinazohusiana na wizara yangu. Kwanza kabla sijaingia kwenye kujibu zile hoja niipongeze sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa sababu kwa nini yeye ni mzee wetu. Katika ulimwengu wa diplomasia yeye amekuwa ndiye *dean* wetu hapa katika Baraza la Wawakilishi na Zanzibar nzima. Tuna imani naye na tunamuunga mkono asilimia mia juu ya mia kwa hotuba yake aliyoleta kwenye Baraza letu.

Mhe. Naibu Spika, katika michango tangu tumeanza bajeti na mpaka leo bajeti ya serikali, jambo moja ambalo linanihusu Wizara kwangu ni kuhusu mambo ya biashara na vyakula kwa ujumla. Waheshimiwa Wajumbe wameonesha wasi wasi wao kwa kuangalia hali ya vyakula nchini hasa katika kipindi hichi cha mwezi wa Ramadhani.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba hali ya vyakula nchini mwetu ni nzuri sana. Na hii imetokana na ukaguzi tuliofanya tarehe 11 na 13 mwezi Mei. Na Wizara imepanga kufanya ukaguzi mwengine kesho kwa ajili ya kujua hali halisi kwa mwezi wa Ramadhani. Lakini Mhe. Naibu Spika, ningeomba nitoe ufafanuzi wa kutaja kiwango halisi cha chakula kiliopo hapa nchini mwetu kwa mwezi huu wa Mei ni matarajio yetu kwa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Kwa mfano katika suala la mchele, sasa hivi mwezi wa Mei, tunayo tuna *tons* elfu kumi na nne, mia tatu na kumi za mchele ambazo hizi ni sawa sawa na matumizi ya miezi miwili. Kwa hesabu kwamba kila mwezi tutatumia *tons* elfu saba na kumi na mbili za mchele. Hivyo, kwa mwezi unaoingia wa Ramadhani hatotukuwa na matatizo makubwa sana ya mchele.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa unga wa ngano tunazo *tons* elfu ishirini na moja, mia moja hamsini na tatu nukta tisa. Hii ni sawa sawa na matumizi ya miezi kama kumi hivi. Kwa hesabu yetu tunatumia kwa mwezi *tons* elfu mbili, mia moja hamsini na mbili za unga ngano ingawa kwa mwezi wa Ramadhani hii idadi huwa inaongezeka, kwa sababu ya 'mahanjumati' wanayofanya wananchi kwa mwezi wa Ramadhani.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kwa upande wa sukari hivi sasa tunazo *tons* elfu kumi na hamsini na tano ambayo ni sawa sawa na matumizi ya miezi saba na nusu. Kwa matumizi ya kila mwezi ya sukari *tons* elfu moja mia nne na tano. Hii pia tunajua kwamba mwezi wa Ramadhani matumizi ya sukari huwa yanaongezeka.

Mhe. Naibu Spika, tunatarajia kwa mwezi huu unaokuja wa mwezi wa Juni kwamba tuna tetesi ya uagiziaji wa mchele *tons* elfu sita, mia sita, kumi na tano. Ndizo ambazo zinatarajiwa kuagizwa kwa mwezi huu unaokuja wa mwezi wa Juni. Na hichi ni kipindi cha wakati wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, hakuna wasi wasi wa kuwepo uhaba wa vyakula hivi sasa. Ingawa kuna tetesi kuna wafanyabiashara baadhi yao wameshaanza kupeleka sukari Tanzania Bara. Na jambo hili tutalitolea uamuzi baada ya wafanyabiashara wetu kesho kuwaeleza hali halisi kwamba sukari inayoletwa Zanzibar na inapata *exemption* ya hali ya juu. Kwa hivyo, ni kwa ajili ya matumizi ya wananchi wa Zanzibar.

Pia, Mhe. Naibu Spika, sijatia idadi ya sukari ya Kiwanda cha Mahonda, kiwanda chetu cha sukari ambacho sasa hivi wana *tons* mia tatu na sitini ya sukari ambayo bado hawajaingiza katika soko.

Mhe. Naibu Spika, walizungumza Wajumbe kuhusu suala la *exemption*. Ni kweli vyakula vyetu hivi navyo nchini wanapata *exemption* ya hali ya juu. Kwa sasa hivi Mheshimiwa anayehusiana na mambo ya kutoa misamaha ya kodi ambaye ni Waziri wa Fedha na Mipango ameshatoa miongozo na wale wote ambao wanataka kuagiza vyakula vya ziada kwa ajili ya mwezi wa Ramadhani wanatakiwa wapeleke maombi yao kunakohusika, nako ni Wizara ya Fedha na Mipango. Na utaratibu umeandaliwa wa kuona kwamba serikali haipati hasara kubwa lakini pia na wafanyabiashara wanaweza kuagiza na kuweza kuwapatia vyakula kwa bei nafuu wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo limezungumzwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, ni kuhusu tatizo la saruji. Yeye alisema kwamba serikali inapotokea matatizo ya uhaba wa chakula, uhaba wa vifaa huwa hatuchukuwi hatua na hatutoi taarifa kwa wananchi. Mhe. Naibu Spika, siyo kweli kwa sababu suala la saruji lilivyotokea Wizara yangu ilichukua hatua muafaka ya kukutana waagiziaji wote wa saruji nchini, na kutaka kujua hasa hali halisi ni nini na kimetokea nini mpaka saruji ikapanda bei. Na tuliona kwamba wakati ule kulikuwa na tatizo bandari kwa sababu meli zilikuwa nyingi na zilikuwa haziwezi kutolewa mapema bidhaa zao. Matokeo yake msururu uliokuwa wa vyombo vya bahari ulikuwa ni mrefu na pia hata meli ikitokea Dar-es-Salaam inakutana na msururu mrefu.(*Makofi*)

Lakini tulikaa na kuzungumza na Wizara ya Mawasiliano inayohusika na mambo ya bandari. Na walilichukulia hatua na ndiyo maana bei ya saruji sasa hivi imerudi katika hali ile ile ya zamani. Siyo kwamba bei imepandishwa ni kwa sababu ya gharama zimepanda kutokana na utaratibu mzima wa kupakia na kusambaza katika miji. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo limezungumzwa na Wajumbe ilikuwa ni kuhusu viwanda kwa jumla. Na pia walitaka kujua masuala ya Mahonda. Hili amelijibu kidogo Waziri wa Ardhi, lakini mimi ningetaka niwatoe wasi wasi wananchi wa Zanzibar na hasa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi.

Kwa kusema kwamba suala la viwanda ni suala letu sisi wote na siyo kwamba ni la serikali peke yake. Ningeomba wananchi waanze kuona umuhimu wa kuwa na viwanda. Pia, wakumbuke huko nyuma tulikuwa na viwanda vingi,

lakini vingi vyao vimekufa kutokana na maamuzi yetu. Lakini vyengine vimekufa kutokana na tatizo la soko. Lakini vyengine vimekufa kwa sababu ya hali halisi ya uchumi wa dunia. Ninaweza kutoa mfano wa viwanda wa minazi, kwa mfano vya mbata, mafuta ya nazi, sabuni na kadhalika. Vyote hivi viwanda vilikuwepo na vilikuwa vimetoa ajira kubwa sana kwa wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, viwanda ni muhimu sana kwa maendeleo ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, na katika mkakati wetu wa kufikia uchumi wa kati, sekta ambayo itakuwa inachangia katika hali ya juu itakuwa ni viwanda, biashara na huduma mbali mbali ikiwemo pamoja na utalii. Ninasema hivyo kwa sababu Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kesi ya Kiwanda cha Mahonda, tunazungumza na wawekezaji wa Mahonda.

Mkumbuke kwamba wawekezaji wa Mahonda walichukua kile kiwanda kilikuwa kiko katika hali mbaya sana na wametumia fedha nyingi sana kukifufua kile kiwanda. Kwa hivyo, kile kiwanda siyo cha wawekezaji peke yake, kile kiwanda ni cha Wazanzibari wote. Hivyo, ni vizuri uongozi uliopo Mkoa wa Kaskazini na wananchi wa Kaskazini wakawa na hamu na bashasha na mapenzi na kiwanda kile. Kwa sababu huko nyuma kiwanda kile kilitoa ajira kwa wananchi wengi hasa wa Mkoa wa Kaskazini. Lakini hizi *incident* za moto na mambo mengine yanayotokea kwa kweli yanawavunja moyo wawekezaji wa pale Mahonda.

Lakini na wawekezaji wengine ambao tunataka kuwashajihisha wanatizama mfano wa jinsi serikali inawaangalia hawa wawekezaji wa Mahonda. Mimi binafsi ninafarijika sana kuona kiwanda hichi kina uwezo wa kuzalisha sukari, siyo tu kwa Zanzibar peke yake lakini vile vile kwa kuwezesha kupelekwa sukari hii kule Tanzania Bara ambako kwa sasa hivi wameshaombwa kama sukari ipo nyingi Zanzibar ipelekwe Bara. Tutakuwa na vikao sisi na Mawaziri wanaohusika kuona kiasi gani tutaweza kushajihisha Kiwanda cha Mahonda, kwa sababu kinatoa ajira lakini kinasaidia katika mchango wa pato la Taifa na kinasaidia vile vile katika kutoa kodi ambazo sisi wote tunazitegemea. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nilitaka niseme haya kwa sababu na hasa viwanda ni mambo muhimu. Na mkakati ambao tunatarajia tutauzungumza zaidi katika bajeti yetu tunapokuja kusoma bajeti yetu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, naomba nirejee tena kusema ninaunga mkono bajeti hii ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na ninatarajia Wajumbe nao wataunga mkono bajeti hii. Na wananchi watafurahia kuona kwamba serikali yetu inapanga mambo na ipo katika hatua kubwa zaidi ya kuona mambo yote ambayo tunayapanga yanakwenda.

Lakini moja nimelisahau Mhe.Naibu Spika, ni kuhusu mambo ya biashara. Tunasikia vitendo vya kususia, watu wanasusiwa kuuziwa biashara zao. Naomba niseme kwamba serikali yoyote haiombi radhi. Serikali yoyote haiombi wananchi na tumeshakwisha kuwaomba mara chungu nzima wafanyabiashara kwamba wasichukue hatua hizi za kuwasumbua wananchi wetu. Kwa hivyo, naomba niseme tu kwamba hapo tulipofikia tunafuatilia kwa makini zaidi na hatua tutakazochukua ni kuwanyang'anya leseni wale wote ambao wanafanya vitendo vya kuwabughudhi wananchi wetu. (*Makofi*)

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, kuna watu wengi wanataka kufanya biashara wakisaidiwa na serikali. Kwa hivyo, hawa ambao wameshashiba na wameshapata hali ya juu ya maisha yao, wanaanza kufanya mambo haya ya biashara, wapo watu ambao wanataka kufanya biashara wakiwemo vijana wetu. Kwa hivyo, naomba niwahakikishie tu kama wameshindwa kuendesha biashara wameanza kuwabugua watu, serikali ipo tayari kuwasaidia hasa vijana wetu wachukue nafasi hizi za kufanya biashara ili waweze kuwasaidia wananchi wapate manufaa na vile vile na wao waendelee katika maisha yao. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja hii, ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana tunakushukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Sasa tutampa nafasi Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na baada ya hapo mchangiaji wetu wa mwisho ambaye atakuwa Waziri wa Fedha na Mipango atamalizia kwa mchango wa Mawaziri.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi awali yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataallah*. Ninamshukuru sana kwa kuwawezesha Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa jioni hii kwa wingi kuwemo katika Baraza hili la Wawakilishi na kuweza kuiunga mkono hoja ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuonesha wazi kabisa, hii ni hoja ambayo itatuletea maendeleo na hotuba yake itaelekea katika kumkomboa Mzanzibari kwenye mambo ya maendeleo yote ya visiwa hivi. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kuwashukuru sana wale ambao wamechangia kuhusiana na Hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini wakagusa sehemu kubwa ya Wizara yangu ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo. Nataka kwanza niwatambue waliochangia sana na kuigusa wizara yangu hii na kuwashukuru. Nimshukuru sana Mhe. Shaib Said Ali, Mhe. Ali

Suleiman Ali, Mhe. Rashid Shamsi Kigoma pamoja na Mwakilishi wa Kiwani Mhe. Mussa Foum Mussa. (*Makofi*)

Kwa umoja wao wamegusa sehemu mbili kuu. Wamechangia ni namna gani vyombo vya habari vinaweza kupeleka ujumbe wa elimu kwa wananchi na kuwawezesha kabisa wananchi kuweza kuitekeleza hotuba hii ya Makamu wa Pili wa Rais kivitendo. Lakini pia wametaka kujua ni namna gani wafanyakazi wa tasnia hii ya habari kwa udhaifu wao wa kutoa habari, kwa uhafifu wao wa elimu waliyokuwa nayo ni namna gani wanaweza wakapatiwa mafunzo.

Mhe. Naibu Spika, ninataka nikiri kwamba kazi ya habari ni ngumu. Miongoni mwa kazi ngumu basi na kazi ya habari nayo ni ngumu. Waheshimiwa Wawakilishi sote tutakuwa mashahidi hapa tunaona ndugu zetu hapa ambao wanatufanikishia kulionesha Baraza letu hili tukufu *alive,* kuanzia tunapoingia saa tatu mpaka pale ambapo tunatoka saa mbili ya usiku. Matangazo yamekuwa yana ubora wake bila ya kusita na bila ya picha kukatika. Na kazi hiyo kwa kupitia hotuba hii ya Mhe.Makamu wa Pili wa Rais itakuwa ni endelevu na itaendelea mpaka Baraza litafikia kikimo chake. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ukitazama katika ukurasa wa 24, Kifungu cha 59 Programu Ndogo iliyopanga kufanya shughuli nne muhimu za mwaka 2016/2017 katika hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, inajumuisha tathmini ya kujiandaa na kukabiliana na maafa kwa kutoa mafunzo kwa Shehia zote hamsini. Ninataka niwajuulishe wazi Waheshimiwa Wawakilishi na hususan wale waliochangia kuhusu Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwamba *ZBC television* pamoja na *radio* kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tayari imejidhatiti kuweka vipindi maalum. Na vipindi hivyo vitarushwa kwa kila jimbo vitakapofanya kazi zake.(*Makofi*)

Hivyo *ZBC* itatoa ushirikiano wa dhati kwa Waheshimiwa Wawakilishi kuweza kuvitumia vyombo vyetu vya habari ili kueleza uhalisia wa malengo na mipango waliyojipangia katika majimbo yao. Hii yote imeoneshwa mfano wakati wa pale yalipotokea maafa na namna gani tumeweza kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na tukaweza kuwapa taarifa zote wananchi juu ya namna ya maafa yalivyo na mwisho yalivyoishia na hadi pale ambapo tutaona sasa hivi kuna hatarishi zinajitokeza za maafa. Kwa hivyo, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo itashirikiana vyema na chombo cha hali ya hewa ili kuweza kuwatanabahisha na kuweza kuwapa taarifa kamili wananchi na jamii yote ya Zanzibar kwa ujumla wake.

Mhe. Naibu Spika, ninapenda nimshukuru sana Mhe. Waziri Asiye na Wizara Maalum ameeleza mengi, lakini ninataka nimwambie rekodi yake itakuwa hewani na itaweza kurudishwa na kurushwa mara kwa mara ili wananchi tuwaeleze uhalisia kwa hotuba hii ambayo na yeye ameichangia.(*Makofi*)
Mhe. Naibu Spika, *ZBC* kwa televisheni, redio pamoja na Habari Maelezo itaboresha wazi vipindi vyake vya hali ya hewa kwa kushirikiana na Idara ya Hali ya Hewa na kuonesha hali zote muhimu za hali za hewa ambazo zimeweza kuhatarisha maisha.

Tunawaomba sana wananchi wawe waangalizi wa vyombo vyetu hivi vya redio na televisheni kwa umoja wao na wawe makini katika kusikiliza maelezo yetu baada ya habari, kwani hiyo ni elimu tosha ambayo itawawezesha wao kuwa na kinga pamoja na kujua namna gani wanaweza kujihadhari kabla athari haijatokea.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, inakiri kabisa kutekeleza programu hizi ambazo zimepangwa katika Wizara ya Makamu wa Pili wa Rais, *ZBC* na televisheni, pamoja na vyombo vyake vyengine vya habari vikiwemo habari maelezo, kwa umoja wake vikatoa elimu ya kina na mafunzo ya kina kwa wafanyakazi wake, mafunzo hayo ya muda mfupi na muda mrefu watapatiwa wafanyakazi wetu na watakaposimama hapa baada ya muda mfupi muwaone kwamba wamebadilika baada ya kuongeza ujuzi, maarifa na kuweza sasa kuleta elimu ya vitendo kwa kupitia vyombo hivi vya habari. *(Makofi)*

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, sikuwa na mengi katika kuchangia, isipokuwa sasa kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo, leo nataka nitoe faraja zangu, niushukuru sana uongozi wa *ZBC* televisheni kwa kuweza kuwakumbuka wafanyakazi wa *ZBC* televisheni na redio kuwapatia maposho yao, ingawaje maposho yale hayakidhi kazi ambazo wanazifanya, lakini mwanzo umeanza, naushukuru sana uongozi na sisi tutasimamia kufuatilia tuelewe kwamba jitihada zinazofanywa na Baraza la Wawakilishi kuweza kuwalipa vizuri *ZBC* ili kuwawezesha wafanyakazi wetu waweze kufanya kazi vizuri, posho lile ni lazima lilipwe kama lilivyopelekwa.

Ninataka nilihakikishie Baraza lako kama lilivyopanga kuwalipa wafanyakazi wetu wa *ZBC* televisheni na redio, ambao sasa wanalipa matangazo *live*, basi posho lile watalipwa kama lilivyopangwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa sasa nataka kwa pamoja na wafanyakazi wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, viongozi pamoja na wafanyakazi wote kwa ujumla wake tuunge mkono hoja ya hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Lakini sitopenda kuwasahau, wanachama wote wa Chama cha Mapinduzi hususan wa Jimbo la Amani, kwa umoja wao na mimi kwa niaba yangu naungana nao pamoja kuunga mkono hii hoja na kuipitisha, naomba ipite hapa kwa asilimia zote mia kwa mia.

Waheshimiwa Wawakilishi naomba nitumie fursa hii, hiki sio chombo cha habari ni mdomo wa Mwakilishi, lakini iwe ni kishawishi kizuri cha kuweza kukubali kuipitisha hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa ulaini, urahisi na kwa sababu tumetumia mbinu zote za kuifahamisha na kuielewesha kwa jamii. Hivyo, basi naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante nakushukuru sana Mhe. Waziri. Sasa itakuwa ni zamu ya Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohammed na ndiye atakayekuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa upande wa mawaziri. Baada ya hapo sasa tutampisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na yeye kuja kujibu hoja za Wawakilishi. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Ahsante Mhe. Naibu Spika. Kwanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na uzima aliyonijaalia, naamini na sote humu ametujaalia neema hiyo na kuweza kujadiliana bajeti hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Pili, nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kumsaidia Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein. Vile vile kwa kusimamia vyema shughuli za serikali.

Pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, kwa kazi nzuri anayoifanya katika kusimamia shughuli za ofisi hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Niwapongeze pia watendaji wote, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na watendaji wote wa ofisi hii, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana na ya kupigiwa mfano. *(Makofi)*

Vile vile nichukue nafasi hii Mhe. Naibu Spika, niipongeze sana serikali kwa kazi kubwa na juhudi kubwa wanayoifanya au inayoifanya serikali yetu katika kuwahudumia wananchi wake. Mifano dhahiri ni pale wananchi walipopata maafa ya mvua kubwa iliyonyesha tarehe 17 Aprili 2016, serikali ilichukua

juhudi kubwa ya kuwasaidia waathirika wote ambao wanakadiriwa zaidi ya watu 3,000 walipata athari mbali mbali kutokana na mvua zile.

Mhe. Naibu Spika, pia niipongeze serikali kwa jinsi ilivyoshughulikia suala la kipindupindu, kwa kupitia wizara husika ya afya, watendaji wamechukua juhudi kubwa, lakini viongozi wa Mikoa na Wilaya wamesaidiana sana katika kuifanya kazi ile ya kulisaidia taifa letu kuondokana na tatizo hili. Matokeo yake tumeyaona wagonjwa wameanza kupungua, lakini sasa ni wajibu wetu sote viongozi, lakini na wananchi kudumisha hali ya usafi kwa mazingira yetu ili tuweze kuepukana na tatizo la kipindupindu, tufuate masharti na kanuni za afya bora.

Mhe. Naibu Spika, nataka kuchangia maeneo kama matatu au manne. Eneo la kwanza ni Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Suala hili lilizungumzwa na Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Jang'ombe, lakini vile vile lilizungumzwa na Mhe. Mussa Foum Mussa wa Jimbo la Kiwani.

Mhe. Naibu Spika, suala la Mfuko wa Jimbo lipo kisheria, sheria iliyopitishwa mwaka 2012 sheria namba 4 na sheria hii Mhe. Naibu Spika, imeweka utaratibu mzima wa jinsi ya kuendesha Mfuko wa Maendeleo wa Jimbo na ulianza mbali tokea mwaka 2012, na kwa wakati huo mfuko ulikuwa ukitolewa ulikuwa ni shilingi milioni kumi (10,000,000)/- kwa kila jimbo. Lakini baadae serikali ikaongeza mfuko huo kwa maana ya kila jimbo sasa likawa linapata shilingi milioni 15,000,000/-, na hivi sasa serikali kwa kujali wananchi wake imeongeza mfuko huo na sasa ni milioni 20,000,000/-.

Mhe. Naibu Spika, suala la Mfuko wa Jimbo msimamizi mkubwa wao ni Mhe. Mwakilishi mwenyewe. Mfuko wa Jimbo ukienda vizuri ni kwa sababu ya usimamizi mzuri wa Mhe. Mwakilishi mwenyewe, utaratibu upo, sheria iko wazi na ndani ya sheria ile inasema usimamizi huo utafanyika kupitia kamati ya mfuko, na kamati ya mfuko imeelezwa ndani ya sheria yenyewe wajumbe wake. Mhe. Mwakilishi mwenyekiti, Madiwani wawili katika jimbo hilo watakaochaguliwa na Mhe. Mwakilishi. Lakini kuna Masheha wawili ndani ya jimbo hilo nao watakaochaguliwa na Mhe. Mwakilishi mwenyewe.

Pia kunatakiwa awepo mjumbe kutoka Asasi za Kiraia *Civil Society Organization* mmoja. Wajumbe wawili ni watu wanaoheshimika katika lile jimbo, lakini na mwengine awemo mtu mmoja miongoni mwa watu wenye mahitaji maalum, iko wazi kabisa *(Makofi)*

Lakini *practice* Mhe. Naibu Spika, katika majimbo mengi muongozo huu wa kisheria haufuatwi, baadhi ya majimbo na hapa tumeona katika taarifa ile iliyotoka kwa *CAG* juzi, kwamba kuna baadhi ya majimbo kamati zile zimeundwa kwa utaratibu mwengine nje ya utaratibu uliopendekezwa kwenye sheria.

Pia sheria iko wazi katika kuweka *account,* na *account* hii *signatory* waweka saini watu watokane na kamati hii, watu wawili watakaotokana na kamati hii. Vile vile katika kuhakikisha miradi iliyowasilishwa, kwa sababu utaratibu uko wazi ni lazima miradi iwe ya kijamii *community based programmes*, na miradi hiyo ni lazima itokane na kamati hii na kuna fomu maalum wanatakiwa wajaze na fomu hiyo inawasilishwa kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini baada ya kutumia fedha hizo kunatakiwa kupelekwe marejesho, na hapo napo kunakuwepo na changamoto nyingi.

Manunuzi nayo yanatakiwa yafuate sheria ya manunuzi, sio utaratibu wowote ule. Sasa Mhe. Naibu Spika, kama tutafuata muongozo sisi Waheshimiwa Wawakilishi tutakaosimamia mifuko hiyo au tutakaosimamia fedha hizo, basi kwa asilimia kubwa sana tutakuwa tumetatua tatizo ambalo linazikumba fedha zinazotolewa kupitia Mfuko wa Jimbo.

Mhe.Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka nilisemee ni suala la fidia, fidia ya kupitia kwenye mradi huu wa *ZUSP* ambalo limezungumzwa hapa nadhani na Mhe. Hamza Hassan Juma kama sikosei nafikiri ndiye aliyelizungumza hilo suala.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba fedha za fidia ziko tayari, serikali imefanya juhudi kubwa sana ili kuhakikisha fedha hizo zinapatikana na sio fedha kidogo, ni karibu bilioni 5.2 kufidia kwenye mradi wa *ZUSP* katika ile misingi inayochimbwa ya kutoa maji ya mvua. Tunatarajia baada ya kukamilika *process* katika kipindi kifupi, pengine mwezi wa Julai tutaanza kulipa fidia hizo kwa wale wanaohusika. *(Makofi)*

Jambo la tatu ambalo pia lilizungumzwa na Mhe. Hamza Hassan Juma, ni la hizi fedha za wakandarasi, kwa maana ya ma- *contractors*. Nadhani alisema kwamba fedha hizi huwa zinachelewa kutolewa na kuchelewa huko kunasababisha wakati mwengine hasara kubwa serikalini, kwa sababu mbele tunalipa fedha nyingi zaidi. Nakiri kwamba iko miradi ambayo bado wakandarasi wanaidai serikali. Pia tuifahamu kwamba katika kuwalipa wakandarasi hao, ni lazima ijiridhishe kwamba haya madai ni sahihi. Nasema hivyo kwa sababu kuna baadhi ya miradi Mhe. Naibu Spika, wakandarasi

wanapotoa *tender* zao, huwa wana-*quote* bei za chini ili waweze kupata kazi. Lakini wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo lile ongezeko linakuwa kubwa mno.

Mhe. Naibu Spika, mtu anaweza aka-*quote* kwa shilingi milioni 20,000,000/- lakini *variation* yake ikawa zaidi ya asilimia 55 au asilimia 60, hii ni hatari kubwa. Haiwezekani kabisa, lazima hapa patakuwa na makosa kwenye kuandaa mkataba huo. Lakini huwezi ukawa na *variation* inayozidi asilimia 50 au 60, hizi ni pesa za umma na ni lazima tuzisimamie vizuri, na kwa namna hiyo Wizara ya Fedha na Mipango haijakataa kulipa pesa za anayetudai yoyote, lakini si kwa miradi hii ya ukandarasi, lakini hata wazabuni wengine, ni lazima tunapopata yale maombi ya malipo basi tujiridhishe kwa kufanya uhakiki, ili kile tunachokilipa tuhakikishe kweli ndicho kima anachostahiki.

Kwa hivyo, hilo nilisema nilitolee taarifa hasa Wajumbe wa Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, waelewe Wizara ya Fedha na Mipango imo katika hatua mbali mbali sasa hivi za kuhakiki, mara baada ya uhakiki huu kumalizika basi kile kinachodaiwa kimestahiki kwa yule anayetudai mzabuni, basi atalipwa fedha zake kama ilivyotokezea huko nyuma wakandarasi hao kulipwa fedha zao.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni suala ambalo liliulizwa na Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame, yeye aliuliza kwenye hiki kitabu cha mapato na matumizi ya bajeti, kwa maana ya *budget assessment*. Katika mwaka 2014/2015 ile *column* ameona tumeweka ziro tupu na mwaka 2015/2016 nako kuna ziro tupu. Lakini ndani ya kitabu humu kuna fedha zilizotolewa na kutumika.

Naomba nimfahamishe Mhe. Mwakilishi Dkt. Mwinyihaji Makame, ni kwamba hilo limetokea kutokana na mabadiliko ya muundo kwa mawizara uliofanyika hivi karibuni. Kwa sababu katika mabadiliko hayo kuna wizara zimeunganishwa, lakini kuna idara mbali mbali zimekwenda kwenye wizara nyengine. Sasa isingekuwa kazi rahisi kuweza kuijaza ile *column*, kwa sababu ingebidi sasa uunganishe ya kutoka wizara moja na wizara nyengine na wakati mwengine zile *budget items* huwa hazilingani. Sasa kwa mwaka huu tutautumia kama ndio *base*, lakini kwa mwaka wa fedha unaokuja *column* zile zitakuwa zimejazwa kikawaida.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache, naomba na mimi niungane na wenzangu wote waliosema hapa kwamba wanaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana, nakushukuru Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Kwanza kabla ya kumpisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nitampisha Mhe. Mohammed Aboud Mohammed; Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na yeye kidogo aweze kujibu hoja za wajumbe. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri ningekuomba baada tu ya kumaliza kujibu hoja, ningekuomba utengue kanuni kwa ajili ya kuongeza muda, kwa sababu leo tunataka hapa zege lisilale. Sasa tukimaliza baada ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, tunaanza kupitisha vifungu. Kwa hivyo, ningekuomba na shughuli hiyo nayo uifanye pamoja na hiyo ambayo utaifanya sasa hivi. Mhe. Waziri karibu sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba ile kazi uliyonituma kuifanya mwisho baada ya maelezo, niifanye kabla ya maelezo ili hata mimi isije ikanikuta njiani najibu hoja.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda ulioko mbele yetu hautoshi kukamilisha kazi iliyo mbele yetu ya kukamilisha bajeti ya Ofisi hii ya Makamu wa Pili wa Rais. Kwa hivyo, naliomba Baraza lako tukufu liweke kando kanuni ya muda ili tuweze kumaliza kazi iliyo mbele yetu ya kupitisha hotuba ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ametoa hoja ya kutengua kanuni ya muda. Kwa hivyo, wale wanaokubali wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. Mhe. Waziri karibu. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kuimaliza vyema kazi iliyokuwa mbele yetu.

Sasa kwa heshima kabisa naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutuwezesha kuwepo katika Baraza hili na kufanya majukumu yetu kama tulivyojipangia.Namshukuru yeye *Allah* maana ndio muweza wa kila kitu, baada ya maelezo hayo naomba nikushukuru wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu.

Aidha nichukue fursa hii nimshukuru na kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuongoza nchi yetu kwa uadilifu mkubwa, umakini, hekima na busara. Tuzidi kumuombea aendelee kufanya wajibu wake huo kwa vizuri zaidi.

Aidha nimshukuru na kumpongeza sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa namna ambavyo anatuongoza katika Wizara yetu na namna ambavyo anavyotekeleza majukumu yake katika kuitumikia nchi yetu, Mwenyezi Mungu azidi kumuwezesha aweze kufanya kazi zake. Aidha nimshukuru sana Mhe. Spika, wewe Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza hili kwa kazi kubwa na nzuri mnayoifanya ya kuongoza Baraza letu.

Aidha nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mwanasheria Mkuu wetu wa Serikali kwa kazi kubwa anayofanya, sio tu ya kushirikiana na ofisi yetu lakini kwa taasisi zote za Serikali anavyotekeleza majukumu yake.

Aidha nivishukuru sana vyombo vya ulinzi na usalama kwa kusimamia amani na utulivu wa nchi yetu. Shukurani za pekee Mhe. Naibu Spika, ziende kwa kamati yetu hii ya kusimamia viongozi wakuu wa kitaifa na Wajumbe wa Baraza letu tukufu wote kwa namna ambavyo wanatupa mashirikiano makubwa ndani ya Serikali. Mwenyezi Mungu awazidishie kuwapa uwezo mkubwa tuendelee na shughuli zetu kwa salama na amani na uvulivu.

Mhe. Naibu Spika, aidha niitumie nafasi hii kuwatakia wananchi wote wa Zanzibar Ramadhan Kareem ambayo si muda mrefu tutakuwa tunayo. Pia nitoe pole kwa wale wote kwa njia moja au nyengine waliokumbwa na misiba na maafa mbali mbali katika kipindi chote cha mwaka uliokwisha, Mwenyezi Mungu awape moyo wa subira na awape kila la kheri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo kwanza na mimi niungane na wenzangu walionitangulia kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, napenda niwaombe sana wajumbe wenzangu wa Baraza hili tukufu waiunge mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, kwa sababu naamini kabisa kuunga kwao mkono hoja hii itakuwa ni fundisho na funzo kwa wapinzani wetu, ili waelewe makosa yao na waache kabisa vitimbi vyao. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, napenda pia nitoe shukurani maalum, kwa wananchi wote wa Zanzibar kwa kushirikiana kikamilifu katika utekelezaji wa Ilani yetu ya

Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2010/2016. Hapa shukurani za pekee nimpelekee Mhe. Rais kwa namna alivyosimamia utekelezaji huo wa ilani na tukaweza kupindukia zaidi ya asilimia 95 ya utekelezaji huu wa ilani. Kuna mambo mahususi Mhe. Rais wetu ameyasimamia kwa ukaribu mno, yakiwemo ukuaji wa uchumi wa nchi yetu ambao ndugu yangu Dkt. Khalid Salum Mohamed Waziri wa fedha alielezea kwa kina wakati akiwasilisha hotuba ya bajeti ya Serikali.

Vile vile Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alielezea haya kwa kina. Aidha Mheshimiwa katika utekelezaji wa ilani alifanya kazi kubwa ya kusimamia huduma za afya. Na leo sote ni mashahidi namna ambavyo tumepiga hatua katika upande wa afya, Mhe. Rais ameweza vile vile kusimamia kwa karibu mno huduma za elimu na tumepiga hatua kubwa sana, ameweza kusimamia ahadi yake ya kupandisha mishahara na nyote ni mashahidi mnaona namna hatua zinavyochukuliwa katika kufikia uamuzi huo, lakini ameweza kufanya kazi kubwa ya mfano katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki kwa wazee wetu wenye umri wa miaka 70 kuweza kupata pencheni ya kila mwezi. Ameweza pia kupandisha bei ya karafuu na kuimarisha zao la karafuu, ameweza kusimamia ununuzi wa meli mpya ya kisasa ambayo inatoa huduma kati ya Unguja na Pemba. Ameimarisha kwa kazi kubwa sana Miundombinu vikiwemo viwanja vya ndege, ujenzi, *terminal* mpya, bandari na kadhalika, lakini kazi moja kubwa kabisa ambayo Wazanzibari tulizungumza kwa muda mrefu lakini Rais wetu amethubutu kuikamilisha ni suala la uanzaji wa utafutaji wa mafuta na gesi asilia.

Naamini Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atalieleza kwa kina. Aidha ameweza kusimamia vizuri sana suala zima la utawala bora na haki za binadamu nchini kwetu, mafanikio makubwa ameweza kuweka nchi katika hali ya amani na utulivu na nyote ni mashahidi wa siasa za uchochezi za makusudi za kutaka kuharibu amani hiyo, lakini ubingwa na umahiri wa Dkt. Ali Mohamed Shein umewezesha nchi yetu kubaki katika hali ya amani na utulivu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ufupi nchi yetu imetulia mambo yanakwenda vizuri, licha ya vitimbi na vipapura vya wanasiasa wachache ambayo Mhe. Rafiki yangu Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi na Waziri asiye na Wizara maalum amelieleza kwa kina vitimbi hivyo vya wapinzani wetu.

Mheshimiwa mimi nadhani mambo yanayofanyika mengine ni ya aibu kwa karne ya leo kutaka watu kugomeana au watu kususiana, kuna mambo ya msingi ya kuyafikiria katika nchi yetu. Nchi yetu ndogo, ardhi yake ndogo, idadi ya watu inaongezeka tuna matatizo ya msingi ya upungufu wa maji

nchini, tuna matatizo ya msingi ya kupambana na ajira nchini, tuna matatizo ya msingi ya kuimarisha uchumi wetu.

Unapoona viongozi wanashadidia migomo, wanapandikiza siasa za chuki, hao ni viongozi wamepitwa na wakati, na ni wakati wa Wazanzibari kuwadharau, kuwasahau na watafute viongozi ambao wana dira ya kuendesha nchi katika karne hii ya 21.

Mhe. Naibu Spika, ni aibu sana kusikia watu wanaambiwa wagomeane kupanda magari, wagomeane kwenye kuvusha wananchi kutoka eneo moja kwenda eneo jengine ima kwa bodi ima kwa madau, au kususiana kwa misikiti, kususiana kwa maiti ni jambo haliingii akilini kabisa kabisa. Kubwa zaidi unawakataza wafanyabiashara wasilipe kodi, wafanyabiashara lazima watanabahi kutolipa kodi ni kosa la jinai, wafanyabiashara ni mawakala tu kwa kukusanya kodi kwa niaba ya Serikali kufanya vyenginevyo ikiwa hukuziwasilisha kunakotakiwa maana yake ni wizi wa mchana, na hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wale ambao watakwepa kodi. Lakini kwa kufanya hivyo sio tu unaidhulumu Serikali kupata haki yake, lakini unawadhulumu wananchi kupata huduma zao za msingi zikiwemo afya, elimu n.k.

Kwa hivyo mimi ninachoamini huo ndio uvunjaji mkubwa wa haki za binadamu kuliko aina yoyote. Ni kichekesho kikubwa kuona kwamba wao wanasema watatupeleka sisi *ICC,* wao ndio wangepaswa kupelekwa *ICC* sasa hivi, dunia inaelewa hilo wananchi muwache kudanganywa kwa mambo ambayo hayawezi kufanyika, wanajipa tamaa za fisi ambazo haziwezekani, Serikali imeundwa, uchaguzi umemalizika, uchaguzi mwengine mwaka 2020. (*Makofi*)

J

ambo la msingi hapo ni kusimamia amani ya nchi hii, amani ndio kitu muhimu, rasilimali pekee ya Wazanzibari ni amani na mtu yeyote yule anayehatarisha amani si kiongozi bali ni hasidi wa nchi hii, lazima wananchi tutanabahi kwamba wale wachochezi wa amani sio wao wanaoathirika, wanaoathirika ni wale wanaotiwa katika kundi wakashiriki katika vitendo vya uvunjifu wa amani.

Kwa hivyo ujue hao viongozi wanaowaambia kuharibu amani, wao ndio wa mwanzo kukimbia wakakaa mahala mbali zaidi na hapa, na wakaachia nyie muingie katika matatizo, kwa hivyo umefika wakati wa kutanabahi na kuwajua nani mwema nani mbaya wa nchi hii, kwa hivyo tuwasikilize wema wa nchi hii na tuwakatae wabaya wa nchi hii itikadi za siasa zisitufikishe mahala

tukachukiana tukalumbana tukagombana, tuna wajibu mkubwa wa kujenga nchi yetu na kuzipatia ufumbuzi changamoto zilizo mbele yetu (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba sana sote kwa pamoja huu ni ulimwengu wa karne ya Sayansi na teknolojia, mawazo yetu yaelekee huko sio migomo, sio kususia, sio chuki, sio uhasama, twende tufanye kazi kitaalamu, tupige hatua, tunahitaji sisi tulipo leo na vizazi vyetu vinavyokuja kesho.

Tunapokosea sisi vizazi vijavyo vitatuuliza tumefanya nini kujengea mustakbali mwema wa vizazi hivi, kwa hivyo tujue wale wote ambao wanafanya kwa makusudi kuharibu, kugombanisha, kuchafua amani, hao hawana imani kabisa kabisa na Zanzibar, na mimi niseme uongozi sio sura ya mtu, uongozi ni majaaliwa ya Mwenyezi Mungu aliyomtunukia mja wake. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, sote ni mashahidi tumeona nani ametakiwa na Mwenyezi Mungu awe kiongozi wetu, juu ya hila, ghilba, ujanja, na mbinu za kuharibu uchaguzi matokeo yake yule yule aliyetakiwa na Mwenyezi Mungu kuwa Rais wetu ndio amekuwa, wale wale waliotakiwa na Mwenyezi Mungu kuwa Wawakilishi ndio wamekuwa wawakilishi wetu, na wale wale waliotakiwa na Mwenyezi Mungu kuwa madiwani ndio Madiwani wetu. Sasa Mwenyezi Mungu humpa amtakae, na anampa kwa sababu ya vigezo vyake na kigezo cha mwanzo ni kusimamia amani na utulivu, ukiona umekoseshwa unajulikana kwamba nchi hii utaitia katika gharika. Na kama huyafuati maamuzi ya Mwenyezi Mungu basi usitafute mtu wa kugombana naye, ujue yupo wa kugombana naye. (*Makofi*)

Kwa hivyo, mimi naomba sana viongozi wetu tukae pamoja tushirikiane tujenge nchi yetu, huo ndio msimamo wa Serikali na huo ndio uamuzi wetu wa pamoja wa kujenga nchi yetu.

Baada ya maelezo hayo ya jumla sasa niende moja kwa moja kutokana na kila sekta ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Lakini kabla ya kufanya hivyo nataka tena kwa mara nyengine niwapongeze sana sana Waheshimiwa Manaibu Waziri na Mawaziri ambao wametoa ufafanuzi wa kutosha katika kila sekta zao, naamini sana Waheshimiwa wajumbe mumeelewa ufafanuzi huo, na naamini sana mtakuwa mmekubaliana nao, kwa sababu umetolewa kwa umahiri mkubwa na kwa taaluma ya hali ya juu, kwa hivyo nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Waziri pia nawapongeza Wajumbe wote waliochangia hotuba hii. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, tukianza na Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa. Mhe. Omar Seif Abeid Mwenyekiti wetu wa kamati kwa niaba ya kamati na Waheshimiwa wengine walichangia sana katika eneo hili, wakiwemo Mhe. Mohammed Ngaza Jecha, Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mhe. Rashid Makame Shamsi, Mhe. Suleiman Sarahan Said, Mhe. Masoud Abrahman Masoud, Mhe. Said Mohammed Said na Mhe. Hassan Khamis Hafidh. Walichangia sana katika suala hili la kukabiliana na maafa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niseme ushauri huu tumeupokea na tutaufanyia kazi ushauri wenu ulikuwa wa kina na dira ya kufanyia kazi katika eneo hili, lakini napenda tu nieleze kwamba Kamisheni hii ya kukabiliana na maafa ni mjumuiko wa Wizara zote za Serikali chini ya Mwenyekiti Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hiyo ndio Kamisheni ya kukabiliana na maafa.

Katika Serikali pale aliyekuwa hayumo ni Mhe. Rais peke yake, lakini Mawaziri wote na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama ni wajumbe katika kamisheni hii ya kukabiliana na maafa chini ya uenyekiti wa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Ipo *Secretariat* ambayo ipo chini ya kamisheni ndio inaratibu na kutoa miongozo ya utekelezaji wa kazi, katika kutoa miongozo hiyo kuna watekelezaji na watekelezaji sio *Secretariat* ya Kamisheni ya kukabiliana na maafa, watekelezaji ziko taasisi mbali mbali za Serikali zikiwemo KMKM, Idara ya Uokozi na Zimamoto, Polisi, JWTZ na wengine hao hasa ndio watekelezaji yanapotokea maafa au majanga.

Kwa msingi huu taasisi hizo ndio zinazopaswa kuwa na vifaa na vitendea kazi mbali mbali, ile *secretariat* inachotakiwa kuwa nacho ni vitu vinavyotoa huduma za kibinadamu kama vile mahema, machela, chakula, magodoro, maji, *gloves* n.k. Kwa hivyo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushirikiana na Kamisheni ilivyokifanya ni kuwasiliana na nchi rafiki, taasisi za kimataifa katika kuangalia uwezekano wa kupata vifaa vya kisasa kwa ajili ya kusaidia kazi zetu hizi ili masuala ya uokozi na matatizo yanavyojitokeza katika nchi yaweze kupata majibu sahihi.

Kwa sasa tunashirikiana na *UNICEF* na *UNDP* katika kutengeneza mambo vizuri kuweka mipango mizuri, mikakati mizuri ya kuweza kufanikisha lengo hilo, tayari tumeshamaliza suala la sera ya maafa, tumemaliza mpango wa kukabiliana na maafa, na tumeweka mkakati wa mawasiliano mapya. Sasa lengo letu ni kuzidi kuwasiliana na nchi zile ambazo tayari tumewasiliana nazo ili zisaidie katika kukabiliana na matatizo ya maafa.

Kuhusu kwa upande wa *simulation exercise* hii tunakuwa tunaifanya lakini ina utaratibu wake wa kufanyika na ina maandalizi yake, na mara nyingi tunapoifanya huwa tunashirikiana na wenzetu wa *UNICEF*, kwa mwaka huu hatutofanya, lakini tunajenga maandalizi ya kufanya *simulation exercise* kwa mwaka unaokuja, kwa hivyo waheshimiwa Wajumbe naomba tuvute subra tungojee tukamilishe maandalizi kwa mwaka huu na mwakani zoezi hili litafanyika kwa kushirikiana na wenzetu wa *UNICEF* ili kuliweka kwa utaratibu mzuri utakaoleta tija kwetu.

Yapo maelezo kwamba watu wetu wakati yalipotokezea maafa kuna sehemu hawakufika, inawezekana ikatokea hivyo, lakini taarifa tulizonazo watu wetu wa kufanya tathmini ya maafa katika kila shehia kazi hiyo imefanyika na tathmini ipo. Kwa hiyo, tunajua kila kilichotokea katika kila shehia, na ndio maana hatua zikachukuliwa, na hatua zetu zilizochukuliwa zimeweza kupongezwa na *WHO*, *UNICEF*, *Red Cross* na mashirika makubwa makubwa ya habari kama *BBC* na wengine. Wamesema Zanzibar ni mfano katika Afrika katika kuchukua hatua hizi.

Kwa hivyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wajumbe tusijione tuko nyuma sana katika mambo haya, tunayoyafanya yako katika hatua nzuri. Hata wenzetu wa Bara hawawezi kuweka kambi wakaweza kuzisimamia na kuhakikisha watu wetu wanapata huduma zote za lazima zinazotakiwa katika mbio na kwa usafi kama ambavyo tunaweza kufanya. Kwa hiyo, tunayoyafanya yana sura nzuri na yanakubalika kwa vigezo vyote. Naomba tushirikiane zaidi ili kuhakikisha kwamba shughuli zetu hizi tunazifanya kila siku kwa kuongezeka hadhi yake.

Kwa upande wa mgao Waheshimiwa Wajumbe walitaka kujua ni kiasi gani cha fedha kimetumika tokea lilipoanza suala hili la maafa katika mwaka huu. Fedha zilizotolewa na serikali ni milioni 87,045,000, michango ya wafadhili mbali mbali ambayo haijatumika mpaka sasa imewekwa katika mfuko wa maafa ni milioni 15,288,150. Chakula kilichotolewa katika kusaidia kambi kilikuwa na thamani ya shilingi milioni 40,693,150. Kwa hiyo, kulikuwa ni chakula, huduma za usafi, huduma za usafiri, huduma za mawasiliano ndio zilizokuwa zinahitajika katika kambi pale, kwa sababu ilibidi hata watoto tuwapeleke skuli, watoto waliokuwepo pale walikuwa wanapelekwa skuli kwa gari. Huduma zote hizo zilifanywa na serikali na watu waliochangia chakula.

Kwa hiyo, kwanza nataka nichukue fursa hii kuwapongeza sana wale wote waliojitolea kwa njia moja au nyengine kuunga mkono jitihada za serikali katika kuhakikisha watu wetu hawa wanapata huduma nzuri, huduma bora na wanashughulikiwa ipasavyo.

Pia niipongeze serikali yetu kwa kuwa mstari wa mbele kwa kukubali kubeba dhima hii kubwa, si jambo jepesi, na kila inapotokea serikali inafanya hivyo. Chakula kilichobaki tumekigawa kama ifuatavyo.

Kwanza tuliwapa kituo cha kulelea watoto Mazizini pakti 12, pakti 12 wakapewa wazee Sebleni na pakti 12 wakapewa wazee wa Welezo. Kwa hiyo, sasa chakula chote kile kimeshagaiwa. Nini hatua tunayochukua ili mambo haya yasijirudie.

Mhe. Naibu Spika, serikali iliunda kamati maalum ya wataalamu kufuatilia kwa kina mwenendo mzima wa mambo haya yakiwemo hata ule mmong'onyoko wa ardhi, kutuama kwa maji, kujengwa kiholela na kujenga katika njia za maji na kadhalika.

Pamoja na maji yanayotuama na kazi hiyo ya wataalamu imekamilika wameleta ripoti safi sana, na mimi nataka niwapongeze sana wataalamu wetu kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya. Hivi sasa hatua inayofuata ni kwenda kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu na baadae suala hili kupelekwa serikalini kwa uamuzi wa mwisho ili utekelezaji uanze. Kwa hiyo, sasa ugonjwa umejulikana na majibu yamejulikana, sasa tunangojea maelekezo ya serikali nini kifanyike baada ya hatua hizo nilizosema. Kwa hiyo, hicho ndicho kilichopangwa katika kumaliza tatizo hili ili lisijirudie mara kwa mara.

Hizi hatua nyengine mnazoziona za *ZUSP* na nyengine ni sehemu tu ya *component* ya mradi mkubwa ambayo itafanyika huko mbele katika kuondoa matatizo ya msingi yanayosababisha mafuriko na yanayosababisha kutuama kwa maji, yanayosababisha ardhi yetu inasababisha kudidimia kwa nyumba na kadhalika.

Kuhusu *TASAF* waheshimiwa eneo hili limechangiwa sana na kamati yenyewe na Mhe. Rashid Makame Shamsi pamoja na Mhe. Masoud Abrahman Masoud. Nataka niseme kwamba kwanza ushauri tunaupokea na ningependa kidogo nieleze kuhusu habari ya *TASAF*.

Leo tuko awamu ya tatu ya *TASAF* tulikuwa na awamu ya kwanza ya *TASAF*, tukawa na awamu ya pili ya *TASAF*. Awamu ya kwanza na ya pili tulijishughulisha zaidi na ujenzi wa miradi ya miundombinu ikiwemo miundombinu ya elimu, miundombinu ya afya, miundombinu ya kilimo, miundombinu ya masoko, miundombinu ya maji na miundombinu ya barabara ndio iliyokuwa *TASAF I* na *II*.

TASAF III imelenga zaidi katika kunusuru kaya masikini na ndio maana uko mpango wa kuzisaidia kaya masikini na zinategemea na mazingira ya familia, na namna unavyosomesha watoto wako na idadi ya watoto wako. Ruzuku inayotolewa ni kati ya 20,000 na 76,000 kwa mwezi kwa kila kaya. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana sana, Rais wetu wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mstaafu na aliyepo kwa mashirikiano makubwa ya kuhakikisha kwamba mradi huu wa *TASAF* unafanya kazi ya kusaidia wananchi wetu. Maana ni usimamizi wa Marais wetu ndio uliofanya tuchukue mkopo huu kutoka *World Bank* kusaidia watu wetu.

Namna gani wananchi wanashirikishwa.Waheshimiwa Wajumbe wananchi wetu wanashirikishwa kigezo namba moja cha kufikia hatua ya kuwatambua wanaofaa kupata msaada huu ni wananchi wenyewe katika shehia zao. Kuna mikutano mikuu ya shehia husika inafanyika kutoa maamuzi na mapendekezo ya kutambua nani anafaa kupata ruzuku hii. Kwa hiyo, mambo yote haya yanakuwa ni ya wananchi wenyewe katika shehia zao. Na kuna usimamizi katika kila shehia ya kamati ya watu 14 inayosimamia *process* nzima mpaka ya kupata zile fedha zinapokuja katika kaya. Lakini kweli kulijitokeza tatizo la baadhi ya watu ambayo walikuwa hawapaswi kupata msaada huu na wakawemo.

Imegundulikana baada ya kufanya tathmini maalum katika mwezi wa Aprili na Mei Unguja na Pemba waliokosa sifa wameonekana ni watu 450, na mwezi huu hawatopata fedha hizo za kaya. Kwa Unguja ni watu 158 na kwa Pemba ni watu 292, na tathmini itaendelea kufanywa kwa sababu zoezi ni endelevu wale wanao-*qualify* wataingia kupata msaada huo.

Kwa hiyo, kila hatua zitachukuliwa ili kuhakikisha kwamba mambo haya yanakwenda vizuri kwa haki na yanawasaidia wananchi wetu. Pale ambapo panatokea kasoro hatua zitachukuliwa kurekebisha kasoro hizo. Sisi kama binadamu hatuwezi kuwa na sifa za ukamilifu kwa asilimia mia moja, yatatokea mapungufu ya hapa na pale lakini wajibu wetu kwa ushauri wenu na kwa ushauri wa wananchi tunarekebisha hayo ili tusonge mbele katika kuwatekelezea na kuwahudumikia wananchi wetu. Kwa ujumla *TASAF III* inafanya kazi nzuri.

Kuhusu Mfuko wa Jimbo sina haja ya kurudia, namshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha amelieleza jambo hili kwa kina.

Kuhusu miradi ile ambayo sasa imeshindwa kuendelea na ilikuwa imeanzishwa miradi hii kupitia Mfuko wa *TASAF*. Wajibu wa *TASAF* ilikuwa ni kusaidia ile miradi ifanye kazi, baada ya miradi kufanya kazi sekta husika sasa ndio wajibu wake kuichukua ile miradi na kuiendeleza. Kwa hiyo, tungetegemea sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa kushirikiana na sekta husika munaisimamia miradi iliyo katika maeneo yenu ili ifanye wajibu wake, wajibu wa mfuko wa *TASAF* umemalizika, ile kwenu kutoa fedha kwa wananchi wale waweze kupata miradi ile, na ile ilikuwa ni miradi yao. Kwa hivyo, yanapotokea mapungufu sasa ni wajibu wetu sote kurekebisha mapungufu yale, ili miradi hiyo ichukue nafasi yake.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa ahadi kumi za Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, naomba nizitaje.

1. Ni ahadi ya mipira ya kusambaza maji safi na salama katika Kijiji cha Kilombero, ahadi hiyo imekamilika.
2. Boti kwa vijana walioamua kuachana na matumizi ya dawa za kulevya katika Kijiji cha Kiombamvua, ahadi imekamilika.
3. Shilingi milioni tano kwa ajili ya ujenzi wa kibanda katika mashine ya maji katika Kijiji cha Kiombamvua, ahadi imekamilika.
4. Ahadi ya vipaza sauti kwa kikundi cha dufu cha Kijiji cha Kiwani Micheweni Pemba ya milioni 1,600,000, ahadi imekamilika.
5. Boti na mashine kwa vijana wa Kijiji cha Makangale, Kaskazini Pemba yenye thamani ya 8,000,000, ahadi hii imekamilika.
6. Kikundi cha "Wingi si Hoja" cha Kojani nayo ahadi imekwenda vizuri.
7. Ahadi ya shilingi milioni 3,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Skuli ya Alhamis *Camp*, ahadi imekamilishwa.
8. Ahadi nyengine ni ahadi ya vipaza sauti kwa ajili ya Jumuiya ya Kuendeleza Madrasa ya Matemwe, ahadi hii bado inaendelea kufatiliwa tujue hatma yake.
9. Ahadi ya kompyuta na *printer* kwa ajili ya skuli ya binafsi Upenja, ahadi imekamilika; na
10. Ahadi ya mashine ya *photocopy* na kompyuta kwa ajili ya Skuli ya Mahudusi, Mkoa wa Kusini Pemba.

Tutaendelea kufuatilia ahadi na pale pale penye kasoro popote pale Waheshimiwa Wawakilishi nanyi mna wajibu wa kututanabahisha sisi kama nilivyosema ni binadamu, mapungufu yanaweza yakatokea.

Kwa upande wa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali eneo hili limechangiwa sana na kamati na Mhe. Yussuf Hassan Iddi na Mhe. Shehe Hamad Mattar, Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame na Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa).

Waheshimiwa kwanza kulikuwa kuna wasi wasi, je kiwanda hiki kitaweza kujiendesha wenyewe ikiwa sasa pato analolipata serikalini ni dogo halikidhi haja ya kuendesha kiwanda hicho.

Jibu kuwa wakala ndio jibu sahihi la kuendesha kiwanda hiki, kwa sababu tatizo kubwa la msingi yalikuwa ni manne.

Moja kwanza kulikuwa na uchache wa vifaa vyenyewe vya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, la pili ni utaalamu wa kukiendesha kiwanda chenyewe, la tatu ni mtaji wa kufanyia biashara, lakini la nne ni uwezo wa *access* ile ya kutumia zile fedha zinapoingia, maana hapo nyuma ikiwa kama idara hata wakikusanya hizo pesa lazima ziende Wizara ya Fedha hawezi kuingia katika mzunguko wa biashara.

Sasa ukiwa na uwakala watakuwa na *account* yao, kwa hiyo ile nguvu sasa ya kufanya biashara hata ukiwapa msingi mdogo wataweza kwenda. Sasa nini majibu ya hayo matatu ya juu niliyoyaeleza kuhusu uchache wa vifaa.
Sasa napenda niwapongeze sana Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Serikali ya Oman kwa msaada mkubwa waliotupa wa kutusaidia vifaa vya uchapishaji. Nina haki ya kujisifu kidogo kwamba kiwanda chetu kitakuwa cha mfano baada ya kukamilika ufungaji wa mitambo, kwa zaidi ya asilimia 90 mitambo imewasili na imefungwa, tumo katika hatua za mwisho za kukamilisha na hakuna kiwanda chochote Zanzibar hapa kinachoweza kushindana nacho kivifaa.

Kwa hivyo, sasa vifaa vipo, vipi tutapata utaalamu. Hawa wakandarasi wetu walioleta vifaa katika miezi mitatu ya kwanza wajibu wao wa kwanza ni kuwataalamisha watu wetu na kusimamia shughuli nzima ya uzalishaji katika Kiwanda cha Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

La pili dhana yetu kama serikali ni kuwa na makubaliano maalum baada ya ile miezi mitatu ili tuwa-*return* baadhi yao waendelee kutoa mafunzo kwa watu wetu na wasimamie uzalishaji ili tuweze kushindana na yeyote yule; tuwe na uwezo mzuri sasa wa kukiweza kukiendesha kiwanda hiki kibiashara na kutoa huduma kikamilifu kwa serikali.

Kwa hiyo, hata huu mtaji mdogo ambao tutapewa kwa mwaka huu utatuwezesha kwa kiasi fulani kusukuma mbele kiwanda chetu. Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi musiwe na wasi wasi na hatua ambazo serikali inachukua katika kuhakikisha kiwanda hiki kinafanya kazi. Kuna mitambo mipya 25 ambayo inafungwa pale ikiwemo ya *security printing*, ikiwemo ya kufanya hizo *posters* kubwa kubwa, ikiwemo ya kutengeneza maboksi, kufanya *labeling* ya aina yoyote, kiwanda cha kisasa chenye sifa zote, tuko tayari kushindana na yoyote. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kwa nini mwaka huu wa kwanza tumeweka kiwango kidogo cha makusanyo ya mapato. Kwa kweli kwa mwaka wa kwanza lazima Waheshimiwa Wajumbe mutuhurumie, huu ni mwaka wa kwanza ni mwaka sio tu wa uzalishaji lakini ni mwaka pia wa majaribio. Kwa hivyo, sasa tuko katika majaribio, tuko katika kufanya kazi ya uzalishaji, baada ya mwaka huu wa majaribirio mwakani sasa tutaweka kiwango halisi kutokana na matokeo yatakayojitokeza mwaka huu.

Kwa hiyo, naomba sana Waheshimiwa mutukubalie kwamba kiwango tulichokiweka kile cha makusanyo ya milioni mia saba na kitu, mutukubalie kiwango hicho ili tuendelee kukusanya kwa kiwango hicho ikitokea zaidi sote tujipongeze, lakini kwa kuanza mtupe nguvu hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu vyeti vya kuzaliwa kwa kuwa sasa mashine zipo na utaratibu mzuri utawekwa, vyeti vya kuzaliwa haitokuwa tena tatizo. Tutashirikiana na wenzetu wa Tawala za Mikoa kuhakikisha kwamba fedha zao wanazozipata za bajeti zinaingia, tutashirikiana na Waziri wa Fedha hapa ikiwezekana zinaingia moja kwa moja ili shughuli iende vizuri. Na pia serikali itakuwa na mpango maalum wa kusimamia taasisi yoyote ya serikali itakayochapisha nje ya wizara yetu kwa maana ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, wizara hiyo lazima tuiulize kwa nini ukaenda nje. Kwa sababu huduma nzuri utapata, bei nzuri itakuwepo na tutakuwa tunakiimarisha kiwanda chetu, wewe kwa nini ukatae kuleta huku, hapa itabidi tukuulize una mpango gani, ikiwa ni harufu ya rushwa basi Mamlaka ipo ile ya kusimamia mambo haya.

Mhe. Naibu Spika, jengine hapa ambalo liliwagusa Idara hii ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali ni suala la fedha za malipo zinaonekana vespa, *ciao* zote milioni 2,500,000. Nataka niseme watakaonunua kiwanda hiki ni vespa sio *ciao,* lakini kile kifungu cha matumizi na ndio ilivyo *programme* kinaonesha vespa, *ciao* kila usafiri wa magurudumu mawili unaonekana pale, lakini wao wanakwenda kununua vespa hawanunui *ciao*. Kwa hivyo, kiwango kile ni cha

vespa, kwa hiyo naamini Waheshimiwa Wajumbe mtaturidhia tuendelee na ununuzi huo, kwa maana ile ile ya kuimarisha kiwanda chetu kiweze kufanya kazi zake za kuwahudumia wananchi pamoja na serikali.

Tume ya Uchaguzi. Maelezo mengi ya Tume ya Uchaguzi atakuja kuyatoa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, napenda tu mimi niwashukuru kamati, Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mhe. Shehe Hamad Mattar, Mhe. Mussa Foum Mussa, Mhe. Hamza Hassan Juma kwa kuchangia katika eneo hili. Lakini kama tulivyosema kwamba uchaguzi umemalizika, na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atupe uhai na uzima kwa uchaguzi mwengine hapo 2020. *(Makofi)*

Kuhusu walioharibu uchaguzi. Uchunguzi unaendelea na wale wote watakaobainika mkondo wa sheria utachukua nafasi yake.

Suala la Ajira kwa Tume. Waheshimiwa nataka tuelewane kidogo, kwamba wako waajiriwa wa muda na waajiriwa wa kudumu. Waajiriwa wa muda inabidi uwaajiri wakati wa uchaguzi tu, na ukiwaajiri kwa kudumu utawalipa mshahara kwa miaka mitano ama bahati mbaya itokee *by-election* tena ndio watafanya kazi. Kwa hivyo, haiwi mantiki kuwa waajiriwa wa muda nao wawe katika uajiri wa kudumu, na taratibu za ajira ni zile zile zinazofuatwa kwa utaratibu wote katika sekta ya umma. Ni kwamba Tume ya Utumishi Serikalini ndio hutoa matangazo na ndio hufanya maamuzi ya nani na nani aajiriwe sio Tume ya Uchaguzi. Kwa hiyo, hilo liko kisheria na litaendelea kuwa hivyo.

Kwa upande wa Baraza la Wawakilishi. Waheshimiwa kuna hatua mbali mbali za Baraza la Wawakilishi tumefanikiwa, tunalo tatizo la msingi la *echo* humu ndani na hasa unaposimama hapa inakuwa tabu na Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri ni mashahidi wanajua tatizo la hapa, unaweza kusema huko kwa nguvu nyingi sana ukasema mpaka unapasuka lakini kusikilikana hapa ndio kishindo. Kusimama hapa sio kazi rahisi waheshimiwa, mnaona hivi anavyofika Mwenyekiti akija hapa pana mbinde yake, hapa ukikosea maana yake umekosea. Kwa hiyo, tunakaa kwa heshima na taadhima kutaka kujibu maswali yenu, kutaka kutoa hoja, kufafanua ili muweze kuelewa lakini lazima tusikie.

Mimi nakubaliana kabisa umuhimu wa kumaliza tatizo la *echo* katika ukumbi wetu huu jitihada zimeanza. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe tutaendelea kushirikiana na Baraza la Wawakilishi ili tatizo hili lipate ufumbuzi.

Kuhusu ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Pemba. Tumefanya juhudi sana na nia yetu ukumbi ule utumike na ufanye kazi, lakini katika hali halisi katika mwaka huu wa fedha nyote mnajua mtihani wetu tusingeweza kutenga fungu la kuimarisha ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Pemba.

Tupeane subira ili mwakani *Inshaallah* tuone, maana kuna gharama katika kuutengeneza ukumbi ule ufikie hadhi yake ili waheshimiwa mkienda pale mpate hadhi yenu. Hatuwezi kwenda hali ile ilivyo sasa. Kuezeka lile paa tu kunataka zaidi ya shilingi 366,000,000 mbali ya matengenezo mengine. Kwa hiyo, nawaomba sana waheshimiwa mtupe muda tushughulikie jambo hili, naamini tutalishughulikia vizuri kwa hadhi yenu ili ukumbi ule ufanye kazi inayotakiwa.

Kwa upande wa udhibiti wa dawa za kulevya. Eneo hili lilichangiwa sana na kamati yetu. Limechangiwa na Mhe. Moh'd Mgaza Jecha, Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, Mhe. Rashid Makame Shamsi, Mhe. Masoud Abrahman Masoud na pia Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), Mhe. Shaib Said na Mhe. Abdalla Diwani.

Jambo hili ni kubwa na linataka mashirikiano ya pamoja; serikali, wananchi, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na viongozi wote. Sio jambo jepesi, ni jambo gumu linahitaji mashirikiano. Lakini niseme tu, Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya ina wajibu wake katika muongozo wa kisera, wajibu wake katika kusimamia na kutoa miongozo, lakini watekelezaji wakuu katika jambo hili ni suala zima la ufuatiliaji wa kesi ambapo sekta tatu ndio zinahusika moja kwa moja; Polisi, Ofisi ya *DPP* na Mahakama. Sasa hapa ndipo mtihani mkubwa ulipo, yako matukio mengi yametokea katika eneo hilo, sasa baada ya kutafakariwa kwa kina sekta tatu hizi zimeamua zije na utaratibu maalum wanaoita *case flow management*, maana yake kukiwa na utaratibu wa pamoja katika ufuatiliaji wa dawa hizi za kulevya. Kwa maana kuwe na mashirikiano makubwa zaidi kati ya Polisi, Ofisi ya *DPP* na Mahakama.

Mhe. Naibu Spika, lakini jambo moja muhimu hapa liko kwa wananchi kuwa tayari kutoa ushahidi. Moja katika tatizo eneo hili ni wananchi kuogopa au kutokuwa tayari kutoa ushahidi, sasa tusipokuwa tayari kutoa ushahidi tutaendelea kupata matatizo sana kwa watu wetu. Nakubali kwamba wapo watu wanaojifanya wao Maree, (mabingwa) kwa njia moja au nyengine kuharibu utaratibu wetu huu wa kudhibiti dawa za kulevya. Lakini nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe na wananchi serikali ya awamu ya saba kipindi hiki cha pili nia, dhamira ni kubomoa mtandao mzima wa dawa za kulevya. *(Makofi)*

Hivi sasa tunashauriana kwa karibu sana na wenzetu kwa upande wa Tanzania Bara kubuni kila hatua ya kuchukua ili tuchukue sote, lakini tunawaombeni Waheshimiwa kuna hatua kali zitakazochukuliwa dhidi ya jambo hili. Tunawaomba mtusaidie tukianza kazi isiwe tena Mheshimiwa hivi na hivi, tuacheni tufanye kazi tuwashughulikie watu hao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa sheria ya madawa ya kulevya, sheria hii haina matatizo, sheria iko vizuri, ya karibuni tu, tatizo kama nilivyosema mwanzo lipo kwenye usimamizi na wasimamizi wakubwa ni Polisi, *DPP* na Mahakama. Kesi hizi lazima zipate majibu. Kwa hiyo, sheria nzuri inakidhi haja, inatoa hukumu kali, cha msingi ni usimamizi wa sheria yenyewe, lakini naamini huo utaratibu ambao tunaupanga kwa kushirikiana na wenzetu kutoka Tanzania Bara na huu utaratibu uliowekwa wa *case flow management,* majibu yatapatikana.

Vile vile Waheshimiwa walitaka kujua kiwango cha madawa yaliyokamatwa. Kati ya mwaka 2013 na 2016 jumla ya kilo 604.91 ya madawa haramu ya kulevya yalikamatwa ambayo kati ya hayo bangi iliongoza kwa kuwa kilo 500.43, *heroine* kilo 39.24, *cocaine* kilo 32, mirungi kilo 44, *valium* kilo 3.41. Kesi hizo zimeweza kupelekwa Mahakamani na watuhumiwa 531 walitiwa mbaroni, na hivi sasa ziko kesi ambazo zimeshughulikiwa na bado kesi nyengine zinaendelea. Kwa hivyo, kwa sababu ya jambo hili kuwa liko Mahakamani huwezi kulisemea sana kwa mujibu wa sheria.

Waheshimiwa hususan Mhe. Rashid Makame Shamsi alitaka kujua kuhusu watoa taarifa wanalindwa vipi? Kwa mujibu wa sheria ya udhibiti wa madawa ya kulevya kifungu 32(1) na (2) kimetoa mwongozo wa kumlinda mtoa taarifa pamoja na adhabu kwa yeyote atakayevujisha taarifa za raia mwema alizozitoa kwa wahusika. Kwa hiyo, naamini sana kwamba sasa kwa kiasi kikubwa huwa haitokei sana kutolewa zile siri za raia wema wanaopeleka na watu wengi waliweza kutiwa mbaroni.

Niseme tu kwamba kuna mkakati maalum juu ya vyombo vya ulinzi na usalama, vyote vinashirikiana vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Zanzibar katika kupambana na jambo hili, pamoja na kupambana na wale watu wanaogeuza ukweli wa jambo hili ikiwemo kutoa taarifa au kuyabadili madawa ya kulevya baada ya kuwa madawa ya kulevya kuwa unga wa ngano ama saruji, yote hayo yanashughulikiwa na vyombo hivi.

Kuhusu ujenzi wa nyumba ya Kidimni ya *Rehabilitation Centre,* tunaamini katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 itamalizika. Walitaka kujua

waheshimiwa walioathirika katika Zanzibar ni wangapi. Kwanza kwa takwimu za kidunia wastani wa waathirika ni kama asilimia 1 ya wanadamu wote peke yake, lakini kwa Zanzibar ni kati ya watu 7,000 mpaka 10,000 ndio walioathirika na madawa ya kulevya. Ukitizama haijafikia hicho kiwango cha asilimia 1, lakini huwezi kujisifu kwa sababu tatizo lipo na kubwa. Kwa hivyo, kwa pamoja lazima tushirikiane na hasa kwa upande wa *heroine,* kwa maana ya udungaji wa sindano. Walioathirika kwa hapa Unguja ni watu 3,000 na kwa Pemba ni watu 200; kwa hivyo jumla ni watu 3,200 ndio wanaathirika kwa kujidunga sindano.

Waliofaidika na *Sober House* ambao watu walipita pale ni kama 7,881; wanaume walikuwa 7,482 na wanawake walikuwa 394. Kutoka Unguja walikuwa 5,654 na kutoka Pemba ni 1,825. Kwa sasa kila nyumba inaruhusiwa kukaa watu 25, kwa hivyo kwa sasa hivi tunao watu 300 katika *sober houses*.

Sober houses zinaendeshwa na watu binafsi, inachofanya serikali inatoa ruzuku ya shilingi 1,500,000 kwa mwaka. Kadiri ya uwezo wa serikali utakavyokuwa mzuri na kadiri ya hizi *sober houses* zitakapoweza kufanya vizuri, wajibu wake serikali itafikiria ushirikiano wa zaidi kwa sababu zimetoa *figure* kubwa na tunaona ni jambo la msingi kuzisaidia ili kufanya wajibu wake vizuri.

Waheshimiwa Wajumbe hususan kamati ilikuwa na wasiwasi wa matumizi ya shilingi 200,075,000 kwa ajili ya *laundry*. Waheshimiwa sio *laundry* kwa maana ya kufua nguo, *laundry* kwa maana ya kujenga chumba hicho cha *laundry* yenyewe, kuweka mashine za kisasa, kuweka miundombinu yake, kupatikana umeme na maji. Kwa hiyo kuwa na *laundry* kamili ya kufanyia kazi hii. Mimi nadhani kwa fedha hizo zinakidhi haja, sio fedha nyingi ambazo kuweza kusema tuzipunguze tuzipeleke kwa Mpiga Chapa Mkuu wa serikali. Nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tukubaliane kuwapa hizi pesa ikatengenezwe *laundry* tuwasaidie watu wetu hawa wanafanya kazi kubwa.

Jamani mtihani huu wa madawa ya kulevya watoto wetu wamekuwa kama zezeta vile, tunapopata angalau wakakubali kuondoka kule ili waje wajiunge warudi katika jamii wawe watoto wema tushukuru sana. Hali ya watoto wa madawa ya kulevya kuwa ni nusu binadamu nusu maiti, hawako katika hali ya ubinadamu kabisa. Watoto hawa wanafikia kiwango wanaweza kumuua hata mzee wao, mtu anaweza kumuua baba yake, kumuua mama yake na wote kuwa akili hazimo. Kwa hivyo, inapotokea kwa vyovyote vile ikasaidia mbinu yoyote inayosaidia katika kuwarudisha watoto hawa wawe salama, nafikiri mbinu hiyo tusii-*discourage,* tuiunge mkono mambo yaende vizuri. Hali ile ni mbaya sana.

Kuhusu maambukizi ya UKIMWI. Takwimu zinaonesha utafiti wa mwaka 2007 maambukizi yalikuwa asilimia 0.6 na utafiti wa mwaka 2012 unaonesha maambukizi ni asilimia 1. Haya yanaonesha ni maambukizi madogo katika ukanda wetu huu wa nchi za jangwa la Sahara. Kwa hivyo, sisi tuna nafuu kidogo kuliko wengine, lakini sisemi kwamba nafuu ndio tusiongeze nguvu ya kupambana na UKIMWI, tunapaswa kuchukua kila hatua za kupambana na janga hili la UKIMWI. Hivi sasa tunashirikisha taasisi mbali mbali za kidini, taasisi za kiraia, na wahusika wote ili kufanya kazi kwa pamoja kupambana na jambo hili na elimu inatolewa.

Inaonekana maambukizi yanawakuta zaidi yale makundi maalum, ndiyo aliyoyazungumzia sana Mhe. Suleiman Sarahan Said, yale yamechukua nafasi kubwa zaidi, *Inshaallah* ndugu zetu hawa wataelewa tatizo hili kutokana na taaluma inayotolewa ili yasiwakumbe maambukizi haya.

Kuhusu Asasi za Kiraia. Tume imefanya zoezi la kuorodhesha na kuzitathmini asasi za kiraia mara kwa mara, na zoezi la mwisho lilifanyika mwaka 2014 na hivi karibuni zoezi jengine litafanyika kufanya tathmini kwa asasi hizo ili kuhakikisha zinafanya kazi zinazotarajiwa na kujiepusha na asasi za mifukoni. Kwa hiyo, kazi hii itafanyika Waheshimiwa ili kusitokee wajanja tena wakawa hawafanyi ile kazi nzuri ambayo inakusudiwa kuifanya.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa watu wenye ulemavu. Wajumbe wengi wamesema kwamba bado Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijatambua vizuri suala la watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa serikali imefanya jitihada kubwa ya kutambua kundi hili. Mimi naamini kabisa ni raia wenzetu wanaohitaji kuhurumiwa, wanahitaji tushirikiane nao na wao wapewe mchango wao katika taifa kutokana na mazingira yao. Kwa hiyo, serikali sio tu imeweza kuanzisha Idara ya Watu wenye Ulemavu, imeweza kuweka Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu, imeweza kuanzisha Sera na Sheria ya Watu wenye Ulemavu, imeweza kutoa ruzuku kwa jumuiya na vikundi mbali mbali vinavyohusiana na watu wenye ulemavu na ikaendelea kufanya usajili kwa kila kikundi ambacho kitasaidia watu wenye ulemavu.

Sasa hata mipango yetu ya ujenzi ya miundombinu tunaweka sana kipaumbele cha kuwarahisishia watu wenye ulemavu wapate unafuu. Kwa hivyo, ni mtazamo wa serikali utakaokuwa unatilia mkazo kwenye ujenzi wetu wa barabara, ujenzi wa nyumba, *airports* na kadhalika, kila jambo hili tunaweka mkakati ili kutambua umuhimu wa wenzetu wenye ulemavu.

Kwa hivyo, ningependa Waheshimiwa muelewe nia na dhamira ya serikali ni kushirikiana na makundi yote haya muhimu ili kufanya kazi nao kwa pamoja, tuwasaidie na kadiri serikali itakavyokuwa na uwezo basi itaongeza nguvu zake. Mengine Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakuja kuyaelezea kwa kina.

Kuhusu Sherehe na Maadhimisho. Waheshimiwa Wajumbe ni kweli zipo sherehe tunaweza kupunguza fedha lakini sio Sherehe za Mapinduzi ya Mwaka 1964. Kwa hiyo lolote na liwe, lakini lazima tusherehekee Mapinduzi yetu ya mwaka 1964. Sherehe nyengine zote tunaweza kupunguza na hata hizi za Mapinduzi tunapunguza lakini lazima tuzisherehekee, kwa sababu ni Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, Waheshimiwa ndiyo yaliyotuleta hapa tulipo leo. (*Makofi*)

Ni Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 ndio yaliyotufanya kupiga hatua hii ambayo tumetulia, na Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 ndio yameleta Muungano wetu. Wapo wanaoyatizama kwa jicho baya, wanasherehekea tuyapunguzie kasi hilo halitotokea ng'o! (*Makofi*)

Kwa hiyo, ninachosema Waheshimiwa tutafanya kila jitihada fedha zinazotokana na shughuli hizi zifanyike vizuri, zisitumike vibaya, na yeyote atakayezitumia vibaya mkondo wa sheria utachukua nafasi yake. (*Makofi*)

Pia liko lalamiko la kuwa kumeongezeka matumizi, ni kwamba fedha zilizoongezeka za matumizi zinatokana na majumuisho ya mishahara, posho maalum na mchango wa serikali katika mfuko wa *ZSSF*.

Kwa mwaka 2015/16 Bajeti ilikuwa milioni thamanini na saba laki mbili na hamsini na nane elfu, (87,258,000), lakini kwa 2016/17 Bajeti ni milioni mia moja na kumi na saba na thamanini na mbili elfu (117,082,000), lakini hiyo ni kwa sababu ya mishahara, posho maalum na mchango wa mfuko wa *ZSSF* ndio maana ya kuongezeka kiwango.

Kuhusu ukodishaji wa milango ile 8 ya maduka, milioni tisa laki tatu na elfu kumi (9,310,000) kwa mwaka huu hatuwezi kufanya marekebisho. Maana tumeshafanya nao mikataba hawa wananchi ambao tunawakodisha, lakini ushauri wa Wajumbe tunaupokea kwa miaka inayokuja tuweze kufanya marekebisho hayo ili kodi iongezeke ya milango ile.

Kuhusu ukodishaji wa vifaa mbali mbali kwa sasa pia vifaa vyenyewe haviko katika hadhi kubwa lazima tujue kwamba kiwango hichi tulichoweka cha fedha milioni tatu ndio ambayo tunaona ni kiwango halisi.

Tunawaomba Waheshimiwa kwenye eneo hili mtupe uvumilivu ili tuweze kujipanga zaidi tuiimarishe Idara hii iwe na vifaa vya kisasa baadae ndio tuweze kutoa kodi stahiki na kuwa na kipato kikubwa zaidi.

Kuhusu sherehe zinazofanyika Tanzania Bara mara nyingi hizi huwa ni sherehe mbili, sherehe ya Uhuru wa Tanzania Bara na sherehe za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na ya tatu ni ile siku ya Mashujaa. Na kwa kawaida viongozi wa Zanzibar wanapokwenda kule wanatakiwa wajitegemee wenyewe, kama wale wa Tanzania Bara wanapokuja kwenye sherehe zetu hapa wanatakiwa wajitegemee wenyewe. Lakini kwa wananchi wanaopelekwa kutoka Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba kwenda Tanzania Bara hizi hulipiwa na Afisi ya Waziri Mkuu kwa sababu hupata mualiko maalum. Huo ndio utaratibu unaofanyika.

Nimalizie kuhusu Madiwani. Waheshimiwa walizungumzia kuhusu suala la madiwani. Waheshimiwa kutokana na sheria mpya lazima kwanza kutoke tangazo rasmi ndipo hatua nyengine zichukuliwe za kuchagua viongozi katika serikali za mitaa kwa maana ya kuunda Halmashauri, Mabaraza ya Mji au Manispaa.

Tuna furaha kusema tangazo rasmi sasa limetoka, kwa hivyo hatua nyengine zitafuata. Lakini kwa upande wa kula kiapo. Kula kiapo inatakiwa ndani ya wiki nne kutoka siku ya kuchaguliwa au kuteuliwa uwe umekula kiapo kama dua. Kwa hiyo, hiyo ndio hasa hali halisi yetu kwa upande huu.

Waheshimiwa Wajumbe kwa sababu ya muda na kwa sababu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakuja hapa awatambue Waheshimiwa mmoja mmoja aliyechangia, na atakuja na yeye kuwaomba muipitishe bajeti yetu baada ya kutoa ufafanuzi mbali mbali. Na mimi kwa haya machache naomba nirudie kuwashukuru sana, na nawaomba tena muipitishe bajeti yetu hii kwa asilimia mia moja. Ahsanteni sana. (*Makofi*).

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima, na tukafika leo hapa kuhitimisha hotuba ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Pili niwashukuru Wajumbe wote waliochangia hotuba hii ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, najua michango yao, ushauri wao, mapendekezo yao yote haya yalikuwa na nia ya kufanikisha shughuli za Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Napenda niwahahikishie Afisi yangu itazingatia michango yao yote, ili kufanikisha utelekezaji wa kazi zetu, kufikia malengo tuliyojiwekea.

Pia niwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa kutoa ufafanuzi wa kina kuhusiana na mambo mbali mbali yaliyoelezwa katika Baraza lako tukufu, kuhusiana na sekta zao na kuyajibu kwa ufasaha na kwa uwazi kabisa.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda sana kumshukuru Mhe. Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum Mhe. Said Soud Said, kwa namna alivyoelezea hali halisi ya siasa kule Pemba na hali halisi ya siasa kwa jumla. Kule kwetu kulikuwa na mtu mmoja alikuwa anaitwa Said Soud alikuwa anatisha sana. Sasa naona Said Soud huyu naye lazima atakuwa tishio kwa wale jamaa kule. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, napenda na mimi kuungana na Wajumbe kuipongeza Tume ya Uchaguzi, naungana nao na mimi kwa kuipongeza Tume ya Uchaguzi kwa kusimamia vizuri sana uchaguzi wa marudio wa tarehe 20 Machi 2016.

Najua walikuwa wavumilivu sana, walisikia mengi na yalisemwa mengi kwamba uchaguzi huu hauwezi kurudiwa, watakuja watu wa *Commonwealth* hapa, watakuja watu wa Umoja wa Mataifa, uchaguzi haurudiwi na kadhalika. Lakini Tume ya Uchaguzi imesimama imara na wakaweza kuusimamia uchaguzi wa tarehe 20 na ukafanyika kwa mafanikio makubwa sana. (*Makofi*)

Wengi wamesema uchaguzi umekwisha haurudi tena mpaka 2020. Wenzetu hawa walioamua kutia mpira kwapani shauri yao, sisi tulioamua kuendelea tunashukuru Mungu kufika hapa tulipo leo. Tumefanya uchaguzi kwa amani na utulivu, Chama cha Mapinduzi kimeshinda kwa asilimia 91.4, tumeunda serikali na leo tuko kwenye Baraza la Wawakilishi kupitisha Bajeti ya Serikali yetu kwa mwaka 2016/2017. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema maelezo hayo naomba kuwatambua waliochangia hotuba ya Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kama ifuatavyo:-

Mhe. Omar Seif Abeid, Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi wa Wakuu wa Serikali.
Mhe. Omar Seif Abeid
Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
Mhe. Yussuf Hassan Iddi
Mhe. Shehe Hamad Mattar
Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf Al-wardy
Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini
Mhe. Bahati Khamis Kombo

Mhe. Zaina Abdalla Salum
Mhe. Rashid Makame Shamsi
Mhe. Suleiman Sarahani Said
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Masoud Abdrahman Masoud
Mhe. Mussa Foum Mussa
Mhe. Mohamed Ahmada Salum
Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi
Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
Mhe. Naibu Waziri wa Afya
Mhe. Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum (Mhe. Said Soud Said)
Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira
Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, na
Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Naibu Spika, nataka nirudie kidogo kwenye Tume ya Uchaguzi. Wenzetu wanasema Tume ya Uchaguzi lazima iondoke, ndani humu wamesema Tume ya Uchaguzi iendelee kuwepo. (*Makofi*)

Nataka niseme tu kwamba Tume hii ya Uchaguzi itaendelea kuwepo, kwa sababu masharti ya kuiondoa tume hii ni makubwa. Rais alikuwa na uwezo wa kuiteua hana uwezo wa kuiondoa kwa sababu tume hii kuiondoa lazima iende kwa mujibu wa Katiba. Kwa sababu tume hii inalindwa na katiba kwanza labda tume hii ijiuzulu wenyewe. Kwa hivyo, vyenginevyo haiwezekani. Labda tume hii iundiwe tume iichunguze kama kweli inaweza kuendelea na kazi hiyo, jambo ambalo pia nalo ni gumu.

Tatu tume hii mpaka ifike muda wake, na tume hii kuondoka mpaka 2018. Kwa hivyo, wanaosema wale jamaa wale kwamba tume hii iondoke haiwezekani. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, wengi humu ndani walizungumzia kuhusu suala la gesi na mafuta. Kwanza nachukua fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira kwa maelezo yake juu ya suala hili. Nakubaliana naye kwamba suala la mafuta na gesi asilia ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Hivyo, suala la kuwashikirisha wadau wote katika hatua za mwanzo za utungaji wa sheria, wa Sera, Sheria na Miongozo mingine ni muhimu sana.

Aidha kuhusu suala la Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuwapa uzoefu na kusimamia suala la mafuta na gesi asilia katika nchi nyengine pia lina umuhimu wake. Hivyo, naomba ifahamike kwa kuletwa na kusomwa kwa mswada huo kwa mara ya kwanza katika Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika, hakutazuia kufanyika hatua mbali mbali zikiwemo za Baraza la Wawakilishi kuwapeleka Wajumbe wake katika nchi mbali mbali.

Katika nchi zilizofanikiwa kwa sababu ya kuwa na mafuta na gesi asilia na zile nchi ambazo hazikufanikiwa ili ziweze kufananisha. Waliofanikiwa wamefanyaje, waliokuwa hawakufanikiwa wamefanya makosa yepi na sisi tufanye nini.

Mhe. Naibu Spika, kwa umuhimu mkubwa sana, napenda kuwashukuru Mhe. Rais Mstaafu Dkt Jakaya Mrisho Kikwete na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt Ali Mohamed Shein, kwa busara zao zilizopelekea kupeka mswada wa sheria Bungeni kulitoa suala la mafuta na gesi asilia kwenye orodha ya mambo ya Muungano. Kama sio busara hiyo ina maana ingebidi tungojee mpaka Katiba Mpya iliyopendekezwa iweze kupigiwa kura, jambo ambalo lingechukua muda mrefu na leo tusingekuwa tunazungumzia suala la mafuta na gesi asilia. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la ajira za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda kulifahamisha Baraza lako tukufu kuwa hii ni moja kati ya mada muhimu zilizozungumzwa katika vikao vya Muungano vinavyojadili hoja na changamoto za Muungano ambalo limeshapatiwa ufumbuzi.

Katika makubaliano hayo imeamulika kuwa katika kila ajira za sekta ya Muungano asilimia 21 zitatengwa kwa ajili ya Zanzibar na asilimia 79 kwa Tanzania Bara. Katika utekelezaji wa suala hili tayari Wizara zote za SMZ na SMT zimeshajuilishwa na zipo katika hatua za utekelezaji.

Kuhusu suala la ajira za walimu, serikali imelichukua na italifanyia kazi ipasavyo suala hili ili kuhakikisha kwamba walimu waliohitimu wanapata ajira na hatimae kunyanyua na kiwango cha elimu nchini. Nafikiri Waziri wa Elimu amelieleza hili.

Mhe. Naibu Spika, mapambano zaidi ya rushwa na uhujumu uchumi. Serikali inaendelea kuziwezesha taasisi ilizoziunda kusimamia masuala haya ili kuhakikisha zitatelekeza majukumu yake ipasavyo.

Aidha Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tayari ameshamteua Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya viongozi wa Umma ili kuhakikisha kuwa Tume hiyo inaanza kazi zake za kutekeza majukumu yake.

Ni matumaini yangu kwamba kuanza kazi kwa Tume hii kutaondosha matumizi mabaya ya madaraka na Afisi za Serikali. Nachukua nafasi hii kuvitaka vyombo vyote vilivyoundwa kusimamia maadili ya viongozi, vita dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi kutokuwa na muhali na mtu au taasisi yoyote itakayokiuka maadili katika kuwahudumia wananchi.

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu washirikiane na Tume hii ya Maadili watakapokuja kuwahoji, kuwauliza maswali wajibu kwa ufasaha na waeleze hali ya ukweli. Kama si hivyo mutakuwa munavunja sheria, na Tume hii ya kisheria inaweza kumpeleka mtu Mahakamani. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kuhusu nafasi za kisiasa kwa watu wenye mahitaji maalum. Serikali inatambua umuhimu na mchango wa watu wenye ulemavu katika ujenzi wa taifa letu. Kwa kutambua hilo, serikali inaendelea na utaratibu wa uandaaji wa sera ya watu wenye ulemavu ambayo ndiyo itakayotoa dira ya ushirikishwaji kwa watu wenye ulemavu katika nyanja zote zikiwa za kisiasa, kiuchumi na kijamii. (*Makofi*)

Ninachukua nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wawakilishi kuwa na subra, na suala hili linapewa umuhimu unaostahiki. Hata hivyo wenzetu wa Tanzania Bara wameshaonesha njia kwa kuteua wenzetu wawili wenye ulemavu kwa kuweka mmoja Naibu Waziri na mmoja Naibu Katibu Mkuu. (*Makofi*)

Kwa hivyo na hapa kwetu bila shaka haya yatatendeka. Karibuni nilitembelea Ofisi za Watu Wenye Ulemavu na nimezungumza nao na nimewaahidi kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafanya kila linalowezekana kila mahali ambapo wenzetu wenye ulemavu wanazo sifa za kufanya kazi pale, lazima waajiriwe pale. Kwa hivyo hayo yatatekelezwa. (*Makofi*)

Kuhusu suala zima la amani na utulivu wa nchi. Wengi wamelizungumza hilo lakini kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwamba bado serikali inaendelea kusisitiza kwamba suala hili halina mjadala, na kwamba serikali haitomvumilia mtu au kikundi chochote ambacho kitaonesha dalili za uvunjifu wa amani.

Ninachukua fursa hii kuwaomba wananchi kuendeleza kutunza amani iliyopo na kuripoti vitendo vyovyote vinavyoashiria uvunjifu wa amani. Pia ninavitaka

vyombo vyote vinavyosimamia amani na usalama wa nchi kuendelea kutekeleza majukumu yao ipasavyo ili kuhakikisha amani na usalama wa nchi yetu vinaendelea kudumu. Ninaviagiza vyombo vyetu vya usalama kuhakikisha kwamba kuwachukulia hatua wale ambao wanaojaribu kuvunja sheria ya nchi hii au kuhatarisha amani na utulivu, wawachukulie hatua kali za kisheria. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, limezungumzwa hapa suala la uwiano wa majimbo kwa nafasi ya Ubunge na Uwawakilishi. Hivi karibuni Tume ya Uchaguzi Zanzibar ilikata majimbo hamsini, kutoka hamsini kwenda hamsini na nne. Hii ilikuwa ni kwa mujibu wa Ibara ya 120 (1) ya Katiba ya Zanzibar ya 1984. Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ina mamlaka ya kugawa majimbo ya uchaguzi ya Zanzibar kwa madhumuni ya uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani ili kwa uchaguzi wa 2015 ambao ulifanyika tarehe 20 Machi, 2016. Zanzibar, Tume ya Uchaguzi iligawa majimbo na kuongeza idadi kutoka hamsini hadi hamsini na nne.

Ibara ya 74 (6) (c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inaipa mamlaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi kugawa majimbo ya uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano na Tanzania na Wabunge. Katika uchaguzi mkuu wa 2015, Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliongeza majimbo kutoka mia mbili na thalathini na tisa hadi mia mbili na sitini na nne kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kati ya haya, majimbo mia mbili na kumi na nne ni ya Tanzania Bara na majimbo hamsini yalibaki Tanzania Zanzibar.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi haikuweza kuongeza majimbo ya uchaguzi kwa upande wa Zanzibar kwa sababu ya matakwa ya Kikataba. Chini ya 98(1) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 ili kubadilisha idadi ya Wabunge hamsini kutoka Zanzibar ni lazima Katiba ibadilishwe na kuungwa mkono na Wabunge wa pande zote za Muungano kwa kiwango kilichoainishwa.

Aidha, Tume ya Uchaguzi Zanzibar ilipokamilisha ugawaji wa majimbo kwa kuongeza majimbo manne kwa uchaguzi wa Zanzibar, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilikuwa limemaliza vikao vyake na baadae kuvunjwa. Hivyo kwa wakati huo isingewezekana kukamilisha mchakato wa kurekebisha Katiba ili kuweza kuongeza idadi ya Wabunge visiwani kwa majimbo manne kwa uchaguzi wa 2015.

Kwa kifupi kwa uchaguzi wa 2015, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilitangaza jumla ya majimbo mia mbili na sitini ya uchaguzi nchi nzima, yakiwemo hamsini tu ya Zanzibar. Hivyo hakuna ugawaji mpya utakaofanyika kwa majimbo ya uchaguzi kwa majimbo ya uchaguzi kwa 2015. Ni kwa uchaguzi wa 2020 ndipo Tume ya Taifa katika kugawa majimbo upande wa Zanzibar, itakapozingatia ongezeko la majimbo kama ilivyofanywa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

Nimeona hili nilieleze kwa kirefu kwa sababu aliyezungumza suala hili, alisema tayari watu walikuwa wana-*trot* kwenye majimbo mapya. Sasa ni vyema sasa hivi wangojee mpaka mwaka 2020 pindi majimbo yatakapatikana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ussi Yahya alizungumzia juu ya suala moja hapa Zanzibar anayetembea huko Wilayani na kujiita Rais. Mhe. Naibu Spika, kwanza huo ni uvunjifu wa sheria na usimamizi wa vyombo vya sheria lazima vichukue hatua inayostahili. Lakini tunajua Rais ni mmoja Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye amepata ridhaa ya wananchi wa Zanzibar. Aliyechaguliwa kwa asilimia 91.4. (*Makofi*)

Wanaojiita Marais, ninakumbuka ule wakati nilipokuwa mdogo, wakati wa siku kuu tunapokwenda pale Mnazi Mmoja kwenye mabanda, nikakuta banda moja limezungushwa magunia halafu lina vikaragosi vinafanya hivi. Sasa hao wanaojiita Marais ni sawa sawa na vikaragosi. Rais anajulikana ni Dkt. Ali Mohamed Shein na siyo mtu mwengine yeyote. Wanayemtangaza yeye kwamba ni Rais wanafanya makosa, tena makubwa sana ya kisheria. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mwisho naona mambo mengi yamezungumzwa na Mhe. Waziri wa Nchi (O) Makamu wa Pili wa Rais, sina haja ya kusema mengi kwa sababu ya muda. Lakini namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kujibu maswali mengi sana ya Wajumbe. Hivyo inabidi yale mengine ambayo hatukuwahi kuyataja kwa sababu ilikuwa ni maswali tutafuta namna ya kuyajibu. Lakini niseme lile la Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini. Alisema kwa sababu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inashughulikia mawizara yote, basi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kulikuwa na *desk officers*, ni wazo zuri na tutalishughulikia ipasavyo.

Kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Majimbo Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ameeleza vizuri, lakini kuna maombi ya kwamba wafanyiwe semina. Naona ni vizuri na wazo zuri linaweza kusimamia semina hiyo ikafanywa na Waziri wa Fedha na Mipango anaweza akasaidia katika hilo. (*Makofi*)

Mhe. Rashid Makame alisema kwamba mwaka 2012 nilitoa ahadi kwa taasisi. Sasa hakusema ni taasisi ipi na ilikuwa ni ahadi gani. Kwa hivyo naomba tuonane ili anifahamishe zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mambo mengi yamezungumzwa. Umezungumzwa ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Pemba. Tutaushughulikia hali ya kiuchumi ikiruhusu. Maana ukumbi ule unahitaji matengenezo makubwa. Mimi mwenyewe niliutembelea nikaona kazi ambayo inahitajika kwa ukumbi ule mpaka ukaweza kufanya vizuri.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa kabla sijatoa hoja, naomba radhi niliwaacha Wajumbe wawili sikuwataja katika orodha ile waliochangia. Nao ni Mhe. Mohammed Said Mohammed na Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Nawaomba radhi sana.

Baada ya hapo Mhe.Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Niwashukuru Wajumbe wote kwa michango yao, na sasa baada ya maelezo hayo naomba kutoa hoja kwamba Baraza liidhinishe fedha zilizoombwa kama zilivyoombwa katika hotuba yangu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa maelezo yako. Sasa inabidi Waheshimiwa Wajumbe niulize kwamba kama hoja ya Makamu wa Pili wa Rais inaungwa mkono. Wanaounga mkono hoja wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aje na yeye kuliomba Baraza kwa ajili ya kukaa Baraza kama Kamati. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Nchi (O) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, sasa naliomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya

Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU - CO 1 OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Kifungu C0 104	Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa	Shs.12, 360,000/-
Kifungu C0 106	Idara ya Upigaji Chapa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali	Shs.781, 406,000/-
Jumla Kuu		**Shs.793,766,000/-**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu PC 0101	Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais	Shs.756, 466,000/-
Jumla Kuu		**Shs.756, 466,000/-**

(Kifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bilaya Mabadiliko yoyote)

Kifungu PC 0102

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi hii kutaka ufafanuzi kidogo kwa sababu hii hotuba ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tayari nilikwishaiunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabla sijaja katika hoja yangu nilikuwa ninataka nimshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohamed kwa ufafanuzi wa masuala ambayo niliuliza akanijibu. Na ninashukuru sana kwa umakini wake katika kuhakikisha kwamba kila fedha ya serikali itakayotoka lazima ihakikiwe. Lakini nilikuwa nina ombi moja tu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ajaribu zaidi kuangalia watendaji wake waliosimamia fedha za miradi ya maendeleo hasa zinazotoka kwa wafadhili. Wakati mwengine katika wizara

kuna mambo yanakuwa wameshakubaliana kwenye wizara. Lakini inapotakiwa fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kunakuwa na ugumu wa kupatikana zile fedha na ndiyo ile hoja yangu niliyozungumza kwamba wakati mwengine Mhe. Mwenyekiti, inawezekana huku wizara tayari imeshakubaliana, lakini Wizara ya Fedha na Mipango wanakuwa wagumu katika kutoa fedha. Lakini kwa kauli yake ninamshukuru sana aweze kusimamia vizuri hili suala ili lisije kutuongezea ile kwamba fedha inakaa muda mrefu halafu inakuja kutuongezea *interest*. Ninakuja katika hoja.

Mhe. Mwenyekiti, nilipochangia kutokana na muda ulikuwa mdogo kuna baadhi ya maeneo niliyapeleka kwa maandishi, nilimpelekea Mhe. Waziri kuhusu suala la madiwani.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tumechaguliwa pamoja na madiwani, lakini mpaka leo madiwani wetu Mhe. Mwenyekiti, bado hawajaapishwa, hawajakula kiapo, hawajachagua viongozi wao wakiwemo Mameya na Wenyeviti wa Halmashauri, jambo ambalo litakwamisha sana shughuli za maendeleo na hasa katika mwezi huu wa Ramadhani Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu inapiga marufuku masuala ya maftari ya pamoja, tumeshasema ng'ombe wasifugwe, Shaurimoyo ndio ng'ombe wengi na punda wengi. Kwa hivyo, wale madiwani Mhe. Mwenyekiti, ndio watakaotusaidia katika kuratibu hizi shughuli.

Sasa mpaka leo hawajaapishwa, hebu tuambiwe na serikali, lini madiwani wetu wataapishwa ili tuweze kuwapata Mameya wetu, pamoja na Wenyeviti wa Halmashauri, ili waweze kutusaidia kazi katika majimbo yetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru sana ndugu yangu Mhe. Hamza Hassan Juma kwa namna ambavyo anayasimamia mambo, ili mambo yetu yaende vizuri kwa tija ya wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikubaliane na yeye kwamba ni kweli baada ya viongozi kuchaguliwa wanahitaji kutekeleza majukumu yao. Lakini kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti, tunatekeleza matakwa ya sheria, na kwa sababu sheria yetu hii ni mpya, inabidi taratibu fulani zifuatwe na zikamilike ili tangazo rasmi la serikali na hatua nyengine zifuate. Kwa kuwa sasa tangazo rasmi la serikali limetoka, hivyo sina shaka yoyote, hicho anachokisema Mhe. Hamza Hassan, ndio hicho hicho tunachokitaka serikali. Kwa hivyo, kuanzia sasa wakati wowote hatua hizo zitachukua mkondo wake.

Mhe. Mwenyekiti, lile suala la mwanzo ambalo amelizungumza lilimgusa Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango hapa, ameninong'oneza niliseme kabisa kwamba ushauri wake Mhe. Hamza Hassan ameupokea na ataufanyia kazi kwa maslahi ya nchi yetu ili tusonge mbele. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi wakati nachangia nilizungumza mustakbali mzima juu ya maafa ya mabadiliko ya hali ya nchi katika Jimbo langu la Jang'ombe. Kuna kero kubwa sana ambayo mara kwa mara imekuwa likitokea juu ya mashimo yasiyopatiwa ufumbuzi mpaka dakika hii. Namuomba Mhe. Waziri anieleze imekuwaje mpaka dakika hii sijapata ufumbuzi na wala sijui lini lile tatizo langu la pale kwenye eneo langu la Jang'ombe litaweza kutatuliwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana ndugu yangu Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Huu hasa ndio umahiri na umakini wa Waheshimiwa Wawakilishi wa CCM, hongereni sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilieleza hivi kwamba serikali imeunda kamati maalum ya wataalamu ili waipitie kwa kina sana, matatizo yote na changamoto zilizojitokeza kwa ajili ya mustakbali mwema wa nchi yetu, hususan katika suala zima la kutuama kwa maji, mmomonyoko wa ardhi, ujenzi holela na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu kwamba kamati hiyo ya wataalamu ilifanya kazi nzuri. Napenda nirudie kuipongeza kamati hiyo kwa kazi iliyofanya, yakiwemo mapendekezo ya eneo la Jimbo la Jang'ombe.

Kwa hivyo, Mhe. Abdalla Maulid nakuomba ndugu yangu utustahamilie na utupitishie mambo haya yaende vizuri ili tuweze kusimamia vizuri hatua iliyobaki. Kama nilivyosema baada ya kumaliza utaratibu huu wa ripoti ya wataalamu, taarifa ile inakwenda kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu baada ya kutoka kwenye Kamati ya Makatibu Wakuu itakwenda serikalini kwa maana ya Baraza la Mapinduzi, kwa muongozo wa hatua za kuchukuliwa, kwa sababu kuna mambo mengi pale ambayo itabidi yachukuliwe ikiwemo kuvunjwa kwa nyumba na kuwasaidia watu waliovunjiwa nyumba na miradi mikubwa ya ujenzi, kwa sababu inatakiwa kujengwa mitaro mingi mikubwa inayotoka mbali sana, kuanzia kwenye maji makubwa yanayotuama pale Mwanakwerekwe kule Ziwa Maboga na maeneo mengine. Kwa hivyo, huu ni

mradi mkubwa sana na unahitaji fedha nyingi, na inahitajika tafakuri kubwa na kuwekwa utaratibu mzuri wa kukamilisha suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, nayajua matatizo wanayoyapata ndugu zangu wa Jang'ombe, Kwahani na mwahala mwengine, lakini tunajua hali yetu ya kiuchumi inahitaji tafakari na kubuni mikakati sahihi ili kuondoa tatizo hilo. Naamini kwa umahiri wako na Serikali yetu ya Mapinduzi chini ya Chama chetu cha Mapinduzi tutafanikiwa kutekeleza wajibu huo, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa tena. Pamoja na majibu mazuri na ufafanuzi mzuri wa Mhe. Waziri, lakini naomba uniambie na unipe muda kama mwakani 2018 au 2020, kwa sababu imekuwa kero ya muda mrefu sana.

Mimi nakumbuka toka ni mdogo yale masuala yalikuwepo. Sasa hivi nimekuwa kiongozi kwa sababu yananiuma sana, niko tayari kukamata shilingi yako mpaka nijue ni lini utanipa *time limit*, ambayo ikifika mwaka 2017/2018 basi matatizo yale pale Jang'ombe tumeshayatatua.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema huo ndio umahiri wa Wajumbe wetu wa Baraza la Wawakilishi kutokana na CCM na wana imani kubwa na wananchi na hawataki yatokee mateso, kero na usumbufu kwa wananchi, na ndio maana wanayauliza haya.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hisia hizo hizo alizonazo Mhe. Mwakilishi ndio hisia hizo hizo inazo serikali, tusingependa kabisa wananchi wetu wasumbuke, tusingependa kabisa kuwepo na matatizo na changamoto hizo, nia na dhamira ni kuondosha changamoto hizo. Kama nilivyosema tayari hili jambo limefanyiwa kazi kwa ripoti iliyotayarishwa vizuri, lakini ni jambo ambalo linahitaji fedha nyingi, kwa sababu ni eneo kubwa. Sio suala la pale Jang'ombe tu, chanzo chake ni kikubwa, maji chini yamejaa katika visiwa vyetu vya Zanzibar, na kutokana na maji kutuama sana hasa kwenye lile eneo la Mwanakwerekwe Ziwa Maboga, na kwengine na watu kujenga katika njia za maji, wamesababisha maji yasipite katika njia zake yakaenda baharini maji, matokeo yake maji yanakaa chini ya nyumba zetu. Sasa sio jambo jepesi ambalo naweza kulitolea muda hapa nikasema kwamba mwaka huu jambo hili limekwisha.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema awali kwamba hii programu inakwenda serikalini kwa maelekezo, kutakuwa na miradi mingi, kutahitajika fedha nyingi

na pengine maeneo mengine tutawashirikisha wahisani. Nikasema *component* moja tu ya *ZUSP* ile, nimeona mabilioni mangapi ya shilingi yanatumika katika mradi ule mdogo, huo ni mradi mkubwa sana unaohitaji tafakuri ya kina.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Abdalla Maulid atukubalie, kwa sasa siwezi kutoa muda, lakini naamini wananchi wa Jimbo la Jang'ombe wameshakuona umakini wako, umahiri wako na hiki hakitokuwa kipindi cha kwanza, nakuombea dua sasa uendelee kwa miaka mingi ijayo na Mwenyezi Mungu akupe afya na umri uweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Tuendelee, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Haya. Tuendelee.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii, na mimi kwa upande wangu wa Jimbo la Welezo ni Magharibi, kuna kero nyingi hasa kero za njia, kwa hivyo zinasababisha maafa kila siku kule Welezo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nenda kwenye hoja moja kwa moja.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Hoja yangu ni kwamba nataka kauli ya serikali, lini serikali itashughulikia zile njia hasa njia ile ya kwenda kule Kinuni, ambayo wazazi hawafiki barabarani wanajifungulia njiani kila siku na kule kunaishi watu wengi na pa kupita hawana.

Nataka kauli ya serikali iliyo thabiti ambayo lini au mwaka gani itaanza kuitatua kero hii. Kadhalika njia ya *Mkapa Road* kila siku inaua watu kwa sababu haina vituo na haina mikato ya kusimama daladala. Nataka kauli ya serikali lini njia hii itawekewa vitu hivyo, ili vifo vya wananchi wetu viondoke kwa kufa kila siku. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema ni wajibu wetu Waheshimiwa Wawakilishi kuwatetea wananchi wetu. Kama nilivyosema kwamba huo ndio umahiri wa viongozi hawa wanaotokana na CCM, wanajali matakwa ya watu, shida za watu na wanakuwa tayari kuwatumikia watu. Kwa msingi huo wanataka matatizo yaliopo kwa wananchi yaondoke, na ni mtazamo huo huo ambao serikali inao katika kutafutia ufumbuzi matatizo ya wananchi.

Kwa kuwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais amealikwa kwenda kutembelea eneo hilo, kuona hali halisi ilivyo ya njia hizo. Naomba Mhe. Hassan Khamis

avute subira amngojee Mhe. Makamu wa Pili atakuja kupanga kuja huko ili kuona tatizo lilivyo. Kama mlivyosema hapa Waheshimiwa Wajumbe, kwamba Mhe. Makamu wa Pili ni jembe, na jembe hili litafanya kazi yake kutatua matatizo ya wananchi na ndio msingi wake. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Naomba tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu PC 0102	Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali	
Kifungu ST 010201	Programu ndogo ya Kukabiliana na Maafa	Shs 850,867,000
Kifungu ST 010202	Programu ndogo ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa	Shs 1,037,082,000
Kifungu ST 010203	Programu ndogo ya Shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya Muungano	Shs 8,561,838,000
Kifungu ST 010204	Programu ndogo ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dar es Salaam	Shs 447,517,000
Kifungu ST 010205	Programu ndogo ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu	Shs 462,121,000
	Jumla ya Kifungu	**100,359,426,000**

Kifungu PC 0103	Programu Kuu ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa	
Kifungu ST 010301	Programu ndogo ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa	Shs 873,940,000

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, sina haja ya kumsimamisha waziri, lakini nataka kutoa maelezo tu kwamba nilipokuwa nikichangia nilisema kwamba, mapato yalielezwa kwa miaka miwili mfululizo milioni 600, na *projection* kwa mwaka ujao imeongezwa kidogo sana, kiwanda kile tumeshakipa mitambo mipya, tunatarajia na utendaji wao uwe maradufu. Lakini kwa *projection* uliowapa tunawapa *limitation* ya kuongeza mapato, tunawapa *room* ya kutofanya kazi vizuri. Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Waziri aichukue hiyo *concern* yangu, ili tukisimamie vizuri kiwanda kile kifanye kazi ipasavyo. Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tuendelee.

Kifungu ST 010301	Programu ndogo ya Usimamizi wa Shughuli za Upigaji Chapa	Shs 873,940,000
	Jumla ya Kifungu	**Shs 873,940,000**
Kifungu PC 0104	Programu Kuu ya Uongozi na Utawala	
Kifungu ST 010401	Programu ndogo ya Uongozi na Utawala	Shs 2,093,000,000
Kifungu ST 010402	Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti	Shs 286,925,000
Kifungu ST 010403	Programu ndogo Ofisi Kuu Pemba	Shs 570,450,000
	Jumla ya Kifungu	Shs **2,857,468,000**
	Jumla Kuu:	Shs **15,847,300,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C02 BARAZA LA WAWAKILISHI

Kifungu PC 0201	Programu Kuu ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na kusimamia Taasisi za Serikali	
Kifungu ST 020101	Programu ndogo ya Kutunga Sheria, Kupitisha Bajeti na Kusimamia Taasisi za Serikali	Shs 6,542,950,000
	Jumla ya Kifungu	**Shs 6,542,950,000**

Kifungu PC 0202

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, samahani kwanza naingia jikoni, maana naingia kwenye Baraza la Wawakilishi. Wakati nilipokuwa nikichangia nilisononeshwa sana na kutokuwa na miundombinu ya walemavu katika Baraza letu la Wawakilishi. Sasa nimuombe Mhe. Waziri atwambie ni lini itafanywa miundombinu ya ndugu zetu walemavu kupanda juu kwenye Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa aliyesimama sasa hivi ni ndugu yangu, mwenzangu wa karibu sana na namuheshimu sana Mhe. Mohammed Said Dimwa, na kwa kuwa dhamira

yetu ni moja na wizara yetu pia imepewa jukumu la kushughulikia watu wenye ulemavu.

Kwa hivyo, tutafanya kila jitihada ili kuona Baraza letu la Wawakilishi linatoa namna njema ya kutengeneza miundombinu itakayosaidia ndugu zetu hawa.

Mhe. Mwenyekiti, naelewa mwaka huu ugumu wake wa fedha kutokana na hali halisi ambayo sote tunaelewa, lakini naamini sana tulianza kitambo mipango hii tokea kipindi kilichokwisha kuona ni namna gani tunaweza kuwezesha Baraza letu hili likawa na miundombinu hiyo ya kusaidia ndugu zetu hawa wenye ulemavu.

Kwa kweli jambo hili inapaswa sote tushirikiane, maana kuna ule msemo unaosema kwamba 'ukiwa huna ulemavu leo basi unaweza kuwa kesho'. Tumuombe Mwenyezi Mungu atusaidie tuwe katika hali nzuri ili na wenzetu hawa tuwapunguzie kila aina ya shida zao wapate nguvu ya kufanya mambo yao na wasamehewe makosa yao na sote tusamehewe makosa yetu.

Namuhakikishia Mhe. Mohammed Said tutajitahidi, tunauona umuhimu huo, tushirikiane katika kulikamilisha jambo hili.

Mhe. Mohammed Said Mohammed(Dimwa): Mhe. Mwenyekiti, nimemuamini sana Mhe. Waziri kwa maneno yake, na vile vile namuheshimu sana kwa maneno yake na mimi niko kwenye Kamati hii, lakini nilikuwa nataka niombe tu, ni utafiti upi ambao umefanyika wa kuweza kuona *lift* inaweza kugharimu kiasi gani ili kuwaondoshea kadhia refu hii hawa ndugu zetu walemavu na baadae kunieleza basi nitaomba tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Mohammed Said kwa namna ya maswali yake ya kitaalamu sana, ambayo yanatupa changamoto kubwa ya kujitayarisha kufanya wajibu wetu. Kwa kuwa kulikuwa kuna jitihada fulani zimefanyika, lakini kwa sasa kwa kuwa sina takwimu hapa mkononi zile za gharama na kadhalika. Lakini tulianza kuzungumzia suala la kuwa na *lift*, na kuna uwezekano sana wa kuwa na *lift* hapa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mohammed Said atupe muda, tutamletea maelezo kwa kina kwa maandishi, kwa sababu hapa sasa sina haya, lakini dhamira ni kulishughulikia jambo hili, kazi hii imeshaanza nataka nimuhakikishie itafanyika katika miaka ijayo ili kuliondoa tatizo ambalo sote linatukera.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa ninamuamini sana Mhe. Waziri na maneno yake huwa hayumbi yumbi naomba tuendelee.

Fungu PC0202 Programu Kuu ya uongozi na utawala wa Baraza la Wawakilishi

Kifungu PC 020201	Programu ya Uongozi na Utawala Baraza la Wawakilishi	Shs 7,873,457,000
Kifungu PC 020202	Afisi Kuu Pemba	Shs 2,722,093,000
	Jumla ya Fungu	**Shs 10,565,550,000**
	JUMLA KUU	**Shs 17,138,500,000**

Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C03 TUME YA UCHAGUZI

Kifungu C 0301	Utawala Unguja	Shs 310,000,000
	JUMLA KUU	**Shs 310,000,000**

Kifungu C 0302 Programu kuu ya Usimamizi wa Kazi

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti wakati nilipokuwa nikichangia katika Tume hii ya Uchaguzi nilikuwa nataka kujua hatua ambazo Tume ya Uchaguzi wengi watu walikuwa wameharibu uchaguzi kwa makusudi, lakini nataka kujua hatua gani mpaka sasa zimechukuliwa kwa wale wenzetu walioharibu uchaguzi huo na kusababisha hasara kubwa kwa Serikali.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Ni kweli jambo hili sio tu linamuumiza yeye lakini Serikali na wananchi kwa jumla hawakupenda kabisa waone vituko na vitendo vilivyofanywa kwa makusudi kuharibu uchaguzi wetu, lakini kwa sababu wale waliofanya uchaguzi hawakuwa pamoja na Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu akatoa hukumu sahihi, ukafanywa uchaguzi mwengine kwa salama usalimini na matokeo yake ndio haya tunayoyaona leo humu ndani.

Nataka nimhakikishie Mheshimiwa kama maelezo yangu ya awali nilivyosema kwamba uchunguzi unaendelea, kwa sababu mtandao ulikuwa mrefu uliwahusu wengi, sio tu watendaji kwenye Tume ya Uchaguzi au baadhi ya watu lakini pia wapo wanasiasa kutoka pande zote, katika itikadi zote, ambao wamefanya njama za kuuharibu uchaguzi huu, kwa hivyo ninachomuomba Mhe.

Mohammed Said atupe muda, kwa sababu kuna watu wanaoshughulikia jambo hili kwa utaalamu mzuri, kwa umakini ipo siku kazi yake itakamilika na wale wote walioshiriki kuharibu uchaguzi hatutomuonea haya hata awe kiongozi ana ukubwa gani katika chama cha siasa, basi hatua za kisheria zitachukuliwa.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nimesoma sana na nikaelewa matamshi mazuri sana ya seneta Mhe. Waziri na kuelewa nini anachokusudia, lakini nataka kusema tu kwa sababu wananchi walio wengi sana wa Jimbo la Mpendae na majimbo mengine ya Zanzibar wanahitaji suala hili lifanywe kwa haraka zaidi, ili waone basi Serikali imechukua hatua thabiti ili tuendelee basi tunahitaji kufanya kwa haraka zaidi. Vile vile Mhe. Waziri amenitia kwenye tawhid kwa Mungu naomba tuendelee.

Kifungu C 0302	Program kuu ya usimamizi wa Kazi za Utawala na uendeshaji wa Shughuli ya Tume ya Uchaguzi Zanzibar	Shs	1,174,812,000
Kifungu C 0302	Program ndogo ya uendeshaji wa Shughuli za Kiutala ya Tume ya Uchaguzi Pemba	Shs	185,388,000
	JUMLA	Shs	1,360,200,000
	JUMLA KUU	Shs	**1,360,200,000**

Fungu C 04 Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Kifungu C 0401 Program Kuu ya Udhibiti

Mhe. Nadir Abdulatif Yussuf Alwardy: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kuna swali langu niliuliza kwenye masuala ya dawa za kulevya nilikuwa naomba Mhe. Waziri anihakikishie au anijibu ni mapapa mangapi wanaouza unga ndani ya Zanzibar wamekamatwa mpaka sasa hivi. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kwa kuwa naendeleza majibu yangu pale kwamba kuna watuhumiwa 531 wametiwa mbaroni na wamefikishwa Mahakamani, na kwa kuwa wengine kesi zao zimeamuliwa, lakini kesi nyengine bado zinaendelea na kwa kuwa jambo hili liko Mahakamani hatuna nafasi kubwa sana ya kulizungumza katika Baraza lako hili.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia katika Tume hii ya Dawa za kulevya nilisema kwamba ni taasisi pekee ambayo ina

bajeti ndogo, lakini katika majumuisho Mhe. Waziri sikumsikia kugusia suala hili nilikuwa naomba ufafanuzi zaidi. Na lini Serikali itaongeza bajeti hii ya Tume za dawa za kulevya.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Sote tunaelewa kwamba bajeti hii ni ndogo, lakini hii ni kutokana na hali halisi ya uwezo wetu wa kiuchumi, pale ambapo mambo yatakuwa mazuri na kama mlivyomsikia hapa leo Mhe. Makamu wa Pili wa Rais anasema katika Baraza hili tutasoma kwa mara ya kwanza Mswada ule wa Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia, hiyo ni mbinu na mkakati wa kuelekea kuimarisha uchumi wetu ili hali yetu itakapokuwa nzuri basi mambo yote haya yatakuwa na bajeti nzuri, kwa sasa tuende kutokana na hali ilivyo, sungura huyu mdogo tunagawana kwa ule ukubwa wake, ili shughuli nyengine zipate nafasi yake ya kuendeshwa.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri ameelezea kutokana na hali halisi ilivyo lakini kauli hizi zinakuwa kila mwaka, bado hali ya fedha si nzuri, ni lini hali ya fedha itakuwa nzuri.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Kama alikuwa ananisikiliza kwa kina ataona maelezo yangu ya majumuisho yalikuwa na hekima fulani, pale ninaposema kuna wenzetu wanatutoa katika mstari ili muda mwingi tushughulikie na mambo ya siasa na tuache mambo ya msingi ya kuimarisha uchumi wa nchi yetu, ndio hawa wanaopitapita huko wakasema maneno ili Serikali itoke katika mstari baada ya kushughulikia mambo ya msingi ya kuimarisha uchumi wetu na kujitayarisha katika karne hii ya 21 katika suala zima la Sayansi na Teknolojia, ambao kuimarika kwa sayansi na wataalamu wetu wakajikita huko ndipo tunapopata ufumbuzi wa namna gani basi katika eneo dogo hili likawa na uchumi mkubwa.

Juu ya udogo wa Serikali yetu tukawa na uchumi mkubwa na soko kubwa, kwa hivyo haya ndio mambo ya msingi ya kuangalia kwamba sasa tunayo *challenge*, ardhi yetu kweli ndogo, idadi ya watu inaongezeka basi tuige mfano wa China wanaongezeka lakini wanaongezeka na utaalamu.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Yussuf Hassan Iddi sote kwa pamoja hili jambo sio la Serikali peke yake, hii hali halisi ni yetu sote, kwa hivyo tuhubiri sasa kuelimisha wenzetu waelewe, waache kupotosha umma, washirikiane na sisi tujenge nchi yetu ili tuepukane na hizi siasa za Maji taka na sasa tuwe makini katika kuimarisha uchumi wa nchi yetu, uchumi wetu ukiwa tayari mambo yote haya yatakuwa tayari.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mimi labda Mhe. Waziri anihakikishie tu kwamba bajeti ya mwakani 2017/18 basi fungu hili la Tume ya Dawa za Kulevya anaweza akaliongeza, akiniahidi basi Mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, hii bajeti ni yetu sote ya wananchi wote, Serikali na wananchi kwa jumla inategemea uwezo wetu utakaofanya katika kuzalisha. Hapa ninachosema bado tuendelee kuelimisha wenzetu namshukuru sana Mhe. Said Soud kwa kiasi fulani leo amewaelimisha ndugu zetu hawa, huu umasikini wetu unachangiwa na siasa za upotoshaji unatutoa katika mstari. Wakibadilika hawa na wananchi waelewe hilo kwamba matatizo yetu haya ya umasikini kuna watu wanayachangia na wanawapenda sana, wajue hao wanaowapenda wanawakandamiza, wanawadumaza wana *sabotage* kuimarika kwa uchumi wetu. Watoke huko tushirikiane tufanye mambo twende mbele, nchi inahitaji kubadilika, huu si ulimwengu wa kususiana tena wala kugomeana, ni ulimwengu wa sayansi na teknolojia. Anayefanya kugomea amepitwa na wakati, hana maana ya kuongoza nchi hii kwetu.

Kwa hivyo ninachosema tu Mheshimiwa hali yetu ikiwa nzuri kwa pamoja mambo haya tutayabadilisha sana.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mheshimiwa tuendelee.

Mhe. Abdalla Ali Kombo: Mimi sizungumzii sungura nazungumzia *information*, kweli haturuhusiwi kujua Mahakama imefanya nini, lakini pia haiwezekani watu mia tano Serikali haina habari katika watu mia tano hawa hakuna kinachoendelea, kuna baadhi ya siku sote mashahidi tunasikiliza Redio Zanzibar asubuhi kuna mambo ya mawio yanatujulisha mambo yote ya Mahakamani mpaka aliyeiba nazi mpaka kifungo alichofungwa.

Je, mpaka leo hii watu mia tano hawa Serikali haijapewa taarifa yoyote, na Mahakama kweli hatuwezi kuingilia, lakini katika watu mia tano hawa hakuna taarifa yoyote, tunawaambia nini wananchi na watu hawa wakishakukamatwa asubuhi na kwenye magazeti yote tunajuilishwa lakini wananchi sasa hivi hatuwapi *feedback* kuna nini. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri bado sijaridhika unipe maelezo ya kutosha kuhusiana na kifungu hiki.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kwa mujibu wa Kanuni ya 98(c) inasema hivi: Haihusu jambo ambalo wakati huo liko mbele ya Mahakama popote katika Zanzibar au katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hivyo

nafikiria sana kwamba hili hatutoweza kulijadili hapa kutokana na hali halisi ya sheria zetu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mheshimiwa pia kanuni zetu haziruhusu kujenga hoja ya kuzuia fungu wakati hukuchangia, Mheshimiwa hakuchangia katika bajeti hii. (*Makofi*)

Kifungu C 0401 Programu Kuu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya

Kifungu C 040101	Programu ndogo ya Udhibiti wa Usafirishaji na Usambazaji wa dawa za kulevya	Shs 53,313,000
Kifungu C 040102	Programu ndogo ya Kinga ya Msingi ya Mahitaji na Matumizi ya Dawa za Kulevya	Shs 35,500,000

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi katika maelezo yangu ya mwanzo nilithubutu kusema kwamba pale Jang'ombe ni sehemu moja ambapo panatumiwa sana madawa ya kulevya hata mimi kupewa nafasi ya ulezi kwa wale jamaa ambao wanaacha madawa ya kulevya katika sehemu zangu za Jang'ombe pale Mental Hospital.

Sasa sijui Serikali inatwambia nini mpaka dakika hii kwa sababu baada ya kupungua kasi ya uingizaji madawa Zanzibar nafikiria sasa hivi yameongezeka juu ya ukali wa Rais wa Jamhuri ya Muungao wa Tanzania na zile sehemu nyingi tu ambazo zinajulikana kuuza madawa ya kulevya hivi vipisipisi, na wale waingizaji wakubwa nathubutu kusema kwamba wanatambulika.

Sijui Serikali kwa hili inatwambia vipi ili kuweza kudhibiti wale watumiaji wadogo wadogo na hao waingizaji wa madawa ya kulevya wakubwa.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, namheshimu sana ndugu yangu Shehe Abdalla Maulid Diwani lakini nafikiri maelezo tumeyasema kwa kina, na utaratibu wetu hurudii maneno ambayo yamezungumzwa, sasa kurudia majibu ambayo tayari tumeyajibu yana msingi wa kucheleweshe muda hapa.

Lakini napenda tu niseme kwamba Serikali na sote viongozi tuna wajibu wa kupambana na jambo hili baya la madawa ya kulevya, jambo hili linaathiri vijana wetu, kwa hivyo jambo hili si la Serikali peke yake, jambo hili ni letu

sote Waheshimiwa Wawakilishi, wananchi Serikali lazima tujipange kwa nguvu zote tufanye hivyo.

Hata hivyo, nimesema kuna kikosi maalum tunashirikiana na wenzetu katika Jamhuri ya Muungano na hapa Zanzibar kufanya mkakati huu kutekeleza wajibu wetu. Nilisema hapa kwamba waheshimiwa tutakapochukua hatua msije kutuomba fulani ndugu yangu fulani jamaa yangu fulani hivi, *sheria ni msumeno*, shughuli itafanyika sitaki niiseme lakini nakuhakikishieni shughuli itafanyika na itamkuta kila ambaye anakwenda kinyume. Nia yetu ni kupambana na watu hawa, hawa ni maadui kabisa wa nchi yetu, maadui wa watoto wetu, maadui wa maendeleo ya nchi yetu. Kwa hivyo, la msingi ni kushirikiana tukatafuta ufumbuzi wa tatizo hili. Hili si jambo la serikali peke yake, wala si jambo la kulitolea ahadi peke yetu kama serikali, ni jambo la mashirikiano, la kupambana kwa vita yote ili kuondoa tatizo hili.

Waheshimiwa Wawakilishi mihemuko katika maeneo mnayaona, mambo haya mnapoyaona unatakiwa utoe taarifa ili yashughulikiwe vizuri. Sasa tusifichane, ukimuona mtu anafanya shughuli hii basi tuambizane shughuli iende, ni jambo la mashirikiano linataka nguvu ya pamoja na naamini kwa namna tulivyojipanga tutafikia hatua kubwa zaidi.

Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni kweli nakubaliana na yeye, maelezo yake mazuri ambayo hayana dosari, lakini tukumbuke kwamba katika kipindi kilichopita hii taasisi ya madawa ya kulevya ilikuwa chini ya Makamu wa Kwanza wa Rais na imevumbua watumiaji wengi wa madawa ya kulevya kulikoni muda huu, yaani ilishindwa kufanya kazi zake ipasavyo na sasa imepelekwa kwenye Ofisi ya Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais. Je, unatuhakikishia vipi kwamba tutafanya mkakati maalum wa kuweza kupunguza hao watumiaji wa madawa ya kulevya?

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kama utakuwa umemuelewa vizuri mwanzo kabisa Mhe. Waziri alipokuwa anajibu swali, anasema haya yote ameshayaeleza alipokuwa anajibu hoja, na ameeleza vizuri sana. Sasa unapouliza swali tena ina maana alirudie lile jibu ambalo tayari ameshalisema, laa kama una ziada au hujaridhika basi uliza katika *angle* hiyo ya kutoridhika, lakini sio kulirudia tena suala hili.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sawa Mwenyekiti unajua nilizungumzia hilo kwa sababu yalizidi katika miaka hii mitano iliyopita, ndio maana napata wasi wasi kwamba tumebadilisha wizara kutoka kwenye Makamu wa Kwanza na kuja Makamu wa Pili. Nafikiri ni suala la msingi bado ni kwamba je watakuwa na utaratibu gani kuyapunguza, nafikiri ilikuwa nipate jibu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba utaratibu ni ule niliosema awali kwamba tuna vyombo vyetu hivi vya ulinzi na usalama vinashirikiana katika kufanya kazi ya *intelligence* katika kupambana, na vile vile tumeanzisha huu utaratibu wa *case flow management*, msingi wake kila muhusika atakayetiwa mbaroni hizo kesi ziende kwa haraka na wasipate namna ya kupenyuka katika ushahidi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa tushirikiane naye katika kulipatia ufumbuzi jambo hili, hakuna muujiza mwengine zaidi ya huu nilioutaja.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mheshimiwa tuendelee.

Jumla Ndogo	**Shs 35,500,000**
Jumla Kuu	**Shs <u>88,813,000</u>**

(*Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu PC0402

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, wakati nikichangia nilikuwa nimeonesha hisia zangu kali sana jinsi ya jimbo langu lilivyoathirika na madawa ya kulevya, na wakati huo huo Tume hii imeeleza ni kuratibu. Sisi hatutaki kuratibiwa, kwa sababu hatuipi tume hii meno, kwa nini tunaleta sheria hapa ya kuunda Mahakama ya Rushwa, Mahakama ya Uhujumu Uchumi tusilete sheria hapa ya kuweza kushughulikia madawa ya kulevya.

Nataka maelezo ni lini serikali italeta sheria ili tupitishe tuone basi tunaunda Mahakama hii maalum ya kuweza kushughulikia jambo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba tunayo sheria nzuri Nam. 9 ya mwaka 2009 tatizo ni utekelezaji wa sheria yenyewe, wala tatizo sio Tume ya Kudhibiti Madawa. Nimesema hapa kwamba tatizo ni pale kwenye utekelezaji tuna Polisi, tuna Ofisi ya *DPP* na Mahakama, sasa ili kupata majibu mazuri tumeamua kufanya kazi *jointly* kati ya Polisi, Ofisi ya *DPP* na Mahakama ndio itakayotoa jibu,

lakini licha ya hivyo tunaunda kikosi maalum chenye ushirikiano na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano katika kupambana na jambo hili.

Sheria ni nzuri sana, ukiipitia utaiona si suala la sheria, ni suala la utekelezaji wa sheria. Hawa wajumbe wa tume ni raia tu, Polisi ndio wenye mamlaka ya kisheria ya kumtia mtu mbaroni, ya kumkamata na kumpeleka, na Katiba yetu inampa nafasi *DPP* kuchunguza ushahidi wa polisi aone ipo mantiki ya kushtakiwa hii nchi ya kidemokrasia, ionekane ushahidi huu, pale inapoonekana na kosa sasa anapokuwa na ushahidi wa kutosha wa kutetea Mahakamani anakwenda Mahakamani kutetea kesi yake, na ukiwa na ushahidi mzuri unamshinda muhalifu, muhalifu anafungwa hatua zinaendelea.

Kwa hiyo, la msingi hapa tumetaka hizi taasisi tatu zikae pamoja zifanye hivyo ndio kubwa ninaloweza kulisema, lakini sheria iko vizuri tu Nam. 9 ya 2009. Ahsante sana Mwenyekiti.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri kanikoroga kweli kweli, kwa sababu tukiendelea siku zote hatupati ushahidi na sifikirii kama tutapata ushahidi juu ya mambo haya tunapeleka unga *red handed* tutaambiwa sukari. Marekani alienda kumchukua Manuel Noriega moja kwa moja hata hakumpeleka kwa *DPP* wala wapi akamfunga. Mheshimiwa tukiendelea kusubiri kupata ushahidi kamili tukizunguka kwa *DPP* tutaendelea kuuana, tutaendelea ndugu zetu kuua. Tuendelee Mheshimiwa.

Kifungu PC 0402	Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Dawa za Kulevya	
Kifungu SC 040201	Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa Tume ya Dawa za Kulevya	Shs 288,381,000
Kifungu SC040202	Programu ndogo ya Kuratibu Shughuli za Tume ya Dawa za Kulevya Pemba	Shs 62,706,000
Jumla		**Shs <u>351,870,000</u>**
Jumla Kuu		**Shs <u>439,900,000</u>**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU C05 - TUME YA UKIMWI

Kifungu PC 0501	Programu Kuu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa Ukimwi	
Kifungu SC 050101	Programu ya Mawasiliano na Utetezi	Shs 248,959,000
Kifungu SC 050102	Programu ya Uratibu wa Muitiko wa Taifa wa Ukimwi	Shs 492,705,000

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, tunazidi kushauri ili tuweke mambo yetu sawa, Mhe. Waziri kwa sababu hizi wizara zimeungana, tunamuomba radhi sana atufahamu, hatuna nia mbaya tupo wenyewe humu, kwa hiyo lazima tuyarekebishe mambo.

Mhe. Mwenyekiti, katika Tume ya Ukimwi tunaijua tume hii ilikuwa wizara gani huko ilikotoka. Sasa kwenye muundo wake unatia shaka sana, nimeangalia nafasi za kazi kwenye uratibu wa muitikio wa taifa wa ukimwi kuna *Manager* wa Sera na Mipango kwenye C73, kuna Afisa Sera, kuna Mwanasheria, kuna Afisa Mipango, kuna Afisa Miradi, kuna maafisa watano waliopo sasa hivi na mwakani wanaendelea tena hivyo hivyo, kuna haja gani kazi ni hizo hizo Mheshimiwa.

Sasa mimi ombi langu ni dogo tu kwa Mhe. Waziri kama nilivyosema, tunasaidia kuweka mambo sawa, anikubalie tu ilivyokuwa wao sasa imekuja hii idara kwao upya ni idara mpya kwao, ni kitengo kipya wafanye *review* tu ule muundo tuone wale maafisa waliopo kweli wanahitajika, isiwe watu wamechukuliwa kuwekwa tu pale wafanye kazi zile walikuwa wanafanya kazi nyengine za siasa katika ofisi ile iliyopita, wala haitushindi Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu **wa Pili wa Rais:** Mhe. Mwenyekiti, ninapopata ushauri wa mtu mzito kama Dkt. Mwinyihaji Makame sidhani kama unakatalika, kwa hiyo wewe ni mtu mzima, ana mawazo mengi na nia yake ni kujenga, tutafuatilia jambo hili na ushauri tunaupokea.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mheshimiwa tuendelee.

Kifungu SC 050102	Programu ya Uratibu wa Muitiko wa Taifa wa Ukimwi	Shs 492,705,000
	Jumla Kuu	Shs **741,665,000**

(*Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu PC 0502	Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji	
Kifungu SC 050201	Programu Ndogo ya Uratibu wa Masuala ya Ukimwi Pemba	Shs 137,978,000
Kifungu SC 050202	Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji Unguja	Shs 326,533,000

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, kwa *spirit* ile ile ya kujenga, ukiangalia kwenye idadi ya watenda kazi ambao wamewekwa kwa *sub-programme* hii ya utawala na uendeshaji SC050202 kuna kada mmoja ameitwa Katibu wa Sheha. Sasa nilikuwa najiuliza Katibu wa Sheha kwenye kada hii katika utawala na uendeshaji hapa katika *level* hii ya *coordination* ya Tume ya Ukimwi inaingia vipi kada hii ya Katibu ya Sheha, C73 ataiona Mhe. Waziri akiangalia buku kwenye C73 kuna kada hapo 11136 Katibu wa Sheha ni *printing mistake* au Katibu wa Sheha kaingiaje hapa, hilo nilikuwa najiuliza au kama ni sawa mimi sina matatizo, lakini nilitaka kujua tu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kwa sheria yetu mpya hii ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Katibu wa Sheha yuko kisheria na ni mtu mzito sana. Kwa hiyo, hakuna makosa kuweko Katibu wa Sheha ikiwa kama kuna jambo jengine Mheshimiwa atueleze kama nilivyosema tupo hapa kusikiliza ushauri na maelekezo ili tufikie hatua nzuri ya utekelezaji wa majukumu yetu.

Saa zote tuko tayari kupokea ushauri na namuheshimu sana Dkt. Mwinyihaji ni mfanyakazi wa siku nyingi wa serikali na mwanasiasa mahiri sana. Kwa hiyo, sina wasi wasi naye katika ushauri wake, lakini hayo ndio maelezo yangu Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Dkt. Mwinyihaji tuendelee?

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, mimi nitamruhusu Mhe. Waziri tuendelee, tuta-*discus* zaidi baadae lakini wasi wasi kwamba hizi kada zote zilizowekwa hapa kwenye C73 ziko kwenye makao makuu wizarani, Mkurugenzi, Meneja wa Fedha, Afisa Utawala, Afisa Manunuzi wote hawa waajiriwa wako huko, sasa huyu Katibu wa Sheha naye kila shehia tutamchukua tumlete au vipi? Sasa nataka kusema naruhusu tuendelee Mheshimiwa, tuta-discus zaidi, nina wasi wasi kidogo au ndio wale niliowazungumza mwanzo pengine tumechukua watu tu kuwaweka kumbe tumeficha ficha mambo. Mheshimiwa tuendelee.

Kifungu SC 050202	Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji Unguja	Shs 326,533,000
	Jumla	Shs **464,511,000**
	Jumla Kuu	Shs **1,206,176,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa, sasa niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa utulivu wenu lakini kwa wale ambao wametoa michango mbali mbali pamoja na Manaibu Waziri na Mawaziri niwashukuru sana kwa michango yote ambayo tunaamini kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili itayafanyia kazi yale ambayo tumekubaliana nayo hapa, lakini yale ambayo yameonekana kwamba ni muhimu.

Kwa hiyo, niitakie wizara utekelezaji mwema na pamoja na Makamu wa Pili kila la kheri na wepesi pamoja na waziri wake na wepesi wa kufanya shughuli zake. Baada ya kusema hayo machache waheshimiwa naahirisha kikao hadi kesho tarehe 31/05/2016, saa 3:00 asubuhi.

(Saa 3:54 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 31/05/2016 saa 3:00 asubuhi)